

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

William MacDonald

Everyday Publications Inc.
310 Killaly Street W
Port Colborne ON L3K 6A6
Canada

*Copyright © 1996
par William MacDonald*

ISBN 978-0-88873-137-1

Traduction par G.I. Harlow

Imprimé au Canada

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Ukurasa

<i>Utangulizi</i>	4
Matayo	5
Marko	36
Luka	57
Yoane	88
Matendo	111
Waroma	138
1 Wakorinto	152
2 Wakorinto	169
Wagalatia	180
Waefeso	186
Wafilipi	193
Wakolosayi	199
1 Watesalonika	203
2 Watesalonika	209
1 Timoteo	214
2 Timoteo	221
Tito	225
Filemono	228
Waebrania	230
Yakobo	242
1 Petro	247
2 Petro	253
1 Yoane	257
2 Yoane	263
3 Yoane	265
Yuda	267
Ufunuo	270

UTANGULIZI

Mwandishi wa kitabu hiki ni mwalimu wa kujulikana wa Neno la Mungu na anakwisha kuandika vitabu vingi.

Anajua kueleza maneno waziwazi. Watu wote wanaosoma kitabu hiki pamoja na Agano Jipywa wata-pata faida kwa roho zao, si neno kama wamejua maneno machache au mengi mbele.

Habari Njema kama alivyoandika MATAYO

MWANZO

Matayo alikuwa akilipiza watu kodi siku moja wakati Yesu alipopita. Wakati Mwokozi alisema naye, “Unifuate,” Matayo aliacha kazi yake na maneno yake mengine, akageuka mwanafunzi mwaminifu wa Bwana. Kwa wakati wa nyuma Yesu alimchagua kuwa mmoja wa mitume kumi na wawili, na nyuma ya miaka mingine Matayo alichaguliwa kuandika Habari Njema ya kwanza.

Kusudi na shauri la Matayo

Kusudi la Matayo ndani ya Habari Njema hii ni kuonyesha ya kwamba Yesu wa Nazareti ni Masiya na Mfalme wa Israeli, wa pekee aliystahili kuwa na ruhusa kuketi juu ya kiti cha kifalme cha Daudi. Ndani ya sura mbili Matayo anatupasha juu ya kuzaliwa na utoto wa Kristo; sura kumi na sita ni juu ya utumishi wake katika Galilaya, karibu sura mbili juu ya utumishi wake katika Perea kwa upande wa mashariki wa Yorodani; karibu sura saba kwa juma lake la mwisho katika Yerusalem kufika kusulibishwa kwake; na sura moja juu ya kuonekana kwake kwa watu nyuma ya ufufuko wake. Kitabu hiki si habari zote za maisha ya Kristo, lakini matukio haya toka maisha na utumishi wake pamoja zinamfunua kama Mpakaliwa wa Mungu.

UMBO LA MATAYO

1. Kizazi na kuzaliwa kwa Masiya-Mfalme (sura 1)
2. Mwanzo wa maisha ya Masiya-Mfalme (sura 2)
3. Matayarisho wa Masiya kwa kazi yake, na mwanzo wa kazi hii, (sura 3–4)
4. Sheria za ufalme (sura 5–7)
5. Maajabu ya uwezo na neema ya Masiya, na mawazo mbali-mbali ya watu juu yao (8:1 – 9:35).
6. Mitume ya Masiya-Mfalme wanatumwa kuhubiri kwa Israeli (9:36 – 10:42)
7. Matata yanaanza (sura 11).
8. Masiya-Mfalme anakataliwa na viongozi vyta Wayuda (sura 12)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

9. Mfalme anatangaza namna mpya ya Ufalme itakayoendelea kwa wakati kwa sababu Waisraeli walimkataa (13:1-52)
10. Masiya anaendelea kutenda kwa neema lakini uadui unaongezeka (13:53 – 18:35)
11. Mfalme anakwenda Yerusalem (sura 19–20)
12. Masiya-Mfalme anafikia Yerusalem (sura 21–23)
13. Mfalme anaonyesha nini itatokea kufika kuja kwake kwa pili (sura 24–25).
14. Siku zilizotangulia msalaba (26:1-46)
15. Mfalme anasulibishwa (26:47 – 27:66)
16. Ufufuko wa Mfalme; anakutana tena na wanafunzi wake (sura 28).

1. KIZAZI NA KUZALIWA KWA MASIYA-MFALME (Sura 1)

Kizazi cha Yesu (1:1-17)

Kizazi hiki kinahakikisha ya kwamba Yesu anastahili kuketi juu ya kiti cha kifalme cha Daudi kama mwana wa Yosefu. Ndiyo, hakuwa mwana wa Yosefu kabisa, lakini Yosefu alimlea na kumfanya mwana wake. Tunaona hapa kizazi toka Daudi na Solomono na wafalme wa Yuda kufika Yosefu, mume wa Maria aliyezaa Yesu.

Kuzaliwa kwa Yesu (1:18-25)

Nyuma ya kupatana kuolewa na Yosefu, Maria alipata mimba kwa njia ya ajabu ya Roho Mtakatifu. Yosefu hakujua neno hili na alitaka kuvunja ahadi ya ndoa. Lakini malaika alimfahamisha ya kwamba Maria alikuwa na mimba kwa Roho Mtakatifu, na ya kwamba ilipasa mtoto kuitwa Yesu, kwa sababu ataokoa watu wake toka zambi zao. Yosefu hakujua bikira Maria kama ilivyo desturi ya bwana na mke kufika wakati mtoto alipokwisha kuzaliwa, kama alivyotabiri Isaya, Isa. 7:14.

2. MWANZO WA MAISHA YA MASIYA-MFALME (Sura 2)

Kufika kwa waakili (2:1-12)

Muda fulani ulikuwa umepita nyuma ya kuzaliwa kwa Yesu wakati watu wa mataifa, waakili toka mashariki walipofika kuabudu Masiya-Mfalme. Mfalme Herode wa Yudea alikuwa ameambatana na dini ya Wayuda. Alisikia habari za kuzaliwa kwa mtoto atakayekuwa Mfalme wa Wayuda. Aliogopa ya kwamba Mfalme huyu atamnyanganyia kiti cha ufalme, hivi aliuliza viongozi vya Wayuda kama Masiya atazaliwa pahali gani. Wakati aliposikia kwamba atazaliwa kwa Betelehemu, ali-

MATAYO

tuma waakili kwenda kumtafuta kusudi (ndilo neno alilosema) yeze mwenyewe aweze “kumwabudu” pale. Lakini wakati waakili walipokwisha kuona Yesu na mama yake na kutolea Yesu zawadi, walirudi kwa kwa njia nyininge.

Kukimbilia Misri (2:13-23)

Nyuma ya kusikia maonyo ya malaika, Yosefu alikimbilia Misri pamoa na Yesu na Maria (mash. 13-15). Herode alikasirika sana kwa sababu shauri lake kuvumbua pahali mtoto alipokuwa lilizuiwa, basi aliagiza watoto wanaume wote katika Betelehemu na kando kando, walio na miaka miwili na nusu kupita wauawe (mash. 16-18). Yosefu alibaki kwa Misri kufika kufa kwa Herode, kisha alisafiri na jamaa yake kwenda Nazareti, akakaa pale (mash. 19-23).

3. MATAYARISHO YA MASIYA KWA KAZI YAKE, NA MWANZO WA KAZI HII (Sura 3 – 4)

Kazi ya Yoane Mbatizaji (3:1-12)

Miaka 28 au 29 ilipita tangu mwisho wa sura 2 na mwanzo wa sura 3. Wakati Bwana Yesu alipokuwa na miaka 30 alikuwa tayari kuanza kazi yake katikati ya watu. Lakini kwanza Yoane Mbatizaji alitangaza habari zake. Alikuwa akiita taifa la Israeli kutubu na kuwa na roho tayari kwa kufika kwa Mfalme. Ilipasa Wayuda kuonyesha kwa njia ya kubatizwa katika Yorodani ya kwamba walitubu. Wengi wao walfanya hivi na roho ya kweli, lakini wengine, kama Wafarisayo na Wasadukayo, walibatizwa kwa kuonekana tu. Yoane alisema ya kwamba wale waliobatizwa na roho ya kweli watabatizwa na Roho Mtakatifu, lakini wale wengine watabatizwa kwa moto ya hukumu ya Mungu.

Ubatizo wa Yesu (3:13-17)

Wakati Yesu alipoomba Yoane kumbatiza, Yoane alijaribu kuktata akisema hakustahili kubatiza Bwana wake. Ndiyo, Yesu hakuwa na zambi alizohitaji kutubu, lakini alieleza ya kwamba kwa njia ya kubatizwa alijionyesha kuwa mmoja na baki lenye kutubu katika Israeli. Ulikuwa kama mfano kuonyesha ya kwamba atatimiza haki yote kwa njia ya kubatizwa katika mauti kwa Kalvari na kwa njia ya kufufuliwa tena.

Kujaribiwa kwa Yesu (4:1-11)

Majaribu ya Yesu toka Shetani yalionyesha ya kwamba yeze ni mkamilifu kabisa na alistahili kwa kila njia kuwa Mfalme. Majaribu matatu ndiyo haya: (1) kuishi kwa mkate tu, (2) kujaribu Mungu kwa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

njia ya kufanya tendo la kushangaza, na (3) kupokea falme za dunia toka mkono wa Shetani. Maneno haya yanafuatana na majaribu ya Shetani kwa Hawa — mti ulikuwa mzuri kwa chakula, ulipendeza macho, na ulikuwa mti wa kutamaaniwa (Mwa. 3:6). Yanafuatana vilevile na maneno Yoane aliyosema juu ya dunia, kama tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima (1 Yn. 2:16). Yesu alishinda majaribu haya matatu yote kwa njia ya kutaja mashairi toka Torati. Kisha Shetani alimwacha.

Mwanzo wa utumishi wa Yesu (4:12-25)

Sasa Bwana alianza kazi yake kubwa kwa Galilaya. Alihama toka Nazareti kukaa katika Kapernaumu; akahubiri ya kwamba ufalme wa Mungu ulikuwa umefika (kwani Mfalme alikuwa amekuja); akaita Petro, Anderea, Yakobo, na Yoane kuwa wanafunzi; akaponyesha watu wengi pahali mbalimbali katika Galilaya. Matayo anasema ya kwamba maneno haya yalitimiza unabii wa Isaya juu ya kutokea kwa nuru kwa watu wa Galilaya (Isa. 9:1,2; 42:6,7).

4. SHERIA ZA UFALME (Sura 5-7)

Sifa za heri na misano (5:1-16)

Hotuba Mlimani (sura 5-7) ni sheria za ufalme. Sifa za heri (mash. 1-12) ni ufananusi wa wenyeji wazuri. Wanasawanishwa na chumvi na nuru (mash. 13-16). Halafu toka shairi 17 kufika 6:34 tunaona haki kubwa zaidi ya ufalme.

Kristo na sheria (5:17-19)

Kwanza Kristo alisema na nguvu ya kwamba hakufika kuharibu torati lakini kuitimiza. Ailiitimiza kabisa, si kwa njia ya kuitii kwa maneno yote wakati alipokuwa hapa duniani tu, lakini zaidi ya ile aliitimiza kwa njia ya kulipa azabu yetu nzima wakati alipokufa msalabani.

Haki ya kweli (5:20)

Alisema na nguvu ya kwamba ni lazima kwa wanafunzi wake kuwa na mwenendo wa haki kupita ule wa waandishi na Wafarisayo. Haki ya watu wale ilikuwa haki ya kuonekana tu, usafi kwa desturi za dini, lakini haikugeuza roho zao.

Kupatana mbele ya kuabudu (5:21-26)

Sheria iliagiza, “Usiue,” lakini Yesu alisema ya kwamba haifai hata kukasirikia ndugu yako (mash.21-22). *Uuaji unaanza na kasi-rani*. Kwa sababu hii inapasa waamini kupatana tena mbio nyuma ya kugombana, magomvi haya yasigeuke mashitaki makubwa. Mungu

MATAYO

anapokea kuabudu kwa watu wale tu wanaokwisha kupatana na ndugu zao (mash. 23-26).

Mwanzo wa tamaa (5:27-30)

Sheria ilisema, “Usizini,” lakini Yesu alisema, “Usiangalie mwanamke na tamaa” (mash. 27-28). Kuangalia na tamaa ndio mwanzo wa uzini. Hivi ni lazima kwa waamini kutawala macho yao, ndiyo maneno wanayotazama, na mikono yao, ndiyo maneno wanayofanya (mash. 29-30).

Yesu na kuachana (5:31-32)

Sheria ilisema mwanamume akitaka kuacha mke wake, alihitaji kumpa barua ya kuachana tu, lakini Yesu alisema kwamba kuna sababu moja tu kwa kuachana, ndiyo uasherati wa mume au mke. Kuondosha mke kwa sababu yo yote nyingine ni kumsukuma kutenda uzini, na kuoa mwanamke aliyeondoshwa ni uzini vilevile.

Yesu anakataza watu kuapa (5:33-37)

Sheria ilifundisha ya kwamba ukitoa kiapo, ni lazima kwako kutimiza kiapo hiki, lakini Yesu alikataza watu kuapa. Ingepasa masemo yetu kuwa masemo ya haki kila mara hata kiapo hakihitajiji kuya-hakikisha. Watu wengine wanafikili mashairi haya ni juu ya viapo juu ya maneno tutakayofanya wakati wa kuja, si juu ya viapo kuhakikisha kweli ya ushuhuda mbele ya serikali (kama juu ya maneno tulioona).

Shavu la pili na kilometre ya pili (5:38-42)

Sheria ilisema, “Rudisha mabaya kwa mabaya uliyotendewa,” lakin Yesu alisema, “Lipa maovu na mema. Geuza shavu la pili, maana yake mtu akikulazimisha kubeba mizigo yake kwa kilometre moja, ukae tayari kuibeba kwa kilometre ya pili vilevile na roho nzuri. Lipa kila tendo linalokosa adabu na tendo la mapendo.”

Mwenendo wa mapendo (5:43-48)

Sheria ilisema, “Upende jirani yako, na, Uchukie adui yako,” lakin Yesu alisema, “Pendeni adui zenu.” Kwa njia hii utaonyesha ya kwamba wewe ni mtoto wa Mungu kwani yeye ni mwema kwa watu wote.

Wema bila matangazo (6:1-4)

Haki ya ufalme inakataa unafiki kwa maneno ya dini, na kutenda matendo mema kwa kuonekana mbele ya watu (sh.1). Ni sharti kutoa sadaka kwa siri, si kwa kuonekana mbele ya watu.

Mfano mzuri wa maombi (6:5-15)

Haifai watu kuomba na kusudi ya kuonekana kama watu watawa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kabisa, wala haifai waombe maombi marefu wakisema maneno fulani tena na tena (mash. 5-8). Ni vizuri kuanza maombi na kuabudu, kisha kuomba juu ya mapenzi ya Mungu na ufalme wake kwanza mbele ya kuomba juu ya maneno yetu wenyewe. Inatupasa kuomba kupewa mahitaji yetu ya kila siku, tuweze kusamehewa kama tunavyosamehe wengine, na kuponyeshwa toka majaribu (mash. 9-13). Kama tukikataa kusamehe watu wengine, tusizanie Mungu Baba yetu atatusamehe sisi (mash. 14-15).

Kufunga chakula bila kuonekana (6:16-18)

Tusitangaze kwa watu wengine ya kwamba tunafunga chakula; vizuri Mungu tu ajue neno hili.

Hazina mbinguni (6:19-24)

Mungu anakataza wenyiji wa mbinguni (ndio watu wake) kushinda na kazi ya kujivimbisia mali duniani kwa wakati wa kuja, kwani hawawezi kujua nini itatokea, na itawashinda kuweka roho juu ya kazi ya Mungu na maneno yao wenyewe vilevile.

Utunzi wa Bwana (6:25-34)

Haifai wasumbuke juu ya kuwa na vyakula na mavazi. Mungu anapatia ndege vyakula na anapamba maua vizuri sana; basi atatunza vilevile wale ambao wanamweka yeye na kazi yake kwanza. Hivi Bwana anafanya agano na watu wake: kama wataweka ufalme wake na haki yake kwanza, yeye atawalinda na kuwapa vyote wanavyohitaji kwa wakati wa kuja. Halafu bila kuhitaji kusumbuka juu ya mahitaji yao kwa wakati wa kuja wanaweza kujitoa kumtumikia yeye na roho moja.

Musihukumu (7:1-5)

Roho ya kuhukumu na kulaumu bule haifai ndani ya ufalme. Hatuna ruhusa kuhukumu wengine juu ya makosa yao kama sisi tunakosa kwa njia hizi hata kupita.

Lulu mbele ya nguruwe (7:6)

Hatuamrishwi kushiriki kweli za ufalme na watu wanaozidi matukano na jeuri.

Kudumu katika maombi (7:7-11)

Inatupasa kudumu ndani ya maombi tukiamini na kujua kabisa ya kwamba Mungu anakusudi kufanya maneno yale tu yatakayokuwa baraka kwetu.

Namna gani kutendea wengine (7:12)

Tunaagizwa kutendea wengine namna tunetaka wao watutendee sisi.

MATAYO

Njia mbili (7:13-14)

Mlango kwa wafuata wa Kristo ni mwembamba na njia ambayo inawapasa kutembea ndani yake ni nguvu, lakini inawafikisha kwa maisha ya baraka zaidi. Maisha ya wale ambao hawajitawali wenyewe na wanaofuata njia ile pana hayana faida kwa Bwana. Unaweza kutumia mashairi haya kuhubiri Habari Njema vilevile.

Namna gani kutambua nabii wa haki (7:15-20)

Tunaweza kufahamu kama mtu ni nabii wa kweli au wa uwongo kwa njia ya mwenendo wake. Nabii wa kweli atakuwa na maisha matakatifu.

Wenye kukiri Kristo bila imani ya kweli (7:21-23)

Wanafunzi wa kweli wanafanya mapenzi ya Mungu. Mara nyingine wale wanaokiri Kristo lakini wasio wanafunzi wa kweli wanatumia masemo ya dini, hata kutenda kazi za dini, lakini mwishoni udanganyifu wao utaonekana wazi.

Wajengaji namna mbili (7:24-27)

Mwenye akili hasikii tu maneno ya Yesu lakini anayatii vilevile. Anajenga maisha yake juu ya msingi wa nguvu. Mpumbavu anachagua njia yake mwenyewe, kisha hana kitu kumsaidia na kumtegemeza kwa wakati wa taabu.

Makutano wanashangaa (7:28-29)

Wakati Yesu alipomaliza mafundisho haya ya ajabu, makutano walishangaa sana juu ya namna alivyosema na amri. Kabisa!

5. MAAJABU YA UWEZO NA NEEMA YA MASIYA, NA MAWAZO MBALIMBALI YA WATU JUU YAO (8:1 – 9:35)

Maajabu ya kuponyesha ya Masiya (8:1-17)

Toka 8:1 kufika 9:35 tunapata habari za mengine ya maajabu ya uwezo na neema Masiya aliyoleta, na mawazo mbalimbali ya watu juu yao. Kwanza, Yesu aliponyesha mkoma Myuda kwa njia ya kumgusa tu (mash. 1-4). Nyuma yake aliponyesha mtumishi wa akida Mtaifa kwa njia ya kusema neno tu, hata kama ye ye mwenyewe hakuwa pahali mtumishi alipokuwa (mash. 5-13). Halafu aliponyesha mama ya mke wa Petro kwa njia ya kugusa mkono wake (mash. 14-15). Mwishoni aliponyesha watu wengi na kufungua wengine toka utawala wa pepo wachafu (mash. 16-17). Tunaweza kusawanisha maneno haya na namna yanavyofuatana na: (1) utumishi wa Kristo kwa Israeli wakati alipofika mara ya kwanza; (2) utumishi wake kwa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

wakati wa sasa kwa Mataifa; (3) kazi yake kurudisha Waisraeli wanaoamini wakati atakapokuja mara ya pili; na (4) utumishi wake kwa makutano ya watu kwa muda wa miaka elfu moja.

Mapimo kwa wale amba wanajiita wanafunzi (8:18-22)

Watu wawili waliofikili watafuata Yesu walijifunza ya kwamba *labda* itawapasa kuishi bila nyumba, na ya kwamba itakuwa *lazima* kwao kumweka yeche kwanza mbele ya jamaa na rafiki zao.

Bwana wa upopo na bahari (8:23-27)

Upopo na bahari zilitii Yesu. Tufani kubwa lililokuwa baharini mwa Galilaya lilitulia kwa agizo la Bwana.

Pepo wachafu wenyewe kutii na nguruwe (8:28-34)

Pepo wachafu walimtii. Waliondokea watu wawili wakati Bwana alipowaagiza kufanya hivi, kisha wakaingia ndani ya nguruwe 2,000 walokimbia mara moja na kuingia baharini.

Tufani na bahari zinamtii. Pepo wachafu wanamtii. Watu tu wanamwasi!

Mgonjwa wa kupooza anaponyeshwa (9:1-8)

Waandishi walikasirika kabisa wakati Mwokozi alipomwambia mwenye kupooza ya kwamba zambi zake zilisamehewa, kwani hawakuamini ya kwamba aliweza kusamehe zambi. Hivi Bwana akita-ka waweze kuona uwezo wake na macho, aliponyesha mwili wa mwenye kupooza. Hatujui kama waandishi walishangaa, lakini makutano walishangaa sana.

Ushuhuda wa mwandishi mwenyewe (9:9-13)

Mwandishi wa Habari Njema hii anatupasha sasa habari za kuokolewa kwake mwenyewe na za karamu aliyofanya ili rafiki zake waweze kukutana na Yesu vilevile. Wakati Wafarisayo waliponungu-nika kwa sababu Yesu alikuwa na urafiki na wenyewe zambi namna hii, aliaambia ya kwamba alikuja kuita wenyewe zambi, si watu wa dini wenyewe kiburi, kutubu.

Jibu kwa ulizo juu ya kufunga (9:14-17)

Halafu Bwana alijibu maulizo ya wengine wa wanafunzi wa Yoane. Kwanza, wanafunzi wa Yesu hawakufunga chakula kwa sababu Bwana alikuwa pamoja nao; watafunga wakati atakapowaondokea. Vilevile, haiwezekani kuchanganya sheria na neema, maana viriba vya zamani vya dini ya Wayuda na mvinyo mpya ya dini ya kikristo.

Maajabu matatu mwengine ya kuponyesha (9:18-35)

Maajabu haya matatu ni mfano wa namna matukio yanavyofuatana

MATAYO

wakati mwenye zambi anapookolewa. 1) Habari za binti ya mtawala ni mfano wa mfu katika zambi akipata uzima (9:18-19, 23-26). 2) Vipofu wawili wale waliotambua Yesu kama Masiya na kupata kuona ni mfano wa macho ya roho ya mwenye zambi yakipata kuona (mash. 27-31). 3) Kama bubu alivyowezeshwa kusema, vivyo hivi ulimi wa mwamini wa sasa anafunguliwa aweze kushuhudia Yesu (mash. 32-34). Hatushangai juu ya kasirani ya adui za Kristo wakati walipoona maajabu haya.

Saa Yesu alipokuwa akikwenda kusaidia binti ya mtawala, mwanamke mmoja alipita kwa shida katikati ya watu kufika karibu na Bwana, akagusa vazi lake na kuponyeshwa (mash. 20-22).

6. MITUME WA MASIYA-MFALME WANATUMWA KUHUBIRI KWA ISRAELI (9:36 – 10:42)

Huruma kwa wapotevu (9:36-38)

Wakati Mwokozi alipoona makutano kama kondoo bila mchungaji, aliagiza wanafunzi wake kuomba Bwana kutuma watenda kazi kwa mavuno.

Yesu anatuma wanafunzi kumi na wawili (10:1-15)

Sura hii inaendelea na habari tulizosoma kwa mwisho wa sura 9. Mara nyingi Mungu anaita watu wale wanaoomba Bwana kutuma watenda kazi. Sharti Wakristo wanaoomba Bwana kutuma watendaji kazi wakae tayari kwenda *wao wenyewe!* Halafu Masiya-Mfalme aliita mitume kumi na wawili (mash. 1-4) na kuwatuma kwa kondoo wapotevu za nyumba ya Israeli (mash. 5-6). Iliwapasa kutangaza kufika kwa ufalme wa mbinguni kwa njia ya Mfalme mwenyewe, kuhakikisha habari zao na alama za ajabu, na kushiriki Habari Njema na watu pasipo bei (mash. 7-8). Iliwapasa kuamini kwamba Bwana atawapatia vitu walivyohitaji na kukaa na asante pamoja na watu ambaeo waliwakaribisha nyumbani mwao. Wale waliokataa kuwapokea na waliokataa mahubiri yao watapata taabu siku ya hukumu (mash. 9-15).

Maonyo juu ya mateso (10:16-39)

Bwana aliwaambia wafuata wake ya kwamba watu watawatesa na kuwachukia, na nini itawapasa kufanya saa yenyewe (mash. 16-23). Wasifikili watu watawatendea vizuri kupita Bwana wao. Wakae kuogopa Mungu kupita watu, wakumbuke ya kwamba Baba yao anawalinda na kuwapenda sana, na washuhudie Kristo na uhodari mbele ya watu (mash. 24-33).

Aliwafundisha maneno magumu juu ya kuwa wanafunzi wake.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Watu wengine wa nyumba ya mtu watapokea mahubiri ya Habari Njema na wengine watayakataa, hivi mara nyine inapasa Mkristo kuchagua kama atafungana na watu wa jamaa yake au kufuata Kristo. Ingepasa wanafunzi wake kujitoa mzima kwake na kukaa tayari kulipa hata bei kubwa zaidi, ndiyo mauti. Sharti mapendo yetu kwa Kristo yawe makubwa kupita hamu yetu kujiponyesha wenyewe (mash. 34-39).

Juu ya wajumbe wa Kristo (10:40-42)

Inapasa wafuata wa Yesu kukumbuka ya kwamba wao ni wajumbe *wa Kristo mwenyewe*. Watu ambaa waliwapokea walipokea Kristo mwenyewe na watapokea zawabu kwa mema ambayo waliwatendea.

7. MATATA YANAANZA (Sura 11)

Yesu anapatisha roho ya Yoane Mbatizaji nguvu (11:1-6)

Matata yanaanza sasa. Yoane Mbatizaji alikuwa amefungwa gerezani, na alianza kuwa na shaka kama Yesu alikuwa Masiya kweli. Bwana alituma wajumbe kumkumbusha ya kwamba alikuwa akitimiza unabii juu ya maajabu ambayo Masiya atayafanya.

Yesu anasifu Yoane Mbatizaji (11:7-15)

Halafu Yesu alisifu Yoane akisema ye ye ni mkubwa kupita nabii, ya kwamba alikuwa mwenye kumtangulia na kwa sababu hii alikuwa na mahali kubwa kupita mtu ye yote mwengine. Kama watu wanganlipokea Yoane Mbatizaji, kama angalitimiza kazi iliyotabiriwa juu ya Elia.

Kukataa na kupokea (11:16-30)

Bwana alisema ya kwamba haikuwezekana kupendeza kizazi kile au taifa la Israeli (mash. 16-19), na alilaumu miji mitatu ya Galilaya kwa sababu ya kutoamini (mash. 20-24). Mwokozi alikuwa akikataliwa na watu lakini alifarijiwa wakati alipokumbuka makusudi ya Mungu Baba aliye juu ya yote (mash. 25-27), kisha aliita wenye kuchoka na kubeba mizigo mizito kuja kwake kupata raha kwa roho na damiri zao (mash. 28-30).

8. MASIYA-MFALME ANAKATALIWA NA VIONGOZI VYA WAYUDA (Sura 12)

Mabishano juu ya kazi za lazima siku ya sabato (12:1-9)

Wafarisayo walikasirika wakati walipoona wanafunzi wa Yesu wakivunja masuke ya ngano siku ya sabato. Yesu aliwaonyesha toka Agano la Kale ya kwamba Sheria ya Musa haikukataaza watu kufanya

MATAYO

kazi za lazima au za rehema siku ya sabato. Aliwaambia ya kuwa kuonyesha rehema ni neno kubwa kupita kushika desturi za dini na ya kwamba yeze mwenyewe ni Bwana wa Sabato.

Mabishano juu ya kuponyesha siku ya sabato (12:10-13)

Halafu Wafarisayo walichambua Yesu juu ya kuponyesha mtu mwenye mkono wa kukauka siku ya sabato. Bwana aliwakumbusha ya kwamba wao wenyewe wangeondosha shimoni siku ya sabato kondoo aliyanguka ndani yake.

Shauri lililofanywa siku ya sabato kuharibu Yesu (12:14-21)

Yesu angaliweza kuwakumbusha vilevile ya kwamba walikuwa wakifanya shauri siku ya sabato kumwua (sh.14)! Lakini hakufanya hivi. Aliendelea tu na kazi yake ya kuponyesha, akitimiza unabii katika Isaya 41:9 na 42:1-4 — Mtumishi mpole anayeleta hukumu mpaka kushinda bila kutumia nguvu au mshindo wa matarumbeta (mash. 15-21).

Kutukana Roho Mtakatifu (12:22-30)

Wakati Yesu alipoponyesha mwenye pepo mchafu, kipofu na bubu, makutano walianza kufikili ya kwamba labda yeze ni Masiya, lakini Wafarisayo walimshitaki kusema alifanya maajabu yake kwa uwezo wa Belzebuli, mkubwa wa pepo wachafu. Kabisa kabisa alifanya maajabu haya kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, hivi Wafarisayo walikuwa wakitukana Roho Mtakatifu kwa njia ya kumwita Shetani. Kwanza Bwana alionyesha upumbavu wa mashitaki yao kwani ni kusema Shetani alikuwa akishindana na yeze mwenyewe. Kisha alionyesha kwamba kwa sababu alitoa pepo wachafu kwa Roho ya Mungu, ufalme wa Mungu ulikuwa umefikia inchi ya Shetani, kumfunga yeze na kuteka vitu vyake.

Zambi isiyoweza kusamehewa (12:31-37)

Sasa Yesu alitangaza ya kwamba Wafarisayo walikuwa wametenda zambi isiyoweza kusamehewa wakati waliposema neno baya juu ya Roho Mtakatifu. Masemo yao yalionyesha nini ilikuwa miyoni mwao. Kuanza saa ile Kristo alitendea Waisraeli namna nyininge. Kukataliwa kwa Kristo na viongozi vyta dini sasa kulikuwa kama unabii ya kwamba atakataliwa na taifa zima vilevile, ndilo neno lililoteka kweli.

Wafarisayo wanataka kuona alama (12:38-42)

Hata kama Kristo alikuwa amefanya maajabu mengi, wengine wa waandishi na Wafarisayo hawakuwa na haya kuomba kuona alama

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kwake! Aliwajibu ya kwamba watapewa alama moja tu, ndio ufufuko wake toka wafu. Wenyeji wa Ninawe, watu wa Mataifa, walikuwa wametubu wakati Yona alipowafikia. Malkia toka kusini, Mtaifa, alifanya safari ndefu kuona Solomon. Lakini Mwana wa Mungu alikaa katikati yao nao walimkataa. Ona ya kwamba Bwana hapendezwi na namna ya imani inayotaka kuona alama.

Mwenye pepo mchafu aliyetengeneza maneno yake (12:43-45)

Habari za Bwana za mwenye pepo mchafu aliye kwisha kusafishwa zilikuwa na maana kubwa kwa wasikiaji wake Wayuda. Pepo mchafu ni mfano wa kuabudu sanamu. Mtu mwenyewe ni mfano wa Israeli. Nyumba iliyo fagiwa na kukaa tupu inasema juu ya Israeli waliokwisha kuacha kuabudu sanamu. Pepo wachafu saba wengine ni mfano wa ibada ya sanamu mbaya kupita yote.

Nyumba ya Israeli waliacha kuabudu sanamu wakati wa uhamisho wao katika Babeli. Nyumba ilikuwa safi na tupu. Lakini kwa wakati wa kuja watashindwa na ibada ya sanamu mbaya zaidi, ndiyo ibada ya Mpanga Kristo, kwa sababu hawakuruhusu Bwana Yesu kuingia.

Ndugu za kweli za Yesu (12:46-50)

Wakati mama na ndugu za Bwana walipofika kusemezana naye, alionyesha wanafunzi wake, akasema *wao* ndio “mama na ndugu” zake. Au kusema alifundisha ya kwamba undugu kwa maneno ya roho ni neno kubwa kubwa kupita undugu wa watu wa dunia. Neno hili ilionyesha tena ya kwamba alikwisha kujitenga na Israeli.

9. MFALME ANATANGAZA NAMNA MPYA YA UFALME ITAKAYOENDELEA KWA WAKATI KWA SABABU WAISAELEI WALIMKATAA (13:1-52)

Yesu anafundisha kando ya bahari (13:1-2)

Ndani ya sura 12 Israeli walikuwa wamekataa Mfalme na ufalme, hivi sasa ufalme utakuwa namna nyingine kwa muda toka kukataliwa kwa Kristo kufika wakati wa kuja kwake mara ya pili. Kwa njia ya mifano juu ya siri za ufalme wa mbinguni Bwana alijulisha wanafunzi nini itatokea wakati asipokuwa duniani.

Mfano wa udongo namna mbalimbali (13:1-9, 18-23)

Mfano wa udongo namna ine unafundisha ya kwamba habari za ufalme zitazaa matunda ndani ya udongo namna moja tu za namna zile ine. Namna tatu nyingine ni mfano wa watu walio waamini kwa kinywa tu bila kuamini kweli kweli. Udongo mzuri tu ni mfano wa waamini wa kweli.

MATAYO

Kwa sababu gani Yesu alisema kwa mifano (13:10-17)

Watu wale waliokuwa tayari kupokea mafundisho yake wangeyafa-hamu, lakini wale waliokusudi miyoni mwao ya kwamba hawataamini watakuwa kama vipofu kwa maneno ya kweli.

Mfano wa ngano na magugu (13:24-30, 36-43)

Mfano wa ngano na magugu unaonyesha vilevile ya kwamba ndani ya ufalme kuna wengine walio waamini wa kweli na wengine ambao wanajiita tu wanafunzi bila imani ya kweli. Yesu ndiye mpandaji mbegu; shamba ni dunia (si Kanisa); mbegu njema ni wana wa ufalme; magugu ni wana wa yule mwovu; na adui ndiye Shetani. Malaika watatenga ngano na magugu wakati Kristo atakapokuja mara ya pili. Wana wa ufalme watafurahi wakati wa utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja; wengine wote wataharibiwa.

Mfano wa mbegu ya haradali (13:31-32)

Mfano wa mbegu ya haradali unaonyesha ya kwamba ufalme utakuwa mdogo wakati wa mwanzo wake lakini utaongezeka sana, na mafundisho mabaya namna namna yataonekana ndani yake. Unaonyesha namna ya ukristo kwa wakati wa sasa lakini *si* Ukristo wa kweli.

Mfano wa chachu (13:33)

Mfano wa chachu ndani ya unga ni mfano wa kuingiza mafundisho ya uwongo ndani ya chakula cha roho cha watu wa Mungu. (Chachu inasema juu ya uovu ndani ya Biblia.) Kama chachu inavyoenea ndani ya unga, vivyo hivyo uovu unaenea ndani ya ufalme.

Mfano inatimiza unabii (13:34-43)

Halafu Matayo anaonyesha ya kwamba Bwana wetu alikuwa akitimiza unabii wa Asafu katika Zaburi 78:2 wakati aliposema kwa njia ya mifano.

Mfano wa hazina iliyofichwa (13:44)

Mfano wa hazina iliyofichwa unaonyesha ya kwamba Kristo aliuza vyote ambavyo alikuwa navyo wakati alipokufa msalabani aweze kununua Israeli.

Mfano wa lulu ya bei kubwa (13:45-46)

Mfano wa lulu ya bei kubwa unatukumbusha ya kwamba Bwana Yesu aliuza vyote ambavyo alikuwa navyo kwa Kalvari kwa kununua Kanisa.

Mfano ya mkila (13:47-50)

Mfano wa saba unaonyesha mkila unaotupwa baharini na kuku-

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

sanya samaki namna namna. Kwa wakati wa mwisho wa muda wa Mateso Makubwa, malaika watatenga wenye haki na waovu. Wenye haki wataingia muda wa utawala wa miaka elfu moja; wazalimu watatupwa ndani ya tanuru ya moto.

Mfano wa mwenye nyumba (13:51-52)

Kwa sababu wanafunzi walisema walifahamu mifano hii, Bwana aliuambia ya kwamba ni lazima kwao kushiriki na watu wengine kweli za zamani toka Agano la Kale na kweli mpya toka mafundisho ya Yesu.

10. MASIYA ANAENDELEA KUTENDA KWA NEEMA, LAKINI UADUI UNAONGEZEKA (13:53 – 18:35)

Yesu anakataliwa kwa Nazareti (13:53-58)

Nyuma ya kumaliza mafundisho yake Yesu akarudia Nazareti, akakuta ya kwamba alikuwa nabii aliyekosa heshima katika inchi yake mwenyewe. Kwa sababu watu wa Nazareti hawakumfurahia walikosa kupata faida kwa njia ya utumishi wake.

Herode aliua Yoane Mbatizaji (14:1-12)

Zamiri ya Herode ilimchokoza wakati aliposikia hahari za utumishi wa Bwana Yesu. Aliogopa ya kwamba Yoane Mbatizaji ambaye alimwua alikuwa amefufuka toka wafu. Mashairi 3-12 yanapasha habari zilizotokea mbele wakati Yoane Mbatizaji alipokufa na namna gani alikuifa. Yoane alikuwa amehamakia Herode juu ya kutenda uzini kwa njia ya kukaa pamoja na mke wa ndugu yake. Mwanamke huyu alingoja kufika wakati Herode alipotoa ahadi kwa binti yake bila kufikili vizuri, kisha alisukuma binti huyu kuomba kupewa kichwa cha Yoane. Basi wanafunzi wa Yoane walizika kiongozi wao, kisha wakakwenda na kupasha habari kwa Yesu Kiongozi wao mkubwa.

Huruma ya Kristo (14:13-36)

Hata kama watu walichukia Bwana kupita na kupita na kumwona kama adui, Bwana aliendelea na utumishi wake wa huruma. Aliponyesha wagonjwa (mash. 13-14), alikulisha wanaume 5,000 pamoja na wanawake na watoto na mikate mitano na samaki wawili (mash. 15-21), alituliza tufani katika Bahari ya Galilaya kusaidia wanafunzi wake walioogopa sana (mash. 22-33), na kupatia wanganga katika Genesareti pumziko kwa njia ya kuponyesha wagonjwa wote (mash. 34-36).

Desturi za watu zinashindana na maagizo ya Mungu (15:1-9)

Waandishi na Wafarisayo walilaumu wanafunzi wa Yesu kusema

MATAYO

walivunja desturi za wazee kwa sababu hawakunawa mikono mbele ya kula. Yesu alijibu kusema Wafarisayo walivunja maagizo ya Mungu kwa njia ya desturi zao. Kwa mfano, walifundisha ya kwamba watu hawahitaji kusaidia wazazi wao wenye mahitaji kwa njia ya kusema tu ya kwamba mali yao ililetwa kwa Mungu.

Uchafu wa kweli unatoka rohoni (15:10-20)

Halafu Yesu alifanya tangazo la kushangaza kabisa, ya kwamba maneno yanayochafua mtu si maneno yanayoingia kinywani lakini yale yanayotoka kwa moyo. Alisema vilevile ya kwamba Wafarisayo walichukizwa juu ya masemo yake kwa sababu walikuwa wapofu kwa roho na kukosa uzima.

Imbwu chini ya meza (15:21-28)

Katika giza la kutoamini kwa Israeli, imani ya mwanamke Mkanana ilingaa kabisa. Alitaka sana kupata kusaidia kwa binti yake, hivi wakati ilipoonekana ya kwamba Bwana alikataa kumsaidia, alisema ye ye ni kama imbwu mdogo wa mataifa tu asiyestahili. Bwana alimsifu kwa imani yake, akaponyesha binti yake.

Yesu anaponyesha makutano makubwa (15:29-31)

Tunafikili ya kwamba watu ambao Yesu aliwaponyesha katika Galilaya walikuwa Mataifa waliokaa ndani ya inchi ya Dekapoli. Tunasoma ya kwamba “wakatkuza Mungu wa Israeli.”

Yesu anakulisha watu kuliko 4,000 (15:32-39)

Wakati Yesu alipokuwa angali kwa upande wa mashariki wa Bahari ya Galilaya, alikulisha wanaume 4,000 pamoja na wanawake na watoto na mikate saba na samaki wachache, na vyakula vilibaki nya kutosha kujaza vitunga saba.

Habari za sura hii ni mfano wa maneno yaliyokuwa yakitonea na yale yatakayoteka. Mabishano na magomvi ya Wafarisayo yanatazama mbele kwa wakati Israeli walipokataa Masiya. Imani ya mwanamke Mkanana ni mfano wa Habari Njema ikihubiriwa kwa Mataifa kwa wakati wa sasa. Kuponyeshwa kwa makutano makubwa na kukulishwa kwa watu 4,000 kunatazamia utawala wa miaka elfu moja kwa wakati wa kuja saa watu wote duniani watakapobarikiwa na afya njema na usitawi.

Alama toka mbinguni (16:1-4)

Wafarisayo na Wasadukayo walionyesha tena kutoamini kwao kwa njia ya kuomba Bwana awaonyeshe alama toka mbingu. Bwana aliwahamakia kwa sababu waliweza kutambua uso wa mbingu lakini si

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

alama za nyakati, maana yake za kuja kwa Masiya na masemo na kazi zake zote za ajabu. Watapewa alama moja tu, ndiyo alama ya ufufuko wake, nayo itakuwa alama ya hukumu yao.

Chachu ya Wafarisayo na mikate ya Yesu (16:5-12)

Wakati wanafunzi walipofika karibu na Bwana tena kwa upande wa mashariki wa bahari, walikuwa wamesahau kuleta vyakula pamoja nao. Hivi, wakati Yesu alipowaonya kukaa na ange kwa chachu ya Wafarisayo na Wasadukayo, walifikili alikuwa akisema juu ya *milate wa kula kwa kinywa*, lakini Bwana alikuwa akisema juu ya *mafundisho mabaya*. Wao wote walikaa kusumbuka kwa sababu ya ukosefu wa chakula hata kama yule aliyekulisha watu 5,000 na 4,000 mbele alikuwa pamoja nao! Hivi aliwakumbusha tena maajabu yale mawili ya kulisha watu. Alikulisha watu 5,000 na mikate 5 na samaki wawili, na vyakula vya kutosha kujaza vitunga 12 vilibaki. Alikulisha watu 4,000 na mikate 7 na samaki wachache, lakini vitunga saba tu vya vyakula vilibaki. Au kusema aliweza kufanya kazi kubwa zaidi na vitu nusu zaidi; maana alikulisha watu wengi kupita, na vyakula vingi zaidi vilibaki!

Kukiri kwa Petro (16:13-20)

Kwa Kaisaria Filipi Yesu alifundisha wanafunzi neno lililo kubwa kupita yote mengine. Sharti wafahamu kabisa kama yeze ni nani. Kama angalikuwa **mtu** mkubwa tu, halafu labda kazi yake haitatimia na isingalikuwa akili nzuri kwao kumfuata. Wakati Petro alipokiri ya kwamba yeze ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, Bwana alitabiri Kanisa lake litajengwa juu ya kweli hii kubwa na milango ya Hadeze haitalishinda, na ya kwamba Petro atafungua mlango wa ufalme (kama alivyo fanya kwa Pentekote na mara nyingine vilevile).

Yesu anatabiri mauti na ufufuko wake (16:21-27)

Sasa wanafunzi walikuwa tayari kusikia habari mbaya zaidi – ya kwamba Kristo atateswa na kuuawa – na habari nzuri zaidi – ya kwamba atafufuliwa tena siku ya tatu. Petro hakukubali ya kwamba Bwana atateswa na kufa, na hakufahamu ya kwamba Bwana alikuwa akimwita yeze na wanafunzi wengine kumfuata na kukataliwa na watu, kuteswa, na hata mauti. Lakini Yesu alieleza ya kwamba utukufu wa ufalme wake duniani utafuata kufa.

Wanafunzi watatu wapendelewa (16:28)

Watatu wa wanafunzi, Petro, Yakobo, na Yoane wataishi kuona Mwana wa Mungu akikuja katika ufalme ule wa utukufu, kama tutakavyoona ndani ya sura inayofuata.

MATAYO

Kugeuzwa sura kwa Kristo (17:1-8)

Maneno yaliyotokea juu ya mlima huu yalionyesha mbele kuja kwa Kristo duniani. Wakati Petro alipoandika juu ya habari hizi nyuma, alisema, “Hatukufuata hadizi zilizotengenezwa kwa hila, wakati tulipowajulisha ninyi uwezo na kuja kwa Bwana wetu ... wakati tulipokuwa pamoja naye katika mlima mtakatifu” (2 Pet. 1:16a, 18b). Bwana alitokea juu ya mlima na utukufu usiofichwa, namna atakavyoonekana kwa wakati wa utawala wake duniani kwa miaka elfu moja. Musa, Elia, Petro, Yakobo, na Yoane walikuwa mifano ya vyeo mbalimbali ndani ya ufalme, wengine wakifika kwa njia ya mauti, wengine kwa njia ya kuhamishwa, na wengine wangali hai kwa wakati mwenyewe. Utukufu wote utakuwa wa Bwana wakati ule, atatukuzwa juu sana kupita Musa na Elia. Atakuwa na pahali pa kwanza.

Ulizo juu ya Elia (17:9-13)

Wanafunzi walifazaika namna gani iliwezekana kwao kuona ufalme mbele hata kama Elia hakuja kwanza, namna Malaki alivyotabiri. Yesu alieleza ya kwamba Elia *alikuwa amekuja* kweli, ya kwamba watu walimwua, na ya kwamba wataua Mwana wa Mungu vilevile. Halafu wanafunzi walifahamu ya kwamba Yoane Mbatizaji alikuwa ametimiza kazi ya Elia.

Hitaji kwa kuomba na kufunga (17:14-21)

Nyuma ya maneno makubwa wanafunzi waliyoona juu ya mlima iliwapasa kushuka bondeni tena katikati ya watu wenye uhitaji. Wanafunzi walikuwa wamejaribu kuponyesha mtu mwenye kifafa lakini walishindwa. Sasa Yesu alimponyesha. Alieleza kwa wanafunzi wake ya kwamba imani yao haikutosha.

Yesu anatabiri tena juu ya kufa na ufufuko wake (17:22-23)

Mwokozi alitabiri tena ya kwamba atatolewa kwa mikono ya adui, atakufa na kufufuka. Wanafunzi walihuzunishwa, labda kwa sababu hawakufahamu vizuri ahadi yake ya kwamba atafufuka.

Yesu na Petro wanalipa kodi (17:24-27)

Petro alianguka wakati alipowaambia watoza kodi katika Kaperennaumu ya kwamba ilipasa Bwana wake kulipa nusu ya shekeli, ndiyo kodi ya hekalu. Yesu alimpundisha juu ya neno hili kwa njia ya kueleza ya kwamba Mwana wa Mungu hakulipa kodi kusaidia nyumba ya Baba yake mwenyewe. Lakini hakutaka kuwa kikwazo kwa watu, hivi alituma Petro kwa Bahari ya Galilaya kutupa ndoana kukamata samaki aliyekuwa na kipande cha mali kinywani mwake na ku-

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

lipa kodi ya hekalu. Mali yenyewe ilitosha sawa kwa Yesu na Petro pamoja.

Unyenyekevu (18:1-4)

Watu wanaita Matayo 18 hotuba juu ya ukubwa na usamehe. Sura hii inaonyesha matendo yanayofaa kwa watu wale wanaotawaliwa na Kristo Mfalme. Wakati Mwokozi alipotazamia mateso na kufa kwake, wanafunzi wake waliwaza juu ya kuwa na ukubwa ndani ya ufalme. Bwana aliwakumbusha ya kwamba ni lazima kwao kuzaliwa tena na kugeuka kama watoto wadogo waweze kuingia ufalme.

Madaraka kwa watoto wadogo (18:5-6)

Hapa Bwana Yesu anafikili juu ya watoto wa roho, ndio wanafunzi wake. Mtu ye yote anayepokea wanafunzi wake anampokea yeye, lakini ye yote ambaye anawakosesha, atapokea hukumu kubwa kupita kuzamishwa ndani ya bahari inayokwenda chini sana.

Kujitawala mwenyewe (18:7-9)

Sharti watu wafanye hata kitu cha nguvu zaidi kujizuiza wasiwe kikwazo kwa watu wengine.

Damani kubwa ya uzima (18:10-14)

Haifai kuzarau hata mwamini mdogo zaidi, kwa sababu malaika wanamsimamia mbele ya Mungu, na Mchungaji mwenye mapendo alimwokoa na anamlinda zaidi. Bwana hataki hata kondoo mpotevu mmoja kupotea.

Namna gani kutendea watenda mabaya (18:15-20)

Inapasa ndugu aliyekosewa na Mkristo mwingine ajaribu kute-geneza neno hili yeye mwenyewe pamoja na mwenye kumkosea. Kama neno hili haliwezekani, vizuri afike pamoja na mtu mmoja au watu wawili karibu na mwenye kumkosea. Kama mtu huyu akikataa kutubu, lazima neno lenyewe lihukumiwe na kanisa. Kama akikataa kunyenyeka maonyo ya kanisa, inapasa waamini kukataa kuwa na ushirika naye.

Usamehe bila kipimo (18:21-35)

Bwana alijibu ulizo la Petro na kusema inatupasa kusamehe ndugu ambaye anatukosea kila mara anapotubu. Halafu aliwapasha mfano juu ya mtumishi aliyekuwa na deni kubwa karibu na mfalme ambayo hakuweza kulipa. Kwa pahali pa kumwuza yeye na jamaa yake kuwa watumwa, mfalme alimhurumia na kumsamehe deni yenyewe. Lakini mtumishi huyu alikuwa na rafiki ambaye alikuwa na deni karibu naye ya mali nusu. Alikataa kusamehe rafiki huyu, lakini alimwumiza na kumtupa gerezani.

MATAYO

Mfalme alikasirika sana wakati aliposikia neno hili hata aliagiza mtumishi afungwe gerezani kufika wakati atakapomaliza kulipa deni yake, maana hata mwisho wa maisha yake.

Mafundisho ya mfano huu ni wazi. Mungu ametusamehe deni kubwa sana na ingetupasa sisi kuwa tayari kusamehe ndugu zetu deni zao ndogo.

11. MFALME ANAKWENDA YERUSALEMA (SURA 19-20)

Kazi ya kuponyesha ya Yesu ngambo ya Yorodani (19:1-2)

Nyuma ya kumaliza utumishi wake katika Galilaya, Bwana Yesu alikwenda Perea kwa upande wa mashariki wa Yorodani. Habari za utumishi wake pale ni ndani ya 19:1 kufika 20:16.

Mafundisho ya Yesu juu ya kuachana na kuoa tena (19:3-9)

Wafarisayo walijaribu kunasa Bwana na ulizo juu ya kuachana wakizani ya kwamba hata akijibu kwa njia gani, jibu lake litamtenga na watu wengi. Yesu aliwakumbusha ya kwamba mapatano ya ndoa inakomboa sheria ya wazazi, ya kwamba watu wawili wanageuka mmoja wakati wanapooa. Alisema ya kwamba wakati wa Agano la Kale watu walikuwa na ruhusa kuachana, lakini desturi ya kuachana halikuwa neno lililokuwa kusudi la Mungu kabisa, na ya kwamba kuanza sasa walikuwa na sababu moja tu kwa kuachana, ndio uzini wa mume au mke.

Mafundisho ya Yesu juu ya kukaa bila kuoa (19:10-12)

Nyuma ya kusikia maneno haya wanafunzi walisema ingekuwa vizuri kukaa bila kuoa, lakini Yesu alisema ya kwamba kukaa bila kuoa ni kwa watu wale tu wanaolazimishwa kukaa hivi kwa sababu ya kuzaliwa hivi au kwa sababu ya kupasuliwa na daktari, au kwa wale wanaochagua kukaa hivi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni.

Yesu anapenda watoto wadogo (19:13-15)

Hata kama wanafunzi walinungunika, Yesu aliweka saa kubariki watoto wadogo na kuwakaribisha kama wenyeji wa mbinguni.

Kijana mwenye mali nyngi (19:16-26)

Kijana mwenye mali nyngi aliuliza Bwana nini ilimpasa kufanya kupata uzima wa milele. Kwanza Yesu alimjaribu kuona kama atamkiri kuwa Mungu, lakini kijana hakufanya hivi. Halafu Bwana alitumia sheria ya Musa kujaribu kufahamisha mtu yule ya kwamba yeze ni mwenye zambi. Kama kweli angalipenda jirani yake kama yeze mwenyewe, kama angalikuwa tayari kuuza vitu vyake vyote na

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kuwapa masikini, lakini kijana alikwenda zake na huzuni kwa sababu alikuwa na mali nyingi. Halafu Bwana alisema na wanafunzi wake ya kwamba haiwezekani kwa mtajiri kuokolewa. Wayuda walifikili ya kuwa mali nyingi ni alama ya baraka ya Mungu, hivi wanafunzi wali-fazaika *nani* ataweba kuokolewa. Inawezekana kwa njia ya ajabu ya uwezo wa Mungu tu.

Zawabu katika usalme (19:27-30)

Petro alijisifu kusema wanafunzi hawakuwa kama yule kijana mwenye mali lakini walikuwa wameacha yote kufuata Kristo, aauliza kama zawabu yao itakuwa nini. Bwana aliahidi kuwapa kazi ya hesima kwa wakati wa utawala wake wa miaka elfu pamoja na zawabu kubwa kwa wakati wa maisha yao duniani na kwa milele. Lakini alionya Petro vilevile ya kwamba haifai awe na roho ya kupigania bei, kwa sababu wengi waliokuwa *kwanza* katika usalme kwa njia ya saa watakuwa *wa mwisho* kwa maneno ya kupokea zawabu.

Neema ni namna nyingine na haki (20:1-16)

Mfano wa watenda kazi katika shamba la mizabibu ni maonyo ya Kristo ya kwamba haifai kuwa na roho ya kupigania bei na Bwana. Asubui mapema watenda kazi wengine walipatana na bwana ya kazi kutumika mchana kutwa kwa dinari moja (mshahara uliokubaliwa kwa watenda kazi shambani kwa wakati ule). Watenda kazi wengine walioingizwa kwa kazi saa tatu ya asubui, saa tisa na saa 11 waliacha maneno ya hesabu ya mshahara wao kwa mikono ya bwana wao. Wakati wao wote walipopokea dinari moja saa kazi yao ilipokwisha mangaribi, wale walikodishwa *kwanza* walinungunika sana. Lakini bwana wao aliwakumbusha ya kwamba walipokea mshahara walipatana juu yake. Kwa sababu ya neema yake kipimo cha mshahara wa watu wote wengine kilikuwa sawasawa na ule wa watu wa *kwanza*. Neema ni vizuri kuliko haki. Wale walikodishwa *kwanza* walipokea mshahara wao nyuma ya wengine wote, na wale walioanza kazi nyuma ya wengine wote walilipwa *kwanza*.

Yesu anatabiri tena juu ya mauti na ufufuko wake tena (20:17-19)

Siku ya mwisho ya safari yao kwenda Yerusalem Yesu aliwamchia wanafunzi tena ya kwamba atatiwa kwa mikono ya adui, kuza-rauliwa, kupigwa, na kusulibishwa. Lakini pamoja na tangazo hili la huzuni lilikuwa tangazo la kushinda kila mara, ndilo ya kwamba nyuma ya kufa kwake atafufuliwa. Habari hizi zitawasaidia kujua ya kwamba Bwana wao atashinda nao watashinda pamoja naye.

Mama mwenye kutakia wana wake heshima (20:20-28)

Mama ya Yakobo na Yoane aliomba Bwana wana wake waweze

MATAYO

kupewa pahali pa heshima katika ufalme. Yesu alieleza ya kwamba Baba hatagawa pahali pale kwa watu wo wote tu, lakini kama zawabu kwa wale walioteswa na hata kufa kwa ajili ya Kristo. Aliongeza kusema ya kwamba ndani ya ufalme wake wale walio wakubwa wa kweli si wale wanaotawala watu wengine lakini wale ambao wanawatumikia.

Yesu anaponyesha vipofu wawili (20:29-34)

Wakati Yesu alipoondokea Yeriko kusudi aende Yerusalem, vipo-fu wawili walimtambua kuwa Masiya, wakalialia nyuma yake wakiomba waweze kupata kuona. Yesu aligusa macho yao, macho yao yalifunguliwa nao walimuata.

12. KUFIKA KWA MASIYA-MFALME KWA YERUSALEMA (Sura 21-23)

Mwingilio wa shangwe (21:1-11)

Kwa upande wa mashariki wa mlima wa Mizeituni, Yesu alituma wanafunzi wawili kwenda Betania kuleta punda pamoja na mwana-punda. Alitumika na nyama hawa wakati alipoingia Yerusalem na shangwe kama mfalme, kwa kutimiza unabii wa Isaya na Zekaria. Makutano walimsalimu na furaha na wengine walifunika njia mbele yake na matawi na mavazi asichokozwe na mavumbi.

Yesu anasafisha hekalu (21:12-16)

Yesu alikwenda mara moja kwa viwanja vya hekalu, akafukuza wabadilisha feza, akiwashitaki juu ya kugeuza nyumba ya Mungu kuwa pango la wadanganyi (mash. 12-13). Wakati viongozi vya Wajuda kwa maneno ya dini walipomshitaki juu ya maajabu yake ya rehema na juu ya kuruhusu watoto kumsalimu kama Masiya, aliwayamazisha na Zaburi 8:2 — watoto wadogo watamsifu kama watu wakubwa wakikataa kufanya hivi (mash. 14-16)!

Yesu analaani mtini (21:17-22)

Yesu alishinda usiku kwa Betania, lakini asubui alishika njia kurudia Yerusalem. Njiani alilaani mtini usizae matunda tena kamwe, na mara moja mtini ulikauka. Wakati wanafunzi waliposhangaa juu ya neno hili, aliwaambia ya kwamba wakiwa na imani wataweza kuagiza hata milima kuhamishwa, na kupata majibu mingi mno kwa maombi yao. Mti huu haukuwa na tini zisizokomea kwanza katika mwezi wa ine, ndilo neno lililohakikisha ya kwamba hautazaa matunda kwa mwezi wa mnane vilevile.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Maulizo juu ya amri ya Mfalme (21:23-27)

Katika viwanja nya hekalu viongozi waliuliza Kristo juu ya amri yake kufanya maneno haya. Yesu alijua ya kwamba walikuwa waki-jaribu kumnasa, akawashitusha kwa njia ya kuuliza kama utumishi wa Yoane Mbatizaji ilitoka kwa Mungu. Kama wakisema hapana, makutano wataacha kuwafuata. Kama wakisema ndiyo, basi kwa nini hawakutii Yoane kwa njia ya kutubu na kuamini Kristo? Wakati walipokataa kujibu ulizo la Yesu, Yesu alikataa vilevile kujibu ulizo lao.

Mfano wa wana wawili (21:28-32)

Na mfano huu Yesu alihamakia wakubwa wa makuhani na wazee kwa sababu hawakutii wakati Yoane alipowaita kutubu na kuamini. Walikuwa kama mwana wa pili wakisema walikubali mahubiri ya Yoane lakini hawakuyatii. Watoza kodi na makahaba walikuwa kama mwana wa kwanza. Waliona mwito wa Yoane bule kwanza, lakini mwishoni walitii.

Mfano wa shamba la mizabibu (21:33-46)

Ndani ya mfano huu mwenye nyumba alikuwa Mungu, shamba la mizabibu lilikuwa Israeli, na walimaji walikuwa viongozi nya dini. Manabii ndio watumishi waliotumwa kutafuta matunda. Yesu alikuwa mwana wa nyumba ambaye walisema juu yake, “Huyu ni mriti; kuje-ni na tumwue.”

Wakati wakubwa wa makuhani na Wafarisayo walipohukumu walimaji ndani ya mfano na kusema walistahili kuangamizwa walijihuku-mu wenye kama wenye kustahili kufa kwa sababu ya mauti ya Mwana wa Mungu. Yesu alitaja shairi 22 la Zaburi 118 na kusema ya kwamba wao ndio wajengaji ambao walimkataa, ndiye jiwe. Atatukuzwa, nao watashushwa na ufalme utaondolewa kwao na kuletwa kwa Mataifa walioamini. Walifahamu maana ya masemo yake, waka-aka kumwua, lakini watu walikaa kumheshimu kama nabii.

Mfano wa karamu ya arusi (22:1-14)

Kwa njia ya mfano huu Yesu alionyesha tena ya kwamba taifa la Israeli liliopendelewa litawekwa kando, na watu wazarauliwa wa Mataifa wataketi kama wageni mezani. Mungu alitayarisha karamu ya ndoa kwa Mwana wake, akaita watu kwanza kwa njia ya Yoane Mbatizaji na wanafunzi, nyuma yake aliwaita tena wakati karamu ilipokuwa tayari. Labda watu haya ni mfano wa mitume wakihubiri kwa Israeli kwa muda wa kitabu cha Matendo. Lakini Israeli wali-kataa kuja. Basi Mungu alituma “majeshi” yake, ndio majeshi ya askari ya Waroma walioharibu Yerusalem A.D.70. Kisha Mungu ali-

MATAYO

ita mara ya tatu watu wo wote waliokubali kufika, na chumba cha karamu kilijazwa na watu wa Mataifa walioamini. Hata hivi, ilipasa wageni kuвая vazi la ndoa liliowekwa tayari na mwenye kukaribisha wageni, ndiye Kristo.

Lipeni Kaisari (22:15-22)

Wafarisayo na Waherode walijaribu kutega Bwana na ulizo juu ya kutii Kaisari. Yesu alitumia kipande cha feza chenye picha ya Kaisari kuonyesha ya kwamba hata ikiwapasa kulipa kodi kwa Kaisari, kutii Mungu ni neno kubwa zaidi.

Ndugu saba kwa bibi-arusi mmoja (22:23-33)

Wasadukayo hawakuamini ya kwamba watu watafufuliwa, hivi walitunga habari za mwanamke aliyeolewa kwa ndugu saba, mmoja nyuma ya mwingine; kisha waliuliza nani atakuwa mume wake mbinguni. Walijaribu kufanyiza ufufuko kuonekana kama kitu cha kuchekesha wakizania ni neno lisilowezekana. Bwana aliwajibu kusema ya kwamba hawakuja Maandiko kwani hakuna neno ndani ya Biblia kusema watu watakaa kama mume na mke mbinguni. Hawakuja uwezo wa Mungu vilevile. Maandiko yanaita Mungu Mungu wa Abrahamu, Isaka, na Yakobo, watu waliokufa wote. Lakini Mungu si Mungu wa wafu lakini wa walio hai. Maana yake ndiyo ya kwamba ni lazima kwa Mungu kufufua miili ya Abrahamu, Isaka na Yakobo toka kaburi.

Amri iliyo kubwa (22:34-40)

Mtu mwenye kujua sheria ya Musa kabisa aliuliza Bwana kwa ajili ya Wafarisayo, "amri gani iliyo kubwa?" Yesu alimwambia ya kwamba ni kupenda Mungu na roho, kutaka, akili yote, na nguvu zote za mwili, na kupenda jirani yake namna anavyojipenda mwenyewe.

Mwana wa Mungu na Mwana wa watu (22:41-46)

Halafu Yesu aliuliza Wafarisayo kama walifikili Masiya atakuwa mwana wa nani. Walijibu, "Mwana wa Daudi." Halafu Yesu alitaja Zaburi 110:1, ndilo shairi linalokubaliwa kusema juu ya Masiya. Ndani ya shairi hili Daudi aliita Masiya *Bwana* wake. Hawakuweza kueleza namna gani Masiya aliweza kuwa Mwana wa Daudi na Bwana wa Daudi vilevile! Yesu mwenyewe ndiye jibu la ulizo hili. Kwa njia ya kuzaliwa duniani alikuwa *Mwana* wa Daudi, lakini akiwa Mungu alikuwa *Bwana* wa Daudi vilevile.

Yesu anaonyesha maalama ya Wafarisayo (23:1-12)

Masemo ya Mwokozi wetu juu ya waandishi na Wafarisayo yali-kuwa makali sana lakini yalikuwa ya haki vilevile. Mafundisho yao

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

yalikuwa vizuri, lakini si matendo yao! Waliweka mizigo mizito juu ya watu wengine, lakini hawakuwa tayari kuwasaidia kuibeba. Walijionyesha kuwa wenyewe kupenda Mungu sana, walitafuta pahali pa heshima zaidi katikati ya watu, na walipenda kuitwa na majina ya heshima. Maneno haya yalisukuma Yesu kukataza wanafunzi wake wasiache watu kuwaita mwalimu au baba, kwa sababu kwa maneno ya roho, Mungu tu ni Baba yetu na Roho Mtakatifu Mwalimu wetu. Inapasa wale wanaotaka kuwa wakubwa wajinyenyekeze kutumikia watu wengine.

Yesu analaumu Wafarisayo (23:13-33)

Halafu Bwana alitangaza ole nane kwa wadanganyifu wenyewe kiburi hawa wa dini. Hawakutaka wao wenyewe neema ya Mungu, na hawakutaka watu wengine kuipokea vilevile. Waliiba mali ya wajane, kisha walijaribu kuonekana watakatifu kwa njia ya maombi marefu. Walikuwa na bidii sana kufanyiza watu kuwa wageuzi, kisha waliwfundisha kuwa watu waovu zaidi. Walifundisha watu namna gani waliweza kutoa viapo ambavyo hawalazimishwi kuvitimiza. Waliweka roho sana juu ya kulipa zaka ya mboga shambani lakini si juu ya kuwa na haki, rehema na uaminifu. Waliweka roho juu ya kuonekana kama watu wanaokaa vizuri, lakini miyo yao ilijaa na choyo na roho ya kujibembeleza wenyewe. Walikuwa kama makaburi yaliyopakaliwa pembe yaliyoonekana vizuri inje, lakini ndani yalijaa kuoza. Waliheshimu manabii mbele ya watu, lakini ndani ya roho zao walifanya shauri kuua Nabii aliyekuwa mkubwa kupita manabii wote wengine. Walikuwa nyoka, na wana wa majoka na hawataweza kuepuka Hadeze hata kidogo.

Wote waliouawa kwa imani yao tangu mwanzo hata mwisho wa muda wa Agano la Kale (23:34-36)

Waandishi na Wafarisayo hawa watapiga, kutesa na kuua wajumbe ambaio Bwana Yesu atatumwa kwao, na kwa njia ya kufanya hivi watajivimbishia hatia ya uuaji wa wote waliouawa, toka Abeli, ndiye wa kwanza aliyekufa kwa imani yake (Mwanzo 4) kufika Zekaria, ndiye wa mwisho katika Agano la Kale (2 Mambo 24:20-21, ndicho kitabu cha mwisho ndani ya Biblia ya Kiebrania).

Mapendo ya Yesu kwa Yerusalem (23:37-39)

Nyuma ya kutoa malaumu haya makali zaidi, Bwana Yesu alitoa machozi juu ya Yerusalem. Hata kama watu walitendea wajumbe wake na ukali sana, angewakokota kwake na mapendo. Lakini hawakutaka kuja. Basi hekalu lao, mji wao, na taifa lao, watakuwa ukiwa kufika wakati baki la Israeli wenyewe imani watakapopokea Masiya na Mfalme wao wakati atakapokuja tena.

MATAYO

13. MFALME ANAONYESHA NINI ITATOKEA KUFIKA KUJA KWAKE MARA YA PILI (Sura 24-25)

Uharibifu wa hekalu (24:1-2)

Katika hotuba kwa mlima wa Mizeituni, Mfalme anaonyesha maneno yatakayotokea kufika wakati wa kuja kwake kwa pili. Wanafunzi walikuwa wakiwaza juu ya mapambo ya jengo la hekalu, lakini Yesu alikuwa akikumbuka ya kwamba litaharibiwa na Waroma kwa A.D.70.

Alama za mwisho wa eoni (24:3-14)

Ndani ya jibu lake kwa maulizo ya wanafunzi juu ya mlima wa Mizeituni Bwana alionyesha kwanza namna gani maneno mengine tunayoona kwa wakati wa sasa yataongezeka sana kwa sehemu ya kwanza ya Mateso – masiya za uwongo, vita na matetesvi ya vita, njaa, tauni, matetemeko ya inchi, mateso ya waamini, manabii wa uwongo, na kupunguka kwa mapendo ya watu. Lakini imani ya kweli itadumu, na Habari Njema ya ufalme itatangazwa pahali pote duniani.

Chukizo la uharibifu (24:15-28)

Katikati ya muda wa Mateso sanamu la kuchukiza sana itasi-mamishwa ndani ya hekalu kwa Yerusalem, kama Danieli alivyo-tabiri mbele. Hili litakuwa alama ya mwanzo wa Mateso *makubwa*, muda wa taabu kubwa zaidi tangu zamani. Saa ile inapasa watu walio katika Yudea kukimbia mbio. Masiya za uwongo na manabii wa uwongo watadanganya watu kwa njia ya kufanya maajabu makubwa. Habari ya kwamba Masiya ni kwa pahali fulani si kweli, kwa sababu kuja kwa Kristo kutaonekana pahali mbalimbali kama umeme. Waovu namna zote na wenye kutoamini hawataepuka hukumu.

Alama ya kuja kwa Kristo (24:29-35)

Kwa mwisho wa Mateso Makubwa kutakuwa na alama mbinguni. Halafu Mwana wa watu atarudia dunia kwa uwezo na utukufu mku-bwa. Malaika watakusanya kwa inchi ya Israeli Wayuda wachaguliwa wake toka duniani pote waliposambazwa.

Kama mtini ukitoa majani unaonyesha ya kwamba wakati wa juu kali ni karibu, vivyo hivyo kusimamishwa kwa serikali ya Israeli kunaonyesha ya kwamba kuja kwa pili kwa Masiya ni karibu. Taifa la Wayuda wanaokataa Kristo hawatapita kufika wakati maneno haya yote yatakaptomizwa.

Mifano ya muda wakati Masiya atakapokuja (24:36-51)

Mungu tu anajua siku na saa Kristo atakapokuja tena. Atakuja

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

gafula wakati watu wanapoendelea na maneno yao ya kila siku bila kufikili juu ya kurudi kwake, kama ilivyokuwa kwa wakati wa Noa. Mtu mmoja ataondolewa kwa hukumu, mwingine ataachwa kuingia ufalme (mash. 36-41). Sharti watu waangalie, kwa sababu Bwana atakuja wakati watu wasipofikili juu yake (mash. 42-44). Watumishi wenye akili watashinda na kazi ya kulisha watu wa Mungu. Watumishi waovu watakataa ya kwamba kuja kwake ni karibu na wataanza kupiga watumishi wengine na kulewa. Wakati Mfalme atakapokuja, ataazibu wadanganyi hawa wasioamini na kuwashukumu pamoja na wadanganyifu wote wengine.

Mabikira namna mbili (25:1-13)

Mfano wa mabikira kumi unaonyesha tena ya kwamba ni sharti kuangalia. Wao wote walikuwa wakilala wakati gafula kulipokuwa na tangazo kusema bwana arusi alikuwa akikaribia! Mabikira wenye akili walikuwa na mafuta ndani ya taa zao, wakakwenda kukutana naye. Mabikira wapumbavu wasiokuwa tayari hawakuweza kuingia kushiriki ndani ya karamu ya ndoa. Kristo ndiye bwana arusi, anayefika duniani, si kwa arusi, lakini kwa *karamu* ya arusi. (Arusi itakuwa mbinguni, Efe. 5:27, nyuma ya kuondoshwa kwa kanisa duniani.) Mabikira wenye akili ni waamini wa kweli, wanaoingia muda wa miaka elfu pamoja na Bwana. Mabikira wapumbavu si wenye kuamini kweli. Wanasema wanatazamia Masiya lakini wanakosa Roho Mtakatifu.

Talanta ni kwa kutumiwa (25:14-30)

Mfano wa talanta unafundisha ya kwamba wakati Mfalme atakaporudi atatoa zawabu kwa kazi ya watumishi wake wa kweli na ataazibu uovu wa watumishi wadanganyifu. Watu wawili wa kwanza walipokea hesabu mbalimbali ya talanta lakini kila mmoja alipata hesabu yenyewe tena kwa njia ya kutumika nazo. Hivi zawabu yao ilikuwa sawasawa. Mtu wa tatu alikuwa na masemo makali tu kwa bwana wake na kutoa uzuru kwa sababu gani hakufanya kazi na mali ambayo bwana alimpa. Bwana alimlaani kusema ye ye ni mwovu na mvivu, aliagiza atupwe katika giza la inje, maana Hadeze.

Kondoo na mbuzi (25:31-46)

Wakati Kristo atakaporudi, atahukumu mataifa, wanaoitwa hapa kondoo na mbuzi. Mataifa kondoo ndio wale walioshi, kuvika, na kufikia Wayuda waamini, ndio ndugu za Kristo kwa muda wa Mateso Makubwa. Mataifa mbuzi ndio wale wasiotunza *watu* wa Kristo, hivi kabisa kabisa hawakumtunza *Yeye*. Mataifa kondoo watafurahi wakati

MATAYO

wa utawala wa utukufu wa Kristo; mataifa mbuzi watakwenda kuingia katika azabu ya milele.

Habari hizi si juu ya hukumu kwa kiti kikubwa cheupe itaka-yokuwa kwa mwisho wa muda wa miaka elfu moja.

14. SIKU ZILIZOTANGULIA MSALABA (26:1-46)

Shauri baya kuua Yesu (26:1-5)

Hata saa Yesu alipokuwa akijulisha wanafunzi wake ya kwamba kusulibishwa kwake kulikuwa karibu, viongozi nya maneno ya dini walikutana kufanya shauri namna gani watamwua.

Kupakaliwa mafuta kwa Betania (26:6-13)

Mwanamke mmoja (katika Yoane 12:3 tunaona kwamba alikuwa Maria ya Betania) alifikia nyumba ya Simoni mkoma katika Betania, akamwanga marasi ya bei ya damani sana juu ya kichwa cha Kristo. Wanafunzi, zaidi Yuda walifikili tendo hili lilikuwa baya kwa sababu lilipoteza mali bule. Bwana alifanya tendo lake la mapendo na ibada ukumbusho wa daima, akisema watu watalikumbuka pahali gani Habari Njema itakapohubiriwa. Na kweli imetokea hivi.

Vipande makumi tatu nya feza (26:14-16)

Sasa saa imefika kwa Yuda kutia bei juu ya Bwana wake. Ali-pigania bei na wakubwa wa makuhani kumtoa kwa mikono yao kwa vipande 30 nya feza, kisha alingoja saa wakati atakapopata njia kufanya hivi.

Kula Pasaka (26:17-25)

Siku ya kwanza ya karamu ya mikate pasipo chachu Yesu alikutana na wanafunzi wake ndani ya chumba cha juu nyumbani ambayo ali-ichagua waweze kula Pasaka pale. Wakati walipokuwa wakiendelea na karamu aliwapasha habari za kushitisha sana ya kwamba mmoja wao atamtoa kwa mikono ya adui. Wao wote walianza kuona shaka juu ya roho zao wenyewe kufika wakati Kristo aliposema atakuwa yule aliye-chovya pamoja naye katika sahani, alimwita na jina lake na kusema ingalikuwa heri kwake kama asingalizaliwa.

Yesu anasimamisha Karamu ya Ukumbusho (26:26-35)

Kisha Mwokozi alisimamisha karamu ya ukumbusho, akitumia mkate na mvinyo kama mifano ya mwili na damu yake. Aliwaambia wanafunzi ya kwamba hatakunywa pamoja nao tena kufika wakati atakaporudi duniani kutawala (mash. 26-29). Nyuma ya kuimba wimbo walitoka Yerusalem, wakakwenda shamba la Getesemané,

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kwa mtelemuko wa mangaribi wa mlima wa Mizeituni. Pale aliwambia ya kwamba wao wote watamwacha nyuma ya saa chache. Wakati Petro aliposema, “Sivyo, hata kidogo!” Yesu alijibu, “Usiku huu … mara tatu.”

Maumivu makubwa shambani (26:36-46)

Shambani pamoja na Petro, Yakobo na Yoane, Bwana Yesu alikuwa na uchungu mkubwa sana ndani ya maombi hata alitoa jasho kama matone makubwa ya damu (Luka 22:44). Mara tatu aliomba kikombe kiweze kumpitia, lakini kama yakiwa mapenzi ya Mungu tu. Mara tatu wanafunzi watatu walishindwa na usingizi. Kisha saa ilifika kwa Bwana kukutana na makutano wenye makelele.

15. KUSULIBISHWA KWA MFALME (26:47 – 27:66)

Bwana anatolewa kwa adui na kufungwa shambani mwa Getesemané (26:47-56)

Yuda alifika pamoja na makutano, akakwenda karibu na Yesu, akambusu, ndiyo alama waliyopatana juu yake kufahamisha watu kama mshitakiwa alikuwa nani. Mmoja wa wanafunzi (katika Yoane 18:10 tunaona ya kwamba alikuwa Petro), alifuta upanga wake, akakatia mtumishi wa kuhani mkubwa sikio. Yesu alihamakia Petro, akimkumbusha ya kwamba angaliweza kuita majeshi kumi na mawili ya malaika, lakini kama angalifanya hivi, tendo hili lingaliharibu kusudi la kufika kwake duniani. Kisha alionyeshea makutano ya kwamba haikufaa kwao kufika na panga na magongo kufunga mtu asiye-amsha maasi kamwe lakini aliyefundisha na roho kimya tu. Saa ileile wanafunzi wakaacha Bwana wao, wakakimbia kwa giza la usiku.

Bwana Yesu alihukumiwa mara mbili; alihukumiwa na watu wa dini wa Wayuda, na wa serikali wa Roma. Kila hukumu ilikuwa na sehemu tatu. Matayo anaanza na sehemu ya pili ya hukumu yake na Wayuda, iliyotokea mbele ya kupambazuka kwa asubui, na iliyokuwa mbele ya Kayafa na wakubwa. Mwishoni watu wawili walitoa ushuhuda ya kuwa Yesu alisema ataharibu hekalu na kulijenga tena ndani ya siku tatu. Lakini neno kubwa zaidi lilikuwa ushuhuda wa Mwokozi mwenyewe, nyuma ya kuapishwa ya kwamba alikuwa Kristo, Mwana wa Mungu, atakayerudi siku nyingine kwa uwezo na utukufu mkuubwa. Kuhani mkubwa alisema haya ndiyo matukano; basi makutano walilalamika kwamba Yesu alistahili kuuawa.

Petro alikana Bwana mara tatu (26:69-75)

Inje katika kiwanja Petro aliogopa sana sana ya kwamba atapata

MATAYO

hatari hata alikana Bwana tena na tena, mara tatu. Wakati jogoo alipowika, Petro alitoa machozi machungu.

Yesu mbele ya wakubwa (27:1-2)

Watu hawakufikili ni taratibu kufanya hukumu usiku, hivi viongozi kwa maneno ya dini walikutana asubui kusibitisha hukumu ya kufa. Kisha walituma Bwana Yesu kwa Pontio Pilato kwa sehemu ya kwanza ya hukumu yake mbele ya serikali ya Waroma.

Yuda anajuta na kujiua mwenyewe (27:3-10)

Yuda alifahamu sasa ya kwamba alikosa sana wakati alipotoa Bwana wake mikononi mwa adui, akajaribu kusukuma wakubwa wa makuhani na wazee kukamata tena mali ambayo walimpa. Wakati walipokataa, alitupa mali yenyewe ndani ya hekalu, kisha alikwenda, aka-jiua mwenyewe. Wakubwa wa makuhani walifikili ni vizuri kutumia mali hii kununua shamba la mfinyanzi liwe pahali kwa kuzika wageni.

Yesu mbele ya Pilato (27:11-26)

Hukumu mbele ya Pilato ilikuwa ya kuchekesha tu. Liwali ali-shangaa juu ya roho ya utulivu ya Yesu. Hakuona kitu alichoweza kumshitaki juu yake, lakini hata hivi alishindwa na Wayuda wakati walipozidi kumsukuma, akawafungulia Baraba, mvunja sheria, na kutoa Yesu asulibishwe.

Yesu anazarauliwa na askari (27:27-31)

Askari Waroma walipeleka Yesu ndani ya Praitorio, wakamzarau kwa njia ya kumvika vazi jekundu, taji ya miiba, na kuweka tete mikononi mwake kama fimbo ya mfalme. Walimheshimu kama mfalme kwa hila, wakamtemea mate, wakampiga na tete, kisha walimpeleka kwa Kalvari.

Yesu anasulibishwa (27:32-44)

Halafu maneno yalitokea mbiombio. Simoni, mtu wa Kurene alilazimishwa kubeba msalaba wa Yesu. Askari walimpa Yesu kinyweo kilichoweza kupunguza maumivu mwilini mwake, lakini alikataa kunywa. Halafu Bwana wa utukufu alifungwa na misumari juu ya msalaba wa haya — zambi kubwa zaidi. Askari walipiga kura kwa mavazi yake, kisha waliweka juu ya msalaba mashitaki yake yaliyoandikwa,

“HUYU NI YESU MFALME WA WAYUDA”.

Wanyanganyi wawili waliosulibishwa pamoja naye walimzarau wakizania hakuweza kujiponyesha mwenyewe. Viongozi vyta dini walifanya vivyo hivyo na watu waliopita njiani vilevile.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Kristo anakufa kwa wazalimu (27:45-56)

Ndani ya saa tatu za giza Mwokozi alibeba azabu kwa zambi zetu, kisha alilalamika mara mbili na sauti kubwa, akatoa roho yake. Kwa dakika ile ile pazia hekaluni lilipasuliwa kwa vipande viwili, inchi ilititemeka, miamba ilipasuka, makaburi yalifunguliwa. Wale waliolinda Yesu waliogopa sana, wakifahamu ya kwamba alikuwa kweli Mwana wa Mungu. Hata saa ile wengine wa wanawake waaminifu waliofuata na kutumikia Bwana mbele walikaa karibu na msalaba.

Kristo alizikwa ndani ya kaburi la Yosefu (27:57-61)

Yosefu wa Arimatea alipata ruhusa toka Pilato kuzika mwili wa Yesu. Alitumia kaburi lake mwenyewe lililochimbwa toka miamba. Nyuma ya kufunga mwili ndani ya nguo safi aliuweka ndani ya kaburi, kisha alifingirisha jiwe kubwa mbele ya mlango wake.

Walinzi Waroma kwa kaburi (27:62-66)

Kesho yake wakubwa wa makuhani na Wafarisayo walipewa ruhusa kuagiza walinzi kuchunga kaburi, wanafunzi wa Yesu wasiibe mwili wake na kwa njia hii kuaminisha watu ya kwamba alikuwa amefufuka. Kwa macho yao neno hili lingalikuwa hata baya kupita neno alilosema mbele kwamba yeche ni Masiya na Mwana wa Mungu.

16. UFUFUKO WA MFALME. ANAKUTANA TENA NA WANAFUNZI WAKE KATIKA GALILAYA (Sura 28)

Habari Njema kubwa (28:1-10)

Wakati Maria wawili walipokwendea kaburi asubui mapema siku ya kwanza ya juma, kulikuwa na tetemeko kubwa la inchi wakati malaika aliposhuka na kufingirisha jiwe. Aliwaambia wanawake ya kwamba Kristo alikuwa amefufuka na atakutana na wanafunzi kwa Galilaya. Wakati walipoondoka mbio kupasha habari hizi njema, Bwana mwenyewe aliwasalimu, akapokea kuabudu kwao na kuwatuma kuwaambia wengine maneno ambayo waliyaona.

Uwongo mkubwa (28:11-15)

Sasa walinzi walikuwa wamepata nguvu tena nyuma ya kuzima roho, wakakwendea wakubwa wa makuhani na habari zao za haya. Makuhani waliwapa mali kusudi waseme wanafunzi waliiba mwili wakati wao wenyewe, ndio walinzi walipolala usingizi. Basi neno hili lingaliwezekana kweli? Namna gani askari waliweza kujua nini ili-tokea wakati walipokuwa wakilala usingizi? Hata hivi watu wanaliyamini hata sasa.

MATAYO

Amri kubwa (28:16-20)

Nyuma ya ufuluko wake Bwana alitokea wanafunzi wake katika Galilaya, akawaamuru kwenda duniani pote kufanya wanafunzi, kuwabatiza, na kuwafundisha kutii maagizo yake yote. Halafu aliahidi kuwa pamoja nao hata mwisho wa eoni.

Amri hii kubwa halikugeuzwa kamwe. Hata leo Bwana anaamuru watu wake kufanya hivi.

Habari Njema kama alivyoandika MARKO

MWANZO

Mwandishi

Habari Njema ya pili iliandikwa na Yoane Marko, mtumishi wa Bwana aliyeanza vizuri, kisha alishindwa kwa wakati (Mdo. 15:38). Mwishoni alirudishwa kwa kazi ya Bwana (2 Tim. 4:11).

Kusudi la Mwandishi

Kusudi la Marko lilikuwa kuonyesha Bwana Yesu kama Mtumishi Mkamilifu. Habari Njema hii ni Habari Njema ya kazi kupita nyingine. Matukio yanafuatana mbio mbio. Masemo kama “mara moja” yanaonekana tena na tena. Habari zenyewe ni fupi. Marko anasema zaidi juu ya matendo ya Bwana kupita masemo yake. Aliandika habari za maajabu 19 lakini za mifano mine tu.

Shairi kubwa

Shairi kubwa ni 10:45, “*Mwana wa watu hakuja kutumikiwa ila kutumika na kutoa uzima wake uwe ukombozi wa wengi.*”

UMBO LA MARKO

1. Matukio kwa mwanzo wa utumishi wa Mtumishi Mkamilifu (1:1-13)
2. Kazi na masemo ya Mtumishi katika Galilaya na pahali pengine (1:14 – 9:50)
3. Kazi ya Mtumishi akipita Perea kwenda Yerusalem (Sura 10)
4. Mwisho wa kazi ya Mtumishi katika Yerusalem (Sura 11-13)
5. Mauti ya Mtumishi kuwa ukombozi kwa watu wengi (Sura 14-15)
6. Ufufuko wa Mtumishi na kwenda kwake mbinguni (Sura 16)

1. MATUKIO KWA MWANZO WA UTUMISHI WA MTUMISHI MKAMILIFU (1:1-13)

Utumishi wa Yoane Mbatizaji (1:1-8)

Marko haandiki habari za kizazi, kuzaliwa na utoto wa Yesu kwa sababu habari hizi si neno kubwa ndani ya maisha ya mtumishi. Anaanza na habari za Yoane Mbatizaji, mtangulizi wa Masiya,

MARKO

aliyekuwa kutimiza unabii, akihubiri ubatizo wa toba. Aliishi bila vitu vya kubembeleza mwili na alionyesha na nguvu ya kwamba utumishi wa Masiya ni mkubwa kupita utumishi wake mwenyewe.

Ubatizo wa Yesu (1:9-11)

Wakati Yoane alipobatiza Yesu, Roho Mtakatifu alimshukia kama hua, na Mungu alitoa sauti toka mbingu kusema huyu ni Mwana wake mpendwa.

Kujaribiwa kwa Yesu (1:12-13)

Kisha Mwokozi alikwenda peke yake jangwani, akajaribiwa na Shetani kwa siku 40 katikati ya nyama wakali. Kwa mwisho wa muda ule, malaika walimtumikia.

2. KAZI NA MASEMO YA MTUMISHI KATIKA GALILAYA NA PAHALI PENGINE (1:14 – 9:50)

Mwanzo wa utumishi wa Yesu (1:14-15)

Marko haandiki juu ya utumishi wa Bwana katika Yudea (Yoane 1:19 – 4:54). Anaanza na habari za utumishi wake mkubwa katika Galilaya. Yesu alitangaza ya kwamba yeye, Mfalme aliita watu kwa ufalme wake, na ya kwamba ingepasa watu kutubu na kuamini Habari Njema ili waweze kuingia ufalme.

Yesu anaita wavuvi wane (1:16-20)

Kwa pwani ya Bahari ya Galilaya, Bwana aliita wavuvi wane: Simoni, Anderea, Yakobo, na Yoane. Wao wote wane waliacha mikila yao wageuke wavuvi wa watu.

Maajabu ya kuponyesha ya Masiya (1:21-34)

Yesu alifundisha na uwezo kabisa katika sunagogi kwa Kapernaumu. Aliponyesha vilevile mtu mwenye pepo mchafu, na watu walishangaa. Habari za ajabu hii zilienea katika Galilaya nzima (mash. 21-28). Nyuma kidogo aliponyesha mama ya mke wa Petro aliyekuwa na homa, vilevile watu wengi wengine waliofikia nyumba pahali alipokuwa, na alitoa pepo wachafu wengi (mash. 29-34). Alifanya maajabu haya yote ndani ya muda wa siku moja.

Yesu anahubiri katika inchi nzima ya Galilaya (1:35-39)

Nyuma ya maombi ya asubui Yesu aliondokea Kapernaumu, akaanza kuhubiri pahali mbalimbali katika Galilaya.

Yesu anasafisha mkoma (1:40-45)

Kwa pahali pamoja alijibu kusihii kwa mkoma mmoja, akamponye-

MAFUNDISHO JUU YA AGANO JIPYA

sha kwa njia ya kumgusa. Alikataza mtu mwenyewe asieneze habari za kuponyeshwa kwake, akamwagiza kwenda kwa kuhani na kutoa sadaka iliyofaa. Lakini mkoma alitangaza habari zenyewe sana, hivi ilipasa Bwana Yesu kwenda jangwani. Watu wengi walimfuata.

Mwenye kupooza anaponyeshwa (2:1-12)

Wakati Yesu alipokwisha kurudia Kapernaumu watu wengi sana walizunguka nyumba pahali alipokuwa hata watu hawa wane hawakuweza kufika karibu naye na mtu huyu mwenye kupooza. Basi walitboa dari, wakashusha mgonjwa mbele ya Bwana. Wakati Bwana alipomwambia mtu huyu ya kwamba zambi zake zimesamehewa, wengine wa waandishi walinungunika kusema anatukana. Kwa kufahamisha wanungunikaji hawa ya kwamba zambi za mtu huyu zilikuwa zimesamehewa kweli, Yesu alimwagiza kusimama, kubeba kitanda chake na kutembea. Mtu huyu alifanya hivi mara moja hata watu walishangaa.

Yesu anaita Matayo (Lawi), mtoza kodi (2:13-17)

Mtoza kodi alisikia mwito wa Kristo, akaacha yote na kumfuata. Alitayarisha karamu ili rafiki zake waweze kukutana na Yesu pale. Waandishi walinungunika kwa wanafunzi ya kwamba Bwana wao alikula pamoja na wenye zambi. Bwana Yesu aliwakumbusha ya kwamba alikuja kuita wenye zambi, si wale ambao walijihesabu kuwa wenye haki.

Ulizo na jibu juu ya kufunga (2:18-22)

Wakati wanafunzi wa Yoane na wa Wafarisayo walipouliza kwa sababu gani wanafunzi wa Yesu hawakufunga chakula, Yesu alijibu ya kwamba hawakuhitaji kufunga kufika wakati atakapowaondokea; kisha watafunga. Alitumia mifano miwili kuonyesha ya kwamba muda mpya umeanza, na ya kwamba haikuwezekana kuchanganya furaha na mchemuko wake na desturi za zamani zisizogeuka, na kawaida za dini. Sheria na neema ni mbalimbali kabisa.

Mabishano juu ya kazi za lazima siku ya sabato (2:23-28)

Habari hizi zinaonyesha ya kwamba desturi za dini ya Wayuda na uhuru wa Habari Njema hazipatani. Wafarisayo walihukumu wanafunzi juu ya kuchuma masuke ya ngano siku ya sabato. Yesu aliwakumbusha ya kwamba Daudi na watu wake walikula mikate ya onyesho iliyopaswa kuliwa na makuhani tu. Kwa sababu mfalme alikataliwa Mungu alikubali kwa ye ye kufanya hivi. Kisha Bwana alionyesha ya kwamba sabato ilifanywa kwa faida ya watu, si kuwa mzigo kwao, na ya kwamba ye ye, Mwana wa watu, alikuwa Bwana wa sabato.

MARKO

Mabishano juu ya kuponyesha siku ya sabato (3:1-6)

Kulikuwa na mabishano mengine juu ya sabato katika sunagogi wakati Yesu alipokutana na mtu mmoja mwenye mkono uliopooza. Mbele ya kumponyesha Yesu aliuliza Wafarisayo kama sheria ya sabato ilikataza watu kutenda mema siku ya sabato! Walifiliki haifai kwaye kuponyesha watu siku ya sabato lakini hawakufikili ilikuwa vibaya kwa wakubwa kufanya shauri kumwua siku yenye! Wakati wasipoweza kujibu ulizo lake bila kujihukumu wenye, Yesu aliponyesha mtu mwenye. Halafu Wafarisayo walifika karibu na Waherode. Waherode walikuwa adui zao tangu zamani, lakini sasa walifungana pamoja kufanya shauri kuua Bwana.

Maajabu mengine ya kuponyesha (3:7-12)

Makutano makubwa walikusanyika wakati Yesu alipokuwa kwa Bahari ya Galilaya, naye aliponyesha watu wengi. Pepo wachafu walimkiri kuwa mwana wa Mungu, lakini aliwakataza wasitangazesi kazi ya pepo wachafu kufunua neno hili kubwa.

Yesu alitura mitume kumi na wawili (3:13-21)

Kisha Yesu aliita mitume 12 kuwa pamoja naye, na kwenda kuhubiri, kuponyesha watu na kutokeza pepo wachafu (mash. 13-19). Wakati ndugu zake waliposikia habari za mambo aliyofanya, walikwenda kumkamata wakizani alikuwa wazimu (mash. 20-21). Huzuni kabisa! hata watu wa jamaa yake mwenye hawakumfurahia!

Kutukana Roho Mtakatifu (3:22-30)

Waandishi walimshitaki kusema alitoa pepo wachafu kwa uwezo wa Belzebuli. Kwa njia ya kusema hivi walifanya zambi isiyoweza kusamehewa. Yesu alionyesha uwongo wa mashitaki yao kwa njia ya kuonyesha ya kwamba yakiwa kweli Shetani angalishindana naye mwenye. Kabisa kabisa maajabu ya Kristo yalionyesha maangamizi ya Shetani, kwani mwenye kunyanganya vitu vya nyumba ya yule mwenye nguvu alikuwa Yesu. Waandishi walianguka wakati waliposema maajabu ya Roho Mtakatifu yalifanya na mkubwa wa pepo wachafu; hawatasamehewa kamwe kwa zambi ile.

Ndugu wa kweli za Yesu (3:31-35)

Wakati Maria na ndugu za Yesu walipokuja kusemezana naye, alitangaza ya kwamba jamaa mpya ya Mungu ndio wale wanaofanya mapenzi ya Mungu.

Mfano wa udongo namna ine (4:1-20)

Toka chombo Yesu alifundisha mifano ya ufalme wa Mungu.

MAFUNDISHO JUU YA AGANO JIPYA

Mfano wa kwanza ulikuwa juu ya udongo namna ine zinazoonyesha vipimo mbalimbali vyat hamu ya roho za watu kupokea Neno la Mungu.

Udongo kando ya njia ulikuwa nguvu sana na mbegu hazikuweza kuingia ndani yake, basi ndege walikuja, wakazimeza.

Pahali pa mwamba palifunika na udongo nusu tu usiotosha kwa mbegu kuota.

Mbegu zilizoanguka katikati ya miiba hazikuota vilevile, kwani miiba iliota kuwa mikubwa na kuzuiza nuru isifikie mbegu nazoz hazikuzaa matunda.

Udongo mzuri – ulikuwa wa kutosha na miiba haikuota ndani yake. Mbegu zote zilizopandwa ndani yake zilizaa kwa vipimo mbalimbali. Udongo mzuri ni mfano wa waamini wa kweli. Wao tu wanawenza kuzaa matunda kwa Mungu.

Mfano wa taa inayowaka (4:21-25)

Mfano wa taa inayowaka inafundisha ya kwamba sharti wale wanaosikia kweli za Mungu wazipashe na watu wengine. Haifai kuficha kweli hizi chini ya kitunga, maana yake haifai mtu kuacha kazi yake mwenyewe kula saa zake zote hata hana saa tena kutumikia Bwana. Wala haifai kuficha kweli hizi chini ya kitanda, maana kuacha raha na uvivu kumzuiza asitangaze Habari Njema. Inapasa wanafunzi kueleza kweli ya Mungu kila pahali wanapokuta watu walio tayari kusikia. Kila mara mwanafunzi anapopokea kweli nyingine na kuiacha kufanya kazi ndani ya maisha yake, atapewa kweli nyingine tena. Lakini kama asipotumia kweli ambayo anaipokea atapoteza vilevile kweli ambayo aliipokea mbele.

Mfano wa mbegu zinazoota kwa siri (4:26-29)

Mfano wa mbegu zinazoota kwa siri uliandikwa ndani ya Habari Njema ya Marko tu. Ni siri kwa njia yake Neno la Mungu linafanya kazi ndani ya mioyo ya watu na kuzaa matunda kwa utukufu wa Mungu, bila nguvu au akili ya mtu. Kwa wakati wa kufaa matunda yanayoiva yanavunwa.

Mfano wa mbegu ya haradali (4:30-34)

Mfano wa mbegu ya haradali unaonyesha kukua kwa ufalme toka mwanzo mdogo kugeuka mkubwa kupita kipimo. Si ya kawaida kwa mbegu ya haradali kugeuka mti mkubwa wa kutosha kwa ndege kuje-nega vioto vyao ndani yake. Vivyo hivyo ukristo utageuka jamii kubwa ya watu ambaa wanajiita Wakristo lakini wanaopokea mafundisho ya uwongo namna namna katikati yao.

MARKO

Bwana wa zoruba na mawimbi (4:35-41)

Zoruba kubwa ya upopo ulikuja wakati Yesu na wanafunzi walipokuwa wakivuka Bahari ya Galilaya kwenda kwa pwani ya mashariki. Wanafunzi waliogopa ya kwamba watazama ndani ya bahari, wakaamsha Bwana wao aliyelala usingizi, wakamhamakia kwa sababu ilioneckana ya kwamba hakuweka roho juu ya hatari yao. Yesu aliamka, akahamakia upopo nao ulikoma na bahari ilitulia. Kisha alihamakia wanafunzi wake kwa sababu walikosa imani. Walishangaa sana wakati walipoona uwezo wake mkubwa — na ya kwamba hata upopo na mawimbi yalimtii!

Pepo wachafu wanaotii, na nguruwe (5:1-20)

Katika inchi ya Wagerase Yesu alitoa pepo wachafu katika mtu wa jeuri zaidi, akaruhusu pepo kuingia kundi la nguruwe. Hivi nguruwe elfu mbili walitelemuka mlima mbio sana na kuzama baharini. Wakati wachungaji wao waliporudi mjini na habari hizi, makutano ya watu walitoka kuona mtu yule aliyekuwa na pepo wachafu mbele. Kwanza waliogopa, lakini nyuma waliomba Yesu kuondoka inchini mwao. Yule aliyeponyeshwa alitaka kwenda pamoja na Bwana, lakini Yesu alisema naye kurudia nyumba yake na kushuhudia uwezo na rehema ya Mungu.

Msichana mwenye miaka 12 na mwanamke mwenye ugonjwa kwa miaka 12 (5:21-43)

Mmoja wa wakubwa wa sunagogi, jina lake Yairo alisihi Bwana kuponyesha binti yake mwenye miaka 12 aliyekuwa karibu kufa. Wakati alipokuwa akiendea nyumba ya Yairo mwanamke mmoja mwenye taabu kubwa alizuiza Yesu njiani. Alikuwa ameteswa kwa miaka 12 na ugonjwa wa kutoka damu. Akipita katikati ya watu alifika karibu na Yesu, akagusa vazi lake, akaponyeshwa mara moja. Mbele ya kuweza kupita tena katikati ya watu na kwenda zake, Yesu alimwita kusimama mbele ya watu na kumkiri kama Mwokozi wake. Kisha alimruhusu kwenda zake na salama.

Saa ile ile wajumbe walifika na habari kusema binti ya Yairo alikuwa amefa. Walisema si faida kwa Bwana Yesu kuja. Lakini Bwana alikwendea nyumba ya Yairo pamoja na Petro, Yakobo na Yoane, akaagiza msichana kusimama, akamrudisha kwa watu wa jamaa yake. Aliwakataza kutangaza habari za ajabu hii, ili sifa ya watu wenyre roho ya kugeukageuka isimzuize kwenda msalaba.

Yesu anakataliwa kwa Nazareti (6:1-6)

Yesu alirudia Nazareti na kufundisha katika sunagogi, lakini watu hawakutambua kama yeche ni nani. Walifikili alikuwa namna ya

MAFUNDISHO JUU YA AGANO JIPYA

wanaume wote wengine wa mji wao. Mwokozi alisema ya kwamba mara nytingine nabii haheshimiwi na watu wa mji wake mwenyewe, lakini pahali pengine watu wanampokea vizuri. Kwa sababu ya kutoamini kwao watu wa Nazareti hawakupata faida ya utumishi wake. Mwana wa Mungu alishangaa juu ya neno hili, akaondoka na kwenda vijiji vingine kando kando.

Yesu anatuma wanafunzi kumi na wawili (6:7-13)

Wakati umefika kutuma wanafunzi kwa kazi yao. Waliagizwa kwenda wawili wawili pamoja kutoa pepo wachafu. Iliwapasa kwenda bila vyakula na mali wakiamini ya kwamba Mungu atawapa vyote watakavyohitaji. Wakubali kukaa pamoja na watu wo wote ambaa waliwaita kulala kwao kufika wakati walipoondoka pahali pale. Watu wa pahali po pote wakiwataa, haikuwa lazima kwao kubaki pale. Basi wakakwenda zao, wakihubiri toba, wakitoa pepo wachafu na kupakaa na mafuta na kuponyesha wagonjwa. Watu wakikataa wanafunzi ilikuwa kama walikataa Bwana mwenyewe na watapata hukumu kali.

Herode anaua Yoane Mbatizaji (6:14-29)

Wakati Herode aliposikia habari za maajabu ya Yesu, aliogopa ya kwamba Yoane Mbatizaji ambaye alimwua mbele alikuwa amefufuka (mash. 14-16).

Mwandishi wa kitabu hiki alirudi sasa kwa habari za kufa kwa Yoane. Yoane alikuwa amehamakia Herode juu ya kuoa mke wa ndugu yake, ndilo neno lisilokuwa halali. Herodia alingoja kupata njia kujilipiza kisasi. Alipata njia kwa karamu ya siku ya kuzaliwa kwa Herode. Michezo ya binti ya Herodia ilipendeza Herode sana hata aliahidi kumpa msichana kitu cho chote alichotaka, hata nusu ya ufalme wake. Mama ya msichana alimsukuma kuomba kupewa kichwa cha Yoane Mbatizaji juu ya sahani. Basi wanafunzi wa Yoane walizika mwili wake, kisha walikwenda kupasha Yesu habari.

Watu elfu tano wanakulishwa (6:30-44)

Mitume walirudia Kapernaumu na walihitaji kupumzika, hivi Yesu aliwapeleka kwa pahali pa kimya kando ya Bahari ya Galilaya. Kama ilivyokuwa kila mara, watu wengi waliwafuata na Yesu aliwfundisha kufika kuingia kwa usiku. Hata kama wanafunzi hawakufurahi, alikulisha watu 5,000 na mikate mitano na samaki miwili, na vyakula vilibaki kujaza vitunga 12.

Kutembea juu ya maji (6:45-52)

Nyuma ya kutuma wanafunzi wake ndani ya chombo ngambo ya mangaribi ya Bahari ya Galilaya Yesu alipanda kilima kuomba.

MARKO

Aliwaona toka pale wakitaabika kwa kuvuta makasia kwa sababu ya kushindana kwa upepo, akakwenda kufika karibu nao akitembea juu ya maji. Waliogopa sana wakati walipomwona wakifikili ni kivuli! Lakini wakati aliposema nao na kuingia chombo, upepo ukakoma. Hata nyuma ya kumwona akilisha watu 5,000 wanafunzi walishangaa bila kufahamu ya kwamba aliweza kufanya maneno yote.

Watu wengi walifuata Yesu hata Kapernaumu (6:53-56)

Ngambo ya mangaribi ya bahari alisongwa na wagonjwa wengi. Kila pahali alipokwenda, watu walifikisha wagonjwa karibu naye. Kila mtu aliyegusa hata pindo la vazi lake aliponyeshwa.

Desturi za watu zinashindana na maagizo ya Mungu (7:1-13)

Wafarisayo na waandishi walinungunikia Yesu kwa sababu wanafunzi wake hawakushika desturi zao za kunawa mbele ya kula. Bwana aliwaita wadanganyifu walioheshimu desturi zao kupita Neno la Mungu. Kama mfano wa neno hili alitaja desturi yao ya kuepu kusaidia wazazi wao kwa njia ya kusema tu ya kwamba mali yenye ilitolewa kwa Mungu au kwa hekalu. Kwa njia hii walifanyiza bule agizo la Mungu kuheshimu wazazi wao.

Uchafu wa kweli unatoka rohoni (7:14-23)

Halafu Yesu aliongeza ya kwamba si vitu vinavyoingia kinywa cha mtu (kama vyakula vinavyokuliwa na mikono isiyochafuwa) vinavyochafua roho, lakini maneno yanayotoka roho yake (kama desturi za watu zinazoona Neno la Mungu bule). Kwa njia ya kusema hivi Yesu aliondosha tofauti iliyokuwa ndani ya Agano la Kale kwa maneno ya vyakula, akatangaza ya kwamba vyakula vyote ni safi. Neno linachafua ndilo zambi kama uzini, wizi, uuaji, udanganyifu, na kiburi.

Bila shaka wanafunzi walishituka sana wakati waliposikia Bwana akisema vyakula vyote ni safi.

Imbwa chini ya meza (7:24-30)

Wakati Yesu aliposafiri kwa upande wa kaskazini-mangaribi kwendwa Tiro na Sidona, alikutana na mwanamke mtaifa mwenye kukata tamaa. Mwanamke huyu alimsihi kusaidia binti yake aliyekuwa na pepo mchafu. Ni kama Bwana Yesu alikataa kwanza, akisema mwanamke alikuwa Mtaifa, lakini ye ye mwenyewe alitumwa kwa Wayuda waliohesabu watu wa Mataifa kama imbwa. Lakini mwanamke huyu alikuwa na imani iliyokaa kuongezeka kwa kipimo Bwana alichojaribu kukataa kumsaidia. Mwishoni alipewa zawabu kwa imani yake wakati Yesu alipoponyesha binti yake toka mbali. Wakati mwanamke alipofika nyumbani mwake, msichana alikuwa amepona.

MAFUNDISHO JUU YA AGANO JIPYA

Yesu anaponyesha kiziwi na bubu (7:31-37)

Yesu alirudi kwa upande wa mashariki wa bahari ya Galilaya, akakutana pale na kiziwi aliyejkuwa bubu vilevile. Akimwondosha katikati ya watu na kwenda naye kando, aligusa masikio na ulimi wa mtu yule, akaagiza zifunguliwe, basi mtu yule aliwezeshe wa kusema na kusikia kama watu wengine. Bwana aliomba watu wasitangaze habari za ajabu hili, lakini walizidi kuasi agizo lake, wakishangaa juu ya wema na uwezo wake.

Yesu anakulisha watu kupita elfu ine (8:1-9)

Bwana alikulisha tena makutano makubwa ya watu wenye njaa. Mara hii alitumika na mikate saba na samaki wadogo wachache kulisha watu 4,000. Vitunga saba vilivyojaa mavunjiko vilibaki. Tunafikili watu hawa walikuwa watu wa Mataifa, kwani Dekapoli palikuwa pahali pa Mataifa.

Kutafuta alama toka mbinguni (8:10-12)

Kwa upande wa mangaribi wa bahari ya Galilaya, Wafarisayo walitaka alama toka mbinguni. Yesu akiugua katika roho aliwaambia ya kuwa hakutakuwa na alama nydingine.

Chachu ya Wafarisayo na mikate ya Yesu (8:13-21)

Akivuka bahari tena kwenda mashariki Bwana alionya wanafunzi wake juu ya chachu ya Wafarisayo (unafiki) na chachu ya Herode (mashaka, uovu, mapendo kwa anasa ya dunia). Wanafunzi walifikili alikuwa akisema juu ya mkate kwa sababu walisahau kuleta vyakula. Hivi Bwana aliwaliza maneno tisa. Maulizo matano ya kwanza yaliwahamakia juu ya ugumu na uzito wa miyo yao. Maulizo mane ya mwisho yaliwahamakia juu ya kusumbukia mahitaji yao wakati yeze alipokuwa pamoja nao.

Yesu anaponyesha kipofu kwa Betesaida (8:22-26)

Kwa sababu Bwana Yesu alikuwa amehukumu Betesaida mbele (Matayo 11:21-24), alipeleka kipofu inje ya mji mbele ya kumwezesha kuona tena. Hakumponyesha mbio, lakini polepole, lakini mtu mwenyewe alipona kabisa. Yesu alimkataza kutoa ushuhuda njini kwa sababu uovu wao ulikuwa umezidi kupita kipimo.

Kukiri kwa Petro (8:27-30)

Kwa Kaisari Filipi Petro alikiri Yesu kuwa Kristo, si mtu mkubwa tu kama Yoane Mbatizaji, Elia, au mmoja wa manabii. Mara hii vilevile Bwana alikataza wanafunzi wasitangaze habari hizi.

MARKO

Yesu anatabiri kwamba atakufa na kufufuka (8:31-33)

Halafu Bwana alipasha wanafunzi wazi ya kwamba itampasa kuteswa, kukataliwa, kuuawa, na kufufuka tena. Petro alimhamakia juu ya kusema maneno namna hii, lakini Yesu alimhamakia ye ye kwa sababu ya kusema kama Shetani, maana alishindana na mapenzi ya Mungu.

Kuchukua msalaba (8:34-38)

Kristo alieleza ya kwamba wanafunzi wakimfuata, itawapasa kujikana wenyewe na kuchagua njia ambayo iliweza kuwapatia laumu, mateso, na kufa. Kama wakiishi kwa faida yao wenyewe watakosa kupata yaliyo ya faida zaidi kwa maisha ya sasa. Kama wakipoteza uzima wao kwa njia ya kutumikia Kristo, maisha yao yatakuwa na faida zaidi. Ni hasara kabisa kujipatia ulimwengu wote kwa pahali pa kutumia uzima wao kuzaa matunda yatakayodumu milele. Wale wanaojaribu kuepuka laumu kwa ajili ya Kristo watapata haya kubwa zaidi wakati atakaporudi duniani na uwezo na utukufu mkubwa.

Kristo anageuzwa sura (9:1-10)

Habari hizi zinaendelea na wazo la shairi la mwisho la sura 8, maana zinafunua kama kurudi kwa Mwana wa watu kutakuwa namna gani. Maneno yaliyotokea juu ya mlima yalikuwa mfano mdogo wa utawala wa miaka elfu moja wa Kristo kwa wakati wa kuja na yali-mwonyesha kuwa mwenye sifa zaidi na utukufu usiofichwa. Watatatuwa Agano la Kale na Agano Jipyä watakuwa pale vilevile (mash. 1-4). Wingu la utukufu na sauti ya Baba toka mbingu zilikataa kabisa wazo la Petro ya kwamba vizuri Kristo na Musa na Elia waheshimiwe sawasawa. Wakati waliposhuka mlima Bwana aliwakataza wasiseme juu ya maneno waliyokwisha kuona kufika nyuma ya ufufuko wake (mash. 5-10). Matukio haya yalikuwa kionjo cha mbele kwa wanafunzi wale watatu cha maneno yanayongojea wale wanaofuata Kristo na uaminifu maisha yao mazima. Hata kama ikiwapasa kuli-pa bei kubwa kama wakifuata Kristo hapa duniani, utukufu utakuwa zawabu yao nyuma ya kufa kwao, ndiyo faida kubwa zaidi taabu yote waliyopata.

Ulizo juu ya Elia (9:11-13)

Wanafunzi walifazaika kwa sababu gani Elia hakuja kama mtangu-lizi wa Masiya, kama Malaki alivyotabiri. Yesu alijibu ya kwamba Elia alikuwa amefika kweli (kwa sura ya Yoane Mbatizaji) na alikataliwa. Kukataliwa kwa Yoane kuliyakinisha mashairi katika Agano la Kale yaliyosema itapasa Mwana wa watu kuteswa na kuza-rauliwa.

MAFUNDISHO JUU YA AGANO JIPYA

Hitaji kwa maombi na kufunga (9:14-29)

Wakati Yesu na wanafunzi walipokwisha kushuka mlima walikuta baba mmoja aliyetaabishwa sana kwa sababu ya mwana wake mwenye pepo mchafu aliyesewa na kifafa. Wanafunzi hawakuweza kutoa pepo mchafu. Wakati Yesu alipoagiza pepo kuondokea mtoto, kulikuwa na kifafa kubwa kingine, kisha mwili mdogo wa mtoto ulilala kimya kama maiti. Mwokozi alimsimamisha polepole na kumrudisha kwa baba yake. Wakati wanafunzi walipouliza kwa sababu gani hawa-kuweza kutoa pepo mchafu, Mwokozi alijibu kusema maajabu mengine yanawezekana tu nyuma ya kuweka saa kwa kuomba na kufunga.

Yesu anatabiri tena ya kwamba atakufa na kufufuka (9:30-32)

Sasa Mwokozi aligeuka kwenda kusini kwa upande wa Yerusalem — na msalaba. Alijulisha wanafunzi wake tena waziwazi maneno yatakayotokea.

Unyenyekevu (9:33-37)

Lakini kwa pahali pa kuhuzunika juu ya habari hizi walibishana kama nani katikati yao alikuwa mkubwa zaidi. Wakati walipofikia Kapernaumu, Yesu aliwakumbusha ya kwamba njia kupata ukubwa ni kutumikia wengine na unyenyekevu. Alieleza ya kwamba neno jema lo lote tunalotendea mtoto ni kama tunalitenda kwa Bwana mwenyewe au kwa Mungu Baba.

Kuchunga wafuata wa Bwana (9:38-41)

Kisha Yoane alisema ya kwamba walikuwa wamekataza mtu aliyekuwa akitoa pepo wachafu kwa jina la Yesu. Bwana alieleza ya kwamba ndani ya kazi ya Mungu, mwamini ye yote asiyeshindana naye ni kwa upande wake. Aliwaambia ya kwamba hata neno dogo lo lote, hata neno dogo sana, linalofanywa kwa jina lake litapata zawabu.

Kujitawala mwenyewe (9:42-50)

Lakini ingalikuwa vizuri kwa mtu kuzamishwa ndani ya maji kupita kwa mtu huyu kukwalisha mmoja wa wadogo hawa wenye imani wasitembee katika utakatifu na kweli. Ni lazima kwa wale wanao-jaribu kufuata Bwana kwelikweli kushindana saa zote na tamaa ya mwili. Kupoteza kiungo cha mwili kama mkono au mguu, ni vizuri kupita kukwalishwa na kiungo hiki na kwenda Gehena! Kama mwami-ni akiacha kuwa kama chumvi kwa sababu hahukumu na ukali tamaa ya mwili, maisha yake hayatakuwa na faida tena.

MARKO

3. KAZI YA MTUMISHI WAKATI ALIPOPITA PEREA KWENDA YERUSALEMA (Sura 10)

Mafundisho ya Yesu juu ya kuachana na kuoaa tena (10:1-12)

Nyuma ya kufikia Perea, kwa upande wa mashariki wa Yorodani, Wafarisayo walimwuliza kama ni halali kwa mume kuacha mke wake. Mwokozi aliwakumbusha Neno la Mungu – neno hili lilikubaliwa na Musa, lakini kusudi la Mungu lilikuwa tangu mwanzo ya kwamba haifai mtu kuvunja ndoa kwa njia ya kuachana. Wakati hata wanafunzi walipofazaika juu ya neno hili, Bwana alisema wazi ya kwamba mtu akioa tena nyuma ya kuachana anatenda uzini. (Lakini katika Matayo 19:9 alitaja sababu moja linaloleta ruhusa kwa watu kuachana.)

Yesu anapenda watoto wadogo (10:13-16)

Wanafunzi walijaribu kufukuza wazazi walioleta watoto wao karibu na Yesu aweze kuwabariki lakini Bwana aliwakaribisha. Alieleza ya kwamba ufalme wa Mungu ni wa watoto na wa wenyewe imani na unyenyekevu namna ya mtoto.

Kijana mwenye mali nyngi (10:17-22)

Wakati tajiri mmoja alipouliza nini ilimpasa kufanya kuriti uzima wa milele, Mwokozi alimkumbusha sheria ya Musa kumfahamisha hitaji kubwa la roho yake na ya kwamba hataweza kuriti ufalme kwa njia ya kufanya kitu. Tajiri alisema alikuwa ametimiza amri tano juu ya namna tunavyopaswa kutendea wenzetu. Lakini kama akipenda jirani yake kweli kweli kama yeze mwenyewe, atauza vyote alivyo navyo na kutumia mali yenyewe kusaidia watu masikini. Mtu huyu alikwenda zake na huzuni kwa sababu alikuwa na mali nyngi.

Zawabu katika ufalme (10:23-31)

Halafu Yesu alisema ni nguvu sana kwa wenyewe mali nyngi kuingia ufalme. Alisema ni nyepesi kwa ngamia kupita katika tundu la shindano (hata neno hili haliwezekani!) kuliko tajiri kuingia ufalme. Wanafunzi walishangaa kwa sababu walifikili mali ni alama ya baraka ya Mungu. Yesu alijibu ya kwamba maneno yasiyowezekana kwa watu yanawezekana kwa Mungu, maana Mungu anaweza kusaidia tajiri asitegemee mali yake.

Wakati Petro alipouliza kama yeze na wanafunzi wengine watapokea nini kwa sababu ya kuacha vyote, Yesu aliahidi watapokea mapato ya 10,000% kwa wakati wa sasa na uzima wa milele kwa wakati wa kuja. Lakini alionya Petro ya kwamba akiwa na roho ya kupigania bei labda atakuwa mtu wa mwisho kupokea zawabu!

MAFUNDISHO JUU YA AGANO JIPYA

Yesu anatabiri tena ya kwamba atakufa na kufufuka (10:32-34)

Mwokozi alitangulia wanafunzi wake njiani kwenda Yerusalem, hata kama alijua ya kwamba pale atatolewa kwa viongozi wa dini, kuhukumiwa, kutolewa kwa mikono ya Mataifa, kuzarauliwa, kupigwa, kutemewa mate, kuuawa — na kufufuliwa tena siku ya tatu. Wanafunzi walishangaa juu ya bidii yake kufanya mapenzi ya Mungu bila woga.

Mama mwenye kutaka ukubwa kwa wana wake (10:35-45)

Haikuwa saa nzuri kwa Yakobo na Yoane kubishana juu ya kuwa na pahali pa heshima katika ufalme! Yesu alieleza ya kwamba pahali pale patakuwa kwa wale walioteswa zaidi na kuwa na uaminifu zaidi kwa Kristo. Wanafunzi wengine walisikia mazungumzo haya na hawakupendezwa hata kidogo na Yakobo na Yoane — labda kwa sababu walitamani pahali pale pa heshima wao wenyewe! Yesu ali-wakumbusha tena ya kwamba ukubwa katika ufalme wake unapatikana kwa njia ya utumishi. Yeye mwenyewe, Mtumishi mkamili-fu, alikuwa mfano mzuri kabisa wa neno hili.

Yesu aliwezesha Baratimayo kuona (10:46-52)

Bwana na wanafunzi walivuka Yorodani, wakafikia Yeriko, pahali walipokutana na Baratimayo. Hata kama Baratimayo alikuwa kipofu, alifahamu Yesu ni Masiya, akamwomba aweze kupata kuona. Alisema wazi neno alilotaka na alilipata — aliweza kuona tena, kisha alifuata Yesu.

4. MWISHO WA KAZI YA MTUMISHI MKAMILIFU KATIKA YERUSALEMA (Sura 11-13)

Mwingilio wa shangwe (11:1-11)

Sasa tunaanza kusoma juu ya juma la mwisho la utumishi wa Yesu. Alikuwa amefikia mtelemko wa mashariki wa mlima wa Mizeituni na alikuwa tayari kujionyesha wazi kama Masiya-Mfalme wa Israeli. Wanafunzi walipata mwana-punda ambaye Mwokozi alisema nao juu yake. Bwana alikalia nyama huyu kwenda Yerusalem akitembea juu ya zulia ya mavazi na matawi. Watu walilalamika na shangwe wakati Yesu alipoingia mji na kwendea viwanja nya hekalu. Usiku ule alirudia Betania.

Yesu analaani mtini (11:12-14)

Kesho yake Yesu alilaani mtini kwa sababu haukuwa na tini za mbele ya wakati. Alijua kwamba tini za mbele zikikosa, mti ule hau-

MARKO

tazaa matunda kamwe. Mti huu ni mfano wa Israeli waliokuwa na majani (walikiri kuwa watu wa Mungu) lakini wasiozaa matunda kwa Mungu. Sehemu ya taifa wasioamini wanalaaniwa na hawatakuwa na faida kwa Mungu daima. Lakini Waisraeli wanaoamini wataokolewa.

Yesu anasafisha hekalu (11:15-19)

Sasa Yesu alifukuza watu waliobadilisha feza hekaluni, kama ali-
vyofanya mbele vilevile kwa mwanzo wa utumishi wake katikati ya
watu. Waandishi na Wafarisayo walikasirika sana na wangalimwua
palepale, lakini waliogopa watu.

Mtini uliokauka (11:20-26)

Wakati wanafunzi walipoona ya kwamba mtini ulikuwa umekauka
usiku, waliomba Bwana kueleza neno hili. Alionyesha ya kwamba
mambo magumu yanaweza kuondoshwa kwa njia ya imani. Lakini
alioneza neno moja lingine mara moja, ndilo hili: tukitaka Mungu
kujibu maombi yetu ni lazima kwetu kuwa na roho ya usamehe.

Maulizo juu ya amri ya Mfalme (11:27-33)

Viongozi kwa maneno ya dini waliuliza pahali gani Kristo alipopata
amri yake. Aliwijibu kwa njia ya kuuliza kama Yoane Mbatizaji
alitumwa na Mungu. Kama wakisema sivyo, makutano watawa-
kasirikia. Kama wakisema ndiyo, ingaliwapasa kutii agizo la Yoane
kutubu. Wakati walipokataa kujibu, Bwana alikataa kusemezana nao
juu ya amri yake.

Mfano wa shamba la mizabibu (12:1-12)

Ndani ya mfano wa shamba la mizabibu, Bwana Yesu alishitaki
watawala Wayuda juu ya kukataa Mwana wa Mungu. Mwenye sha-
mba ndiye Mungu, na shamba la mizabibu ni pahali pa mapendeleo pa
Israeli. Boma la miti ilikuwa sheria ya Musa na walimaji walikuwa
viongozi kwa maneno ya dini. Waliua watumishi wa Mungu, manabii,
na mwishoni waliua Mwana wake mpendwa. Hivi Mungu atawaharibu
na kuwapa Mataifa pahali pao pa mapendeleo. Maneno haya yote ya-
litimiza Maandiko katika Agano la Kale yaliyotabiri ya kwamba taifa
la Israeli watakatala Masiya na ya kwamba Mungu atatukiza Mwana
wake. Viongozi vya Wayuda walifahamu maana ya mfano huu,
wakataka kuharibu Bwana, lakini hawakuweza kwa sababu wakati
wake ulikuwa haujafika bado.

Lipeni Kaisari (12:13-17)

Wafarisayo na Waherode walikaa na uadui sana, lakini wali-
fungana pamoja kujaribu kutega Yesu kwa njia ya kuuliza kama ni
halali kulipa kodi kwa serikali ya Waroma. Kama akisema ndiyo,

MAFUNDISHO JUU YA AGANO JIPYA

Wayuda wengi watageuka adui zake. Kama akisema sivyo, Wafarisayo na Waherode watamshitaki kwa serikali kama haini. Yesu alitumia kipande cha feza kama mfano kuwaagiza kulipa kodi kwa Kaisari na kwa Mungu. Walikuwa wakilipa kodi kwa Kaisari, lakini si kwa Mungu.

Ndugu saba kwa bibi arusi mmoja (12:18-27)

Wasadukayo walijaribu kuzihaki kweli ya ufufuko wa mwili kwa njia ya kupasha habari za mwanamke mmoja aliyeoa ndugu saba, mmoja nyuma ya mwingine. Kisha mwanamke alikufa vilevile. Waliuliza Yesu kama atakuwa mke wa nani katika ufufuko. Yesu aliwajibu kusema ya kwamba hawakujua maneno Maandiko yanayofundisha juu ya ufufuko, wala uwezo wa Mungu anayefufua wafu. Alisema mbinguni watu hawakai pamoja kama mume na mke, na alionyesha ya kwamba, kwa sababu Mungu ni Mungu aliye hai, ni lazima kwake kufufua Abrahamu, Isaka, na Yakobo.

Amri iliyo kubwa (12:28-34)

Wakati mwandishi alipouliza amri gani ndiyo kubwa zaidi, Yesu alijibu kusema, “Penda Mungu na roho yote.” Kisha aliongeza kusema ya kwamba amri ya pili ni “kupenda jirani yako kama wewe mwenyewe.” Mwandishi alikubali jibu hili na roho moja na Mwokozi alimwambia ya kwamba ye ye si mbali na ufalme wa Mungu.

Mwana wa Mungu na Mwana wa watu (12:35-37)

Sasa Yesu alikuwa na ulizo kwa watu katika kiwanja cha hekalu. Waandishi walijibu vizuri ya kwamba Masiya atakuwa Mwana wa Daudi. Basi ikiwa hivi, namna gani Daudi (ndani ya Zaburi 110:1) alimwita Bwana? Jibu kwa ulizo hili ndilo hili: Kama Mwana wa Daudi, Masiya atakuwa na mwili wa mtu, na kama Bwana wa Daudi atakuwa Mungu.

Yesu alilaumu waandishi (12:38-40)

Halafu Mwokozi alilaumu waandishi kwa sababu walipenda kuonekana mbele ya watu wakivaa mavazi marefu na kuitwa majina ya heshima, walipenda kukaa pahali pa mbele katika karamu, waliiba mali ya wajane na kuomba maombi ya udanganyifu.

Sengi mbili za mjane (12:41-44)

Ona tofauti katikati ya choyo ya waandishi na mapendo kwa Mungu ya mjane huyu aliyetia mali yake yote kwa Bwana ndani ya sanduku ya hazina hekaluni. Yesu alionyesha ya kwamba watu wengine wenye mali walitoa mali vilevile, lakini mjane huyu masikini

MARKO

alitoa hata kama alikuwa masikini. Kwa mafikili ya Mwokozi ukubwa wa zawadi yake ulipita zawadi za watu wote wengine pamoja.

Uharibifu wa hekalu (13:1-2)

Wakati mmoja wa wanafunzi aliposifu ujenzi wa hekalu, Mwokozi alisema hekalu litaharibiwa kabisa hata jiwe halitabaki juu ya jiwe pasipo kubomolewa.

Alama za mwisho wa dunia (13:3-8)

Juu ya Mlima wa Mizeituni, Bwana alipasha wanafunzi habari za maneno yaliyokuwa karibu kutokea na yale yatakayotokea kwa wakati wa kuja. Ndani ya hotuba hii habari za uharibifu wa hekalu kwa A.D. 70 zinaunganika na Mateso Makubwa yatakayokuwa miaka mingi nyuma, na kuja kwa pili kwa Bwana. Haifai watu wake wadanganywe na masiya za uwongo kwa wakati wa “mwanzo wa uchungu,” na haifai wafikili habari za vita na uvumi wa vita ni alama ya mwisho. Muda wa mateso makubwa zaidi utafuata maneno haya.

Yesu anaonya ya kwamba watateswa (13:9-13)

Wafuata wake watahukumiwa kwa baraza za hukumu za watu wa dini na za serikali. Habari Njema ya ufalme itahubiriwa kwa mataifa yote. Waamini wanaoteswa na kushitakiwa watasaidiwa na Mungu kujisimamia. Wale walio waaminifu kwa Bwana watatolewa kwa adui zao, hata na ndugu zao wenyewe. Mtu akitaka kuokolewa haifai akane Kristo lakini ashinde hata mwisho.

Chukizo la uharibifu (13:14-23)

Shairi 14 linatufikisha kwa pahali pa katikati pa Mateso Makubwa wakati sanamu ya kuchukiza mno itakaposimamishwa hekaluni. Sharti watu wakimbie toka Yudea wakati ule bila kupeleka vitu vyao pamoja nao. Utakuwa wakati wa mateso makubwa zaidi tangu zamani na itapaswa Mungu kufupisha muda wenyewe kusaidia watu wake. “Masiya” wa uwongo wenyewe kufanya maajabu watatokea, lakini haifai waamini wadanganywe nao.

Alama ya kuja kwa Kristo (13:24-27)

Kwa mwisho wa Mateso Makubwa kutakuwa na msukosuko mbinguni, ndiyo alama ya kurudi kwa Mwana wa watu na uwezo na utukufu mkubwa. Malaika zake watakusanya wachaguliwa wake toka pahali pote duniani wafurahi katika baraka za ufalme wake wa ajabu.

Mfano wa mtini (13:28-31)

Kama majani ya mtini yanavyoonyesha kwamba wakati wa jua kali ni karibu, vivyo hivyo maana ya maneno tuliyosoma sasa tu ni ya

MAFUNDISHO JUU YA AGANO JIPYA

kwamba kurudi kwa Bwana ni karibu. Taifa la Wayuda wanaokana Kristo hawatatoweka kufika maneno yote yatakapokwisha kutimizwa.

Mifano ya muda wa kurudi kwa Bwana (13:32-37)

Wakati wa kurudi kwake haujulikani. Hata Bwana Yesu, kama Mtumishi Mkamilifu, hakujuishwa habari hizi azifunue kwa watu. Kama msafiri anayefanya safari ndefu, inawezekana kwa Mwokozi kurudi kwa wakati wo wote, hivi inapasa watu wake kuangalia na kuomba.

5. MAUTI YA MTUMISHI KUWA UKOMBOZI KWA WATU WENGI (Sura 14-15)

Shauri kuua Yesu (14:1-2)

Ilikuwa siku ya kazi tatu ya juma la mwisho. Wakubwa wa makuhani na waandishi walitaka kuua Bwana Yesu, lakini waliogopa ku-fanya hivi wakati wa Pasaka.

Yesu alipakaliwa mafuta kwa Betania (14:3-9)

Kwa chakula Simoni mkomaa alichotayarisha kuheshimu Yesu, mwanamke mmoja (jina lake halitajwi) alipakaa kichwa cha Bwana na marasi ya bei kubwa. Wengine wa wageni kwa karamu walifikili kufanya hivi kulikuwa kupoteza mali bule, lakini Bwana aliwahamakia juu ya manunguniko yao. Mwanamke alikuwa amekamata njia hii kupakaa mwili wa Bwana kwa maziko, naye atakumbukwa pahali pote duniani kwa sababu ya tendo hili.

Vipande makumi tatu vya feza (14:10-11)

Kwa saa hii Yuda alipatana na wakubwa wa makuhani kutoa Bwana wake kwa mali.

Kula Pasaka (14:12-21)

Tunafikili sasa ilikuwa siku ya kazi ine. Wanafunzi wawili walifanya maneno ambayo Bwana aliwaagiza, wakakuta chumba kikubwa juu ya nyumba. Pale wao wote walikula Pasaka ya mwisho pamoja. Saa yenye Yesu alionyesha yule ambaye atamtoa kwa adui zake kwa njia ya kumpa kipande cha mkate kilichochovywa ndani ya mchuzi wa nyama.

Yesu anasimamisha Karamu ya Ukumbusho (14:22-26)

Nyuma ya kutoka kwa Yuda (Yoane 13:30), Yesu alisimamisha karamu ya ukumbusho. Kwa mwisho wa karamu waliimba, kisha wakakwendea mlima wa Mizeituni.

MARKO

Yesu anatabiri ya kwamba Petro atamkana (14:27-31)

Njiani Mwokozi alisema na wanafunzi ya kwamba wao wote watamwacha usiku ule; lakini hatawakataa kwa sababu ya neno hili lakini atakutana nao katika Galilaya nyuma ya ufufuko wake. Petro alisema na nguvu ya kwamba hatakana Bwana kamwe, lakini Yesu alisema “mara tatu” kwa pahali pa “kamwe”. Wanafunzi wengine walifungana na Petro kusema watakuwa waaminifu kwa Bwana.

Maumivu makubwa shambani (14:32-42)

Katika shamba la Getesemane Yesu aliwaza juu ya taabu kubwa ya kubeba zambi za dunia, mzigo wa shida na hofu. Hakupata jibu kwa ombi lake kikombe kimwondolee. Neno hili lilionyesha ya kwamba hakuna njia nyingine kwa wenye zambi kuokolewa ila kwa njia ya kufa kwake kwa msalaba. Bwana alirudi mara tatu nyuma ya kuomba na kila mara alikuta Petro, Yakobo na Yoane wakilala. Halafu saa ya kwenda ilifika.

Yesu anatolewa kwa adui na kufungwa kwa Getesemane (14:43-52)

Yuda alikuwa akingoja na kundi la watu wenye panga na magongo. Alikuwa amepatana nao juu ya alama kuwafahamisha kama iliwapasa kukamata mtu gani, ndiyo busu, hivi sasa alibusu Bwana. Halafu watu wenye panga walimkamata. Mmoja wa wanafunzi (Petro), akijaribu kusimamia Bwana wake alikata sikio la mtumishi wa kuhani mkubwa. (Yesu alifanya ajabu kurudisha sikio lenyewe, kama tunavyosoma ndani ya Habari Njema ya Luka.) Ilikuwa nguvu kufahamu kwa sababu gani walifunga Bwana Yesu na nguvu wakati alipokuwa amekaa pamoja nao siku nyingi akifundisha na salama kwa kiwanja cha hekalu. Lakini ilikuwa lazima kwa Maandiko kutimizwa. Labda kijana aliyekimbia wichi akiacha nguo yake mikononi mwa askari alikuwa Marko.

Yesu mbele ya Kayafa (14:53-54)

Hukumu ya Bwana mbele ya wakubwa wa dini ilikuwa na sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ilikuwa mbele ya kuhani mkubwa wakati Petro alipoketi inje akiota moto pamoja na watumishi waliozunguka moto.

Yesu mbele ya wakubwa (14:55-65)

Ni kama shairi 55 linaanza sehemu ya pili ya hukumu hii, ndilo kusanyiko la wakubwa saa sita ya usiku. Ushuhuda wa washuhuda haukupatana na kwa mwanzo Yesu hakujiбу kuhani mkubwa. Lakini wakati kuhani alipouliza Bwana waziwazi kama yeche ni Masiya, Mwokozi alijibu kusema ni kweli, na ya kwamba siku nyingine ataru-

MAFUNDISHO JUU YA AGANO JIPYA

di duniani na kuonyeshwa wazi kuwa Mungu. Kuhani mkubwa alifahamu masemo yake, akamshitaki juu ya matukano, basi wakubwa wote walimhukumu kufa. Tunashangaa juu ya maneno ambayo walimtendea, ndiyo kumtemea mate usoni, kufunga macho yake na kitambaa, kisha kusema naye kutaja majina ya wale ambaao walimpiga.

Petro alikana Bwana mara tatu (14:66-72)

Inje, katika kiwanja, Petro alikana Bwana mara tatu ndani ya muda mfupi. Wakati jogoo alipowika mara ya pili, Petro alikumbuka masemo ya Bwana, akatoa machozi na uchungu kwa sababu ya kosa lake kubwa la kukana Bwana wake.

Yesu mbele ya Pilato (15:1-5)

Shairi 1 linasema juu ya kusanyiko la wakubwa asubui, labda kuhalilisha matendo yao usiku uliopita. Hii ilikuwa sehemu ya tatu ya hukumu ya Yesu mbele ya wakubwa wa dini. Hukumu yake mbele ya serikali ilikuwa na sehemu tatu vilevile: mbele ya Pilato; mbele ya Herode; na mbele ya Pilato tena. Marko hakuandika juu ya sehemu ya hukumu mbele ya Herode na aliandika juu ya kutokea kwa Yesu mara moja tu mbele ya Pilato. Yesu alikubali mbele ya Pilato ya kwamba alikuwa Mfalme wa Wayuda, lakini alikataa kujibu mashitaki ya wakubwa wa makuhani, ndilo neno lililoshangaza Pilato sana.

Baraba anafunguliwa (15:6-15)

Wakati liwali alipokuwa tayari kufungulia watu Yesu au Baraba, waliomba Baraba afunguliwe na Yesu auawe. Pilato, mwenye roho zaifu, alikubali.

Yesu anazarauliwa na askari (15:16-23)

Askari walitembeza Yesu kwa kiwanja cha makao ya liwali, wakamfanyiza mfalme kwa zihaka wakimvika vazi jekundu na taji ya miiba. Nyuma ya kumtendea mabaya na kumzarau, walimkwendesha Kalvari, wakilazimisha Simoni, mtu wa Kurene, kubeba msalaba wake.

Yesu alikataa dawa ambayo waliwapa watu waliohukumiwa kufa.

Yesu anasulibishwa (15:24-36)

Ilikuwa saa tatu ya asubui wakati walipomsulibisha, na maandiko juu ya kichwa chake, "MFALME WA WAYUDA", na wanyanganyi wawili pamoja naye, mmoja kwa mkono wake wa kuume na mwingine kwa kushoto. Watu namna tatu walimzarau — wale walipita njiani, wakubwa wa makuhani na waandishi, na wanyanganyi wale wawili. Kwa azuhuri kufika saa tisa inchi nzima ilikuwa giza.

MARKO

Kwa mwisho wa maumivu yake makubwa Mwokozi alilalamika, “Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha?” Watu wengine walisema alikuwa akiita Elia. Mmoja alimpa siki ndani ya sifongo.

Kristo anakufa kwa wazalimu (15:37-41)

Kisha Yesu alitoa sauti kubwa, akatoa roho. Kwa dakika ile ile pazia la hekalu lilipasuliwa vipande viwili toka juu kwenda chini. Akida Mroma alishangaa kabisa, akasema kwamba aliamini Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Wengine wa wanawake waaminifu walio-fuata Yesu walikuwa pale wakitazama kutoka mbali.

Kristo anazikwa ndani ya kaburi la Yosefu (15:42-47)

Yosefu wa Arimatea alifikia Pilato, akaomba ruhusa kuzika mwili wa Mwokozi. Na mapendo aliufunga na marasi na sanda na kumweka ndani ya kaburi lake mwenyewe, akalitia muhuri kwa njia ya kufingirisha jiwe kubwa mbele ya mlango wake. Wanawake wawili wenyenye jina la Maria walikuwa pale, wakaona pahali mwili wake ulipowekwa.

6. UFUFUKO WA MTUMISHI NA KWENDA KWAKE MBINGUNI (Sura 16)

Habari Njema kubwa (16:1-8)

Nyuma ya kushuka kwa jua siku ya sita, wanawake watatu waliokuwa wafuata wa Yesu walinunua manukato, wapate kupakaa mwili wake. Siku ya kwanza ya juma asubui walifikia kaburi waki-fazaika namna gani wataweza kuondosha lile jiwe. Basi waliona limekwisha kuondoshwa! Ndani ya kaburi waliona malaika ali-yeonekana kama kijana ambaye aliwaambia kwamba Yesu atakutana nao katika Galilaya. Wanawake walikimbia wakitetemeka na kushituka sana, wakaogopa kumwambia mtu ye yote habari za maneno yali-yotoke. (Miigo mitatu ya zamani inakosa mashairi 9-20, lakini mashairi haya ni ndani ya miigo yote mingine kwa Kiyunani na ndani ya Biblia ya Kilatin vilevile.)

Kuonekana kwa Yesu nyuma ya ufufuko wake (16:9-13)

Bwana alitokea kwa Maria Magdalene nyuma ya ufufuko wake, lakini wakati Maria alipojulisha wanafunzi wenyenye huzuni habari hizi, hawakumwamini. Bwana Yesu alitokea vilevile kwa wanafunzi wawili kwa njia kwenda Emau (Luka 24:13-31), lakini wanafunzi kwa Yerusalem hawakuamini habari zao vilevile.

Amri kubwa (16:14-18)

Mangaribi siku ya kwanza ya juma ile Yesu alionekana kwa wanafunzi, akawahamakia kwa sababu hawakuamini ushuhuda wa Maria na

MAFUNDISHO JUU YA AGANO JIPYA

wa wale wanafunzi wawili wengine. Kisha aliwaagiza kwenda kuhubiri Habari Njema kwa watu wote, na kuwabatiza wale walioamini. Aliwaambia ya kwamba alama nyingine zitafuatana nao wanaoamini. Alama hizi zilifanyikana kweli ndani ya kitabu cha Matendo.

Kwenda mbinguni (16:19-20)

Siku 40 nyuma ya ufufuko wake, Bwana wetu Yesu alipanda mbinguni, akaketi kwa mkono wa kuume wa Mungu. Wanafunzi walitii agizo lake kwenda kuhubiri habari njema za wokovu kwa njia ya kuamini Kristo tu, alama Bwana alizoahidi zikifuatana na mahubiri yao.

Habari Njema kama alivyoandika LUKA

MWANZO

Mwandishi na Tarehe

Luka, mganga mpendwa aliyesafiri pamoja na Paulo, aliandika Habari Njema yake karibu A.D. 60. Tunafikili alikuwa kwa Kaisaria kwa wakati ule.

Neno kubwa la Luka

Habari Njema ya Luka inaonyesha Bwana Yesu kama Mwana wa watu, Rafiki ya watoza kodi na wenyе zambi, na Mwokozi wa wanadamu. Inaonyesha utu wa Bwana wetu. Tunasoma juu ya mombi yake hapa kupita ndani ya Habari Njema zote nyingine. Tunasoma juu ya huruma yake tena na tena. Labda ni kwa sababu hii habari za wanawake na watoto zinaonekana sana. Habari Njema ya Luka inajulikana vilevile kama Habari Njema inayoeneza habari za wokovu. Tunaona Habari Njema ikihubiriwa kwa *Mataifa*, na Yesu kama Mwokozi wa dunia. Mwishoni tunaona hapa mafundisho mengi kwa wanafunzi wa Bwana, ndani ya maisha ya Bwana wetu mwenyewe na ndani ya mafundisho yake kwa wanafunzi wake kumi na wawili. Ni mafundisho juu ya kujikana mwenyewe na kukuchukua msalaba. Wale wanaosikia na kutii mafundisho haya watabarikiwa sana ndani ya maisha yao.

UMBO LA LUKA

1. Mwanzo (1:1-4)
2. Kuzaliwa na ujana wa Yesu (1:5 – 2:52)
3. Mtangulizi wa Mwana wa watu, ubatizo wake, kizazi chake na kujaribiwa kwake (3:1 – 4:13)
4. Masemo na kazi za Mwana wa watu katika Galilaya (4:14 – 9:50)
5. Utumishi wa Mwokozi toka Galilaya na kupita kwa Pere a hatu kufikia Yerusalem (9:51 – 19:27)
6. Juma la mwisho la Bwana katika Yerusalem na mauti yake (19:28 – 23:49)
7. Kuzikwa, ufufuko, na kwenda mbinguni kwa Kristo (23:50 – 24:53)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

1. MWANZO (1:1-4)

Luka hakuona yeye mwenyewe maneno alioandika juu yao ndani ya Habari Njema yake, lakini aliongozwa na Roho Mtakatifu ndani ya maneno alioandika. Alitumia maandiko ya watu wengine waliokuwa washuhuda wa maneno haya wao wenyewe. Aliandika ili mtu mmoja, jina lake Teofilo, aweze kujua hakika ya maneno yote aliyofundishwa juu ya maisha na kazi ya Bwana Yesu.

2. KUZALIWA NA UJANA WA YESU (1:5 – 2:52)

Tangazo la Gabrieli kwa Zakaria juu ya kuzaliwa kwa Yoane (1:5-25)

Luka alianza na kutupasha kwanza juu ya wazazi wa Yoane, Zakaria na Elisabeti, watu waliopenda Mungu. Siku moja wakati Zakaria alipofanya kazi yake ya kuhani hekaluni, malaika alimfunulia ya kwamba Elisabeti atazaa mwana atakayeitwa Yoane. Mwana huyu atakuwa mtu wa kujulikana, na atakuwa na kazi kubwa, ndiyo kutangulia Masiya (mash. 5-17). Wakati Zakaria alipokuwa na shaka juu ya neno hili, malaika Gabrieli alimwambia ya kwamba hataweza kusema neno kufika siku mtoto atakapozaliwa. Wakati kuhani aliporudi karibu na watu waliongoja inje ya hekalu, aliweza kusema nao kwa njia ya kutumia mikono yake tu. Kama malaika alivyatobiri, Elisabeti alipata mimba, kisha akajificha kwa miezi mitano (mash. 18-25).

Gabrieli anatangaza habari za kuzaliwa kwa Kristo kwa Maria (1:26-38)

Nyuma ya miezi sita malaika alitokea kwa bikira katika Nazareti, jina lake Maria aliyepatana kuwa mke wa Yosefu. Malaika aliahidi Maria ya kwamba atazaa Mwana atakayeitwa Yesu, na ya kwamba atakuwa Masiya ambaye Mungu aliahidi zamani kwamba atamtuma. Wakati Maria alipofazaika kama neno hili litawezekana namna gani malaika alimfahamisha kwamba itakuwa ajabu ya Roho Mtakatifu. Malaika alimjulisha ya kwamba Elisabeti wa jamaa yake alikuwa na mimba ya miezi sita. Maria alinyenyekea Bwana aweze kutimiza ahadi hii ya ajabu.

Maria anafikia Elisabeti (1:39-45)

Neno la namna nyingine lilitokea wakati Maria alipokwenda kuona Elisabeti — mtoto ndani ya tumbo lake aliruka kwa furaha. Halafu Elisabeti alisalimu Maria akimwita “mama ya Bwana wangu”, aki-bariki Maria na Mwana wake asiyezaliwa bado.

Wimbo wa Maria (1:46-56)

Maria alitukuza Bwana kwa maneno ambayo alikwisha kumfanyia,

LUKA

kwa rehema yake kwa watu wote ambao wanamwogopa katika kila kizazi, na kwa uaminifu wake kutimiza ahadi alizotolea Abrahamu na wazao wake. Nyuma ya kushinda pamoja na Elisabeti miezi mitatu, Maria alirudia Nazareti.

Kuzaliwa na kutahiriwa kwa Yoane Mbatizaji (1:57-66)

Kwa wakati wa kutimia Elisabeti alizaa mwana, kama Gabrieli alivyoahidi. Ndugu zao na rafiki zao walifikili mtoto ataitwa Zakaria, lakini Elisabeti aliwajulisha ya kwamba jina lake lilikuwa Yoane. Kwa kuhakikisha masemo yake waliuliza baba ya mtoto. Mara moja nyuma ya kuandika “Yoane” Zakaria aliweza kusema tena.

Wimbo wa sifa wa Zakaria (1:67-80)

Wimbo wa Zakaria ulisifu Mungu kwa maneno aliyokwisha kufanya, kwa kutimiza unabii na kwa uaminifu wake kutimiza ahadi zake. Unaeleza kazi ya Yoane kama mtangulizi wa Mfalme na ali-sawanisha kuja kwa Kristo na mapambazuko (mash. 67-79). Yesu ni mwanga kutoka juu.

Kwa mwisho wa sura hii tunasoma juu ya Yoane akipata nguvu kwa maficho mbele ya kuonekana katikati ya Israeli (sh.80).

Kuzaliwa kwa Yesu (2:1-7)

Yosefu na Maria walikwenda Betelehemu toka Nazareti waandikwe kama Kaisari Augusto alivyoagiza. Hawakuweza kupata pahali pa kupanga nyumbani mwa wageni, hivi walikaa ndani ya zizi. Ni pale Maria alipozaa Mwana wake na kumlalisha ndani ya sanduku ya kulisha nyama.

Utukufu kwa Mungu aliye juu (2:8-20)

Malaika alitangaza habari za kuzaliwa kwa ajabu kwa Yesu kwa wachungaji kondoo shambani. Aliwajulisha ya kwamba watamkuta amefungwa nguo za kitoto na akilala ndani ya sanduku ya kulisha nyama. Gafula jeshi kubwa la malaika walitoa sifa kwa Mungu. Wachungaji walikwenda Betelehemu, wakakuta Yosefu na Maria na Mtoto, wakawaambia habari za malaika, kisha walirudia kundi lao wakisifu na kutukuza Mungu.

Yesu anatahiriwa na kutolewa kwa Bwana hekaluni (2:21-24)

Nyuma ya siku nane mtoto Yesu alitahiriwa na kupewa jina. Halafu wakati alipokuwa na siku 40, Maria alileta hua wawili kwa kusafishwa kwake mwenyewe (ona Walawi 12:1-6). Nyuma ya kusafishwa kwake yeche na Yosefu walileta Yesu kwa hekalu kumtoa kwa Bwana.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Kuabudu na sifa kwa Simioni (2:25-35)

Wakati maneno haya yalipokuwa yakinoteka, Myuda mmoja mwenye kupenda Mungu, jina lake Simioni alikamata Yesu mikononi mwake na kusema wimbo huu mzuri sana, akisifu Mungu kwa sababu Yule ambaye aliahidi kumtuma alikuwa amefika.

Ushuhuda wa Ana kwa Mkombozi wake (2:36-38)

Nabii mke mzee sana alishukuru Bwana vilevile kwa sababu Mkombozi alikuwa amefika. Alipasha habari zake kwa watu waamini-fu wote katika Yerusalem waliokuwa wakingojea ukombozi.

Miaka ya kwanza ya maisha ya Yesu na kula Pasaka mara ya kwanza (2:39-52)

Wakati Yesu alipokwisha kutolewa kwa Bwana, Yosefu na Maria walirudi pamoja naye kwa Nazareti. Pale alipata nguvu katika mwili, akili, na roho (mash. 39-40).

Wakati alipokuwa na miaka 12 alikwenda Yerusalem kula Pasaka mara ya kwanza. Kwa safari ya kurudi hakuonekana katikati ya wasafiri. Wazazi wake walirudia Yerusalem kumtafuta, wakamkuta akiketi hekaluni akisikiliza mafundisho ya walimu na akiulizana nao. Yosefu na Maria hawakufahamu ya kwamba kijana Yesu aliweka kazi ya Baba yake Mungu kwanza ndani ya maisha yake. Hata hivi alikuwa mtoto mwenye kutii nyumbani mwa jamaa, akizidi kuendelea katika akili, na kimo, na roho na maneno yote mengine (mash. 41-52).

3. MTANGULIZI WA MWANA WA WATU, UBATIZO WAKE, KIZAZI CHAKE NA KUJARIBIWA KWAKE (3:1 – 4:13)

Utumishi wa Yoane Mbatizaji (3:1-17)

Luka hakutoa habari za miaka 18 iliyofuata wakati Yesu aliposhinda katika Nazareti kama Mwana wa mseremala, lakini alitupasha juu ya utumishi wa Yoane Mbatizaji, mtangulizi aliyekuja kutayarisha roho za watu kwa kuja kwa Masiya. Habari hizi zilitabiriwa ndani ya unabii wa Isaya. Alibatiza ndani ya Yorodani watu wale waliotubu, lakini alihamakia wale wasiotubu na roho ya kweli, akiwaagiza kuhakikisha toba yao kwa njia ya kugeuza mwenendo wao. Wasipofanya hivi watahukumiwa. Alionyesha tofauti katikati yake na Kristo akieleza ya kwamba ubatizo wake ulikuwa ubatizo wa inje, wa mwili, lakini ubatizo wa Kristo utakuwa wa roho. Alitukuza Bwana kwa njia ya kusema ye ye mwenyewe hakustahili hata kufungua kamba ya viatu vyake.

LUKA

Yoane Mbatizaji anafungwa gerezani (3:18-20)

Nyuma ya miezi 18 Yoane alifungwa na Herode kwa sababu ali-kuwa amehamakia mfalme juu ya kukaa pamoja na mke wa ndugu yake katika uzini.

Ubatizo wa Yesu (3:21-22)

Yesu alianza kazi yake katikati ya watu sasa kwa njia ya kubatizwa ndani ya Yorodani. Kwa wakati huu Roho Mtakatifu alimshukia na Baba yake alitangaza wazi ya kwamba huyu ni *Mwana wake mpendwa*.

Wazazi wa Yesu (3:23-38)

Kusudi la Habari Njema hii ni kuonyesha ya kwamba Yesu ni Mwana wa watu, hivi inapasa kuonyesha ya kwamba alikuwa mzao wa Adamu. Ona shairi 38. Zaidi ya walimu wanafikili ya kwamba watu hawa ni wazazi wa Maria na ya kwamba Heli (sh. 23) alikuwa mkwe wa Yosefu. Yesu alikuwa Mwana wa *hakika* wa Maria, lakini Yosefu alimtendea kama Mwana wake.

Majaribu ya Yesu (4:1-13)

Yesu alionyesha ukamilifu wa roho yake wakati alipojaribiwa na Shetani jangwani. Alimjaribu kwa maneno ya tamaa ya mwili, tamaa ya macho na kiburi cha uzima, maana yake hamu kuwa na uwezo na vitu vya dunia na kukubaliwa na watu kama mtu mkubwa. Ndani ya majaribu matatu yote Shetani alitaja mashairi ya Biblia. Bwana Yesu alishinda majaribu haya kwa njia ya kutumika na Maandiko kwa utaratibu.

4. MASEMO NA KAZI ZA MWANA WA WATU KATIKA GALILAYA (4:14 – 9:50)

Mwanzo wa utumishi wa Yesu (4:14-15)

Nyuma ya habari za shairi 13 Bwana Yesu alitumika katika Yudea (ona Yoane 2-5). Luka anaendelea na habari za utumishi wake katika Galilaya.

Yesu anakataliwa na watu wa Nazareti (4:16-30)

Siku moja wakati Bwana Yesu alipofikia sunagogi katika Nazareti, alisoma Isaya 61:1-2a, kisha alitangaza ya kwamba ye ye ndiye Masiya ambaye Isaya alisema juu yake. Alikuwa amefika kusaidia watu ndani ya mambo makubwa ambayo yanawasumbusha na kuwatesa, na kutangaza mwanzo wa muda mpya (mash. 16-21). Watu walifurahi juu ya mafundisho haya kwanza, lakini wakati alipotabiri ya kwamba

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

watu wa Nazareti na taifa la Israeli watamkataa, akionyesha kwa maficho ya kwamba atakwenda kwa Mataifa, walijaribu kumtupa chini toka ukingo wa kilima! Basi aliondokea Nazareti, na hatusomi ya kwamba alirudia mji ule tena kamwe (mash. 22-30).

Maajabu ya Masiya kuponyesha watu (4:31-41)

Katika Kapernaumu siku ya sabato alitoa pepo mchafu, aliponyesha mama ya mke wa Petro, na watu wengi wengine. Kwa njia hii alionyesha ya kwamba yeze ni Bwana wa pepo wachafu na gonywa. Pepo ambaeo aliwatoa walijua kwamba yeze ni Mwana wa Mungu, lakini Yesu hakuwaruhusu kumshuhudia mbele ya watu. Hakuweza kukubali ushuhuda wa pepo wachafu.

Yesu anahubiri katika Galilaya (4:42-44)

Kesho yake Yesu wakati alipokwenda kwa pahali pasipo watu karibu na Kapernaumu, makutano wakamtafuta na kufika kwake. Wakamsihi asiondokee pahali pale, lakini Yesu alikuwa na kazi katika miji mingine ya Galilaya vilevile, akakwenda zake.

Yesu anaita wavuvi wane (5:1-11)

Akisimama ndani ya chombo cha Petro mbali kidogo na pwani, Yesu alifundisha watu, kisha alifundisha fundi huyu juu ya kuvua samaki, akamwita kuwa mvuvi wa watu. Petro, pamoja na Yakobo na Yoane waliacha vyote, wakamfuata. (Ona vilevile Marko 1:16-17.)

Yesu anasafisha mkoma (5:12-16)

Nyuma ya kuponyesha mwenye kujaa ukoma, Yesu alimwagiza kufika karibu na kuhani na kutoa zawadi iliyoagizwa na sheria, lakini asiwaambie watu wengine habari za ajabu hili. Mkoma hakutii agizo la kunyamaza, akatangaza habari za kuponyeshwa kwake pahali pote hata watu wengi walifika karibu na Yesu kwa kuponyeshwa. Lakini Yesu akajitenga nao, akakwendea pahali pasipo watu kwa maombi.

Yesu anaponyesha mwenye kupooza (5:17-26)

Basi habari za mafundisho na kazi yake zilijulikana katikati ya watu. Siku moja adui zake Wafarisayo na walimu wa sheria walikutana kumwonea makosa, wakamkuta akiponyesha watu wengi. Wanaume wane walileta mwenye kupooza mmoja juu ya kitanda chake kwa nyumba pahali Yesu alipokuwa akiponyesha watu. Kwa sababu ya makutano makubwa hawakuweza kufika karibu naye, basi walimshusha katika matofali ya dari hata alifika katikati ya nyumba, kwa miguu ya Yesu. Yesu akiona imani yao, alisema "Zambi zako zimesamehewa." Masemo haya yalijaza Wafarisayo na waandishi na gazabu. Walisema ni makufuru. Kuhakikisha ya kwamba zambi za

LUKA

mtu huyu zilikuwa zimesamehewa kweli, Bwana alimwagiza kusima-ma na kutembea. Watu walishangaa sana wakati yule aliyekuwa mwenye kupooza mbele alipofanya hivi.

Yesu anaita Matayo, mtoza kodi (5:27-32)

Lawi, aliyeitwa Matayo vilevile, alikuja mara moja wakati Yesu alipomwita, kisha aliita rafiki zake za mbele kwake kwa karamu waweze kukutana na Yesu vilevile. Wakati viongozi vyta dini waliposhitaki Yesu juu ya kula pamoja na wale waliojulikana kama wenyе zambi, Yesu alisema ya kwamba hakuja kuita wenyе haki lakini wenyе zambi kutubu.

Jibu la Yesu juu ya kufunga (5:33-39)

Nyuma yake viongozi vyta dini walishitaki wanafunzi wa Yesu juu ya kutofunga chakula. Yesu aliwajibu ya kwamba hawakuwa na sababu kufunga wakati alipokuwa kwanza pamoja nao, lakini watafunya wakati atakapoondolewa kwao kwa njia ya mauti.

Ndani ya mezali ya mavazi na viriba, Yesu alifundisha ya kwamba haiwezekani kuchanganya muda mpya wa neema na dini ya Wafarisayo isiyokuwa na uzima ndani yake. Desturi zao na kawaida za dini zisizoweza kugeuka hazikupatana na furaha na usitawi wa Wakristo.

Mabishano juu ya kazi za sharti siku ya sabato (6:1-5)

Wafarisayo walishitaki wanafunzi tena, mara hii juu ya kuchuma masuke ya ngano siku ya sabato. Bwana aliwakumbusha ya kwamba Mungu aliruhusu Daudi na watu wake kula mikate ya onyesho hata kama chakula hiki kilikuwa kwa makuhani tu. Mara ile Mungu aligeuza amri hii kidogo kwa sababu mfalme wa kweli wa wakati ule alikataliwa, kama vile Bwana Yesu alivyokataliwa. Vilevile Kristo ni Bwana wa sabato, naye anaweza kutafsiri maana yake ya kweli vizuri zaidi.

Mabishano juu ya kuponyesha wagonjwa siku ya sabato (6:6-11)

Siku ya sabato nytingine, Yesu aliponyesha mtu mwenye mkono wa kupooza. Bwana alionyesha upumbavu wa viongozi ambao walimshitaki juu ya kutenda mema siku ya sabato, wakati wao wenye walipokuwa wakifanya shauri siku ile ile namna gani wataweza kumwua! Lilikuwa kusudi la Mungu kwa sabato kusaidia watu, na wakati tunapofahamu maana yake vizuri, siku ile haituzuizi kutenda kazi za sharti au kazi za rehemaa.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Yesu anatuma wanafunzi kumi na wawili (6:12-16)

Nyuma ya kushinda usiku mzima katika maombi, Yesu alichagua wanafunzi 12. Aliwatura kama watu masikini, si watajiri; wenye njaa, si wenye kushiba; wenye huzuni, si wenye kuchezacheza bule; wenye kuteswa, si wenye kupendwa na watu — kwa ajili ya Mwana wa watu.

Ole juu ya wenye kushiba (6:17-26)

Wakati Yesu alipokuwa akiponyesha wagonjwa alianza kufundisha wanafunzi juu ya kawaida ya ufalme. Alitangaza ole juu ya watu wale waliokuwa na mali nyingi na kushiba na kupendwa na watu wote.

Maisha ya mapendo (6:27-28, 31-36)

Sharti mapendo ya wanafunzi yapite namna ya mapendo ya watu wa dunia wanaopenda tu watu ambao watawapenda, wanaotenda mema kwa wale ambao waliwatendea mema, wanaokopesha kwa kupata faida. Sharti mapendo ya wanafunzi yawe namna ya mapendo ya Mungu ambaye anapenda watu wote bila tofauti.

Shavu la pili na kilometre ya pili (6:29-30)

Bwana aliwaagiza kupenda watu na mapendo namna nyingine watu wasiyoona mbele — mapendo kwa adui na watukanaji na watesaji. Wale wanaopenda hivi hawarudishi mabaya kwa mabaya, wanatoa kupita ambayo watu wanataka kwao na hawatazamii zawabu. Wanafanya watu wengine namna wanavyotaka kufanyiwa.

Musihukumu (6:37-42)

Mapendo namna hii yana rehema, hayahukumu, yanaseamehe na yana ukarimu. Yesu alieleza ya kwamba wanafunzi watakuwa baraka kwa watu wengine kwa kipimo cha hali ya roho yao wenye. Hawataweza kufikisha watu karibu na Mungu kupita kipimo wao wenye walichofika, wala kuwfundisha maneno ambayo hawajui wao wenye. Hawataweza kuona wanafunzi wao kuendelea kupita wao wenye. Na hawataweza kusaidia wanafunzi wao na mashaka wasiyoshinda ndani ya maisha yao wenye.

Namna gani kutambua nabii la kweli (6:43-45)

Watu wanaweza kuzaa matunda kupatana na roho zao tu. Namna walivyo rohoni mwao ni neno kubwa kupita neno lo lote wanalo sema au kutenda.

Wajengaji wapumbavu na wenye akili (6:46-49)

Ni upumbavu kuita Yesu *Bwana* bila kumtii. Mwenye akili anakuja karibu na Kristo na kusikia masemo yake, lakini zaidi ya ile anayatii

LUKA

vilevile. Anaweza kusimama imara ndani ya tufani za maisha haya. Mpumbavu anasikia mafundisho ya Kristo juu ya kumfuata lakini anataka kuishi namna yeye mwenyewe anavyochagua. Wakati anapopata matata hana msingi wa nguvu, na hata *roho* yake ikipona, labda faida ya *maisha* yake itapotea.

Yesu anaponyesha mtumwa wa akida (7:1-10)

Akida mmoja, Mtaifa, aliyependwa na kuheshimiwa na Wayuda, aliomba Wayuda kuomba Yesu kusaidia mtumishi wake mgonjwa. Wakati Yesu alipokuwa njiani kwenda nyumba yake, akida alituma habari kwamba Yesu hakuhitaji kufika kwake yeye mwenyewe kwa sababu aliweza kuponyesha mgonjwa kwa njia ya kusema neno tu. Yesu alishangaa kwa sababu hakukuta imani kubwa namna hii katikati ya Wayuda. Na kweli mtumishi aliponyeshwa na Bwana toka mbali.

Yesu anafufua mwana wa mjane wa Naina (7:11-17)

Wakati Yesu alipokaribia mji wa Naina alikutana na watu walio-kwenda kuzika mwana wa pekee wa mjane. Bwana aliagiza kijana kusimama, uzima uliingia mwili wake tena na Bwana alimrudisha kwa mama yake. Watu walishangaa sana, wakatangaza habari hizi pahali pote katika inchi kandokando.

Yesu anasaidia roho ya Yoane Mbatizaji (7:18-23)

Wakati Yoane Mbatizaji aliyekuwa gerezani aliposikia habari za maajabu yaliyofanywa na Yesu alituma wajumbe wawili kuuliza kama Yesu alikuwa Masiya kweli. Rohoni mwake alifikili, “Kama huyu ni Masiya, kwa nini mimi ninateswa gerezani?” Yesu alituma wajumbe tena kwake wamwambie ya kwamba alikuwa akifanya maajabu yali-yotabiriwa kwamba Masiya atayafanya. Aliongeza neno kusaidia imani ya Yoane, ndiyo ya kwamba kuna baraka kwa wale wasio na shaka juu ya Yesu.

Ushuhuda wa Yesu juu ya Yoane Mbatizaji (7:24-35)

Kisha Yesu alisifu mtangulizi wake, akisema kwamba Yoane hakuwa mtu wa kugeukageuka aliyekaa ndani ya nyumba za wafalme, lakini alikuwa mkubwa kupita manabii wote kwa sababu alikuwa mjumbe wa Masiya. Watu walikubali haki ya Mungu kwa njia ya kupokea ubatizo wa Yoane, lakini viongozi vyao walikataa shauri la Mungu kwa njia ya kukataa mjumbe wake (mash. 24-30).

Bwana aliendelea kusema kwamba haikuwezekana kupendeza Wayuda wa wakati ule. Yoane Mbatizaji alifika katikati yao, mwenye kujikana mwenyewe, wakasema ana pepo. Yesu alifika akikula na kunywa kama watu wote wanavyofanya, wakamwita mlafi na mnywaji.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Mashairi yanayofuata yanaonyesha kwamba wanafunzi wake walisibitisha haki ya masemo yake na hekima yake (mash. 31-35).

Yesu anasamehe mwanamke mwenye zambi (7:36-50)

Wakati Yesu alipofikia nyumba ya Simoni, Mfarisayo, mwanamke mwenye zambi alikuja na kunawa miguu yake na nyole zake, akaibusu na kuipakaa na mafuta. Simoni alisema ya kwamba ingalipasa nabii wa kweli kukaa mbali na wenyenye zambi. Bwana alimwambia habari za watu wawili wenye deni walipotenza mali yao yote lakini waliosamehewa deni zao. Simoni alikubali ya kwamba yule aliyesamehewa deni kubwa zaidi angependa mkopeshaji kupita yule mwininge. Kwa njia ya kusema hivi alijihukumu mwenyewe. Hakutendea Bwana na adabu wakati alipofika kwake, lakini maneno ambayo mwanamke huyu alifanya yalionyesha mapendo yake makubwa wazi. Yesu alisema mbele ya watu wote ya kwamba alisamehewa zambi zake. Wakati wengine walipokuwa na shaka rohoni mwao juu ya uwezo wake kusamehe zambi, alisema na mwanamke tena ya kwamba aliokolewa kweli, akamruhusu kwenda zake na salama.

Wanawake wengi walitumikia Yesu (8:1-3)

Wakati Bwana alipoendelea na kazi yake katika Galilaya, akihubiri habari njema ya ufalme, wanawake waliosaidiwa naye mbele walitumikia.

Mfano wa udongo mbalimbali (8:4-15)

Mfano huu unafundisha ya kwamba roho za watu zinaweza kusawanishwa na udongo namna ine. Watu namna tatu wanakiri ya kwamba wanaamini Habari Njema, lakini si kweli. Watu wenye roho namna ya udongo wa ine wana imani ya kweli. Sharti tuangalie sana namna gani tunasikia na kutii Neno la Mungu.

Mfano wa taa inayowaka (8:16-18)

Maana ya mfano huu ni ya kwamba haifai wanafunzi kuacha kazi yao ya biashara (chombo) au uvivu (kitanda) kuwazuiza ndani ya kazi ya kutangaza Habari Njema. Itaonekana wazi kama wasipotii agizo hili. Lakini kama tutikangaza kweli ya Mungu kwa watu wengine, Mungu atatufunulia kweli nyingine tusizojuwa mbele. Kama tusipotumika na kweli tulio nayo tutapoteza.

Ndugu za kweli za Yesu (8:19-21)

Saa mama ya Yesu na ndugu zake walipomfikia, alipata njia kueleza ya kwamba ndugu zake za kweli si wale waliozaliwa ndani ya jamaa moja naye, lakini wale wanaotii Neno la Mungu.

LUKA

Bwana wa upopo na mawimbi (8:22-25)

Ndani ya baki la sura hii, tunaona Yesu kama Bwana wa tufani na mawimbi, pepo wachafu, ugonjwa, na mauti. Zote zinamtii — watu tu wanamwasi. Alituliza tufani juu ya Bahari ya Galilaya, na alituliza woga ndani ya roho za wanafunzi.

Pepo wachafu wanaotii, na nguruwe (8:26-39)

Yesu alitoa pepo wachafu waliokuwa ndani ya Mgerase mmoja na kuwaruhusu kuingia ndani ya kundi la nguruwe. Nguruwe hawa wali-jua wenyewe kwa njia ya kutelemuka kilima mbio na kuzama bahari-ni. Wagerase waliomba Kristo kuondoka kwao naye alifanya hivi, lakini aliacha pale Mgerase mmoja aliyekwisha kuokolewa aweze kuwa mshuhuda wake.

Umri wa miaka 12 na miaka 12 ya mateso (8:40-56)

Makutano walisonga na kuzuiza Mwokozi wakati alipokuwa njiani kwenda karibu na binti ya Yairo. Mwanamke mmoja mwenye taabu ya kutoa damu kwa miaka 12 alifika karibu naye, akagusa upindo wa nguo yake, akaponyeshwa mara moja. Alijaribu kwenda zake kwa siri, lakini Yesu alimwita aweze kukiri mbele ya watu habari zilizokwisha kufanyika ndani ya mwili wake, kisha alimsifu kwa imani yake, akamruhusu kwenda zake na salama (mash. 40-48). Kwa saa ile mjumbe alifika na kumwambia Mwokozi kwamba hakuhitaji kufikia nyumba ya Yairo kwa sababu binti yake alikuwa amekufa. Lakini Bwana alikwenda kwake hata hivi, akafufua binti na kuagiza wazazi wake wasitangaze habari za ajabu hili. Hakuweka roho juu ya sifa ya watu (mash. 49-56).

Yesu anatuma wanafunzi kumi na wawili (9:1-6)

Wakati Kristo alipoanza mwaka wa tatu wa utumishi wake katikati ya watu, alituma wanafunzi 12 kuhubiri na kuponyesha wagonjwa. Iliwapasa kumtegemea ye ye kuwapa vitu walivyohitaji, kuishi maisha isiyi ya anasa, kukaa nyumbani mwa watu wo wote ambao wal-wakaribisha bila kutafuta nyumba nzuri kupita kukaa ndani yake, na kutoka mji wo wote pahali watu walipokataa mahubiri yao ya Habari Njema.

Hata kwa wakati wa sasa inapasa watumishi wa Mungu kuishi kwa imani, kuishi maisha bila mapambo mengi, bila kutafuta pahali pazuri zaidi kwa kupanga, na wakienda pahali gani Mungu anapotumika ndani ya roho za watu.

Uuaji wa Yoane Mbatizaji na Herode (9:7-9)

Herode alifazaika wakati aliposikia ya kwamba mtu mmoja alikuwa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

akifanya maajabu makubwa. Alijua hakuwa Yoane Mbatizaji, na alita-ka kukutana na mwenye kutenda maajabu haya.

Huruma ya Kristo (9:10-17)

Nyuma ya kusikiliza wanafunzi wakitoa habari za safari na mahubiri yao, Bwana aliwapeleka kwa pahali pa jangwa, lakini makutano waliwafuata, hivi hawakuwa na njia tena kupata pumziko. Yesu alihubiri kwa makutano, aliponyesha wagonjwa, kisha alikulisha wanaume 5,000, pamoja na wanawake na watoto, akiwa na mikate mitano na samaki wawili tu. Habari hizi zinaonyesha ya kwamba anaweza kuzidisha vyo vyote ambavyo tunamtolea na kusaidia navyo roho za watu wengi.

Kukiri kwa Petro (9:18-21)

Labda Mungu alitumia ajabu hili kuonyeshea Petro ya kwamba Yesu ni Masiya, Mwana wa Mungu aliye hai. Wanafunzi walijua sasa ya kwamba hakuwa mtu mkubwa tu; alikuwa namna nyingine — hakuna mwingine kama yeye. Lakini aliwaonya wasitangaze habari hizi kwa watu wengine, kwani watu wengi bila imani ya kweli wakianza kumfuata wangaliweza kumzuiza asiendee msalaba.

Yesu anatabiri mauti na ufulufuko wake (9:22-27)

Sasa wanafunzi walijifunza ya kwamba Yesu atateswa, atakataliwa, kuuawa, na kufufuka tena. Aliwaita kumfuata wakijikana wenywewe, wakibeba msalaba, na kujitoo kwa yeye. Mwishoni aliahidi ya kwamba wakati wa kuja watapewa heshima ya kutawala pamoja naye. Shairi 27 linasema juu ya Petro, Yakobo na Yoane. Lilitimizwa ndani ya mashairi 28-36.

Kristo anageuzwa sura (9:28-36)

Saa hii Petro, Yakobo, na Yoane waliona mfano mdogo wa utukufu wa wakati wa kuja saa Kristo atakapotawala kwa miaka elfu moja. Kwa njia ya kungaa kwake anaficha wote wengine. Yeye ni wa kwanza katika yote na Baba alikiri wazi ya kwamba huyu ni Mwana wake mpendwa.

Hitaji kwa maombi na kufunga (9:37-42)

Nyuma ya matukio kwa kilima Yesu alikutana na kijana mwenye pepo. Kijana huyu alitaabishwa sana lakini ilikuwa imeshinda wanafunzi kumsaidia. Yesu aliwahamakia juu ya neno hili, kisha alitoa pepo na kurudisha mtoto kwa baba yake.

Yesu anatabiri tena ya kwamba atakufa na kufufuliwa (9:43-50)

Yesu aliwaambia wanafunzi wake tena ya kwamba mauti yake

LUKA

yalikaribia, lakini wanafunzi hawakufahamu neno hili na waliogopa kumwuliza. Wakati walipoanza kubishana kama nani katikati yao alikuwa mkubwa zaidi, aliwafundisha ya kwamba ukubwa wa kweli ndio kufungana na wale walio wadogo zaidi katikati ya watoto wa Mungu. Aliwaambia vilevile ya kwamba ndani ya kazi ya Mungu mtu ye yote asiyeshindana na Kristo ni kwa upande wake.

5. UTUMISHI WA MWOKOZI TOKA GALILAYA NA KUPITA KWA PEREA HATA KUFIKIA YERUSALEMA (9:51 – 19:27)

Yesu anahamakia roho ya kutovumilia (9:51-56)

Yesu alihamakia wanafunzi juu ya roho yao ya kutovumilia kwa sababu walitaka kuharibu kijiji cha *Wasamaria* waliokataa kumpokea kwa sababu alikuwa akikwenda Yerusalem (mji wa *Wayuda*). Lakini Yesu hakuja kuharibu lakini kuokoa.

Jaribu kwa wale waliotaka kuwa wanafunzi (9:57-62)

Watu watatu walisema wao ni tayari kufuata Bwana kama wanafunzi wake, lakini hawakuwa tayari kujikatalia wenyewe. Wa kwanza hakuwa tayari kuachana na hali njema ya maisha yake. Wa pili aliweka mahitaji ya jamaa yake mbele ya mwito wa Kristo. Wa tatu aliweka roho juu ya kuagana na watu wa nyumba yake (desturi iliyohitaji siku nyingi kwa wakati ule) mbele ya kutii Bwana mara moja na katika maneno yote. Mtu yule alitazama nyuma wakati alipokwisha kuweka mkono wake juu ya jembe la kukokotwa.

Yesu anatuma watu makumi saba (10:1-12)

Mbele Bwana alituma wanafunzi 12 kwa upande wa kaskazini. Sasa alituma watu 70 kwa upande wa kusini kwa njia ambayo ye ye mwenyewe aliyokuwa akifuata kwa safari yake kwenda Yerusalem. Ujumbe wao ulikuwa kwa muda ule tu, lakini mengi ya maneno ambayo Bwana aliwaagiza yana faida hata kwa wakati wa sasa. Yanafuatana na maagizo yake kwa wanafunzi 12 katika 9:1-5.

Kukataa na kupokea (10:13-16)

Yesu alitangaza hukumu juu ya Korazini, Betesaida, na Kapernaumu, miji mitatu ya Galilaya, kwa sababu hawakupokea ma-fundisho yake. Alisema kama watu wa Tiro na Sidona wangalibarikiwa kama wao, wangalitibu katika gunia na majivu.

Watu makumi saba wanarudi na furaha (10:17-20)

Watu 70 walirudi na furaha nyingi — hata pepo wachafu walikuwa wamewatii! Labda jibu la Bwana lilikuwa onyo wasijivune, au alitaka

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kusema baraka waliyoona ilikuwa mfano wa Shetani atakayeanguka toka mbingu kwa wakati wa kuja. Alisema nao ya kwamba *hawataku-fa kufika wakati kazi yao itakapokwisha*. Lakini haifai wafurahi kwa sababu pepo wachafu waliwatii, lakini kwa sababu majina yao yame-andikwa katika mbingu.

Baba na Mwana (10:21-24)

Bwana Yesu alifurahi kwa sababu wanafunzi wake hawakuwa kama watu wenye elimu wa dunia, lakini kama watoto wachanga. Baba alikuwa amempa vitu vyote, naye alifunua Baba hata kama hakuna mtu anayeweza kumjua yeye Mwana. Aliwaambia wanafunzi ya kwamba walikuwa wenye heri kupita watu ambao waliwatangulia kwa sababu waliishi kwa wakati Masiya alipokuwa duniani.

Mfano wa Msamaria Mwema (10:25-37)

Wakati mwana-sheria alipouliza namna gani aliweza kuriti uzima wa milele, Yesu alisema naye kupenda Mungu na roho yake yote na kupenda jirani yake namna alivyojipenda mwenyewe. Akijaribu kujionyesha kuwa mwenye haki, mwana-sheria aliuliza, “Na jirani yangu ni nani?” Kwa kujibu ulizo hili, Bwana Yesu alimwambia mfano wa Msamaria Mwema. Msamaria huyu alifikili juu ya Myuda mwenye hitaji kama jirani yake. Hivi kwa mwana-sheria huyu, Myuda, mtu ye yote mwenye hitaji alikuwa jirani yake.

Maria na Marata waliabudu na kutumikia Yesu (10:38-42)

Siku moja wakati Bwana alipofikia nyumba ya Marata kwa Betania Maria aliketi kwa miguu yake na kusikia Neno lake, lakini Marata alisumbuka na kazi ya kutayarisha chakula ndani ya mafika. Bwana Yesu hakuhamakia Maria kwa sababu hakusaidia ndugu yake lakini alimsifu kwa sababu alichagua neno lililokuwa na faida zaidi. Ali-kemea Marata kwa sababu alisumbuka zaidi.

Mfano wa ombi zuri (11:1-8)

Bwana alitoa mfano huu wakati mwanafunzi mmoja alipomwomba kuwafundisha kuomba. Haifai kusema tu maneno ya ombi hili tena na tena. Bwana alitaka tu kuonyesha maneno gani inatupasa kuomba juu yao.

Kudumu katika maombi (11:9-13)

Kisha alipasha habari za mtu mmoja asiyekuwa na vyakula kulisha rafiki ambaye alimfikia usiku. Mtu huyu alipata vitu alivyohitaji kwa sababu alikaa kuombaomba. Inatupasa sisi vilevile kudumu katika maombi, kutafuta na kupiga hodi. Mungu hatatupa sisi kamwe kitu kisicho kizuri na kwa baraka yetu. Atatupa sisi neno tunalohitaji zaidi — uwezo wa Roho Mtakatifu.

LUKA

Matukano ya Roho Mtakatifu (11:14-23)

Wakati Yesu aliposaidia bubu kuweza kusema tena kwa njia ya kutoa pepo mchafu ndani yake, watu wengine walisema alifanya ajabu hili kwa uwezo wa Belzebuli, mkubwa wa pepo wachafu. Wengine waliomba kwake alama toka mbinguni. Ndani ya mashairi 17-26 Bwana Yesu alijibu mashitaki yao juu ya kufanya ajabu kwa uwezo wa Belzebuli, na ndani ya shairi 29 alijibu ombi lao kwa alama. Kama Yesu akifukuza pepo wachafu kwa uwezo wa Belzebuli, Belzebuli alikuwa akiharibu kazi yake mwenyewe. Vilevile kwa njia ya kuhukumu Yesu juu ya neno hili walihukumu Wayuda wengine waliota pepo. Lakini Yesu alikuwa akitoa pepo wachafu kwa kidole cha Mungu, maana yake kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, na neno hili lilionyesha wazi ya kwamba ufalme wa Mungu umekuja kwao. Kufika wakati ule Shetani alitawala watu wote, lakini sasa Bwana Yesu alikuwa ameshinda Shetani na kufungua wafungwa wake. Wenye kushitaki Kristo hawakuwa *pamoja* naye, hivi walishindana naye.

Kuna zambi tatu (labda hata kupita) zisizoweza kusamehewa: kutukana Roho Mtakatifu; ukafiri; na kufa bila kuamini Kristo.

Mtu aliyekuwa mwenye pepo wachafu mbele (11:24-26)

Taifa la Wayuda walikuwa na pepo mbaya ya kuabudu sanamu mbele. Lakini wakati walipokuwa wafungwa katika Misri, pepo huu aliwaacha. Halafu taifa lilikuwa kama nyumba iliyofagiwa na kupambwa, lakini walikataa kuruhusu Bwana Yesu kuingia na kupanga pale. Hivi aliwaonya ya kwamba kwa wakati wa kuja watafungwa na namna ya kuabudu sanamu hata mbaya kupita. Alikuwa akisema juu ya mpinga Kristo ambaye watamwabudu kwa wakati wa kuja. Kwa zambi hii wataazibiwa hata zaidi kupita azabu yo yote ambayo taifa waliipata mbele.

Baraka ya Yesu kwa wale wanaosikia na kushika Neno la Mungu (11:27-28)

Mwanamke mmoja tusiyejua jina lake alibariki Maria kwa sababu alikuwa mama ya Yesu, lakini Yesu alisema mtu yule anayesikia na kushika Neno la Mungu ni heri zaidi.

Watu wanaomba alama (11:29-32)

Ndani ya shairi 16 watu walitaka kupewa alama, lakini sasa Yesu alisema ya kwamba hawatapewa alama ila moja tu, ndiyo alama ya Yona. Alikuwa akisema juu ya ufufuko wake mwenyewe. Kwa sababu ye ye ni mkubwa kupita Solomono na mkubwa kupita Yona, watu wa wakati Yesu alipokuwa duniani walibarikiwa kupita malkia ya Sheba na watu wa Ninawe, na watahukumiwa kupita wao vilevile.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Taa ya mwili (11:33-36)

Kisha Yesu alikumbusha wasikiaji wake ya kwamba hakuna mtu anayeweka taa inayowaka kwa pahali pa kufichwa au chini ya kitunga. Sivyo; anaiweka juu ya kinara pahali inapoweza kutoa nuru kwa watu wote wanaoingia nyumba. Ndani ya mfano huu Mungu ndiye aliywasha taa. Kwa njia ya Yesu na kazi yake aliletu nuru kwa giza la dunia hii. Kama mtu akikataa kuona nuru, hili si kosa la Mungu (sh.33). Jicho la mtu likiwa safi, maana kama akiwa na hamu kujuu kweli ya Mungu, Mungu ataifunua kwake. Kama kusudi lake si safi atakuwa kama kipofu kwa maneno ya kweli. Yesu anaonya wasikiaji wake kuangalia nuru yao isigeuke giza. Aliwaambia ya kwamba mtu akijitoa mzima kwa Bwana, Nuru ya dunia, roho yake itakuwa nuru kabisa kama vile mwili wake unavyopata nuru wakati anapoketi kwa nuru ya taa (mash. 34-36).

Yesu anasema juu ya Wafarisayo (11:37-44)

Wakati Mfarisayo mmoja aliposhangaa kwa sababu Bwana haku-nawa mbele ya kula chakula, Bwana alihamakia Wafarisayo juu ya choyo, wivu, uzalimu, ukosefu wa mapendo kwa Mungu, kiburi, na ubovu rohoni.

Yesu analaumu Wafarisayo (11:45-54)

Wakati mwana-sheria mmoja aliposhitaki Bwana juu ya kuzarau wana-sheria vilevile, Yesu aliendelea kutaja zambi za wana-sheria — kama kutesa watu kwa njia ya kuwatolea maagizo wagumu wasi-yoweza kutii; kuua watumishi wa Mungu kwa udanganyifu; kunyima watu Neno la Mungu (mash.45-52). Wafarisayo na walimu wa sheria walikasirika juu ya mashitaki ya waziwazi ya Bwana, wakaanza kumsonga kwa nguvu na kuzidi kujaribu kumwangusha ndani ya mase-mo yake wapate njia kumshitaki (mash. 53-54).

Kuogopa Mungu, si watu (12:1-12)

Bwana alitumia maneno haya yaliyokwisha kutokea kuonya wana-funzi wake juu ya chachu (udanganyifu) ya Wafarisayo. Aliwaambia ya kwamba maneno yote waliyokwisha kufanya katika giza yatafunuli-wa, na ya kwamba kweli ya Mungu itashinda. Haifai wanafunzi wagoope mauti ya mwili (kuuawa na Wafarisayo); iliwapasa kuogopa Mungu anayechunga hata ndege lakini zaidi sana watumishi wake. Watu wote ambao wanamkiri kwa wakati wa sasa Bwana atawakiri mbele ya malaika za Mungu, lakini atakana wale ambao wanamkana sasa, na wale wanaotukana Roho Mtakatifu (ndilo neno Wayuda wengine walilokwisha kufanya mbele, 11:15) hawatasamehewa kamwe. Wanafunzi hawahitaji kujitayarisha mbele kwa kujisimamia

LUKA

mbele ya adui; Roho Mtakatifu atawafundisha saa yenye nini itawa-pasa kusema.

Mfano wa tajiri mpumbavu (12:13-21)

Mtu mmoja wa makutano aliomba Bwana kukata maneno katikati yake na ndugu yake juu ya uriti. Lakini Yesu alikuwa na kazi kubwa kupita, hivi alionya mtu huyu juu ya choyo kwa njia ya mfano huu wa tajiri mpumbavu. Mtu yule alivuna vyakula vingi toka shamba lake, hivi alifanya shauri kujenga gala nyingine, akiwaza ya kwamba nyuma yake hatahitaji kutumika kazi tena. Mungu alimjulisha ya kwamba atakufa usiku ule ule na kuacha mali yake yote. Bwana aliongeza kusema ya kwamba ingalikuwa vizuri kupita kwa mtu huyu kuwa na utajiri kwa Mungu.

Bwana ataweka tayari yanayohitajiwa na watumishi wake (12:22-34)

Inapasa wanafunzi kuishi bila masumbuko kwani hawajui nini ita-tokea, hivi haiwezekani kwao kuweka tayari kwa mahitaji yao kwa wakati wa kuja wala hawahitaji kufanya hivi. Kama wakiweka Bwana na kazi yake kwanza yeche atawapa vitu wanavyohitaji nao hawatakosa kamwe kuwa na vyakula na mavazi ya kutosha. Wanajua ya kwamba watariti ufalme, hivi hawahitaji kusumbuka juu ya njia ambayo itawafikisha kule. Lakini ni safari ndefu, hivi haifai wabebi vitu vingi pamoja nao!

Moyo wa mtu ni pahali alipoweka hazina yake. Ni mbinguni, au ni ndani ya banki inayoweza kuharibika.

Hakuna mtu anayejua siku wala saa (12:35-40)

Sharti waishi kila siku wakitazamia na kungojea kurudi kwa Bwana kwani atakuja kwa wakati wasipofikili na itakuwa faida kwao kama akiwakuta wakimngoeja.

Mwito kwa utumishi mwaminifu (12:41-48)

Mafundisho ya mash. 35-40 yalikuwa kwa watu wote walio watumihi wa Mungu. Wakati Bwana atakapokuja na kukuta mmoja wa watumwa wake akiweka roho kabisa juu ya hali ya roho ya wanaume na wanawake, atampa mwanafunzi huyu zawabu kubwa. Kama mtu mwingine akijionyesha kuwa mtumishi wake, lakini anaibia watu wa Mungu na kuwatendea mabaya na kuishi katika anasa, yeche mwenye ataazibiwa pamoja na wasioamini wote wengine. Mtu mwenye mapendeleo makubwa anaagizwa maneno makubwa vilevile. Kuitakuwa na zawabu za kipimo mbalimbali mbinguni na azabu ya kipimo mbalibali katika Hadeze.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Kristo analeta matengano (12:49-53)

Kuja kwa Kristo kulileta matengano, magomvi, mateso, na kumwangika kwa damu. Yeye mwenyewe atabatizwa katika mauti juu ya msalaba, na alisongwa sana kumaliza kazi iliyohitajiwa kwa wokovu wa watu. Wanafunzi wafahamu ya kwamba kutakuwa na matengano nyumbani mwao kwa sababu walifuata Kristo.

Kutambua uso wa mbingu (12:54-59)

Wasioamini waliweza kutabiri kama jua litawaka au kama kutakuwa na tufani, lakini iliwashinda kutambua maana kubwa ya maneno yaliyokuwa yaktitea duniani. Kama wangaliyahafamu kama wangalipatanishwa na Mungu mara moja. Ilikuwa lazima kwao kutubu. Kama wasipofanya hivi watapotea kwa milele.

Yesu anahubiri juu ya toba (13:1-5)

Yesu aliendelea kufundisha juu ya toba. Watu walikuwa wameopgeshwa sana na maneno mabaya mawili yaliyotokea katikati yao kwa wakati ule. Herode alikuwa ameua Wagalilaya wengine, na watu 18 waliuawa wakati mnara wa Siloamu ulipowaangukia. Yesu alionya watu ya kwamba wao wote watapotea kwa maneno ya roho kama wasipotubu, kama vile miili ya watu hawa iliangamia.

Mfano wa mtini usio na matunda (13:6-9)

Ndani ya mfano huu mtini ulikuwa mfano wa Israeli, na shamba la mizabibu lilikuwa mfano wa inchi ya Palestina. Wakati mti usipozaa matunda kwa miaka mitatu (muda wa utumishi wa Bwana Yesu katikati ya watu), mwenye mtini (Mungu) aliagiza ukatwe. Lakini mlimaiji (Kristo au Roho Mtakatifu) aliomba mti uachwe kwa mwaka mmoja mwingine (labda muda kufika mauti ya Stefano). Kama hata kwa mwisho wa wakati ule matunda yasipoonekana, ukatwe basi. Neno hili lilitokea kweli — Yerusalem uliharibiwa na watu walismbazwa.

Yesu anaponyesha mwanamke siku ya sabato (13:10-17)

Mkubwa wa sunagogi alikasirika wakati Yesu alipoponyesha mwanamke mwenye kukunjama siku ya sabato. Bwana alikumbusha yule mdanganyifu ya kwamba aliweza kuwapa nyama zake maji siku ya sabato. Basi kwa nini ilikuwa vibaya kwa Bwana kuponyesha mwanamke Myuda mwenye imani siku ile? Halafu wote walioshindana naye walipata haya, lakini makutano ya watu walifurahi.

Kama yule mdanganyifu angalikuwa na ugonjwa yeche mwenyewe kama angalifurahi kuponyeshwa siku yo yote, hata siku ya sabato!

Mfano wa mbegu ya haradali (13:18-19)

LUKA

Bwana alisawanisha ufalme wa Mungu na mbegu ya haradali ili-yoota kupita kipimo na kugeuka mti pahali ndege walipopanga na kujenga vioto vyao. Vivyo hivyo jamii ya Wakristo ilikaa kuongezeka na watu wengi walifurahi kuingia hata iligeuka pahali pa mafundisho na matendo maovu mengi.

Mfano wa chachu (13:20-21)

Yesu alisawanisha ufalme wa Mungu na chachu vilevile ambayo mwanamke alificha ndani ya unga. Vivyo hivyo mafundisho maovu yalifichwa ndani ya chakula cha roho cha watu wa Mungu na kuchafua mafundisho ya kweli ya Mungu.

Njia mbili (13:22-24)

Wakati Yesu alipokuwa akikwenda Yerusalem, mtu mmoja alimwuliza kama watu wachache tu wataokolewa. Bwana alijibu ulizo hili na agizo kuweka roho sana juu ya kuingia katika mlango mwebamba.

Wale wasio Wakristo wa kweli (13:25-30)

Siku nyingine watu hawataweza kuingia kwa mlango ule kwani saa imepita. Watu watajaribu kuingia, wakisema wameshiriki na Kristo, lakini yeche atasema wao ni wenye kufanya uzalimu. Wayuda wasioamini wataona toka mbali tu wazee wakuu wa zamani wenye hesima katika ufalme, lakini watu wa mataifa walioamini watafurahi na baraka za ajabu za ufalme. Hivi wale walio wa kwanza watakuwa wa mwisho na walio wa mwisho watakuwa wa kwanza.

Shauri la Herode (13:31-33)

Wengine wa Wafarisayo walisema na Yesu (labda kwa udanganyifu) vizuri aondoke pale kwa sababu Herode alikusudi kumwua. Bwana aliwaambia kujulisha mbweha huyu ya kwamba ataendelea na kazi yake kwa wakati, kisha ataitimiza siku ya tatu wakati atakapouawa kwa Yerusalem, ndio mji uliojulikana kwa sababu ya kuua manabii wa Mungu.

Mapendo ya Yesu kwa Yerusalem (13:34-35)

Nyuma ya kusema maneno haya juu ya Yerusalem, Yesu aligeuka na kutoa machozi. Alitaka kuuachilia, lakini sasa hautakuwa na njia tena kuepuka hukumu. Hekalu na inchi zitakuwa ukiwa kufika saa ya kurudi kwa Mfalme wakati atakapokuja mara ya pili.

Yesu anaponyesha mtu siku ya sabato (14:1-6)

Nyumbani mwa Mfarisayo mmoja Bwana aliponyesha mtu siku ya sabato. Akijua ya kwamba wana-sheria na Wafarisayo watamshitaki

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

juu ya neno hili, Yesu aliwakumbusha ya kwamba wangeondosha ngombe yao shimonii siku ya sabato. Kuzidi sana ingalipasa kuwa na huruma kwa mgonjwa huyu.

Mafundisho ya Yesu juu ya unyenyekevu na kukaribisha wageni (14:7-14)

Akiona ya kwamba wageni walijaribu sana kukaa kwa pahali pa heshima zaidi mezani, Kristo aliwaonya ya kwamba haifai kujitafutia ukubwa. Alisema vizuri wakamate pahali pa chini kufika wakati watakapoitwa kuketi pahali pa heshima kupita (mash. 7-11). Kisha aligeuka kwa mwenye nyumba, Mfarisayo, akamjulisha kawaida ya ufalme kwa kukaribisha wageni nyumbani: ni kuita wale wasioweza kukuuta tena — watu masikini, vilema, viwete, vipofu; atapata malipo kwa wakati wa ufufuko (mash. 12-14).

Mfano wa karamu ya ndoa (14:15-24)

Wakati mmoja wa wageni kwa karamu aliposema ingalikuwa vizuri sana kushiriki ndani ya baraka za ufalme, Yesu alijibu na mfano kuonyesha kwamba watu wengi wanaitwa kuingia ufalme lakini wanakataa wakitoa uzuru wa bule namna namna. Basi kama wale walioitwa kwanza (Wayuda) wakikataa kuja, Mungu atasukuma watu wengine (Mataifa) kuingia.

Garama ya kufuata Yesu (14:25-33)

Bwana aliona watu wengi wakimfuata, hivi alianza kuwatolea mafundisho magumu juu ya kumfuata. Lazima mtu ye yote ambaye anamfuata ampende kupita wote. Sharti mwanafunzi wa kweli abebe msalaba wake (wa Kristo) na kumfuata. Kisha alionyesha kwa njia ya mifano miwili ya kwamba mbele ya kuanza kumfuata inapasa mtu kufahamu kwamba bei yake itakuwa nini. Mifano hii ilikuwa juu ya mtu anayejenga mnara, na mfalme anayekwenda na askari wachache kupigana na adui wenye askari wengi. Sharti mwanafunzi aache vyote kufuata Kristo.

Waamini ni chumvi na nuru (14:34-35)

Mwamini, kama chumvi, ana kazi kubwa mbili. Kama asipotimiza maneno haya watu wanamzarau na kumhukumu.

Mfano wa kondoo aliyepotea (15:1-7)

Waandishi na Wafarisayo hawakufurahi hata kidogo kwa sababu Yesu alikula pamoja na watoza kodi na wenye zambi. Yesu alijibu mashitaki yao na mifano mitatu inayoonyesha ya kwamba Mungu ana-furahi sana wakati anapoona wenye zambi wakitubu, lakini hape-ndezwi hata kidogo na wadanganyi wenye kiburi ambaa wanajihesabu

LUKA

kuwa wenye haki na kukataa kukiri zambi na uovu wao.

Ndani ya mfano wa kondoo aliyepotea, Yesu ni Mchungaji kondoo, kondoo aliyepotea ni mwenye zambi anayetubu, watu 99 ni waandishi na Wafarisayo waliofikili hawahitaji kutubu.

Mfano wa pata iliyopotea (15:8-10)

Ndani ya mfano wa pili, pata ni mfano wa mwenye zambi anayetubu, mwanamke ni Roho Mtakatifu, taa ni Neno la Mungu, na pata tisa nyingine ni waandishi na Wafarisayo na watu wote wengine walio wenye kiburi hata hawakubali kukiri zambi na upotetu wao.

Mfano wa mwana mpotevu (15:11-32)

Hapa tunaona Mungu kama baba mwenye wana wawili. Mwana mdogo wao ni mfano wa mwenye zambi anayekubali zambi zake. Mwana wake mkubwa ni mfano wa waandishi na Wafarisayo na wadanganyi wote wengine kwa maneno ya dini wanaochukizwa na rehema ya Mungu kwa wenye zambi. Wale wasiotubu hawafurahishi roho ya Mungu kamwe.

Mfano wa mlinzi mali asiye na haki (16:1-13)

Sasa Yesu aliacha kusema na Wafarisayo na alifundisha wanafunzi wake juu ya kazi ya mlinzi mali. Ndani ya mfano wa mlinzi asiye na haki, mtajiri ni Mungu mwenyewe. Mlinzi mali hakutenda kwa haki lakini alikuwa na shauri ya akili kwa wakati kazi yake ya mlinzi mali itakapokwisha. Alipata sifa kwa sababu ya akili hii, si kwa sababu ya kupoteza mali ya bwana wake. Kama vile mtu yule alifanya shauri aweze kuwa na rafiki wakati kazi yake kama mlinzi mali itakapokwisha, vivyo hivyo inapassa Mkristo kutumia mali ya Bwana wake na akili ili wakati atakapofika mbinguni kutakuwa na wengine ambao watamkaribisha na furaha. Tukiwa waaminifu kwa namna tunavyotumia mali ya dunia, halafu tutakuwa waaminifu vilevile kwa maneno ya mali ya kweli, ndiyo hazina za roho. Tusizanie Bwana atampa mtu hazina ya kweli kama hatendi kwa haki kwa namna anavyotumika na mali ya Bwana wake, ndiyo mali ya dunia. Haiwezekani kuishi kwa mali na Mungu pamoja.

Ufalme na sheria (16:14-18)

Wakati Wafarisayo walipozaraau mafundisho haya, Yesu alionyesha wazi ya kwamba walikuwa wenye choyo ambaa walijionyesha kuwa wenye haki. Madaraka mpya ilikuwa imeanza, na watu, zaidi watoza kodi na wenye zambi, waliingia ndani yake na furaha. Lakini hata ndani ya muda huu mpya ilipasa watu kutembea katika usafi na utakatifu.

Tajiri na Lazaro (16:19-31)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Kumaliza mafundisho yake juu ya kazi ya mlinzi mali, Bwana alipasha habari za tajiri na Lazaro. Maisha yao, mauti yao, na mwisho wao ulikuwa mbalimbali. Tajiri alikwenda Hadeze, masikini katika kifua cha Abrahamu. Tajiri hakuhukumiwa kwa sababu ya mali yake, lakini kwa sababu hakufikili wamasikini, ndilo neno lilioonyesha ya kwamba hakuokolewa. Agano la Kale lilifundisha ya kwamba utajiri ni alama ya baraka na kibali cha Mungu. Basi kwa nini Myuda mwenye mali alikwenda kwa Hadeze? Bwana Yesu alikuwa ametangaza sasa tu mwanzo wa madaraka mpya. Kuanza wakati ule utajiri wa dunia si alama ya baraka ya Mungu.

Sura 16 inakwisha na maonyo ya nguvu kwa Wafarisayo na kwa wote wanaoweka roho sana juu ya mali. Kuishi kwa mali ni hatari kubwa kwa nafsi zao. Kama mtu mmoja alivyosema, “Kuomba chakula duniani ni vizuri kupita kuomba maji katika Hadeze.”

Maonyo ya Yesu juu ya makwao (17:1-3a)

Yesu alionya wanafunzi juu ya ubaya wa kuongoza watu wengine kufanya zambi. Alisema ni vizuri kupita kuuawa kwa njia ya kuazamishwa ndani ya maji!

Usamehe kupita kadiri yote (17:3b-6)

Hatari nytingine ni kukataa kusamehe kila mara ndugu anayetubu tena na tena. Maonyo ya Bwana juu ya kusamehe mara saba siku moja yalisukuma wanafunzi kuomba Bwana kuongeza imani yao. Bwana alijibu kusema neno kubwa si kipimo cha imani yao, lakini namna ya imani yao, na ya kwamba iliwapasa kutumika na imani ambayo walikuwa nayo.

Imani na utumishi (17:7-10)

Ingepasa mtumwa wa Kristo kukubali kuvimbishiwa kazi nydingi, bila kuangalia hitaji la mwili au afya yake. Hata tukitumikia Bwana kwa kipimo gani, bila kuchoka, tungali watumwa wasio na faida waliofanya tu maneno ambayo iliwapasa kufanya.

Yesu anasafisha wakoma kumi (17:11-19)

Habari za wakoma kumi zinaonyesha wazi roho ya kutoshukuru ya watu. Wao wote waliponyeshwa lakini mmoja tu alirudi kushukuru Bwana. Yule mmoja alikuwa Msamaria, si Myuda. Hata kama wote kumi waliponyeshwa toka ukoma, mmoja aliokolewa toka zambi vilevile.

Namna ya ufalme wa Mungu (17:20-21)

Akijibu ulizo la Mfarisayo, Bwana alisema ya kwamba ufalme wa Mungu haukuja na alama ambazo watu waliweza kuziona, lakini

LUKA

ufalme ulikuwa katikati yao, maana Mfalme alikuwa pale pamoja nao.

Yesu anatabiri juu ya wakristo wa uwongo kwa wakati wa mwisho (17:22-25)

Aliwaambia wanafunzi ya kwamba kwa wakati wa kuja watawaza na hamu sana juu ya siku hizi wakati alipokuwa pamoja nao duniani na wakati walipokuwa na ushirika mtamu naye. Wakristo wa uwongo wataonekana, pamoja na habari za kuja kwa Masiya. Lakini watu wataweza kuona na kutambua wazi kuja kwake kwa pili namna walivyoweza kuona lalo. Lakini kwanza atateswa na kukataliwa.

Mfano wa muda utakaotangulia kuja kwa pili kwa Kristo (17:26-37)

Mbele ya kuja kwa pili kwa Kristo watu wataendelea na maneno yao ya kila siku kama watu wa wakati wa Noa na Loti walivyofanya, bila kukumbuka ya kwamba uharibifu wa gafula ulikuwa karibu kuwapatia (mash. 26-29).

Siku ile watu watakaojaribu kuponyesha vitu vyao watakuwa; wale tu watakaokimbia bila kuangalia nyuma watapona. Njia ya pekee ya salama ndiyo kwa mtu kutoa uzima wake kwa ajili ya Kristo. Utakuwa wakati wa mtengano, wakati wengine watakapoondoshwa kwa hukumu na wengine watakapoachiliwa kuingia ufalme wa Kristo. Wote wasio na imani, na wenye kuasi watahukumiwa. Tai ni mfano wa hukumu ya Mungu, na maiti ni mfano wa ukafiri wa dini ya kiyuda na kikristo (mash. 30-37).

Mfano wa mjane aliyedumu (18:1-8)

Mfano wa mjane mwenye kudumu inatufundisha ya kwamba inatupasa kuomba Mungu na bidii bila haya na ya kwamba Mungu atalipiza kisasi wale wanaotesa watu wake wanaoomba namna hii. Yesu alionyesha watu ya kwamba alikuwa na shaka juu ya kukuta wenye imani kama mwanamke huyu wakati atakaporudia dunia. Wakati tunapoona kuongezeka kwa uovu duniani kwa wakati wa sasa, tunafahamu kwamba hakuona shaka bule.

Mfano wa Mfarisayo na mtoza kodi (18:9-14)

Wakati Bwana aliposema mfano huu aliwaza juu ya watu wanaofiki wao ni wenye haki na wanaozarau watu wengine. Mfarisayo alise-maombi, bila kuomba kweli. Yule mtoza kodi alijitaja mwenye zambi, alisihi Mungu kumrehemu, akarudi kwake akiwa amehesabiwa haki.

Yesu anapenda watoto wadogo (18:15-17)

Wanafunzi hawakufurahi wakati mama walipoleta watoto wao karibu na Yesu, wakajaribu kuwazuiza wasifike. Bwana Yesu alitumia

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

tukio hili kufundisha kwamba tunahitaji imani na unyenyekevu namna watoto waliyokuwa nayo kwa kuweza kuingia ufalme.

Mtawala mwenye mali nyingi (18:18-23)

Mtawala mwenye mali nyingi aliuliza Yesu kama ilimpasa kufanya nini kuriti uzima wa milele. Bwana alitaja mafundisho ya sheria kumfahamisha kwamba yeze ni mwenye zambi, lakini kijana alisifusu kusema alikuwa ameshika sheria tangu ujana wake. Halafu Yesu alijibu ya kwamba akipenda jirani yake kama yeze mwenyewe, auze vitu vyake vyote na kuwapa masikini, kisha amfuate yeze. Yule mtawala alihuzunishwa kwa sababu alikuwa na mali nyingi na hakuwa tayari kushiriki mali hii na watu wengine.

Zawabu katika ufalme (18:24-30)

Kisha Bwana alisema kwamba ni nguvu sana kwa watajiri kuingia ufalme. Wanapenda mali na kuitegemea, na neno hili linawazuiza wasitegemee Mwokozi. Wakati Petro alipokumbusha Bwana ya kwamba wanafunzi waliacha vyote kwa kumfuata yeze, Mwokozi alimwambia ya kwamba hakika wale ambao wanajitoa kuishi hivi kwa Bwana watapata faida nyingi kwa wakati wa sasa na wakati wa kuja.

Yesu anatabiri tena kwamba atakufa na kufufuliwa (18:31-34)

Halafu Yesu alipeleka wanafunzi wake kando, akawaambia tena habari za kufa na ufufuko wake, akitaja saa gani na namna gani ma-neno haya yatakayotokea, lakini ni kama hawakufahamu masemo yake.

Yesu aliwezesha kipofu masikini kuona (18:35-43)

Sasa Bwana Yesu aliondokea Perea kwa njia ya kuvuka mto Yorodani, na alikuwa karibu na Yeriko. Kipofu masikini mmoja kando ya njia alifahamu kwamba alikuwa Masiya aliyekuwa akipita, akamsihi kumwezesha kuona. Mwokozi alisema neno, na mtu huyu aliponyeshwa, akageuka mfuata wa Bwana, akitukuza Mungu.

Yesu anafikia nyumba ya Zakayo (19:1-10)

Kuzaliwa tena kwa Zakayo kulihakikisha kwamba shairi 27 la sura 18 ni kweli: inawezekana kwa Mungu kuponyesha watajiri. Kwa sababu saa ilikuwa nusu mtoza kodi alipanda mti aweze kuona Yesu akipita njiani. Bwana alimwona, akamwambia kwamba atafikia nyumba yake. Zakayo aliamini Bwana, na kwa sababu aliquolewa kweli alifanya shauri kuwapa masikini nusu ya mali yake na kulipa kwa vitu vyo vyote alivyoiba. Wakati adui za Yesu walipomshitaki juu ya kula pamoja na wenye zambi kama Zakayo na rafiki zake, Bwana aliwambia kwamba alikuja kutafuta na kuokoa wapotevu.

LUKA

Mfano wa feza kumi (19:11-27)

Ndani ya mfano wa feza kumi mtu mwenye heshima ndiye Yesu, wale watumishi kumi ndio wanafunzi wake, na wenyeji wa inchi ndio taifa la Israeli. Zile feza kumi ni mfano wa vitu vyote ambavyo wanafunzi walikuwa navyo pamoja — saa, Habari Njema, kazi ya kushuhudia Kristo, vivyo hivyo. Taifa la Israeli (watu) walikataa Kristo kama Masiya na mfalme wao. Watumishi (wanafunzi) walihukumiwa kwa namna gani walitumikia na zile feza. Watumishi wawili wa kwanza walipewa amri kwa kipimo cha faida waliyopata. Mtumishi wa tatu, mwanafunzi mwovu, alipoteza yote. Mfalme aliita wenyeji adui na kuwahukumu kufa. Mfano huu unaonyesha ya kwamba ufalme wa Mungu hautaonekana mara moja (ona sh.11), na ya kwamba kutakuwa na muda katikati ya kuja kwa kwanza na kuja kwa pili kwa Kristo. Ndani ya muda huu itapasa watumishi wake kumtumikia na bidii.

6. JUMA LA MWISHO LA BWANA KATIKA YERUSALEMA NA MAUTI YAKE (19:28 – 23:49)

Kuingia Yerusalem na shangwe (19:28-40)

Siku ya kwanza ya juma iliyotangulia kusulibishwa kwake Yesu alifikia kilima cha Zeituni, akatuma wanafunzi wawili kuleta mwana-punda aweze kutembea juu yake saa ya kuingia Yerusalem. Watu walitandika nguo zao njiani mbele yake kupunguza ugumu wa mawe. Wakati alipoingia mji, wafuata wake wakaanza kusifu. Wafarisayo walikasirika, lakini Yesu alisema kama wanafunzi wake wangalinya-maza, *mawe* yatamsifu!

Yesu anatoa machozi juu ya Yerusalem (19:41-44)

Yesu alitoa machozi juu ya Yerusalem wakati alipokaribia mji kwa sababu watu wa mji wangalikaa na salama kama wangalimpokea, lakini sasa saa ya kufanya hivi ilikuwa imepita. Walikuwa wamem-kataa na wataharibiwa. Neno hili lilitokea kweli kwa mwaka A.D. 70 wakati Tito alipoharibu Yerusalem.

Kusafishwa kwa hekalu (19:45-48)

Wakati utumishi wa Yesu katikati ya watu ulipokuwa karibu kwisha Mwokozi alilingia viwanja vya hekalu na kufukuza mara ya pili wenye kufanya biashara pale. (Alifanya hivi mbele kwa mwanzo wa utumishi wake katikati ya watu, Yoane 2:13-17.)

Wakubwa wa Wayuda walitafuta njia kumwua, lakini makutano walikaa kustaajabia Mtu huyu wa Nazareti mwenye kufanya maajabu.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Maulizo juu ya amri ya Mfalme (20:1-8)

Wakati wakubwa wa makuhani na waandishi walipoulima Yesu na jeuri kama alifanya maneno haya na mamlaka gani, Yesu aliwauliza kama Yoane Mbatizaji alipata amri kwa utumishi wake toka Mungu au watu. Kama wakisema, amri yake ilitoka kwa Mungu, ingaliwapa-sa kutubu na kupokea Masiya ambaye Yoane alitangaza habari zake. Kama wakisema ilitoka kwa watu, wangalikasirisha makutano sana kwani watu waliamini Yoane alikuwa nabii wa Mungu. Wakati walipokataa kujobu ulizo lake, Yesu alikataa kuwajibu vilevile.

Mfano wa shamba la mizabibu (20:9-19)

Ndani ya mfano wa shamba la mizabibu, mwenye shamba ni Mungu. Shamba la mizabibu ni mfano wa Israeli. Mwenye shamba alipangisha walimaji ndani ya shamba (viongozi vya taifa la Israeli). Watumishi ambao alituma kukusanya matunda walikuwa manabii. Wakati watawala walipokataa watumishi hawa, Mungu alituma Mwana wake, lakini watawala walimfukuza toka shamba na kumwua. Halafu Yesu alisema walimaji wale waovu wataharibiwa, na Mungu ataingiza Mataifa kwa pahali pao pa baraka. Wajenga Wayuda walikuwa wamekataa Kristo, Jiwe, lakini lilikuwa shauri la Mungu kwa yeze kuheshimiwa zaidi, akamfanyiza jiwe kubwa la pembeni. Wale wanaoangushwa na jiwe hili sasa wanavunjika (taifa la Wayuda lilivunjwa na Waroma). Wakati atakaporudi, atasambaza wasioamini kama mavumbi.

Mumpe Kaisari yaliyo yake (20:20-26)

Wapelelezi wa viongozi kwa maneno ya dini walijaribu kutega Bwana kwa njia ya kuuliza kama ni taratibu kwa Myuda kulipa kodi kwa Kaisari. Kama akisema “sivyo”, wangalimshitaki juu ya kuasi serikali, lakini akisema “ndiyo”, Waherodia na zaidi ya Wayuda watageuka adui zake. Akiomba kupewa dinari, Bwana alijibu, “Mumpe Kaisari vitu vya Kaisari, na Mungu vitu vya Mungu.” Lilikuwa jibu zuri kabisa.

Ndugu saba kwa mke mmoja (20:27-38)

Wasadukayo walitaka kuonyesha kwamba watu hawatafufuliwa toka wafu kwa njia ya kupasha habari hizi zilizoonekana kama maneno ya kuchekesha, na yasiyowezekana. Mwanamke alioa ndugu saba, mmoja nyuma ya mwengine, kisha yeze mwenyewe alikuwa bila kuzaa mtoto. Halafu waliuliza, “Katika ufuluko atakuwa mke wa nani?” Yesu alijibu kwamba watu hawataoa wala kuolewa mbinguni. Alitaja Kutoka 3:6 kuonyesha ya kwamba Mungu ni Mungu wa ufuluko.

LUKA

Mwana wa Mungu na Mwana wa watu (20:39-44)

Wakati iliponekana kwamba Wasadukayo walikubali kweli ya jibu lake, Bwana alitaja Zaburi 110:1. Aliuliza kama itawezekana namna gani kwa Masiya kuwa *Bwana* wa Daudi na *Mwana* wake vilevile. Yeye mwenyewe ni jibu la ulizo hili: Kama *Mungu*, alikuwa Bwana wa Daudi, na kama *Mtu*, alikuwa *Mwana* wake.

Yesu anahukumu udanganyifu wa Wafarisayo na waandishi (20:45-47)

Halafu Bwana alisema wazi na makutano wasidanganywe na waandishi. Alisema walitenda kama walikuwa watu wa *Mungu*, wakipenda kupewa majina ya heshima na pahali pa heshima, lakini walikuwa wakiiba mali ya wajane, pamoja na kuomba maombi marefu. Wataazibiwa na ukali kwa udanganyifu wao.

Sengi za mjane (21:1-4)

Mwokozi aliona watu wakiweka zawadi zao ndani ya sanduku ya hazina hekaluni, akasema mjane masikini alikuwa ameweka zawadi kubwa kuliko wote wengine, kwa sababu alitoa vyote alivyokuwa navyo. (Angaliweza kuchunga moja ya sengi hizi kwa mahitaji yake mwenyewe, hata kama ilikuwa mali nusu sana tu!)

Alama za mwisho wa muda ule (21:5-33)

Ndani ya mashairi 5-33 Yesu anaonyesha kwa ufupi maneno yatakayotokea wakati atakapokuja mara ya pili:

Yerusalem utaangamizwa (mash. 5-6).

Maneno yatakayotokea wakati atakapokuja mara ya pili (mash. 7-19).

Kuangamia kwa Yerusalem na Mateso Makubwa (mash. 20-24).

Alama zitakazotangulia kuja kwake, na ya kwamba ukombozi wa taifa la Israeli utakuwa karibu saa yenye (mash. 25-26).

Alama ya mtini na miti yote, maana kusimamishwa kwa Israeli kama taifa tena, na kuongezeka kwa kiburi ya watu wote duniani juu ya taifa lao wenyewe (mash. 29-33).

Ni kama mashairi haya yanaonyesha kwamba uangamizi wa Yerusalem na kuja kwa pili kwa Bwana kutatokea pamoja.

Kutazamia kuja kwa Kristo (21:34-38)

Kwa mwisho wa sura hii kuna maonyo wakae tayari na kutazamia kuja kwake kila wakati pamoja na maombi.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Mwokozi alifundisha hekaluni kila siku, kisha alikwenda kulala juu ya kilima cha zeituni. Kila asubui watu walimfikia tena kusikia mafundisho mengine.

Shauri kuua Yesu (22:1-2)

Viongozi vya Wayuda kwa maneno ya dini walitafuta njia kuua Yesu bila kuamsha roho za watu.

Vipande 30 vya feza (22:3-6)

Wakati Pasaka ilipokuwa ikikaribia, Yuda alifanya mapatano mabaya sana kutoa Yesu kwa hesabu fulani ya mali.

Ukumbusho wa Pasaka (22:7-20)

Bwana alituma Petro na Yoane mjini kufanya matayarisho kwa Pasaka. Pale, ndani ya chumba kikubwa cha juu, Bwana na wanafunzi walikula Pasaka ya mwisho na karamu ya ukumbusho wa Bwana mara ya kwanza.

Yesu alitabiri kwamba Yuda atamtoa kwa adui zake (22:21-23)

Yuda alikuwa pale kwa Pasaka, lakini alitoka wakati Bwana alipo-kwisha kumpitisha kipande kile cha mkate (Yoane 13:30), hivi hakuwa pale kwa karamu ya ukumbusho. Ilikuwa sharti kwa Yesu kutolewa kwa adui, kuteswa, na kufa, lakini Yuda ye ye mwenyewe alichagua kuwa mwenye kutoa Bwana kwa mikono ya adui zake.

Wanafunzi walibishana juu ya ukubwa (22:24-30)

Kwa wakati huu wa kusibitisha, wakati mauti ya Mwokozi ilipokaribia, wanafunzi walibishana kama nani katikati yao alikuwa mkubwa zaidi! Na saburi Yesu aliwakumbusha ya kwamba wafuata wake wanaonyesha ukubwa wao kwa njia ya kuwa kama wadogo na kutumikia wengine. Kisha aliwasifu kwa sababu walifungana naye hata kwa wakati huu wa taabu, akaahidi kuwapa kazi zenyé amri ndani ya ufalme wake.

Yesu alitabiri kwamba Petro atamkana (22:31-34)

Nyuma ya udanganyifu wa Yuda na tamaa ya ukubwa ya wanafunzi Petro atamkana! Shetani alitaka kupepete Petro, lakini Yesu alikuwa amemwombea naye atarudishwa karibu na Bwana, na mwishoni atapatisha wanafunzi wengine nguvu rohoni.

Mkoba, mfuko, na upanga (22:35-38)

Sasa Bwana alitoa maagizo mengine kwa wanafunzi wake. Alikuwa karibu kuwaondokea, hivi ilipasa wajitayarische kwa mahitaji yao ya wakati ule na kujipatia mkoba, mfuko kwa vyakula, na upanga.

LUKA

Wanafunzi hawakufahamu kwa sababu gani walihitaji upanga, wakafikili kusudi lake lilikuwa kuwawezesha kulinda Bwana asiuawe. Hata walimu wa wakati wa sasa wanafazaika kwa sababu gani Yesu alitaja upanga ndani ya shairi 36.

Maumivu makubwa shambani (22:39-46)

Nyuma ya kula karamu ya Bwana, Mwokozi alikwenda kwa shamba la Getesemanne pamoja na wanafunzi. Halafu akiwaacha alikwendwa mbali kupita, akaomba mara tatu ili kikombe kiweze kumwondoleta, lakini zaidi ya yote aliomba mapenzi ya Mungu yafanyike. Kila mara nyuma ya kumaliza kuomba, alirudi karibu na wanafunzi wake, akawakuta wakilala usingizi.

Bwana anatolewa na Yuda na kufungwa kwa Getesemanne (22:47-53)

Kisha Yuda alifika pamoja na kundi la watu kufunga Mwana wa Mungu. Alimwonyesha kuwa huyu ambaye walimtafuta kwa njia ya kumbusu sana. Mmoja wa wanafunzi (Petro) alijaribu kuponyesha Bwana kwa njia ya kuondosha sikio la mtumishi wa kuhani mkubwa, lakini Bwana alihamakia Petro, akaponyesha yule mtumishi. Kisha Yesu alionyesha upumbavu wao kumfunga ye ye aliye mwalimu mpole tu, si mwasi wa jeuri. Lakini alijua kwamba hii ilikuwa saa yao na hakushindana nao.

Yesu mbele ya Kayafa (22:54-65)

Makutano walipeleka Yesu kwa kuhani mkubwa kwa kuhukumiwa. Nje, kwa kiwanja cha nyumba yake Petro alikana Bwana mara tatu, kama Mwokozi alivyotabiri mbele.

Watu wenye kazi ya kulinda hekalu walizaraau Yesu, wakampiga, wakamfunika macho, wakampiga kwa uso na kusema naye kutaja ni nani ambaye alimpiga.

Yesu mbele ya baraza (22:66-71)

Kwa mapambazuko ya asubui walipeleka Yesu kwa baraza. Watu wa baraza walimwuliza kama alikuwa Masiya. Bwana alijua kwamba si faida kusemezana nao juu ya neno hili, lakini aliwaonya ya kwamba siku nyininge ataketi kwa mkono wa kuume wa Mungu. Wakati walipomwuliza kama alikuwa Mwana wa Mungu, alisema ni kweli. Wakubwa walifikili jibu lake lilikuwa ukufuru na ya kwamba alistahili kufa.

Yesu mbele ya Pilato (23:1-12)

Nyuma ya kusimama mbele ya watu wa baraza asubui siku ya kazi tano Bwana Yesu aliletwa mbele ya Pilato na mashitaki ya kwamba

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

alisukuma watu kuasi serikali ya Roma, kukataa kulipa kodi, na kuji-fanya mwenyewe mfalme. Yesu alisema ya kwamba alikuwa Mfalme wa Wayuda. Pilato alifikili kwamba hakuwa na kosa, lakini makutano walikaa kusukuma na nguvu, hivi Pilato alituma Yesu kwa Herode. Bwana alikataa kujibu maulizo ya jeuri ya mfalme huyu mwovu, hivi Herode alimzihaki na kumrudisha karibu na Pilato.

Baraba anafunguliwa (23:13-25)

Pilato aliamini ya kwamba Yesu hakuwa na kosa, lakini hata hivi alituliza makutano kwa njia ya kufungua Baraba, mwasi wa sheria wa kujulikana, na kutoa Yesu asulibishwe.

Yesu anasulibishwa (23:26-43)

Wanawake walitoa machozi wakati Yesu alipopelekwa kusulibishwa, lakini Bwana alisema nao wajililie wenyewe na watoto wao, kwa sababu ya uharibifu wa kuogopesha utakaopata mji wao.

Wakati walipofikia Kalvari, askari walisulibisha Bwana wa uzima na utukufu, pamoja na mwasi wa sheria mmoja kwa upande wake wa kuume na mwingine kwa upande wa kushoto. Kisha tunasoma juu ya ombi lake kwa Baba yake, Mungu, aweze kuwasamehe, juu ya askari wakigawanya nguo zake, zihaka ya watawala na askari, maandiko yaliyowekwa juu ya msalaba wake, na kuokolewa kwa mmoja wa waasi waliosulibishwa pamoja naye.

Kristo anakufa kwa waovu (23:44-49)

Giza lilikuwa juu ya inchii toka saa sita azuhuri kufika saa tisa. Pazia la hekalu lilipasuka toka juu hata chini. Akiweka roho yake katika mikono ya Baba yake, Yesu alikufa. Habari hizi zinaandikwa na maneno machache, lakini miaka elfu elfu ya milele itahitajiwa kwa kuzifunua.

7. KUZIKWA, UFUFUKO, NA KWENDA MBINGUNI KWA KRISTO (23:50 – 24:53)

Kristo anazikwa ndani ya kaburi la Yosefu (23:50-56)

Mtu mmoja wa baraza aliyeamini kwa siri, jina lake Yosefu, wa Arimatea, alikwendea Pilato, akapata ruhusa kupewa mwili wa Yesu auzike. Alifunga mwili ndani ya kitani safi na kuuweka ndani ya kaburi lililochongwa katika mwamba. Wanawake waaminifu toka Galilaya walikwenda pamoja na Yosefu, wakakusudi kurudi tena na manukato na malasi ya mafuta mengine kwa mwili wa Mpenzi wao.

Habari kubwa, ndizo Habari Njema (24:1-12)

Nyuma ya kupumzika siku ya sabato, wanawake walirudia kaburi na manukato, lakini walikuta jiwe limefingirishwa mbali na kaburi, na

LUKA

mwili haukuwa ndani yake tena! Malaika wawili waliwaambia ya kwamba Yesu alikuwa amefufuka, kama alivyoahidi wakati alipokuwa pamoja nao katika Galilaya (mash. 1-8).

Wanawake walirudia mji na haraka na habari hizi za kushangaza, lakini mitume 11 hawakuwaamini. Hata Petro nyuma ya kufikia kaburi aweze kuona yeche mwenyewe alirudi na kushangaa sana (mash. 9-12).

Njia inayofikisha Emau (24:13-27)

Nyuma kidogo siku ile ile, Bwana Mfufuliwa alionekana kwa wanafunzi wawili waliokuwa wakirudia kijiji kilichoitwa Emau. Wanafunzi hawa hawakujua ni nani huyu aliyetembea pamoja nao, wakampasha habari za maneno makubwa yaliyotoka katika siku zilizopita. Aliwaonyesha ya kwamba kila neno lilitokea namna manabii walivyotabiri mbele juu ya Masyia.

Wanafunzi wa Emau walitambua Yesu (24:28-35)

Lakini wanafunzi hawakumtambua kufika wakati walipofikia nyumba yao na kula chakula pamoja na Mwokozi. Halafu alitoweka na hawakumwona tena. Basi wanafunzi walirudia Yerusalem kupasha mitume 11 habari za maneno yote yaliyokwisha kutokea.

Agizo kubwa (24:36-49)

Siku ya kwanza ya juma, mangaribi, wanafunzi walishikwa na woga mkubwa wakati Yesu alipotokea katikati yao chumbani. Lakini wakati alipowaonyesha alama za kuumia kwake ndani ya mikono na miguu yake walianza kufahamu. Kwa kuhakikisha kwamba alikuwa kweli yeche, alikula samaki iliyopikwa, na asali kidogo pamoja nao. Kisha alieleza namna gani ufufuko wake ultimiza maneno yote ambayo aliwaambia, na unabii katika Agano la Kale. Kwa sababu walikuwa washuhuda wa ufufuko wake, ilikuwa lazima kwao kuhubiri toba na usamehe wa zambi katikati ya mataifa yote (mash. 36-48). Lakini kwanza itawapasa kubaki katika Yerusalem kungojea kuja kwa Roho Mtakatifu (sh. 49).

Kristo anapanda mbinguni (24:50-53)

Siku 40 nyuma ya ufufuko wake, Bwana alipeleka wanafunzi wake kwa mtelemuko wa mashariki wa kilima cha zeituni, aliwabariki, aka-panda mbinguni. Walimwabudu, kisha walirudia Yerusalem na habari hizi kubwa. Walishinda siku kumi zilizofuata wakisifu na kubariki Mungu katika hekalu.

Habari Njema kama alivyoandika YOANE

MWANZO

Kusudi la Yoane

Yoane mwana wa Zebedayo na “mwanafunzi aliyependwa na Yesu anatujulisha kusudi la Habari Njema yake ndani ya 20:31, “. . . mupate kuamini ya kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mupate uzima kwa jina lake.” Shairi hili linafanyiza Habari Njema hii kuwa Habari Njema ya kwanza iliyoandikwa zaidi kutangaza Habari Njema, lakini Habari Njema zote zinaonyeshea watu njia ya wokovu ndani ya Kristo. Ndani ya Habari Njema hii tunaona Yesu zaidi kama Mwana wa Mungu na Mwokozi wa dunia.

Tarehe na yaliyo ndani ya Yoane

Sehemu kubwa sana (90%) ya kitabu hiki siku ndani ya Habari Njema nyingine. Tunafikili ya kwamba Yoane alikoandika karibu na A.D. 85-95 na kusudi la kuongeza juu ya habari zilizoandikwa na Matayo, Marko na Luka. Kwa mfano ndani ya Yoane tu tunasoma habari za utumishi wake katika Yudea (2:13 – 4:54).

“Mimi ni” ndani ya Yoane

Mara saba ndani ya Habari Njema Yesu alisema juu yake mwenyewe, “Mimi ni” — mkate wa uzima (6:35); nuru ya dunia (8:12); mlango (10:7); mchungaji mwema; ufufuko na uzima; njia, kweli na uzima; na mzabibu. Mara saba alijiita mwenyewe “Mimi ni” kama jina, ona 4:26; 6:20; 8:24,28,58; 13:19; 18:5,8 (mara mbili). Kwa njia ya kutumia jina hili alionyesha wazi ya kwamba yeye ni Yehova wa Agano la Kale.

Alama saba za Yoane

Tunasoma juu ya alama saba ambazo Bwana Yesu alifanya mbele ya watu na zinazoonyesha kwamba yeye ni Mungu: kugeuza maji kuwa mvinyo (2:1-12); kuponyesha mwana wa mkubwa wa ufalme (4:46-54); kulisha watu 5,000 (6:1-14); kutembea juu ya bahari ya Galilaya (6:15-21); kuponyesha mtu aliyezaliwa kipofu (9:1-12); na kufufua Lazaro toka wafu (11:1-44); kuwezesha wanafunzi wake kupata samaki wengi (21:1-14).

YOANE

Namna Yoane alivyoandika

Yoane aliandika na maneno yaliyo nyepesi kufahamu, lakini mawazo na mafundisho yake ni makubwa sana.

UMBO LA YOANE

1. Matangulizi: Neno la Milele anakamata mwili (1:1-14)
2. Ushuhuda wa Yoane Mbatizaji juu ya Yesu (1:15-34)
3. Mwaka wa kwanza wa utumishi wa Yesu (1:35 – 4:54)
4. Utumishi katika Yerusalem katika mwaka wa pili (Sura 5)
5. Utumishi katika Galilaya katika mwaka wa tatu (Sura 6)
6. Utumishi katika Yerusalem wakati wa mwaka wa tatu (7:1 – 10:39)
7. Utumishi katika Perea katika mwaka wa tatu (10:40 – 11:57)
8. Mwisho wa utumishi wake kati ya watu (Sura 12)
9. Mafundisho katika chumba cha juu (Sura 13–16)
10. Ombi la Yesu kama kuhanu mkubwa (Sura 17)
11. Yesu alitolewa kwa adui, aliteswa, na kusulibishwa (Sura 18-19)
12. Ufufuko (Sura 20)
13. Kristo mfufuliwa pamoja na watu wake katika Galilaya (Sura 21).

1. MATANGULIZI: NENO LA MILELE ANAKAMATA MWILI (1:1-14)

Yesu ni Neno la milele (kwa kiyunani Neno ni Logos). Alikuwa pamoja na Mungu, yeye ni Mungu, Mwumba, Uzima, na Nuru. Yoane Mbatizaji alitoa ushuhuda ya kwamba yeye ni Nuru ya kweli. Neno alikamata mwili, akakaa duniani. Alikataliwa na watu wake mwenyewe, ndio Wayuda, lakini wale ambao wanampokea, wa Wayuda au Mataifa, wanageuka wana wa Mungu kwa njia ya kuzaliwa tena katika roho.

2. USHUHUDA WA YOANE MBATIZAJI JUU YA YESU (1:15-34)

Kristo alifunua Mungu (1:15-18)

Yoane alitangaza ya kwamba Neno (Yesu)alikuwa hata mbele ya kuzaliwa duniani, ya kwamba alileta neema na kweli, si sheria, na ya kwamba alikuwa Mwana wa Mungu aliyefunua Mungu.

Ushuhuda wa Yoane mbele ya makuhani na Walawi (1:19-28)

Wakati viongozi vya Wayuda walipotuma watu kufahamu kama

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Yoane ni nani, Yoane alikuwa akibatiza watu katika Yorodani. Aliwaambia ya kwamba yeze si Masiya, wala Elia, wala Nabii ambaye Musa aliahidi atakuja. Akiwa mtangulizi wa Masiya, alibatiza kwa maji tu, na hakustahili kusawanishwa na Masiya mwenyewe.

Ushuhuda wa Yoane wakati wa ubatizo wa Kristo (1:29-34)

Kesho yake Yoane alionyesha mbele ya watu a kwamba Yesu ni Mwana-kondoo wa Mungu, Masiya ya Israeli, yule anayebatiza na Roho Mtakaatifu, naye ni Mwana wa Mungu. Yeze mwenyewe alitambua Yesu kuwa Masiya wakati alipoona Roho akishuka na kukaa juu yake wakati wa ubatizo wake.

3. MWAKA WA KWANZA WA UTUMISHI

WA YESU (1:35 – 4:54)

Wanafunzi wa kwanza wa Yesu (1:35-51)

Wawili wa wanafunzi wa Yoane Mbatizaji waliona Yesu kesho yake, wakamfuata. mmoja wao, Anderea, alikwenda kuleta ndugu yake Petro karibu na Yesu. Kesho yake Yesu aliita Filipo, naye aliletta Natanaeli. Natanaeli alikuwa na shaka kwanza, lakini nyuma kidogo alikiri kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na Mfalme wa Israeli. Bwana aliahidi ya kwamba atapata zawabu kwa imani yake kwa njia ya kuona maneno makubwa kuliko.

Ndoa katika Kana (2:1-11)

Alama ya kwanza ambayo Yesu alifanya ilikuwa kugeuza maji kuwa mvinyo kwa karamu ya ndoa katika Kana. Ilikuwa mvinyo nzuri zaidi, na nyingi sana kutosha kabisa.

Kristo alisafisha hekalu (2:12-22)

Nyuma ya kukaa katika Kapernaumu kwa muda mfupi, Bwana alikwenda Yerusalem kwa Pasaka. Pale alionyesha bidii yake kwa nyumba ya Baba yake kwa njia ya kufukuza wenyewe kubadilisha feza toka viwanja vya hekalu. Wayuda waliuliza kuwaonyeshea alama kuhakikisha kwamba alikuwa na ruhusa kufanya hivi, naye aliwaambia kuharibu “hekalu hili” naye atalisimamisha kwa siku tatu. Wayuda walifikili alisema juu ya hekalu lililojengwa na Herode, lakini Yesu alisema juu ya mwili wake. Nyuma ya ufufuko wake tu wanafunzi wake walikumbuka na kufahamu jibu hili.

Kristo anajua watu wote (2:23-25)

Kwa wakati wa Pasaka, watu wengi walisema kwamba waliamini Yesu wakati walipoona alama zake, lakini Yesu alifahamu kwamba hawakuwa waamini wa kweli.

YOANE

Sharti muzaliwe mara ya pili (3:1-21)

Nikodemo alikuwa Mfarisayo na mtawala wa Wayuda. Wakati Yesu alipomwambia kwamba ni lazima kwake kuzaliwa tena kama akitaka kuingia ufalme wa Mungu, Nikodemo alikumbuka tu kwamba haiwezekani kwa mwili wa mtu kuzaliwa mara mbili. Hivi Bwana alieleza ya kwamba kuzaliwa tena ni kazi ya kushangaza, kazi ya ajabu ya Roho ya Mungu tusiyowenza kufahamu, na ya kwamba inafanyikana wakati mwenye zambi anapoamini Mwana wa pekee wa Mungu. Mtu anayeaminu ana uzima wa milele, lakini yule anayekataa kuamini amehukumiwa. Watu hawataki kuamini kwa sababu wanapenda giza (zambi) kupita nuru (haki).

Yoane Mbatizaji alitukuza Yesu (3:22-36)

Yesu alikuwa ameanza utumishi wake kati ya watu, lakini Yoane Mbatizaji aliendelea na kazi yake kwa wakati. Wakati Wayuda walimwambia Yoane kwamba watu wengi walifuata Yesu, kupita hesabu ya wale amba walimuata yeye, Yoane alisema ni vizuri. Yesu alikuwa Masiya, si Yoane. Yesu alikuwa Bwana-arusi; Yoane alikuwa rafiki yake tu. Lazima Yesu azidi; ilipasa Yoane kupunguka. Yesu alitoka mbinguni; Yoane alizaliwa na watu wa dunia. Hata hivi watu wachache walikubali kupokea mafundisho ya Mwokozi. Wale waliomwamini walipokea uzima wa milele. Wale wasioamini walijiwewa chini ya gazabu ya Mungu.

Mwanamke wa Samaria alikutana na Masiya Myuda (4:1-30)

Labda wanafunzi wa Yoane walikuwa na wivu kwa sababu kwa njia ya wanafunzi wake Yesu alibatiza watu wengi kupita Yoane. Labda ni kwa sababu ya neno hili Yesu aliondokea Yudea, akaanza kwenda kwa Galilaya upande wa kaskazini. Njiani alisimama kwa kisima cha Yakobo katika Samaria, akaomba mwanamke mmoja kumpa maji ya kunywa. Halafu alimwambia juu ya maji yaliyo hai na yanayoshibisha kiu kwa milele, akamwonyesha kwamba alihitaji maji haya (kwani mwanamke alikuwa akiishi katika zambi), na alifunua njia ya kweli ya kuabudu. Wanafunzi wakarudi karibu na Bwana, wakashangaa kumwona akisemezana na mwanamke, mwanamke Msamaria! Halafu mwanamke alirudia Sukari, akawaambia watu kwamba ameona Masiya, watu wakatoka mjini kumwona wao wenywewe.

Mavuno ya roho (4:31-38)

Wakati wanafunzi waliposumbuka kwa sababu Bwana wao hayaku-la bado, Yesu aliwaeleza kwamba furaha ya kufanya mapenzi ya Mungu inapita mbali uzuri wa kushibisha mahitaji ya mwili na vyaku-

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

la. Halafu aliwasihii kushiriki ndani ya furaha hii kubwa kwa njia ya kuvuna roho za watu zilizokwisha kukomea. Watu wengine walikuwa wamepanda mbegu lakini wanafunzi walipewa heshima ya kuvuna matunda ya kazi ya watu wengine.

Mwokozi wa ulimwengu (4:39-45)

Wasamaria wengi waliamini kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke, na wengine waliamini kwa sababu ya masemo ya Bwana mwenyewe. Alikaa pamoja nao kwa siku mbili, kisha alikwenda Galilaya. Watu wa Galilaya walimpokea vizuri kupita watu wa Yudea.

Mwana wa mkubwa wa mfalme aliponyeshwa (4:46-54)

Katika Kana mtu mkubwa mmoja wa mfalme alisihii Yesu kuponyesha mwana wake. Wakati mtu huyu alipoonyesha kwamba aliamini bila kuona alama, Yesu alimwambia ya kuwa mwana wake ataishi. Wakati mtu huyu aliporudia nyumba yake alisikia kwamba mwana wake aliponyeshwa saa ile ile Bwana aliposema maneno haya.

4. UTUMISHI KATIKA YERUSALEMA WAKATI WA MWAKA WA PILI (Sura 5)

Mtu aliponyeshwa kwa birika la Betesaida (5:1-9)

Wakati Yesu alipokwenda Yerusalem kwa moja ya karamu za Wayuda, aliponyesha mtu aliyejkuwa mgonjwa kwa miaka 38. Mtu huyu alikuwa amejaribu kuingia birika tena na tena aweze kuponyeshwa, lakini watu wengine waliingia mbele yake kila mara. Basi Yesu alimwigiza kuchukua kitanda chake, halafu mtu huyu aliponyeshwa mara moja.

Wengine walilaumu (5:10-16)

Wayuda wengine walisema si vizuri kwa mtu yule kubeba kitanda chake siku ya sabato, hata kama hawakumsaidia wao wenyewe na wangalifurahi kuponyeshwa siku yo yote ya juma! Kwanza mtu aliyeponyeshwa hakufahamu kama nani alimponyeshwa, lakini nyuma ya kukutana na Bwana katika viwanja vya hekalu, aliwaambia kwamba alikuwa Yesu ambaye alimponyeshwa. Halafu Wayuda walikasirika sana, wakajaribu kuua Yesu kwa kuvunja sabato.

Baba na Mwana ni Sawa (5:17-27)

Walizidi kutaka kuua Yesu wakati aliposema yeye ni sawa na Mungu kwa njia ya kuita Mungu Baba yake. Aliwaambia kwamba alifanya maneno yo yote Baba yake aliyofanya, alijua maneno yote na kufufua wafu kama Mungu, Baba amempa kazi yote ya kuhukumu,

YOANE

watu wote wanamheshimu yeye kama wanavyoheshimu Baba, alikuwa sawa na Mungu kwa njia ya kuleta uzima wa milele, na kwa njia ya kuwa na uzima ndani yake mwenyewe.

Fufuko mbili (5:28-30)

Yesu aliendelea kusema ya kwamba siku moja wafu wote watasikia sauti yake na kutoka kaburini ndani ya fufuo mbili mbalimbali. Alisema vilevile ya kwamba yeye mwenyewe alikuwa mkamilifu kabisa hata hakufanya neno kwa kutaka kwake mwenyewe, lakini alitii Baba ndani ya maneno yote.

Ushuhuda mara ine (5:31-40)

Ndani ya baki la sura hii, Bwana Yesu alisema juu ya maneno mane yaliyoshuhudia kwamba yeye ni Mungu. Alikubali ya kuwa ushuhuda wake mwenyewe hautoshi, hata kama ulikuwa kweli. Lakini alikuwa na ushuhuda wa Yoane Mbatizaji, wa kazi zake mwenyewe, wa Baba yake, na wa maandiko ya Agano la Kale.

Utukufu toka watu, au Mungu (5:41-47)

Wayuda hawakutaka kuja kwake Kristo. Walijipenda wenyewe kupita Mungu. Walitafuta kukubaliwa na watu kupita kukubaliwa na Mungu. Hawakutaka kupokea Kristo, lakini kwa wakati wa kuja watapokea mpinga Kristo. Yesu hatawashitaki mbele ya Baba; maandiko ya Musa yatatosha kuwahukumu.

5. UTUMISHI KATIKA GALILAYA WAKATI WA MWAKA WA TATU (Sura 6)

Kulisha watu 500 (6:1-14)

Kwa upande wa mashariki au kaskazini-mashariki wa Bahari ya Galilaya, Bwana alizidisha mikate mitano na samaki wadogo wawili kutosha kulisha wanaume 5000 pamoja na wanawake na watoto na kuacha vyakula vingine vilivyojaza vitunga 12. Kwa sababu ya alama hii watu wengi waliamini kwamba yeye ndiye Nabii ambaye aliahidiwa, na walitaraji kwamba atawaokoa toka utawala wa Waroma.

Kutembea juu ya maji (6:15-21)

Yesu alifahamu kwamba watu walitaka kumfanya mfalme, neno lisilopatana na mapenzi ya Mungu kwa wakati ule, basi akaondoka kwenda mlimani peke yake. Wakati wanafunzi walipoingia chombo na kurudia Kapernaumu, upopo ukaanza kuvuma. Yesu alikuja kwao akitembea juu ya maji, kisha alituliza upopo na kujifunua kwao akisema, “Ni mimi.” (Jina moja la Bwana ni “Mimi ndiye”. Basi mara moja chombo kilifikia inchi kavu.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Makutano makubwa walifuata Yesu kwenda Kapernaumu (6:22-24)

Kesho yake makutano walivuka bahari ya Galilaya kufuata Yesu hata Kapernaumu. Yesu alijibu maulizo yao kwa njia ya hotuba yake juu ya Mkate wa Uzima. Kwanza aliwajibu na maneno yasiyo nguvu kufahamu, lakini wakati kutokuamini kwao kulipoonekana wazi kupita, mafundisho yake yaligeuka nguvu kupita vilevile.

Chakula chenyе kuharibika na uzima wa milele (6:25-27)

Ni kama ulizo lao la kwanza lilionyesha kwamba watu walimfurahia, lakini aliwaambia ya kwamba walimfurahia tu kwa sababu alikuwa amewalisha. Iliwapasa kufanya kazi kwa chakula cha roho kinachodumu hata uzima wa milele.

Kazi ya Mungu ni kuamini Kristo (6:28-29)

Watu walifazaika kama kazi hii ni kazi ya namna gani. Aliwajibu, "Muniamini mimi."

Yesu mkate toka mbinguni (6:30-33)

Waliomba alama kwake, kama mana ambayo Musa alileta watu. Aliwajibu kusema ya kwamba mama haikuweza kuleta uzima kama mkate wa Mungu.

Yesu ni mkate wa uzima (6:34-40)

Walimwomba, "Bwana ... utupe mkate huu" (sh.34), na Bwana aliwajibu, "Kujeni ... na mwamini." Lakini alijua ya kwamba hawakutaka kuamini. Na alijua vilevile ya kwamba mapenzi ya Mungu yatafanyika hata kama hawakuamini.

Kujitwalia Yesu kunaleta uzima wa milele (6:41-51)

Wayuda hawakufurahi juu ya semo lake kwamba alishuka toka mbinguni, hivi Yesu aliwakumbusha ya kuwa wokovu una sehemu mbili. Kwanza, inapasa Mungu kuvuta mtu. Kisha sharti mtu yule amwamini kwa kupata uzima wa nmilele. Neno hili ni mamoja na kula Mkate aliye hai, na kula mwili wake.

Mafundisho ya Yesu juu ya mwili na damu yake (6:52-59)

Watu walifazaika wakati aliposema atatoa mwili wake watu wapate kula. Bwana hakueleza neno hili, lakini alisema tena kwamba njia ya pekee kupata uzima wa milele ni kula mwili wake na kunywa damu yake. Tunajua kwamba maana yake ni kumwamini, lakini Bwana hakuieleza zaidi kwa sababu ya kutokuamini kwao.

Wanafunzi wengi waliacha kufuata Yesu (6:60-66)

Watu wengi walichukizwa wakati walipowaza juu ya kula mwili

YOANE

wa mtu na kunywa damu. Yesu alijibu ya kwamba kufanya hivi kweli kutakuwa hata nguvu kupita wakati atakapopanda mbinguni. Lakini maana ya masemo yake haikuwa kwa watu kula mwili wake kabisa, lakini kula maneno yake, maana kuamini maneno aliyosema.

Petro alikiri kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu (6:67-71)

Tangu wakati ule watu wengi wasiokuwa waamini wa kweli walacha Yesu. Lakini Petro alisema, “sisi [wanafunzi wake kumi na wawili] tunaamini ya kwamba wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu.” Maana ya jibu la Bwana ilikuwa, “Si ninyi kumi na wawili, lakini kumi na mmoja tu,” kwa sababu alijua Yuda atamtoa kwa adui zake.

6. UTUMISHI KATIKA YERUSALEMA KATIKA MWAKA WA TATU (7:1 – 10:39)

Kutoamini kwa ndugu za Yesu (7:1-9)

Wakati siku kubwa ya vibanda ilipokuwa karibu, ndugu za Yesu walisema naye kwa zarau aende na kujionyesha wazi mbele ya watu. Yesu alijibu kusema saa ya Mungu ilikuwa hajatimia bado kwa ye ye kufunuliwa mbele ya watu. Wao waliishi namna walivyotaka bila kukumbuka mapenzi ya Mungu. Watu wa dunia hawakuwachukia kwa sababu walikuwa watu wa dunia.

Yesu anafundisha kwa siku kubwa ya vibanda (7:10-24)

Wakati ndugu za Yesu walipokwisha kwenda Yerusalem, Yesu alikwenda kule vile kama kwa siri. Wayuda wengine walimtafuta, wengine walimsifu, na wengine walimhukumu, lakini watu wote walilogopa kumsimamia wazi mbele ya watu.

Katikati ya karamu Bwana alianza kufundisha viwanjani mwa hekalu. Alisema mafundisho yake yalitoka kwa Mungu, na mtu ye yote akitaka kujua kweli na roho ya kweli, Mungu ataifunua kwake. Alishitaki Wayuda juu ya kuvunja sheria ya Musa kwa njia ya kufanya shauri kumwua. Walikataa neno hili, wakasema ana pepo. Lakini Yesu aliwakumbusha gazabu yao wakati alipoponyesha mtu siku ya sabato, hata kama walitahiri watoto siku ya sabato.

Makutano walifazaika kama Yesu ni nani (7:25-29)

Watu wa Yerusalem walifazauja kwa sababu gani viongozi waliruhusu Yesu kukaa kufundisha wakati walipokuwa wakifanya shauri kumwua. Labda viongozi waliamini vilevile kwamba ye ye ni Masiya? Walifikili Yesu si Masiya kwa sababu walimjua na pahali alipotoka. Yesu aliwajibu kwamba walimjua kama mtu wa dunia, lakin i hawakufahamu kwamba alitoka kwa Mungu vilevile, maana alikuwa Mungu.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Yesu anaepuka kufungwa (7:30-36)

Kufazaika kwa watu juu ya Yesu ya kama yeche ni Masiya kulisukuma viongozi vyao kwa maneno ya dini kutuma watumishi hekalu kumkamata. Yesu alifazaisha watawala kwa njia ya kusema atawaondokea nyuma kidogo, na halafu watatengwa naye kwa milele.

Yesu aliahidi kuja kwa Roho Mtakatifu (7:37-39)

Siku ya mwisho ya karamu Bwana aliahidi mbele ya watu kwamba Roho Mtakatifu atakuja na kukaa ndani ya wale amba watamwamini. Ahadi hii ilitimizwa siku ya Pentekote.

Mawazo mbalimbali juu ya Yesu (7:40-44)

Watu walikaa kufikili maneno mbalimbali juu ya Yesu.

Yesu alikataliwa na watawala (7:45-52)

Wakati watumishi waliporudi bila kuleta Kristo na kusema maneno juu yake, Wafarisayo waliwashitaki kusema walidanganywa. Wakati Nikodemo alisema na wakubwa ilipasa kusikia Yesu kwanza, walmzarau na kuuliza kama yeche ni Mgalilaya mjinga.

Mwanamke wa uzini mbele ya Nuru ya ulimwengu (7:53 – 8:11)

Habari hizi ni ndani ya zaidi ya maandiko ya zamani, lakini si ndani yao yote. Shairi la kwanza la sura 8 linafungana na 7:53: Wakati watu waliporudia nyumba zao Yesu alikwenda kwa mlima wa Mizeituni.

Kesho yake Yesu alirudia hekaluni. Pale Wafarisayo walileta kwake mwanamke aliyekamatwa akitenda uzini. Waliuliza kama mwanamke alistahili kupata hukumu gani, wakitaraji kumnasa. (Kwa nini hawakuleta mwanamume vilevile?) Bwana alisimamia sheria, akikubali kwamba sharti mwanamke atupiwe mawe, lakini alisema wale wasio na kosa katikati yao watimize hukumu hii. Wakati hakuna mtu aliyefanya hivi, alisema na mwanamke kwenda zake na kuacha kufanya zambi. Habari hizi zinaonyesha roho ya neema ya Bwana wetu kwa wenye zambi.

Yesu alisimamia ushuhuda wake juu yake mwenyewe (8:12-20)

Kila neno Bwana alilosema lilileta mabishano na Wayuda. Wakati aliposema yeche ni nuru ya dunia, walisema kwamba ushuhuda wa mtu juu yake mwenyewe si ushuhuda wa kweli. Yesu alisema ya kwamba ushuhuda wake ulikuwa kweli, na ya kwamba Baba yake alimshuhudia vilevile. Waliuliza na kuzarau kama Baba yake alkuwa wapi. Alijibu kusema kwamba hawakuweza kujua Baba kwa sababu walikataa kuamini ya kuwa yeche ni Mwana wa Mungu.

YOANE

Yesu alitabiri ya kwamba atakwenda zake (8:21-29)

Yesu alisema ya kwamba ataondokea Wayuda, ya kwamba watamtafuta na watakuwa ndani ya zambi zao na kukatiliwa mbali na mbingu kwa milele. Wasikiaji wake walifikili alitaka kujua mwenyewe! Aliwahamakia kwa ujinga wao wa maneno ya Mungu, akasema tena kwamba watakuwa katika zambi zao. Walimwuliza kama yeje ni nani naye alijibu na kusema yeje ni Masiya, kama aliwyowaambia kila mara. Angaliweza kuwaambia maneno mengi, lakini alisema tu maneno ambayo Baba yake alimwonyesha. Wakati watakapokwisha kumsilibishi watajua kwamba alikuwa Masiya kweli, na alikuwa na upatano wa karibu sana na Baba.

Kweli itawaweka ninyi huru (8:30-32)

Bwana Yesu alisema na watu wengi ambao walimwamini ya kwamba kwa njia ya kutii Neno lake watahakikishwa kwamba walikuwa wanafunzi wake kweli, na watafunguliwa toka zambi na kudanganywa na mafundisho ya uwongo.

Wayuda wasioamini si uzao wa Abrahamu kwa maneno ya roho (8:33-47)

Halafu Wayuda wasioamini walianza kubishana naye tena. Walijisifu kusema wao ni uzao wa Abrahamu na hawakuwa katika utumwa kamwe. Yesu alisema kwamba yeje ni tayari kuwaweka huru, na ya kwamba hata wakiwa wazao wa Abrahamu, hawakuwa watoto wake. Damu ya Abrahamu ilikuwa ndani ya miili yao lakini walikosa imani yake miyoni mwao. Walitaka kuua Yesu, ndilo neno lililoonyesha kwamba baba yao alikuwa — Shetani. Walisema hawakuzaliwa katika uzini (labda walitaka kusema kwa maficho ya kwamba Yesu alizaliwa hivi), na ya kwamba Mungu alikuwa Baba yao. Yesu aliwakumbusha ya kwamba kama wakipenda Mungu watampenda yeje vilevile. Hawakufahamu maneno aliyosema, lakini walikataa kukubali mafundisho yake. Walikuwa wauaji, kama baba ya, Shetani. Walikataa kuamini Bwana hata kama hawakuweza hawakuona hata zambi nusu ndani yake. Kwa njia ya kukataa kweli, walihakikisha kwamba hawakuwa watu wa Mungu.

Yesu alifunua wazi kama yeje ni nani (8:48-59)

Walishitaki Bwana Yesu wakisema yeje ni mtu mwenye pepo toka Samaria. Neno hili halikuwa kweli, lakini aliheshimu Baba yake, si yeje mwenyewe, na mtu ye yote akimtii hatakufa kamwe (mauti ya milele). Wayuda walibisha maneno haya wakisema Abrahamu na manabii walikuwa wamekufa. Walifahamu kwamba Yesu alisema yeje ni mkubwa kupita Abrahamu! Yesu alijibu kusema yule ambaye

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

waliita Mungu wao alimheshimu yeye. Aliwaambia ya kwamba aliju Mungu na alikuwa sawa naye, na ya kwamba akibisha neno hili, angalisema uwongo. Halafu aliongeza kusema ya kwamba Abrahamu alitazamia kuona maneno haya, ndiyo siku ya Masiya, na alifurahi kuiona. Hivi Yesu alisema yeye ndiye mwenye kutimiza unabii wote juu ya Masiya. Kwanza Wayuda walimzara, kisha walikamata mawe wamtupie, lakini alijiponyesha kwa njia ya kutoka viwanja nya hekalu.

Mwananume aliyezaliwa kipofu (9:1-12)

Kipofu huyu alimpa Yesu njia kutenda alama ya kuponyesha. Bwana alipakaa macho ya mtu huyu kwa matope na mate, kisha alimwagiza kwenda kunawa, na ajabu lilifanywa – aliweza kuona mara moja. Jirani zake walikuwa na maulizo mengi, na mtu aliyeponyeshwa alijaribu kuyajibu.

Wafarisayo walimwulizaauliza yule aliyeponyeshwa (9:13-17)

Wafarisayo hawakufurahi kwa sababu mtu huyu aliponyeshwa siku ya sabato, wakamwulizaauliza juu ya maneno yaliyotokea. Alijibu maulizo yao, akakataa ya kwamba mtu mwenye kufanya alama namna hii ni mtu wa zambi, na alisema ya kwamba alifikili Yesu alikuwa nabii.

Wafarisayo wakaaulizaauliza wazazi wa yule aliyeponyeshwa (9:18-23)

Kisha Wayuda waliulizaauliza wazazi wa mtu huyu kwa sababu hawakuamini kwamba Yesu aliweza kufanyiza vipofu kuona. Wazazi walisema ya kwamba alama hii ilifanyika kweli, lakini walikataa kuingia ndani ya maneno haya kwa sababu waliogopa watatokezwa toka sunagogi.

Wafarisayo walimtokeza yule aliyeponyeshwa (9:24-34)

Halafu Wayuda waliulizaauliza mtu yule tena. Alishuhudu kwamba alikuwa kipofu mbele lakini sasa aliweza kuona. Ilishinda Wafarisayo kumwogopesha. Alisema na uhodari juu ya Yesu, akionyesha kwamba mawazo yao si sawa. Walimzara, kisha walimtokeza inje.

Yesu alipatisha imani yake nguvu (9:35-38)

Wakati Wayuda walipotokeza mtu yule inje, Yesu alikuwa akingoja kumpokea na kujifunua kwake kama Mwana wa Mungu. Mtu huyu aliamni na mumwabudu.

Yesu anafundisha juu ya upofu wa roho (9:39-41)

Bwana alisema kwamba alikuja duniani kwa kuhukumu. Wale

YOANE

wanaokubali kwamba wao ni vipofu atika roho wataona; wale wasiofahamu hitaji la roho zao watakaa vipofu. Kama Wafarisayo wangalikubali tu ya kwamba hawakuweza kuona, zambi yao ingalikuwa ndogo. Lakini hawakuweza na hawakutaka kuona Mwana wa Mungu aliyekuwa akisimama katikati yao; basi watakaa viofu.

Mchungaji Mwema (10:1-18)

Hotuba juu ya Mchungaji Mwema inafuata habari za sura 9. Mchungaji ndiye Bwana Yesu. Zizi la kondoo ni taifa la Israeli. Zamu ni Roho Mtakatifu akitumika kwa njia ya Yoane Mbatizaji. Wale wasioingia zizi kwa mlango ni watu kama Wafarisayo waliosema walikuwa na amri juu ya Wayuda lakini wasioweza kuhakikisha neno hili. Walikuwa wizi, wanyanganyi, wageni, na watu wa mshahara. Kondoo wengine wasio wa zizi hili ni Mataifa. Kundi moja ni Kamisa, lenye waamini wa Wayuda na Mataifa. Yesu alikuja na maneno yote yaliyohakikisha kwamba yeye ni Masiya, na kondoo za kweli walimtambua. Anaongoza na kulisha kondoo zake, anakufa kwa ajili yao na kufufuliwa tena, na anawapa uzima tele.

Nyumba inayotengwa (10:19-21)

Wengine wa Wayuda walifurahia Yesu, wengine walifikili ana wazimu. Hakuna mtu aliyesimama katikati.

Yesu alitangaza uungu wake kwa karamu ya Kutabaruku (10:22-30)

Nyuma, kwa karamu ya Kutabaruku Wayuda waliuliza kama Yesu ni Masiya. Yesu alijibu kusema ni kweli, na ya kwamba yeye na Baba yake pamoja walileta uzima wa milele kwa kondoo zake.

Wayuda walikataa maneno Yesu aliyo sema (10:31-39)

Wayuda walikuwa tayari kutupia Yesu mawe wakisema alikuwa ametukana wakati alipoonyesha kwamba yeye ni Mungu. Yesu alijibu kama Mungu aliita waamuzi wa Agano la Kale “miungu” kwa sababu walikuwa wajumbe wa Mungu, kuzidi sana ilikuwa haki yake mwenyewe kujiita Mwana wa Mungu. Mungu Baba alikuwa amemtuma duniani toka mbinguni. Vilevile kama wakikataa kuamini masemo yake, ingaliwapasa kusadikishwa na alama zake zilizoonyesha ya kwamba yeye na Baba yake wana uwezo sawasawa.

7. UTUMISHI KATIKA PEREA WAKATI WA MWAKA WA TATU (10:40 – 11:57)

Watu weng wanaamini Yesu (10:40-42)

Wayuda walijaribu kumkamata tena, lakini alipona, akakwenda

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kwa upande wa mashariki wa Yorodani. Watu wengi walimwamini pale, wakikubali ya kwamba ushuhuda wa Yoane juu yake ulikuwa kweli.

Mauti ya Lazaro (11:1-16)

Wakati Maria na Marata walipotuma mjambe kumwambia Yesu kwamba ndugu yao Lazaro alikuwa mgonjwa, Yesu aliwaambia wana-funzi ya kwamba mwisho wa ugonjwa ule utakuwa utukufu wa Mungu, si mauti ya Lazaro. Nyuma ya siku mbili alisema vizuri warudie Yudea pahali Lazaro alipokuwa. Wanafunzi walimkumbusha ya kwamba muda mfupi mbele Wayuda wa pale walijaribu kumtupia mawe. Yesu alijibu kusema hakuna neno haya lililoweza kumpata kufika siku kazi yake ilipokwisha. Alijua sasa ya kwamba Lazaro alikuWa amekufa, hata kama alisema mbele kwamba alilala, aki-sawanisha mauti na kulala.

Yesu ni ufufuko na uzima (11:17-37)

Yesu alifika siku ine nyuma ya kufa kwa Lazaro. Alifariji Marata kwa njia ya kumwambia ndugu yake atafufuka tena, si siku ya mwisho tu lakini sasa. Halafu aliongeza ufunuo huu wa ajabu ya kwamba wakati atakapokuja wale waliokufa katika imani wataishi na waamini walio hai watakwenda mbingu bila kufa. Marata alikiri kwamba Yesu ni Masiya na Mwana wa Mungu, kisha alikimbia kwake na kuleta Maria. Ni kama Maria alikuwa akihuzunika kwa sababu Bwana hukufika mara moja.

Lazaro anaafufuliwa (11:38-44)

Wakati watu walioondosha jiwe kama Yesu alivyoagiza, aliagiza Lazaro kutoka. Lazaro alitoka kaburi lakini hakutembea kwa sababu alifungwa kwanza na sanda. Mara moja wakati watu zilipoondosha alikwenda zake.

Shauri la kuua Yesu (11:45-54)

Wakuwa wa makuhani na Wafarisayo walianza kuogopa kwa sababu wengine wa Wayuda walikuwa wameamini Yesu. Waliogopa kama wengi zaidi watafanya hivi hivi Waroma wataharibu hekalu kusambaza watu. Kayafa, kuhani mkubwa hakufahamu ye ye mwenyewe maana kubwa ya jibu lake. Alitabiri ya kwamba Wayuda hawatakuwa kwa sababu ya Yesu, lakini ya kwamba Yesu atakufa kwa taifa, na atakusanya watu wake toka katikati ya mataifa. Ni kama unabii huu uliongeza kutaka kwa Wayuda kufanya shauri kumwua, hivi Yesu aliondoka pale pamoja na wanafunzi wake, wakakwenda kijiji kimoja karibu na jangwa kilichoitwa Efuraimu.

Watu walitafuta Yesu (11:55-57)

Wakati Pasaka ilipokaribia, watu walikwenda Yerusalem kusudi waweze kuona Yesu. Viongozi kwa maneno ya dini walimtafuta vilevile — kusudi waweze kumkamata kusudi auawe.

**8. MWISHO WA UTUMISHI WA YESU KATIKATI
YA WATU (Sura 12)**

Kupakaliwa mafuta kwa Betania (12:1-8)

Kwa njia ya kwenda Yerusalem kwa Pasaka, Yesu alikaa kwa muda mdogo kwa nyuma ya Lazaro, Maria na Marata. Wakati Maria alipopakaa miguu ya Bwana wake na marasi ya bei gali, Yuda Iskariota alinungunika, akitenda kama alifikili mahitaji ya watu masikini lakini akificha choyo yake mwenyewe. Lakini Bwana alisimamia Maria na kusema hakuna njia nyingi kutumikia Bwana hivi, lakini walikuwa na njia saa zote kutumikia watu masikini.

Shauri kuua Lazaro (12:9-11)

Wakubwa wa makuhani walifanya shauri kuua Lazaro kwani Wayuda wengi waliamini Yesu kwa sababu yake.

Kuingia Yerusalem kama mshindaji (12:12-19)

Ni kama watu walikaribisha Yesu vizuri sana wakati alipofika Yerusalem. Waliweka matawi ya ngazi njiani mbele yake na kutangaza kwamba yeye ni mfalme wa Israeli. Lakini tunajua ya kwamba wengi katikati yao watageuka na kulalamika auawe. Kwanza walilalamika “Hosana” kwa mfalme wao; kisha “asulibishwe”.

Sheria ya mavuno (12:20-26)

Wayunani wengine walitaka kusemezana na Yesu kwa njia ya Filipo na Anderea. Mwokozi alijibu kusema ni lazima kwa mauti kutangulia mavuno. Atatukuzwa kwa njia ya mauti yake kama sadaka, si kwa njia ya kukaa vizuri duniani kama mwalimu. Lazima watumishi wake wamwige na kujitoa wenyewe.

Unabii wa Yesu juu ya maneno yatakayotokea (12:27-33)

Yesu hakuomba aweze kuponyeshwa toka taabu ambayo itampata, lakini Mungu aweze kutukuzwa ndani yake. Kwa dakika ileile Mungu alisema na sauti toka mbinguni ya kwamba amejibu ombi hili. Halafu Yesu alitangaza hukumu ya dunia, kushindwa kwa Shetani, mauti yake mwenyewe kwa njia ya kusulibishwa, na ya kwamba namna zote za watu watakokotwa kwake.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Mwana wa watu ni nani? (12:34-36)

Watu wengine walifazaika namna gani Yesu aliweza kuwa Masiya na kufa vilevile. Kwa njia ya Maandiko walifahamu ya kwamba Masiya ataishi milele. Waliuliza, "Mwana waa watu ni nani?" Alijiita Nuru, na alisema nao kutembea katika nuru, maana wamwamini yeye wakati saa ingali.

Nani aliyeamini habari zetu? (12:37-43)

Yesu alikuwa amefanya maajabu mengi, lakini hata hivi watu wachache walimwamini, kama Isaya alivyotabiri. Kwa sababu ya kutokuamini kwao wengine walipofushwa macho, kama Isaya alivyotabiri miaka mingi mbele. Wengine wa wakubwa walisema walmwamini, lakini hawakumkiri wazi mbele ya watu kwa sababu waliojopa watafukuzwa toka sunagogi.

Maonyo ya Yesu juu ya kutokuamini (12:44-50)

Neno hili lulisukuma Mwokozi kupaza sauti na kuonya watu juu ya hatari ya kutokuamini. Mtu ambaye alimwamini yeye aliamini Baba yake. Kumwona yeye ni kuona Mungu. Alikuja duniani kuwa nuru, si mwamuzi. Wale ambao wanamkataa watahukumiwa na mafundisho yake kwa wakati wa kuja. Alijulisha watu na uaminifu habari za uzima wa milele ambazo Mungu alimwagiza kutangaza.

9. MAFUNDISHO KATIKA CHUMBA CHA JUU (Sura 13-16)

Bwana alifanya kazi ya mtumwa (13:1-11)

Usiku, mbele ya kusulibishwa, Yesu alikutana na wanafunzi wake ndani ya chumba cha juu katika Yerusalem. Wakati walipokuwa wakikula, Shetani alijulisha Yuda kwamba saa imefika kutoa Bwana kwa adui zake.

Bwana akijua vizuri kazi yake na pahali atakapokwenda, alianza kufanya kazi ya mtumwa na kunawa miguu ya wanafunzi. Wakati Petro alipokataa kuacha Bwana kunawa miguu yake, Yesu alitoa mafundisho kwa roho zao. Wanafunzi wake walihitaji kuoshwa mara moja tu kwa kuzaliwa tena, lakini walihitaji kunawiwa miguu mara nyingi kwa Neno la Mungu ili waweze kuwa na upatano mzuri naye na kusafishwa toka uchafu wa dunia. Wanafunzi wote walikuwa safi, maana wameoshwa, ila Yuda.

Yesu alieleza maana ya neno alilofanya (13:12-20)

Halafu Bwana alitoa mafundisho mengine. Walikuwa wamemkiri kuwa Mwalimu na Bwana, hivi iliwapasa kumwiga kwa njia ya

YOANE

kunawana miguu, si miguu ya mwili, lakini roho; si na maji lakini na Neno la Mungu (mash. 12-17). Alisema maneno haya kwa wanafunzi wote ila Yuda. Alikuwa amefahamisha wanafunzi mbele maneno ya Yuda ili wakati neno hili litakapotimia, watajua kwamba yeze ni MIMI NDIYE wa Agano la Kale (mash. 18-20).

Yesu alitabiri kwamba Yuda atamtoa kwa adui (13:21-30)

Wakati Yesu aliposema tena ya kwamba mmoja wao atamtoa kwa mikono ya adui, wanafunzi walifazaika wakitaka kujua alikuwa akisema juu ya nani. Mwishoni aliwafahamisha wazi kwa njia ya kutowelea tonge ndani ya mchuzi na kumpa Yuda. Yule mhaini alitoka mara moja.

Amri mpya (13:31-35)

Akitazamia Kalvari, Yesu alisema ametukuzwa, na Mungu atamtuza kwa njia ya kumfufua toka wafu. Kisha aliwajulisha kwa mba atawaondokea nyuma kidogo nao hawataweza kumfuata kwanza. Lakini aliwaachia amri mpya — kupendana; ndiyo mapendo ya yatakuwa alama ya wanafunzi wake.

Yesu alitabiri kwamba Petro atamkana (13:36-38)

Petro alisihi Bwana kumruhusu kwenda pamoja naye, na hata kutoa uzima wake kwa ajili yake. Lakini Yesu alimjulisha ya kwamba kwa pahali pa kufanya hivi Petro atamkana mara tatu mbele ya asubui!

Yesu anatia wanafunzi wake moyo (14:1-11)

Bwana Yesu aliendelea na hotuba yake katika chumba cha juu na ahadi ya kwamba atakuja tena kupeleka watu wake mbinguni. Alijibu ulizo la Tomasi juu ya njia akisema yeze mwenyewe ndiye njia, njia ya pekee kufika kwa Baba. Jibu hili lilitukuma Filipo kuomba Yesu kuwapeleka kuona Baba. Yesu alieleza kwamba yeze na Baba waliungana karibu karibu hata mtu ye yote ambaye alimwona yeze aliona Baba. Maneno aliyosema na alama alizofanya zilikuwa maneno na kazi za Baba, na ilipasa alama hizi kuaminisha wanafunzi umoja wa Baba na Mwana.

Maombi kwa jina la Yesu (14:12-14)

Kristo aliwaambia wanafunzi wake ya kwamba kama wakiomba kwa jina lake wataweza kufanya maajabu makubwa kupita, maana maajabu yatakayogusa watu wengi zaidi ndani ya sehemu kubwa zaidi ya inchi.

Msaidizi mwingine (14:15-21)

Halafu Mwokozi aliahidi kuomba Baba kutuma “msaidizi mwi-

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

ngine,” ndiye Roho Mtakatifu atakayekaa pamoja na wanafunzi na kuwa ndani yao. Hivi Yesu hatawaacha yatima lakini atarudi karibu nao (kwa njia ya Roho Mtakatifu). Watamwona kwa imani na kufurahi ndani ya ushirika wa karibu naye. Kwa njia ya kutii kwao wataonyesha kwamba walimpenda na watapendwa na Baba na Mwana.

Upatano na Yesu na Baba yake (14:22-24)

Wakati Yuda mwingine (si Yuda Iskariota) alipouliza kwa sababu gani Yesu atajionyesha kwao lakini si kwa dunia (sh.19), Bwana ali-jibu ya kwamba wale tu amba walimpenda na kumtii wanawenza kuwa na ushirika na Baba na yeze mwenyewe.

Bwana aliwaachia salama (14:25-27)

Wakati Kristo atakapokuwa mbali nao, Msaidizi atafundisha wanafunzi na kuwakumbusha maneno ya Mwokozi. Yesu aliwaachia salama yake ili wasisumbuke wala kuwa na woga moyoni.

Furaha kwa sababu Yesu atafika tena karibu na Baba (14:28-31)

Kama wanafunzi wangalimpenda, wangalifurahi kwa sababu alikuwa akirudi mbinguni, na hatazarauliwa na watu tena. Wakati Yesu alipokuwa kwanza duniani, Baba alikuwa mkubwa kupita yeze kwa macho ya watu lakini si kwa uungu wake (sh.28). Wataamini wakati aliporudi mbinguni. Lakini sasa Shetani alikaribia na ilipasa Bwana kutoka na kufanya mapenzi ya Baba yake (mash. 29-31). She-tani ni mtawala wa dunia hii, ndilo neno linaloonekana pahali pote.

Mzabibu wa kweli (15:1-8)

Sharti tufahamu ya kwamba hotuba juu ya mzabibu na matawi ni juu ya utumishi, si wokovu. Yesu ni mzabibu wa kweli, Baba yake ni mlimaji. Tawi lisilozaa matunda ni mwamini anayetembea katika mwili, naye anaazibwa na Bwana. Tawi lenye kuzaa matunda, maana Mkristo anayekaa kupata nguvu katika roho, anasafishwa ili aweze kuzaa matunda kupita. Kuna njia moja tu kwa tawi kuzaa matunda, ndiyo kukaa ndani ya mzabibu. Mkristo asiyekaa ndani ya Bwana atapoteza ushuhuda wake; ni kama watu wanatupa ushuhuda wake katika moto. Kwa njia ya kukaa ndani ya Kristo, mwamini ana uwezo katika maombi yake, na anaonyesha matunda ya Roho, anatukuzu Mungu na kuhakikisha kwamba yeze ni mwanafunzi wa kweli wa Kristo.

Mapendo na furaha kwa njia ya kutii (15:9-17)

Mapendo, utii, na furaha zinafungana pamoja. Mapendo kwa Kristo yanatusukuma kutii maagizo yake, na kama tukitii maagizo

YOANE

yake, tutakaa katika mapendo yake. Halafu neno hili linatujaza na furaha. Maana ya utii ni kupendana hata mauti. Utii unafanyiza waamini rafiki za Kristo, si watumishi tu, na kama wakikuwa rafiki, wanaweza kujua mambo na kazi ya Bwana wao, Wakristo wamechaguliwa kuzaa matunda yatakayokaa, na kuomba na uwezo. Lakini msingi wa maneno haya ndio kupendana katikati yao.

Machukio ya dunia (15:18-25)

Wanafunzi wakae tayari kuchukiwa na kuteswa na watu wa dunia kwa sababu wao wenyewe si wa dunia. Watumishi wasizani watatendewa vizuri kuita Bwana wao. Kama Yesu asingalifika na kusema na dunia na kufanya maajabu yasiyofanywa na wengine, zambi za watu zisingalikuwa kubwa. Lakini sasa zambi yao ilikuwa kuchukia Baba na yeche mwenyewe bila sababu. Hawakuwa na uzuru.

Ushuhuda kwa Kristo kwa wakati wa kuja (15:26-27)

Msaиди atakayekuja, ndiye Roho Mtakatifu, atashuhudia Kristo, na sharti wanafunzi watoe ushuhuda vilevile juu ya maneno waliyoona na kusikia tangu mwanzo.

Wanafunzi watakataliwa (16:1-4)

Yesu alijulisha wanafunzi wake mbele ya kwamba watu watawatokeza kwa masunagogi, na hata kuwaua. Watateswa hivi kwa sababu watu walikataa Yesu, na Baba. Wakijua maneno haya mbele, haya-takuwa kikwazo kwao.

Kazi ya Roho Mtakatifu (16:1-15)

Ilipasa Yesu kuwaambia sasa ya kwamba alikuwa akikwenda zake, hata kama neno hili liliwahuzunisha. Lakini atatuma Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu atakuwa duniani na neno hili litahukumu dunia juu ya zambi ya kukataa Kristo; ataaminisha dunia ya kwamba Kristo ni kweli Mwana wa Mungu, hivi Shetani atahukumiwa pamoja na wasioamini wote. Mwokozi angaliweza kuwaambia wanafunzi maneno mengine vilevile kama wangalikuwa tayari kuyapokea, lakini Roho atakuja na kuwaongoza katika yote yaliyo kweli. Atasema tu maneno abayo Baba atamwongoza kusema na atatkuza Kristo.

Huzuni inaageuka furaha (16:16-22)

Wanafunza watakuwa na huzuni wakati Yesu atakapokufa na nyuma wakati atakaporudi mbinguni. Lakini watafurahi wakati watakapomwona nyuma ya ufufuko wake, wakati Roho Mtakatifu atakapokuja, na nyuma wakati Kristo atakapokuja tena. Wakati watakapomwona tena watasahau mbio huzuni ambayo walikuwa nayo mbele.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Kristo mwenye kushinda dunia (16:23-33)

Wakati Yesu alipokuwa pamoja nao wanafunzi walimwomba ye ye juu ya maneno yao. Sasa waliweza kuomba Baba kwa jina la Yesu na kuua ya kwamba watapata majibu kwa maombi yao. Neno hili litawa-jaza furaha. Kufika wakati ule Bwana Yesu alitumia mifano ndani ya masemo yake, yenyewe maana isiyonekana wazi. Kwa njia ya Roho Mtakatifu atakayekuja, atawenza kusema wazi, nao wataomba kwa Baba katika jina lake. Baba aliwapenda kwa sababu walipenda Mwana na kuamini ya kwamba alikuwa ametoka kwa Baba. Ni kama wanafunzi walifahamu maneno haya, lakini alisema ya kwamba ndani ya saa za giza zilizokuwa mbele yao, wao wote watamwacha — ila Baba. Halafu alieleza ya kwamba alikuwa amesema maneno haya yote kusudi waweze kuwa na salama wakati wa mateso, kwa sababu alikuwa ameshinda dunia.

10. OMBI LA YESU KAMA KUHANI MKUBWA (Sura 17)

Kama Kuhani Mkubwa Bwana wetu aliombea watu wake lakini si dunia. Hakulaumu wafuata wake hata kama walifanya zambi na kuanjuka tena na tena. Anaomba waweze kusitawi katika roho, lakini hakuomba waweze kuwa watajiri. Aliomba maneno saba,mawili kwa ye ye mwenyewe, matatu kwa wanafunzi wake, na wawili kwa wale ambao watamwamini kwa wakati wa kuja.

Ombi la kwanza (17:1-4)

Aliomba Baba aweze kumtukuza kwa njia ya kumfufua toka wafu, ili aweze kutukuza Baba kwa njia ya kuwapa uzima wa milele wote ambao Mungu alimpa.

Ombi la pili (17:5)

Halafu aliomba Baba kumheshimu mbinguni na utukufu ambao alikuwa nao mbele ya kugeuka mtu, lakini sasa kama Mtu na Mungu vilevile.

Yesu alifunua Baba (17:6-10)

Zaidi ya maombi haya, Bwana Yesu alisema ya kwamba alikuwa amefunua Baba kwa wanafunzi wake, alikuwa amewapa maneno ambayo Mungu alimpa ye ye, nao walijua kwamba alitoka kwa Baba. Kama Kuhani Mkubwa aliomba kwa watu wake, si kwa dunia. Lakini neno hili halikani ya kwamba anapenda wapotevu wote duniani.

Ombi la tatu (17:11-12)

Ombi la tatu ni kwa Mungu kulinda wanafunzi. Tunafikili aliwaza

YOANE

waweze kusimama imara katika imani, kwa sababu mara moja nyuma ya mashairi haya tunasoma juu Yuda aliyeacha kumfuata.

Yesu analeta furaha (17:13-14)

Yesu alikuwa akisema maneno haya duniani, ili furaha ya wanafunzi iweze kutimizwa, hata kama dunia iliwachukia.

Ombi la ine (17:15-16)

Ombi la ine: wanafunzi waweze kuchungwa kwa yule mwovu, ndiye Shetani kwani wao si tena wa dunia unaotawaliwa na Shetani.

Ombi la tano (17:17-19)

Ombi la ine: wanafunzi waweze kutakaswa, kuwekwa mbali kwa Mungu katika kweli yake.

Ombi la sita (17:20-23)

Ombi la sita: kwa wote watakaoamini kwa wakati wa kuja, waweze kuwa na moyo moja kunaofanana na Kristo, ili watu wa dunia waweze kuamini ya kwamba Mungu alimtuma.

Ombi la saba (17:24)

Mwishoni, Kristo aliomba ili kwa wakati wa kuja waamini wote waweze kuwa pamoja naye na kutazama utukufu wake.

Mwisho wa maombi (17:25-26)

Ndani ya mashairi mawili ya mwisho ya sura hii Bwana alisema juu ya kazi aliyofanya, na atakayofanya ndani ya maisha ya wanafunzi wake.

11. YESU ALITOLEWA KWA ADUI, ALITESWA, NA KUSULIBISHWA (Sura 18-19)

Alitolewa kwa adui na kufungwakatika Getesemane (18:1-11)

Nyuma ya kwenda kwa Yesu na wanafunzi wake kwa shamba la Getesemane, Yuda alifika na kikosi cha askari kumfunga. Askari na wakubwa wao walishituka kwanza wakati Bwana alipojiita NI MIMI, ndiye Yehova wa Agano la Kale. Petro alijaribu kuzuiza askari kufunga Yesu kwa njia ya kupiga mtumishi wa kuhani mkubwa na upanga, lakini Yesu alisema naye kuacha kufanya hivi.

Yesu mbele ya Kayafa; Petro alimkana mara tatu (18:12-27)

Askari walikamata Mwokozi na kumpeleka kwa Ana, baba ya mke wa Kayafa, kwa sehemu ya kwanza ya hukumu ya dini. Petro aliyekuwa katika kiwanja cha kuhani mkubwa, alikana kwamba yeze ni mwanafunzi wa Yesu (mash. 12-18).

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Wakati alipoulizwa, Bwana alikataa kwamba amesema au kufanya neno baya lo lote, basi mmoja wa watumishi alimpiga kofi. Yesu aliuliza kama walikuwa na ruhusa kumpiga wakati ilipowashinda kuhakikisha kwamba alitenda mabaya. Halafu Ana alimtuma kwa Kayafa, kuhani mkubwa, kwa sehemu ya pili ya hukumu ya dini tusiyosoma habari zake ndani ya Habari Njema ya Yoane. Kwa wakati ule, mbele ya mapambazuko, Petro alikana Bwana mara mbili nyingine (mash. 19-27). Sehemu ya tatu ya hukumu ile ilikuwa asubui mbele ya wakubwa wa makuhanai na wazee wa watu (Mat. 27:1).

Yesu mbele ya Pilato (18:28-40)

Sehemu ya kwanza ya hukumu ya serikali ilikuwa mbele ya Pilato. Liwali huyu ya Waroma alijaribu kusukuma jambo hili kwa Wayuda tena, lakini walimkumbusha kwamba hawakuwa na ruhusa kuhukumu mtu ye yote. Pilato alitangaza kwamba Yesu hakuwa na kosa. Kisha alisema atamfungua kwani ilikuwa desturi kufungua mfungwa mmoja kwa wakati wa Pasaka, lakini makutano walilalamika afungue mnyanganyi jina lake Baraba kwa pahali pa Yesu.

Yesu alizihakiwa na askari (19:1-16)

Pilato alikaa kusema Yesu hakuwa na kosa, lakini makutano walizidi kukusema na nguvu sharti asulibishwe. Walimpiga, walimtia taji la miiba, vazi jekundu, na kumzara ... hii ndiyo namna viumbe waliyotendea Mwumba wao! Liwali aliogopa wakati aliposikia Yesu akisema ye ye ni Mwana wa Mungu, lakini mwishoni, wakati makutano waliyosema Yesu ni mfalme mshindani wa Kaisari, alifanya neno waliloomba.

Yesu anasulibishwa (19:17-27)

Askari walikamata Yesu na kumsulibisha kwa Golgota katikati ya wanyanganyi wawili. Wakati Pilato alipoagizwa andiko liwekwe lililoita Yesu Mfalme wa Wayuda. Wakuwa wa makuhani hawakukubali neno hili hata kidogo, lakini Pilato alikataa kuligeuza. Askari waligawa mavazi ya Mwokozi katikati yao, wakapiga kura kwa kanzu isiyoshonwa. Toka msalaba Yesu aliweka mama yake kwa mikono ya mtume Yoane achungwe naye.

Kristo anakufa kwa wazalimu (19:28-30)

Wakati Mwokozi aliposema ana kiu, askari walimsiki kunywa. Nyuma ya kunywa nusu yake, alilalamika, "Imekwisha" — ndiyo mauti yake kama sadaka kwa wokovu wa wenye zambi, akatoa roho yake.

Mwokozi alichomwa mbavu yake (19:31-37)

Askari walitaka wale waliosulibishwa wafe mbio kwa sababu saba-

YOANE

to ilikuwa imikaribia, hivi walivunja miguu ya wanyanganyi, lakini hawakufanya hivi kwa Yesu kwani waliona kwamba alikuwa amekufa. Lakini askari mmoja alimchoma mbavu yake, na mara moja damu na maji yalitoka.

Kristo alizimwa ndani ya kaburi la Yosefu (19:38-42)

Na ruhusa ya Pilato, Yosefu alikamata mwili wa Yesu na kuufunga ndani ya sanda pamoja na manukato, akamzika ndani ya kaburi lake jipyä.

12. UFUFUKO (Sura 20)

Kaburi wazi (20:1-10)

Wakati Mari Magdalene alipofikia kaburi asubui siku ya kwanza ya juma, alikuta kaburi wazi, basi akakimbia na habari hizi kwa Petro na Yoane. Halafu wao wawili walikimbia kwendea kaburi. Yoane alifika kwanza, lakini Petro alilingia kaburi kwanza na kuona sanda. Kisha Yoane alilingia vilevile, akaamini.

Maria Magdalene (20:11-18)

Wanaume wale wawili walirudi kwao, lakini Maria alibaki kwa kaburi. Kanza aliona malaika wawili, kisha aliona Bwana mwenyewe. Alimtambua mara moja wakati Bwana aliposema jina lake Maria, na ni kama alitaka kumshika miguu. Lakini Yesu alisema ya kwamba atarudi kwa Baba yake. Basi Maria alitii agizo lake, akapelekea wanafunzi habari hizi za ajabu.

Wanafunzi wanatumwa 20:19-23

Mangaribi ile, Bwana Yesu alionekana kwa wanafunzi, akatuliza woga wao, akawaonyesha vidonda vyake na kuwatuma na kionjo cha mbele cha amri ya Roho Mtakatifu, ukaribu na uwezo wake. Lakini Roho Mtakatifu hakutolewa kuwa msaidizi wa daima kufika Pentekote.

Tomasi mwenye shaka anaona na kuamini (20:24-29)

Tomasi alikuwa na shaka wakati aliposikia habari za maneno yaliyokwisha kutokea. Lakini nyuma ya juma moja lingine Yesu alionekana kwa wanafunzi tena, na halafu Tomasi aliamini wakati alipoona alama mwilini wa Kristo za kusulibishwa kwake. Ingalikuwa vizuri kupita kama angaliamini bila kuona kwanza maneno yaliyohakikisha ufufuko wa Yesu.

Yoane aliandika Habari Njema yake na kusudi gani (20:30-31)

Tunaona kusudi hili hapa: “mupate kuamini ya kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mupate uzima kwa jina lake.” Hivi ni kitabu cha Habari Njema kweli.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

13. KRISTO MFUFULIWA PAMOJA NA WATU WAKE KATIKA GALILAYA (Sura 21)

Chakula cha asubui pamoja na Yesu (21:1-14)

Nyuma ya wakati Bwana alionekana kwa wanafunzi nyuma ya kushinda usiku mzima wakivua samaki katika bahari ya Tiberia bila kupata kitu. Aliwaagiza kutupa wavu upande wa kuume wa chombo, na halafu walipata samaki wakubwa 153! Wakati walipofika pwani, waliona kwamba Yesu alikuwa amewatayarishia chakula cha asubui.

Yesu anarudisha Petro (21:15-23)

Kwa mwisho wa chakula Yesu aliulizana na Petro polepole juu ya mapendo yake kwake. Nyuma ya kusikia mara tatu ya kwamba Petro alimpenda, Bwana alimwagiza mara tatu kulisha wana-kondoo na kondoo zake. Halafu Bwana alijulisha Petro kwamba atauawa kwa sababu ya imani yake, akamkataza kusumbuka juu ya maneno yatakayopata wanafunzi wengine. Kazi yake ilikuwa kufuata Kristo yeeye mwenyewe. Hii ndiyo kazi yetu sisi sote.

Habari za mwisho za mwanafunzi mpendwa (21:24-25)

Yoane alisema wazi kwamba hakuandika habari za kazi zote za Yesu. Nafasi ingalikosa duniani nzima kwa vitabu vyote vitaka-voandikwa kwa habari hizi zote.

Matendo ya Mitume

MWANZO

Kitabu cha pili cha Luka

Luka anaendelea na habari zake kuanza na pahali alipoacha kwa mwisho wa Habari Njema yake, ndizo habari za kwenda mbinguni kwa Kristo. Kisha alionyesha namna Habari Njema ilivyoenea katika kizazi kilichofuata Wakristo wa kwanza (muda wa karibu miaka 34).

Sehemu chaguliwa ya historia ya kanisa

Hatupati ndani ya Matendo historia nzima ya Kanisa kwa wakati wa mwanzo wake. Roho Mtakatifu alichagua habari fulani kuonyesha namna gani liliendelea kwa maneno ya Mungu. Kitabu hiki kinaonyesha kutimizwa kwa agizo la Kristo ya kwamba Habari Njema ihubiriwe kwa Wayuda kwanza, kisha kwa Mataifa kama alivyosema katika Matendo 1:8, "... katika Yerusalem, na Yudea yote, na Samaria, na hata mpaka wa dunia." Petro, mtume kwa Wayuda, alioneckana zaidi katika sura 12 za kwanza; nyuma yake Paulo, mtume kwa wasiotahiri (ndio Mataifa) alioneckana zaidi.

Mwito wa Mungu kwa Israeli

Katika muda wa Matendo, Mungu alikaa kuita taifa la Israeli kupokea Bwana Yesu kama Masiya-Mfalme, lakini kwa sababu walizidi kukataa, taifa la Israeli liliwekwa kando na Mataifa waliletwa kwa pahali pa kupokea baraka.

Toka Israeli hata Kanisa

Kwa mwanzo wake Kanisa lilishiriki na dini ya Wayuda, lakini polepole ushirika huu ulipunguka na kwa mwisho wa kitabu, Kanisa lilikuwa limeachana na desturi za dini ya Wayuda, na lilionyesha ya kwamba ni jamii namna nyingine ndani yake Wayuda na Mataifa ni moja katika Kristo.

UMBO LA MATENDO

1. Ahadi ya Bwana nyuma ya kufufuliwa kwake ya kwamba Roho Mtakatifu atakuja (1:1-5)
2. Agizo kwa mitume toka Bwana saa alipokwenda mbinguni (1:6-11)
3. Wanafunzi wanangoja kwa Yerusalem na maombi (1:12-26)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

4. Siku ya Pentekote na kuzaliwa kwa Kanisa (sura 2)
5. Kiwete anaponyeshwa, na agizo la Petro kwa Israeli (sura 3)
6. Kanisa lirateswa na kuongezeka (sura 4-8)
7. Wokovu wa Saulo wa Tarso (9:1-31)
8. Petro alipeleka Habari Njema kwa Mataifa (9:32 – 11:18)
9. Kanisa lilianzwa kwa Antiokia (11:19-30)
10. Mateso toka Herode na kufa kwake (12:1-23)
11. Safari ya kwanza ya Paulo kwa kuhubiri – Galatia (12:24 – 14:28)
12. Kusanyiko kwa Yerusalem (15:1-35)
13. Safari ya pili ya Paulo kwa kuhubiri – Asia Ndogo na Yunani (15:36 - 18:22)
14. Safari ya tatu ya Paulo kwa kuhubiri – Asia Ndogo na Yunani (18:23 - 21:25)
15. Paulo anafungwa na kuhukumiwa (21:26 – 26:32)
16. Safari kwenda Roma na kuharibika kwa merikebu (27:1 – 28:16)
17. Ushuhuda wa Paulo kwa Wayuda katika Roma toka nyumba pahali alipofungwa (28:17-31)

1. AHADI YA BWANA NYUMA YA KUFUFULIWA KWAKE YA KWAMBA ROHO MTAKATIFU ATAUKUJA (1:1-5)

Siku 40 zilikuwa zimepita tangu ufufuko wa Kristo na mitume walikuwa katika Yerusalem. Bwana Yesu aliwaagiza kubaki pale kufika kutimizwa kwa ahadi ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wakati walipokuwa juu ya Mlima wa Mizeituni, waliuliza kama ufalme utarudishwa kwa Israeli wakati gani. Mwokozi aliwaambia ya kwamba kwanza iliwapasa kuwa washuhuda wake kufika hata mwisho wa dunia.

2. AGIZO LA BWANA KWA MITUME SAA ALIPOKWENDA MBINGUNI (1:6-11)

Mara moja nyuma ya maneno haya Bwana Yesu alipanda kwenda mbinguni, na malaika wawili waliondoa mashaka ya wanafunzi ya kwamba atarudi tena namna walivyomwona akikwenda zake.

3. WANAFUNZI WANANGOJA KWA YERUSALEMA NA MAOMBI (1:12-26)

Nyuma ya kurudia mji wanafunzi walikuwa wakiomba pamoja, na Petro alikumbuka Maandiko ya Agano la Kale yaliyoagiza mtu mmoja kuchaguliwa kukomboa Yuda Iskariota. Sharti awe mtu aliyekuwa

MATENDO

pamoja na Bwana Yesu wakati alipokuwa duniani na kumwona nyuma ya ufufuko wake. Walipiga kura na Matia alichaguliwa.

4. SIKU YA PENTEKOTE NA KUZALIWA

KWA KANISA (Sura 2)

Ajabu la Pentekote (2:1-13)

Siku ya Pentekote ilikuwa siku kumi nyuma ya kupanda kwa Kristo mbinguni. Wakati wanafunzi walipokuwa pamoja, Roho ya Mungu alitolewa, kama Bwana alivyoahidi, pamoja na uvumi kama wa upepo unaovuma na nguvu sana, na ndimi kama za moto. Wanafunzi walipokea zawadi ya ajabu ya kuweza kusema mara moja kwa lugha nyingine. Wayuda toka mahali 15 palipozunguka Yerusalem walisikia wanafunzi hawa wa Galilaya wakitangaza matendo makubwa ya Mungu kwa lugha zao, lugha wanafunzi wasizojua mbele.

Elezoo la Pentekote (2:14-21)

Halafu Petro alieleza ya kwamba maneno haya hayakutoka kwa sababu wanafunzi walilewa na mvinyo mpya lakini ya kwamba yalifutana kwa njia nyingine na unabii wa Yoeli juu ya kumwangwa kwa Roho Mtakatifu. Lakini si maneno yote Yoeli aliyatobiri yalitimizwa siku ya Pentekote, na *hayatatimizwa* kufika wakati Kristo ataka-kapokuja kutawala dunia.

Maonyo ya Pentekote (2:22-36)

Na uhdari Petro alishitaki wanaume wa Israeli kusema ni wao walioua Yesu wa Nazareti. Aliongeza tangazo hili la kushangaza, ya kwamba Mungu alikuwa amemfufua toka wafu. Alieleza ya kwamba wakati Daudi aliposema juu ya kufufuliwa toka wafu, hakusema juu yake mwenyewe lakini juu ya Masiya. Sasa neno lenyewe lilikuwa limetokea — Yesu alikuwa Masiya naye alikuwa amefufuliwa na kutukuzwa kwa mkono wa kuume wa Mungu, na alikuwa ametuma kwao Roho ya Mungu.

Tunda la Pentekote (2:37-47)

Mashitaki ya Petro ya kwamba watu wa Israeli walikuwa wame-sulibisha Masiya wao wenyewe yaliwafahamisha zambi yao kubwa. Walisihi Petro kuwalijisha nini iliwapasa kufanya. Petro aliwaagiza “kutubu na kubatizwa wapate ondoleo la zambi” ili waweze kupokea Roho Mtakatifu na kuokolewa toka kizazi kile waliosulibisha Mwo-kozi. Karibu watu 3,000 walitii agizo hili na Kanisa lilianzwa. Waamini wale wa sasa walidumu kukutana pamoja, waliona maajabu yaliyofanywa na mitume, walishiriki mali yao kama wengine walikuwa na hitaji, na walisifu Mungu kwa wokovu wao.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Walidumu katika mafundisho ya mitume, katika ushirika, na katika kuvunja mkate na kuomba. Maneno haya mane ndiyo sharti kwa kila kanisa.

5. KIWETE ANAPONYESHWA, NA AGIZO LA PETRO KWA ISRAELI (Sura 3)

Kuponyeshwa kwa kiwete (3:1-11)

Siku moja wakati Petro na Yoane walipokwenda hekalu, walikutana na kiwete mmoja ambaye aliwaomba kumpa mali. Walimpa neno zuri kupita mali — kwa uwezo wa Yesu aliponyeshwa. Watu walioona ajabu hili walishangaa sana.

Hotuba ya Habari Njema ya Petro (3:12-26)

Neno hili lilimpa Petro njia kuwahubiri Habari Njema. Alieleza ya kwamba si yeze na Yoane walioponyesha mtu huyu — aliquwa *Mungu*, Baba ya Bwana Yesu. Wayuda walikuwa wametoa Yesu kwa Mataifa, walimkataa, waliomba Baraba afunguliwe na Yesu auawe na Waroma. Lakini Mungu alimfufua toka wafu, na sasa ajabu hili lilyanfanya kwa njia ya imani katika jina lake. Na roho ya neema Petro alisema ya kwamba watu walikuwa wametenda kwa ujinga na ya kwamba wakitubu Mungu atasamehe zambi zao na kutuma Yesu karibu nao tena. Kama wasipofanya hivi Bwana atabaki mbinguni kufika wakati atakaporudi kusimamisha ufalme wake duniani. Huu utakuwa muda wa salama na usitawi ambao Musa na manabii walitabiri juu yake. Ahadi hizi za ufalme zilifanya kwa wasikiaji wa Petro na kwa watu wengine vilevile. Kama wakipokea Masiya, zambi zao zitaondoshwa. Wale watakaokataa kusikia Nabii wa Mungu wataharibiwa.

6. KANISA LINATESWA NA KUONGEZEEKA (Sura 4-8)

Petro na Yoane wanafungwa (4:1-4)

Viongozi vya Wayuda kwa maneno ya dini walikasirika sana sana kwa sababu Petro na Yoane walikuwa wakihubiri juu ya Yesu na ufu-fuko, hivi waliwaweka katika kifungo kufika asubui. Kwa wakati ule wanaume 5,000 walikuwa wameamini.

Hotuba ya Petro kwa wakubwa wa baraza (4:5-12)

Kesho yake wanafunzi walismama mbele ya wakubwa wa baraza waeleze kama walifanya maneno haya kwa amri ya nani. Neno hili lilimpa Petro njia kushuhudia Kristo! Alitangaza na uhodari ya kwa-mba yeze na Yoane walikuwa wamefanya maneno haya kwa jina la

MATENDO

Yesu, ndiye aliyeuawa na Wayuda na kufufuliwa na Mungu, na aliyeponyesha kiwete mwenye kuomba mali. Viongozi wa Wayuda walikuwa wamekataa Yesu, lakini alikuwa ametukuzwa na kukalishwa kwa mkono wa kuume wa Mungu, na hakuna njia kwa watu kuokolewa ila kwa yeye.

Mitume wanakatazwa wasihubiri kwa jina la Yesu (4:13-18)

Watu wa baraza walishangaa juu ya uhodari wa mitume na hawakuweza kubisha ya kwamba kiwete huyu aliponyeshwa kweli. Basi walikataza wafuata wa Yesu wasiseme na watu tena juu yake.

Kusikiliza Mungu kupita watu (4:19-22)

Petro na Yoane walieleza ya kwamba iliwapasa kutii Mungu kupita watu, ya kwamba walilazimishwa na Mungu kuhubiri Habari Njema. Nyuma ya kuwaogopesha tena, wakubwa waliwafungua kwani walijua watu wangalisimama kwa upande wa mitume.

Maombi kwa uhodari (4:23-31)

Wakati Petro na Yoane walipojulisha Wakristo wengine habari za maneno yaliyokwisha kutokea wao wote waliomba Bwana juu ya mambo haya. Waliona ya kwamba maneno yaliyokwisha kutokea yali-fanana na Zaburi 2, wakaomba Mungu kuwapa watumishi wake uhodari na kukaa kufanya maajabu kwa njia yao. Pahali walipokutana pali-tikisha, wanafunzi wakajazwa Roho Mtakatifu na kuhubiri na uhodari.

Vitu vyote kwa ushirika (4:32-37)

Waamini katika Yerusalem hawakuweka roho juu ya mali na vitu vyao, wakauza mashamba na nyumba kusaidia waamini wenyewe uhitaji. Barnaba vilevile alileta kwa mitume mali aliypata kwa njia ya kuuza shamba waweze kuitumia kusaidia mahitaji ya waamini wengine.

Kusema uwongo kwa Roho Mtakatifu (5:1-16)

Anania na Safira walifanya hivi vilevile, wakatenda *kwa hila* ya kwamba walilettea mitume mali *yote* waliyopata, lakini walichunga nusu yake kwa mahitaji yao wenye. Wakati Petro alipouliza Anania juu ya udanganyifu huu, Anania alianguka mfu. Kisha Safira alikuja na Petro aliulizana naye juu ya neno hili vilevile. Alikubali ya kwamba ilikuwa kweli, naye vilevile alianguka mfu. Halafu watu walifahamu ya kwamba Mungu anahukumu zambi kanisani, mara nyininge kwa njia ya kushangaza. Walifahamu ya kwamba ni neno kubwa, neno la hatari kufungana na Wakristo. Hata hivi watu wengi sana waliamini na watu wengi zaidi walifikia mitume waweze kuponyeshwa.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Mahubiri, mateso, na kifungo (5:17-28)

Viongozi kwa maneno ya dini walikasirika kwa sababu mitume walikaa kuhubiri Habari Njema, wakawaweka katika kifungo kusudi wahukumiwe kesho yake. Katikati ya usiku malaika alifungua kifungo, akaagiza mitume kurudia hekalu na kukaa kuhubiri. Hivi wakati watumishi walipokwenda asubui kuwaleta kwa hukumu walikuta kifungo kilifungwa salama — lakini wafungwa walikuwa wametoweka! Wangali wakubwa walipofazaika juu ya neno hili, njumbe alifika na habari ya kwamba mitume walikuwa wakihubiri tena katika kiwanja cha hekalu! Mwishoni mitume waliletwa tena kwa baraza kueleza kwa sababu gani walikaa kuasi agizo la wakubwa.

Kutii Mungu kuliko watu (5:29-32)

Basi Petro alipata njia nzuri sana tena kwa kuhubiri! Alisema kwa nguvu ya kwamba wakati maagizo ya Mungu na watu yasipopatana, ni lazima kwa mwamini kutii Mungu. Alishitaki wakubwa tena bila woga juu ya mauti ya Mwana wa Mungu, akawakumbusha ya kwamba Mungu alikuwa amemtukuza kuwa Mkubwa na Mwokozi na alitaka kutoa toba na usamehe kwa jina lake.

Maonyo ya Gamalieli kwa baraza (5:33-42)

Watawala walijaa gazabu hata walifanya shauri kuua wanafunzi, lakini Gamalieli, Mfarisayo mwenye heshima aliwasihii kuwa na kiasi. Alisema kama dini hii mpya isipotoka kwa Mungu, itakwisha nyuma kidogo. Lakini kama ikitoka kwa Mungu kweli, halafu watawala wangeshindana na Mungu! Basi walipokea shauri lake, wakapiga mitume na kuwakataza wasihubiri tena kwa jina la Yesu, wakawafungua. Mitume walikwenda zao na furaha, bila kuogopeshwa hata kidogo, wakaendelea kufundisha na kuhubiri Habari Njema ya Yesu Kristo.

Manunguniko kanisani (6:1-7)

Magomvi ya kwanza kanisani yalikuwa juu ya mali na vyakula. Wengine wa Wayuda waliosema Kiyunani walifikili wajane wa Waebrania wa Yerusalem na Yudea walipewa msaada kupita wajane wao wenyewe. Halafu mitume walisema na waamini wa kanisa vizuri wachague watu saba kuangalia maneno ya magawio ya kila siku. Ni kama zaidi ya wale waliochaguliwa walikuwa Wayuda wenyewe kusema Kiyunani, ndilo neno lililoweza kusaidia roho za wenyewe kununguni. Halafu watu wengi waliokolewa na Kanisa liliendelea na kupata nguvu.

Stefano alishitakiwa juu ya kukufuru (6:8-15)

Stefano alikuwa mmoja wa wale waliochaguliwa kuangalia maneno

MATENDO

ya mali ya kanisa. Alikuwa na ushuhuda wa uwezo kabisa na kufanya maajabu hata wengine katika sunagogi walitaka kumnyamazisha kwa njia ya kushindana naye kwa maneno. Neno hili liliwashinda, hivi waliagiza akamatwe na kuletwa mbele ya wakubwa wa baraza, akiwa ameshitakiwa ya kwamba alisema maneno ya kukufuru juu ya hekalu na sheria ya Musa.

Hotuba ya Stefano (7:1-53)

Ndani ya jibu lake, Stefano alikumbusha wasikiaji wake kwanza kwa ufupi historia ya Abrahamu (mash. 1-8); akaendelea na habari za Yosefu aliyeataliwa na watu wake wenyewe lakini aliyetukuzwa na Mungu kuwa mwokozi wao (mash. 9-19). Musa alijuana vilevile na kukataliwa na watu hata kama Mungu alikuwa amemsimamisha kuwa mwokozi wao (mash. 20-43). Alijibu mashitaki yao ya kwamba alisema maneno mabaya juu ya hekalu kwa njia ya kukumbusha wakubwa wa baraza ya kwamba taifa la Israeli walikuwa wakiabudu majeshi ya mbinguni, ndiyo nyota, kwa wakati ule ule Mungu alipokaa katikati yao hemani. Alikumbusha wasikiaji wake habari za hema kwa wakati wa Yosua na Daudi, kisha alieleza ya kwamba hali ya roho na maisha ya watu ni neno kubwa kupita majengo kwa macho ya Mungu (mash. 44-50).

Alijibu mashitaki yao juu ya kukufuru torati kwa njia ya kusema wao walikuwa wakidumu kushindana na Roho Mtakatifu na hawakushika torati. Walikataa viongozi ambavyo Mungu aliwapa, na waliota hata Bwana Yesu, mwenye haki kwa adui zake auawe. Ni wao waliokosa kushika torati — torati waliyopokea kwa amri ya malaika (mash. 51-53)

Mauti ya kwanza kwa ajili ya Kristo (7:54-60)

Wakati Stefano alipowaambia ya kwamba alikuwa ameona mbingu zimefunguliwa na Yesu akisimama kwa mkono wa kuume wa Mungu, wakubwa walijaa gazabu hata walimfukuza toka mji. Inje ya mji aliuwawa kwa njia ya kutupiwa mawe, akiombea wauaji wake. Kijana mmoja, jina lake Saulo alikuwa katikati ya wale waliotazama maneno haya. Tutaona jina lake tena nyuma.

Kanisa linateswa (8:1-4)

Mauti ya Stefano ulikuwa mwanzo wa mateso makubwa kwa kanisa. Waamini wengi walifukuzwa toka Yerusalema, wakakwenda Yudea na Samaria wakipeleka Habari Njema pamoja nao. Saulo alikuwa mtangulizi wa wale walioanza mateso haya.

Utumishi wa Filipo kwa watu wa Samaria (8:5-25)

Filipo, mmoja wa watumishi wa sura 6, alikwendea Samaria kwa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

upande wa kaskazini, akitangaza Kristo na akifanya maajabu mengi. Mchawi mmoja, jina lake Simoni alisema aliamini na alibatizwa (mash. 5-13). Wakati mitume katika Yerusalem waliposikia ya kwamba Wasamaria wengi walikuwa wameamini Bwana, walituma Petro na Yoane, bila shaka kuonyesha ushirika wao na mambo haya yaliyokuwa yakinoteka. Petro na Yoane waliombea waamini wale wa sasa, wakawewekea mikono. Mara moja Wasamaria walipokea Roho Mtakatifu (mash. 14-17). Simoni alitaka kununua zawadi ya kuwapa watu Roho Mtakatifu kwa njia ya kuwewekea mikono, lakini Petro alimhamakia na nguvu (mash. 18-24). Mitume hawa wawili walirudia Yerusalem, lakini kuanza wakati ule walikaa kuhubiri Habari Njema katika miji ya Samaria (sh.25).

Filipo na mtu wa Etiopia (8:26-40)

Mungu aliita Filipo kuondokea Samaria na kukutana na mwenye mamlaka mmoja wa Etiopia aliyeokuwa akirudi kwake nyuma ya kufikia Yerusalem kuabudu. Wakati Filipo alipokaribia gari lake, towashi alikuwa akisoma Isaya 53. Filipo alimwelezea ya kwamba Isaya alikuwa akisema juu ya Yesu, na kazi yake kwa ajili ya zambi za watu. Mwetiopia aliamini, akabatizwa, akakwenda zake akifurahi. Filipo alipelekwa Azoto kwa njia ya ajabu, na toka pale alifika Kaisaria. Azoto uliitwa Asidodi katika Agano la Kale.

7. WOKOVU WA SAULO WA TARSO (9:1-31)

Nuru toka mbinguni (9:1-9)

Saulo wa Tarso alikuwa akikwenda Damasiki kukamata na kufunga waamini. "Kosa" lao lilikuwa kwamba waliyaminu Kristo. Gafula alianguka chini, bila kuweza kuona kitu, akasikia maonyo ya Bwana mfufufiwa. Alifahamu zambi yake, akageuka kwa Kristo kupokea wokovu na kumtumikia. Kisha alikwenda Damasiki, si tena kutesa watakatifu, lakini kama mmoja wao.

Ubatizo na mahubiri ya kwanza ya Saulo (9:10-22)

Hatushangai juu ya kusita kwa Anania wakati Bwana alipomtuma karibu na Saulo kumwezesha kuona tena, kwani alikumbuka taabu kubwa ambayo Saulo aliletu kwa Wakristo. Lakini wakati alipokwenda na kuwekea Saulo mikono, Saulo aliweza kuona tena, akajazwa Roho Mtakatifu, kisha alibatizwa. Nyuma kidogo Saulo alifikia masunagogi katika Damasiki akitangaza ya kwamba Yesu ni Masiya na Mwana wa Mungu. Watu walistaajabu wakati walipooa adui mkali wa Wakristo alikuwa amegeuka mwenye kusimamia imani ya Wakristo na nguvu. Inashinda watu wa dunia kueleza nini iligeuza Saulo. Kuna jibu zuri moja tu, ndilo hili: alizaliwa tena.

MATENDO

Saulo alikimbia na kushuhudia Kristo katika Yerusalem (9:23-31)

Wayuda walifanya shauri kuua Saulo, hivi ilimpasa kukimbia kwa njia ya kupanda ukuta wa mji usiku na kushuka ngambo yake (mash. 23-25). Hatushangai kuona ya kwamba waamini katika Yersalema walikuwa na shaka juu ya Saulo kwanza, lakini Barnaba, mwenye roho ya mapendo, alimpokea kama rafiki. Wakristo walihamini nyuma kidogo ya kwamba Saulo alikuwa mwamini wa kweli wakati walipomsikia akihubiri na uhodari kwa jina la Bwana. Walifahamu ya kwamba Wayuda toka Yunani walitaka kumwua, hivi walimfikisha kwa Kaisaria. Pale aliingia merikebu, akakwenda Tarso. Kisha Kanisa walikaa kwanza na salama, wakapata nguvu rohoni na hesabu ya Wakristo iliongezeka (mash. 26-31).

8. PETRO ANAPELEKA HABARI NJEMA KWA MATAIFA (9:32 – 11:18)

Petro aliponyesha mwanamume mmoja, na mwanamke mmoja alifufuliwa (9:32-43)

Sasa tunasoma tena juu ya Petro. Kwa Luda alikutana na mtu mmoja, jina lake Ainea, aliyekuwa mwenye kupooza tangu miaka minane. Kwa jina la Yesu Kristo Petro aliponyesha. Kwa Yopa kulikuwa mwanamke mmoja, jina lake Dorika, aliyejulikana sana kwa sababu ya matendo yake mema. Watu walihuzunishwa sana wakati alipokufa, kufika wakati Petro aliposema naye, “Tabita, amka!” Alifufuliwa mara moja toka mauti. Watu wengi sana walihamini Bwana kwa sababu ya maajabu haya mawili. Pale Yopa Petro alipanga nyumbani mwa Simoni, mtengenezaji ngozi.

Ono la Kornelio (10:1-8)

Habari Njema ilikuwa imehubiriwa kwa Wayuda na Wasamaria. Sasa saa ilifika kwa watu wa Mataifa kuisikia vilevile. Neno hili lili-fanyikana kwa akida la askari mia. Mtu huyu, Mroma, alikaa kwa Kaisaria. Alikuwa Mtaifa, lakini hata hivi aliabudu Mungu pamoja na maombi na kuwapa wenye mahitaji sadaka nyangi. Bwana alionekana kwake ndani ya ono, akamwagiza kutuma wajumbe karibu na Petro kwa Yopa naye atamwambia nini ilimpasa kufanya.

Ono la Petro (10:9-16)

Ilikuwa desturi kwa Petro aliyefungwa na sheria za dini ya Wayuda kuepuwa watu wa Mataifa kama watu wachafu, hivi ilikuwa lazima kwa roho yake kutayarishwa kwa neno hili. Alikuwa juu ya dari ya nyumba ya Simoni, mtengenezaji ngozi, wakati ndani ya ono alipoona chombo kama nguo kubwa kikishuka toka mbinguni. Ndani ya cho-

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

mbo kulikuwa nyama namna namna na nyama zinazotambaa na ndege. Petro alisikia agizo kuua na kula, lakini mtume alikataa kufanya hivi kwanza kwani hajakula mbele nyama vichafu. Sauti toka mbinguni ilimkataza kuita vichafu vitu ambavyo Mungu alivyotakasa. Maneno haya yalitokea mara tatu, kisha chombo kilipokewa tena mbinguni. Maana ya ono hili ndilo ya kwamba Mataifa si wachafu na ya kwamba ilipasa Petro kuwapokea.

Petro aliitwa kwenda Kaisaria (10:17-23)

Wakati Petro alipokuwa akijaribu kufahamu maneno haya, wajumbe toka Kornelio walifika, wakaeleza ya kwamba bwana wao alitala Petro kwenda Kaisaria. Petro aliwakaribisha na kuwapangisha, kisha alisafiri pamoja nao kwa Kaisaria kesho yake, akiongozwa na Roho Mtakatifu.

Petro alihubiri kwa Mataifa (10:24-43)

Mbele ya kufika kwao Kornelio alikusanya jamaa yake na rafiki zake. Wakati Petro alipofika, ye ye na Kornelio walipashana habari za maono ambayo yaliwakutanisha. Kisha Petro alihubiri Habari Njema juu ya maisha, kufa na ufufuko wa Bwana Yesu na ya kwamba kuna usamehe wa zambi kwa wale wanaoamini.

Roho Mtakatifu aliangukia waamini wa Mataifa (10:44-48)

Hata saa Petro alipokuwa akihubiri, Roho Mtakatifu aliangukia watu wale walioamini nao wakasema kwa lugha, hata Wayuda waliokuwa pale vilevile walishangaa sana. Petro alifahamu ya kwamba Mungu alipokea Mataifa vilevile namna alivyopokea Wayuda, akaagiza Konelio na watu wa nyumba yake kubatizwa. Ona namna matukio yalifuatana: Waliamini, walipokea Roho Mtakatifu, kisha walibatizwa.

Petro alisimamia neema ya Mungu kwa Mataifa (11:1-18)

Wengine wa waamini Wayuda kwa Yerusalem walifazaika wakati waliposikia habari za ushirika wa Petro na watu wa Mataifa. Hivi Petro aliwapasha habari hizi zote, namna chombo kiliviyoshuka toka mbinguni, agizo la Roho Mtakatifu kwaye kwenda Kaisaria, ono la Kornelio ndani yake aliagizwa kutuma watu kuita Petro, na namna Roho Mtakatifu alivyoangukia Kornelio na nyumba yake wakati walipoamini. Wakati waamini katika Yerusalem waliposikia habari hizi walifahamu ya kwamba Mungu alikuwa ameokoa Mataifa namna alivyookoa Wayuda.

MATENDO

9. KANISA LILIANZWA KWA ANTIOKIA (11:19-30)

Kuenea kwa Habari Njema (11:19-21)

Sasa tunasoma tena juu ya mteso yaliyopata kanisa nyuma ya kuuawa kwa Stefano. Wale waliosambazwa toka Yerusalem walipeleka Habari Njema kwa Wayuda katika Foiniki, Kipuro na Kurene. Kisha Habari Njema ilifikia Antioquia, ndio mji toka pale Paulo nao waliofungana naye ndani ya kazi ya Mungu walianza safari zao kupeleka Habari Njema kwa Mataifa.

Barnaba na Saulo kwa kanisa katika Antioquia (11:22-26)

Wakati kanisa katika Yerusalem waliposikia habari za baraka ya Habari Njema katika Antioquia, walituma Barnaba kuangalia neno hili. Aliona mara moja ya kwamba Mungu alikuwa akifanya kazi pale kwa uwezo, hivi alionya waamini kuendelea kwa Bwana. Kisha akifahamu ya kwamba Saulo angeweza kusaidia kanisa hili la sasa, alikwenda Tarso, akamleta kwa Antioquia, wakafundisha waamini pale pamoja kwa mwaka mmoja. Wanafunzi waliitwa kwanza Wakristo katika Antioquia.

Waamini wa Antioquia walituma zawadi kwa wale katika Yerusalem (11:27-30)

Kwa wakati ule manabii walifikia Antioquia toka Yerusalem, na mmoja wao, jina lake Agabo, alitabiri ya kwamba kutakuwa na njaa kubwa. Wakati unabii huu ulipotimizwa, waamini wa Mataifa walituma zawadi kwa mikono ya Barnaba na Saulo kusaidia waamini Wayuda katika Yudea. Neno hili lilionyesha ya kwamba uadui wa Wayuda na Mataifa unaondoshwa ndani ya Kristo.

10. MATESO TOKA HERODE NA KUFA KWAKE (12:1-23)

Petro aliponyeshwa toka mauti (12:1-17)

Kwa kupendeza adui za Wakristo, Mfalme Herode Agripa 1 aliagiza Yakobo, ndugu ya Yoane, auawe, na alikusudi kufanya vivyo hivyo na Petro. Usiku uliotangulia siku iliyochaguliwa kwa kuuawa kwake, malaika alitokea ndani ya chumba pahali Petro alipokuwa ndani ya kifungo, akamtoa kule na kumwongoza kutoka gereza, kisha alitoweka. Mtume alikwenda mara moja kwa nyumba ya Maria, mama ya Marko, pahali wanafunzi walipokuwa wakimwombea. Hawakuamini mara moja ya kwamba alikuwa kweli Petro akipiga hodi kwa mlango, lakini mwishoni walimfungulia na halafu walifurahi sana. Petro aliwapasha habari za namna alivyoponyeshwa kwa njia ya ajabu, kisha alikwenda zake.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Hukumu ya walini wa Petro (12:18-19)

Mfalme alikasirika sana sana wakati aliposikia ya kwamba Petro alikuwa ameponyoka. Nyuma ya kuuliza uliza walini aliagiza wauawe.

Mauti ya Herode (12:20-23)

Herode hakufahamu ya kwamba mauti yake mwenyewe ilikuwa karibu. Nyuma ya muda mfupi, mfalme alikuwa katika Kaisaria. Saa yenye we watu toka Tiro na Sidona walifika kutafuta salama naye kwa sababu watu wa inchi yao walisaidiwa na vyakula toka Yudea. Walisema sauti ya Herode ni sauti ya Mungu akisema nao wakati Herode alipokutana nao mbele ya watu wa mji. Kwa sababu Herode alikubali masemo haya ya kumheshimu, malaika ya Bwana alimpiga na ugonjwa mbaya sana, akakufa.

11. SAFARI YA KWANZA YA PAULO KWA KUHUBIRI — GALATIA (12:24 – 14:28)

Habari Njema ilikaa kuenea (12:24-25)

Habari Njema ilikaa kuenea hata kama kulikuwa na ushindani. Nyuma ya kumaliza kazi yao kwa Yerusalem Barnaba na Saulo walirudia Antioquia pamoja na Yoane Marko.

Barnaba na Saulo walitumwa kwa kazi ya Mungu (13:1-3)

Roho Mtakatifu alionyesha kwa manabii na walimu katika kanisa la Antioquia ya kwamba alitaka Barnaba na Saulo kufanya kazi fulani, hivi waliwekeea ndugu hawa wawili mikono, wakawatumwa kwa kazi hii. Huu ndio mwanzo wa safari ya kwanza ya Paulo kwa kuhubiri. Kwa safari hii walizunguka na kufikia pahali pengi katika Asia Ndogo.

Habari Njema kwa Kipuro (13:4-12)

Wajumbe wa Habari Njema walisafiri toka Seleukia kwenda Salami kwa kisanga cha Kipuro, wakahubiri Habari ndani ya masunagogi ya Wayuda pale. Kisha walitambuka kisanga kwenda Pafo pahali mtawala, Sergio Paulo, alipookolewa hata kama mchawi, jina lake Bara-Yesu alishindana nao.

Yoane Marko aliondoka akarudia Yerusalem (13:13-15)

Toka Kipuro walisafiri kwenda Perga na Pamfilia kwa pwani ya kusini ya Asia Ndogo. Yoane Marko aliachana na wahubiri pale, akarudia Yerusalem. Kisha wahubiri waliendelea na safari yao kwenda Antioquia katika Pisidia, kama 160 km toka Perga kwa upande wa kaskazini. Wakubwa wa sunagogi la pahali waliwaomba kufundisha.

MATENDO

Paulo alihubiri kwa Antioquia katika Pisidia (13:16-41)

Ndani ya hotuba yake, Paulo alikumbusha wasikiaji wake ya kwamba Mungu alichagua Israeli, namna alivyowalinda jangwani, na kuwapa inchi ya Kanana, muda wa waamuzi, habari za ufalme wakati Saulo na Daudi walipokuwa wafalme, na utumishi wa Yoane Mbatizaji. Habari hizi zote zilimwongoza kusema juu ya Kristo, kuhukumiwa kwake na watu, mauti yake, kuzikwa kwake, na ufufuko wake uliokwisha kuhakikishwa. Kwa mwisho wa hotuba yake mtume aliwakumbusha ya kwamba Mungu alitaka kusamehe zambi zao na ku wahesabia haki kwa njia ya imani mbali na sheria, akawaonya wasikatae wokovu wa Mungu.

Namna watu walivyopokea Habari Njema (13:42-52)

Wengi wa Wayuda walipokea mafundisho haya vizuri, wakaomba kusikia mengine siku ya sabato ya nyuma (mash. 42-43). Lakini nyuma ya juma moja Wayuda wasioamini walishindana nao sana, hivi Paulo na Barnaba waliwaambia wazi ya kwamba kwa sababu wali-kuwa wakijihukumu wenyewe kuwa watu wasiostahili kupokea uzima wa milele, Habari Njema itahubiriwa kwa Mataifa kuanza saa ile. Wasikiaji wa Mataifa walifurahi kusikia habari hizi, lakini Wayuda walifukuza mitume toka pale. Paulo na Barnaba waliwakungutia mavumbi ya miguu yao, wakakwenda Ikonio (mash. 44-52).

Paulo na Barnaba walipata matata kwa Ikonio (14:1-7)

Mitume walihubiri katika sunagogi kwa Ikonio na Wayuda na Wayunani wengi waliamini, lakini Wayuda wasioamini waliamsha gazabu ya watu wa Mataifa na pamoja walifanya vita juu ya mitume. Paulo na Barnaba walipata habari ya kwamba adui zao walitaka kuwatupia mawe, basi wakakimbia, wakakwenda Listra na Derbe katikati ya Asia Ndogo.

Kwa Listra watu walifikili Paulo na Barnaba ni miungu (14:8-18)

Paulo aliponyesha kiwete kwa Listra. Neno hili lilishangaza watu sana hata walitaka kuabudu mitume kama miungu ya Wayunani. Hata kuhani wa Zeu alitaka kutoa sadaka kubwa ku waheshimu. Wakati mitume walipofahamu maana ya maneno yaliyokuwa yaktitea, walikataa kuabudiwa, wakaonya watu ya kwamba maneno haya si vizuri. Walieleza ya kuwa wao wenyewe walikuwa watu tu waliopewa kazi ya kuhubiri Habari Njema ili watu wageuke toka maneno haya ya bule na kuabudu Mungu aliye hai. Halafu watu waliacha kuwaabudu.

Paulo alitupiwa mawe lakini alipona (14:19-20)

Nyuma kidogo Wayuda toka Antioquia katika Pisidia walifikia Ikonio, wakaamsha uadui katikati ya Mataifa juu ya mitume. Watu

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

wale wale amba waliwaabudu mbele walitaka kuwatendea jeuri sasa. Walitupia Paulo mawe, wakamkokota inje ya mji wakizani walikwisha kumwua. Lakini Paulo alisimama tena, akaondoka kesho yake pamoja na Barnaba, wakakwenda Derbe.

Kusimamisha waamini wa sasa (14:21-28)

Toka Derbe walianza safari ya kurudi kwao, wakafika tena kwa Listra (pahali Paulo alipotupiwa mawe mbele kidogo), Ikonio, na Antioquia. Walisimamisha waamini na kuwafahamisha ya kwamba watapata mateso, na waliwachagulia wazee katika kila kanisa. Halafu walipita katika Pisidia na Pamfilia, wakatelemuka mpaka Atalia. Pale wakaingia merikebu na kurudia Antioquia, wakatoa habari za kazi yao ya kuhubiri Habari Njema, na zaidi namna Habari Njema ilivyohubiriwa kwa Mataifa. Huu ndio mwisho wa safari ya kwanza ya kuhubiri.

12. KUSANYIKO KWA YERUSALEMA (15:1-35)

Mabishano juu ya tohara (15:1-6)

Tangu mwanzo wa Kanisa, kulikuwa na wanafunzi Wayuda waliofundisha ya kwamba imani ndani ya Kristo tu haitoshi kuokoa mtu. Walisema ni lazima waamini watahiriwe vilevile na kushika sheria. Watu wa "jamii" "hii ya "tohara" walikaa katika Yerusalem na kando kando yake. Wakati wengine katikati yao waliposafiri kwenda Antioquia na mafundisho yao, waamini wa pale walituma Paulo, Barnaba, na wengine kwenda Yerusalem kukata neno hili kabisa.

Petro anasimamia wokovu kwa neema kwa njia ya imani peke yake (15:7-11)

Wakati mitume na wazee walipokutana, Petro alianza na kuwakumbusha namna Mungu alivyookoa mtu wa Mataifa, ndiyie Kornelio na watu wa nyumba yake kwa njia ya imani, akauliza kwa sababu gani watawekeea Mataifa mzigo amba utawashinda kubeba. Mungu ali-kuwa akiokoa Wayuda na watu wa Mataifa kwa njia moja tu, ndiyo kwa njia ya imani.

Ushuhuda wa Paulo na Barnaba (15:12)

Kisha Barnaba na Paulo walipasha habari za maneno yaliyotokea wakati walipohubiri Habari Njema kwa Mataifa.

Shauri la Yakobo (15:13-21)

Halafu Yakobo, ndugu ya Bwana Yesu kwa njia ya mama yake Maria, alisema ni kusudi la Mungu kwa muda huu kuchagua katikati ya Mataifa watu kuwa watu kwa jina lake. Masemo yake yalipatana na unabii wa Amosi 9:11,12 pahali tunaposoma ya kwamba nyuma ya

MATENDO

muda wa sasa Mungu atasimamisha tena baki la Israeli wenyewe kuamini wakati Kristo atakapokuja kutawala, na ya kwamba nyuma ya kusimamisha Israeli tena, ataokoa Mataifa wote wanaoitwa na jina lake. Hivi Yakobo alisema tu vizuri waamini wa mataifa wajitenge na vyakula viliviyotolewa kwa sanamu, na uzini, na vitu vilivyo songwa, na damu.

Uzabiti wa kusanyiko kwa Yerusalem (15:22-35)

Masemo ya Yakobo yalikubaliwa, na viongozi katika Yerusalem walitumwaji kwa Antiokia pamoja na Paulo na Barnaba kuhakikisha kwa waamini ya kwamba hawahitaji kutahiriwa lakini ya kwamba inawapasa kujitenga na maneno mane Yakobo aliyotaja (mash. 22-29). Wakati habari hizi zilipofikia Antiokia, Wakristo wali-furahi sana na kulikuwa na roho tamu ya ushirika katikati yao (mash. 30-35).

13. SAFARI YA PILI YA PAULO KWA KUHUBIRI – ASIA NDOGO NA YUNANI (15:36 – 18:22)

Ugomvi juu ya Marko (15:36-41)

Basi saa ilikuwa imefika kwa Paulo na Barnaba kuanza safari ya pili ya kuhubiri, na kusudi la kusimamisha waamini pahali walipohubiri mbele, lakini hawakupatana hata kidogo kama ilipasa Marko kwenda pamoja nao au sivyo. Nyuma ya magomvi makali Barnaba alipeleka Marko pamoja naye na Paulo alichagua Sila. Hatusomi habari nyingine juu ya Barnaba nyuma ya magomvi haya. Paulo na Sila walipita kwa inchi za Suria na Kilikia, wakisimamisha makanisa.

Habari Njema inaingia Europe (16:1-15)

Timoteo aliungana na Paulo na Sila wakati walipofikia Derbe na Listra. Wakiungozwa na Roho walitambuka Asia Ndogo kufika Troa, wakihubiri Habari Njema na kupatisha roho za waamini nguvu (mash. 1-8). Kwa Troa Paulo alikuwa na maono usiku ya mtu katika Makedonia (kwa upande wa kaskazini wa Yunani), akimsihi kwenda kule, basi wakavuka bahari ndani ya merikebu, wakakwenda hata Filipi. Pale mwanamke mmoja, jina lake Ludia alikuwa mtu wa kwanza aliyeamini katika Europe, na kanisa la kwanza katika Europe lili-simamishwa pale (mash. 9-15).

Paulo na Sila katika gereza (16:16-24)

Siku moja kijakazi mmoja mwenye pepo ya kuagua alifuata Saulo na wale waliokuwa pamoja naye, akilalamika juu yao. Wakati Paulo alipotoa pepo mchafu ndani yake kwa jina la Yesu, bwana wa kijakazi

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

walikasirika sana. Walikokota wahubiri hata gereza, kisha waliagiza wapigwe fimbo na kuwekwa katika chumba cha ndani cha gereza.

Mlinzi aliyeamini (16:25-34)

Katikati ya usiku wakati Paulo na Sila walipokuwa wakiimba, gereza ilitikisika sana kwa sababu ya tetemeko la inchi. Mlinzi wa gereza, akiogopa atapoteza kazi yake na hata uzima wake alikuwa karibu kujiua mwenyewe. Paulo na Sila walijibu ulizo lake na kumwelezea njia ya wokovu. Walifanya vivyo kwa jamaa yake nyuma. Wao wote waliamini na kubatizwa, kisha walikulisha wahubiri.

Watawala wa mji waliruhusu Paulo na Sila kwenda zao (16:35-40)

Asubui watawala walifahamu ya kwamba hawakutendea Paulo na Sila kwa haki, hivi waliruhusu Paulo na Sila kufunguliwa na waliwasih i watoke katika mji.

Kanisa lilianzwa katika Tesalonika (17:1-9)

Nyuma ya kuondokea Filipi, Paulo na Sila walipita kwa upande wa kusini-mangaribi hata Amfipoli na Apolonia, kisha waligeuka kwenda mangaribi hata Tesalonika. Pale Saulo alihubiri kwa sabato tatu ndani ya sunagogi. Watu wengi waliamini na kanisa lilianzwa. Wayuda wasioamini waliamsha roho za watu juu ya Yasoni aliyekuwa ame-pokea wahubiri nyumbani mwake, na juu ya waamini wengine. Waamini hawa walifungwa, wakafunguliwa nyuma wakati zamana ilipolipwa kwa ajili yao.

Kutafuta Maandiko katika Beroya (17:10-15)

Wakristo walifikili vizuri wahubiri waondokee Tesalonika, wakawatuma usiku kwa Beroya. Pale Paulo na Sila walikwenda sunagogi mara moja. Wayuda wengi waliamini pale, lakini wakati adui za Paulo katika Tesalonika waliposikia habari hizi, walifika kule na kuanza matata katika Beroya vilevile. Paulo aliondokea Beroya, lakini Sila na Timoteo walibaki pale.

Paulo alihubiri katika Atene (17:16-21)

Paulo alihuzunishwa wakati alipoona kwamba kuabudu sanamu kulizidi katika Atene. Alihubiri ndani ya sunagogi na kwa soko kwa watu wote waliokubali kusikiliza. Wenye hekima namna mbili walifikili Paulo ni mwenye masemo mengi na mhubiri kwa miungu mingine, hivi walifikili vizuri aseme maneno ya roho yake katikati ya Areopago, namna ya baraza ya hukumu yenye uwezo zaidi.

Paulo alitoa hotuba katikati ya Areopago (17:22-31)

Ndani ya hotuba yake Paulo alisema ya kwamba Waatene walikuwa wenye kufuata dini sana lakini walikuwa wakiabudu Mungu asiyeju-

MATENDO

likana. Halafu aliwaambia habari za Mungu wa kweli: Mwumba, Bwana wa mbingu na dunia; asiyekaa ndani ya mahekalu yanayojeingwa kwa mikono ya watu, na asiyehitaji utumishi wa watu; mwenye kutoa baraka zote. Mtume aliendelea kueleza ya kwamba ni Mungu aliyeumba dunia na kufanya kila taifa la watu kuwa wa damu moja. Ni ye ye aliyeandika nyakati na kuweka mipaka ya makao ya watu. Mungu alifanya maneno haya yote ili watu wamtafute na kumkaribia. Watu ni wazao wa Mungu na haifai wafikili juu yake kama sanamu (inayofanywa na mikono ya watu) lakini kama Mungu aliye hai na anayefikili kila mtu. Kwa mia za miaka Mungu hakuangalia ujinga wa Mataifa, lakini sasa anaita kila mtu kutubu, mbele ya siku atakapo-hukumu dunia kwa njia ya Yesu Kristo ambaye alimfufua toka wafu.

Mawazo ya watu juu ya hotuba ya Paulo (17:32-34)

Wakati Paulo alipotaja ufufuko, wengine wa wasikiaji wake walizaraau, wengine walisema watawaza juu ya maneno haya nyuma, wengine waliamini, hata wa watu wa kujulikana mjini. Paulo hakurudia Atene kamwe, ndipo pahali pa elimu ya elimu zote.

Mahubiri katika sunagogi kwa Korinto (18:1-6)

Halafu Paulo alifikia Korinto pahali alipokutana na Akila na Prisila. Ushirika wake nao uliendelea hata mwisho wa maisha yake. Sila na Timoteo walifika kwa Korinto toka Berea, wakafungana tena na Paulo. Wakati Wayuda katika sunagogi waliposhindana na Habari Njema Paulo aliwaambia ya kwamba damu yao ilikuwa juu ya vichwa vyao, akaanza kuhubiri kwa watu wa Mataifa.

Kanisa lilokutana nyumbani kwa Korinto (18:7-11)

Kazi ya Paulo iliendelea na baraka nyingi nyumbani mwa Yusto. Nyuma ya kusikia Bwana akisema naye ndani ya maono, alikaa katika Korinto kwa mwaka mmoja na nusu.

Paulo mbele ya Galio (18:12-17)

Halafu wasioamini Wayuda walikokota Paulo mbele ya Galio, liwali la Akaya, wakamshitaki kusema alifundisha maneno yasi-yopatana na sheria. Galio alikataa kukata neno hili akisema ni mabishano juu ya sheria ya Wayuda naye hakuwa na amri ndani yake. Mara hii alikuwa mkubwa wa sunagogi aliyepigwa, si Paulo.

Paulo alirudia Antioquia (18:18-22)

Ilikuwa saa tena kuanza safari ya kurudia Antioquia. Kwanza walifika Efeso. Walipokewa vizuri ndani ya sunagogi na Akila na Prisila walibaki pale. Paulo aliendelea na safari yake kufikia Kaisaria na Yerusalem, na mwishoni Antioquia.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

14. SAFARI YA TATU YA PAULO KWA KUHUBIRI — ASIA NDOGO NA YUNANI (18:23 – 21:25)

Paulo anapatisha Wakristo wa Galatia na Furugia nguvu (18:23)

Nyuma ya kushinda kwa Antiokia kwa wakati, Paulo alianza safari yake ya tatu akipita katika Galatia na Furugia. Kwa safari hii yeche na wale waliosafiri pamoja naye walikwenda kwa upande wa mangaribi hata Troa, wakavuka bahari kwenda upande wa kaskazini wa Yunani, wakaendelea ndani ya merikebu kufikia upande wa kusini ya Yunani, wakarudia upande wa kaskazini wakisafiri kwa inchi kavu, kisha wakafikia pwani wa mangaribi ya Asia Ndogo, wakaingia merikebu kwenda Kaisaria; toka pale walifikia Yerusalem.

Mahubiri ya Apolo (18:24-28)

Kwanza tunasoma juu ya Efeso. Mhubiri wa uwezo mmoja alikuwa pale jina lake Apolo, aliyekuwa mjinga kwa maneno mengine ya dini ya Wakristo. Nyuma ya kufundishwa na Prisila na Akila alikwenda Korinto. Mungu alibariki mahubiri yake sana pale. Ni vizuri kuona mhubiri mwenye uwezo kuwa na unyenyekevu hata kupokea mafundisho toka wenye kazi ya kufanya hema.

Wanafunzi kumi na wawili wa Yoane Mbatizaji kwa Efeso (19:1-7)

Paulo alikuwa amefikia Efeso sasa na alikutana na wanafunzi kumi na wawili waliobatizwa na Yoane Mbatizaji lakini wasiopokea Roho Mtakatifu bado. Wakati Paulo alipowafundisha ya kwamba walihitaji kuamini Kristo, walifanya hivi na kupokea ubatizo wa Wakristo. Kisha mtume aliwawekea mikono na walipokea Roho Mtakatifu.

Habari Njema inahubiriwa katika nyumba ya darasa (19:8-12)

Paulo alifundisha ndani ya sunagogi kwa miezi mitatu, lakini Wayuda walikuwa na roho ya nguvu na uadui kupita kupita, hivi alilacha kufundisha pale, akakwenda kwa darasa ya Tirano, akakaa kuhubiri na kuponyesha wagonjwa pale kwa miaka miwili. Kwa njia hii wilaya nzima ya Asia waliskia Habari Njema.

Kazi ya Shetani inazuizwa (19:13-20)

Wakati wafumu wa pepo walipojaribu kutoa pepo mchafu kwa jina la Yesu, pepo huyu aliwazarau akisema ya kwamba hawakujulikana katika Hadeze. Mwenye pepo mchafu aliwarukia na kuwaumiza, wakakimbia. Habari hizi zilienea katikati ya watu na wengi wao waliamini Kristo, wakateketeza vitabu vyao vya uchawi.

Baki la safari ya Paulo (19:21-22)

Nyuma ya kutuma Timoteo na Erasto kwa Makedonia, Paulo aliba-

MATENDO

ki kwanza kwa Efeso. Alitaka kwenda Yunani tena, kisha Yerusalem, na mwishoni Roma.

Makelele juu ya dini (19:23-41)

Watu wengi sana waliamini Kristo katika Efeso, hata kazi ya wenye kufanya sanamu ilipunguka sana. Mtu mmoja mwenye kufua feza, jina lake Demetrio, alikutanisha wengine waliokuwa na kazi hii vilevile, akawaonya ya kwamba Paulo alikuwa akiharibu kazi yao na kuleta mashaka juu ya mungu mke wao Diana. Watu wengi walikutana, wakakamata wawili wa wenzi wa Paulo. Paulo alitaka kwenda kuwasaidia, lakini waamini wa pale walimzuiza. Kulikuwa na machafuko makubwa. Myuda mmoja, jina lake Alesanduro alijaribu kusema na watu, lakini watu walikataa kumsikiliza. Mwishoni mkubwa wa mji aliweza kunyamazisha watu kwa njia ya kusifu Efeso kama milinzi wa hekalu la mungu mke mkubwa Diana na kusema hakuna njia kuharibu ishara ya Diana. Aliwaonya vilevile ya kwamba serikali ya Waroma waliweza kuwaazibu kwa sababu ya machafuko haya. Ali-sema kama watu wakiwa na mashitaki ya haki, yaliweza kutengenezwa mbele ya wakubwa katika baraza. Basi makutano walitulizwa, wakakwenda na salama.

Paulo alihubiri katika Makedonia, Yunani, na Troa (20:1-12)

Halafu Paulo aliondokea Efeso, akasafiri kwenda Makedonia (kwa njia ya Troa, ona 2 Wakorinto 2:12-13) kwa miezi mitatu, akapita kwa upande wa kusini wa Yunani, akarudia Makedonia, na Troa. Wakati Paulo alipokuwa akihubiri katika Troa siku ya Bwana saa waamini wa pale walipokutana kuvunja mkate, kijana mmoja aliyeketi kwa dirisha alianguka toka chumba cha juu, akakufa.

Mtume alishuka, akampa uzima tena, kisha akaendelea na mafundisho mpaka asubui mapema.

Maonyo ya Paulo kwa wazee wa Efeso (20:13-35)

Toka Troa Paulo alisafiri kwa pwani ya mangaribi ya Asia Ndogo hata Milet. Pale aliita wazee toka kanisa kwa Efeso kufika kwake.

Ndani ya hotuba nzuri sana aliwakumbusha habari za maisha na utumishi wake katikati yao, akawajulisha ya kwamba alikuwa akisafiri kwenda Yerusalem akifahamu hatawaona tena. Aliwaonya kulinda kondoo, ndio waamini toka hatari ya walimu wa uwongo toka inje ya kanisa, na ya kwamba wengine watasimama hata katikati ya kanisa na kufundisha maneno yasiyo kweli. Aliwaweka kwa neema ya Mungu, akawakumbusha ya kwamba alikuwa amewatumikia bila mshahara lakini alifanya kazi kusudi kupata mali kwa mahitaji yake mwenyewe na ya wale waliosafiri pamoja naye.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Paulo aliagana na wazee (20:36-38)

Kwa mwisho wa hotuba hii Paulo alipiga magoti, akaomba pamoja na wazee. Kisha waliagana na machozi kwa sababu alikuwa amewaambia ya kwamba hawatamwona tena.

Maonyo kwa safari kwenda Yerusalem (21:1-14)

Paulo alisafiri ndani ya merikebu iliyopita kwa upande wa kusini-mangaribi wa Asia Ndogo, kisha ilikwenda kwa upande wa kusini-mashariki. Walipita Kipuro, wakafika Tiro. Paulo alishinda siku saba kwa Tiro na waamini wa pale walimwonya asiende Yerusalem.

Safari iliedelea hata Tolemai na Kaisaria. Pale nabii mmoja jina lake Agabo alitabiri kwa njia ya alama ya kujifunga mikono na miguu ya kwamba Paulo atafungwa kwa Yerusalem na kutolewa kwa Mataifa. Mtume aliona bule maonyo yote ya kwamba angeweza kupata hatari, akaendelea na safari yake kwenda Yerusalem. Huu ulikuwa mwisho wa safari yake ya tatu kwa kuhubiri.

Paulo na kanisa katika Yerusalem (21:15-25)

Wakristo Wayuda walifurahi sana kusikia habari za kazi ya Mungu katikati ya Mataifa, lakini waliogopa wengine wa waamini Wayuda wataleta matata kwa sababu walikuwa wamesikia kwamba Paulo alikuwa amefundisha ya kwamba inapasa waamini Wayuda kuacha kutii sheria ya Musa. Walisema vizuri mtume afungane pamoja na watu wane wengine waliofungwa kwa naziri. Neno hili litaonyesha ya kwamba mashitaki haya yalikuwa bule.

15. PAULO ANAFUNGWA NA KUHUKUMIWA

(21:26 – 26:32)

Askari waliponyesha Paulo toka makutano yenyeye gazabu (21:26-40)

Hata mbele ya mwisho wa naziri Wayuda toka Asia waliona Paulo katika kiwanja cha hekalu, wakaamsha makutano wakishitaki Paulo kusema alisema maneno mabaya juu ya Wayuda, sheria, na hekalu na ya kwamba alileta watu wa Mataifa hekaluni ndani kupita kiwanja cha Mataifa. Walijaribu kumpiga hata kufa lakini askari walifika na kumponyesha na kumwingiza ndani ya nyumba kubwa. Njiani kwenda pale Paulo aliomba ruhusa kusema na makutano. Mkubwa wa askari akifahamu ya kwamba Paulo si Mmisri wa matata, akampa ruhusa. Mtume alianza kusema na watu walinyamaza.

Maisha ya Paulo mbele ya kuokolewa kwake (22:1-5)

Paulo alianza hotuba yake na habari za ujana wake kama Myuda katika Tarso wa Kilikia, mafunzo yake kwa miguu ya Gamalieli,

MATENDO

mwalimu wa kujulikana ambaye alimfundisha sheria za Wayuda. Aliwakumbusha bidii yake kama Myuda. Alikuwa ametesa Wakristo na kujaza vifungo na wale walioamini Yesu. Kuhani mkubwa na wakubwa wa baraza walijua ya kwamba alifanya kazi hii na bidii na utaratibu kabisa. Ni wao ambao walimpa ruhusa kwenda Damasiki na kurudisha Wakristo kwa Yerusalem waweze kuazibowi.

Wokovu wa Paulo (22:6-21)

Halafu alipasha juu ya mambo yaliyotokea siku alipookolewa: nuru kubwa toka mbinguni; sauti ya Yesu aliyetukuzwa ikisema naye; namna alijitoa kwa Kristo; urafiki wa Anania katika Damasiki, ubatizo wake; safari yake kwenda Yerusalem; saa alipokuwa akiomba hekaluni na kuwa katika hali kuzimia roho na Bwana alimwagiza kutoka Yerusalem kwa sababu alimtuma kwa Mataifa.

Kuwa mwenyeji wa Roma kulisaidia Paulo (22:22-30)

Wakati Paulo aliposema juu ya kwenda kwa *Mataifa* na Habari Njema makutano walijaa gazabu na wivu. Walianza kupiga kelele na kulalamika Paulo auawe. Mkubwa wa askari alifikili Paulo alikuwa amefanya zambi kubwa, hivi aliagiza askari kumwingiza ndani ya nyumba kubwa na kupigwa fimbo kumlazimisha kukiri neno ambalo alilifanya. Wakati walipomfunga, Paulo aliuliza na roho ya utulivu kama walikuwa na ruhusa kupiga Mroma asiyehukumiwa bado. Wakati akida aliposikia neno hili alimwambia mkubwa ya kwamba mfungwa huyu alikuwa Mroma. Basi Paulo hakupigwa, hata kama alibaki katika kifungo kufika asubui. Kesho yake mkubwa aliletu Paulo mbele ya wakubwa wa makuhani na baraza, aweze kusikia kama walimshitaki juu ya nini.

Paulo mbele ya baraza (23:1-5)

Akisimama mbele ya baraza Paulo alisema ya kwamba aliishi mbele ya Mungu kwa zamiri safi siku zote. Akisikia neno hili kuhani mkubwa aliagiza apigwe kwa kinywa. Mtume alijibu na ukali lakini aliomba usamehe mbio, akitaja Kutoka 22:28.

Paulo alitiia Wafarisayo (23:6-10)

Akifahamu ya kwamba Wafarisayo na Wasadukayo pale kwa baraza hawakupatana, Paulo alitangaza kwamba ye ye ndiye Mfarisayo aliyekuwa akihukumiwa kwa sababu aliamini ya kuwa wafu wanafufuliwa (Wasadukayo walikana kweli hii). Tangazo hili liliongeza ugomvi katikati ya Wafarisayo na Wasadukayo na kuleta machafuko makubwa ndani ya chumba cha hukumu hata mkubwa aliagiza askari kurudisha Paulo tena kwa nyumba kubwa.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Neema ya Bwana kwa Paulo (23:11)

Usiku ule Bwana alionekana kwa Paulo, akamtia moyo na kusema ya kwamba namna alivyomshuhudia katika Yerusalem, atafanya vivyo hivyo kwa Roma.

Paulo aliponyeshwa toka shauri la Wayuda kumwua (23:12-32)

Kesho yake Wayuda 40 walitoa kiapo kusema hawatakula au kuniya kufika wakati watakapokwisha kuua Paulo. Walifanya shauri kutengeneza njia kwa baraza kukutana na kwa mkubwa kuleta Paulo waweze kuulizana naye habari zake vizuri zaidi, lakini wataua Paulo njiani kwenda kule. Wakati mkubwa aliposikia habari za shauri hili alituma mfungwa wake mbio kwa Kaisaria akichungwa na askari wengi njiani. Mkubwa alituma barua kwa Feliki, mtawala Mroma pale kumfahamisha habari za mfungwa huyu.

Paulo alipelekwa kwa Feliki (23:33-35)

Wakati wapanda farasi walipofika Kaisaria, walimpa Feliki barua na kuweka Paulo mbele yake. Wakati Feliki alipofahamu kwamba Paulo alikuwa mwenyeji wa Roma, alisema atasikia habari zake mara moja wakati wenye kumshitaki watakapofika toka Yerusalem. Kufika saa ile Paulo alilindwa ndani ya nyumba ya Herode.

Mashitaki juu ya Paulo (24:1-9)

Nyuma ya siku tano kuhani mkubwa na wakubwa wengine wa baraza walifika toka Yerusalem na Paulo aliletwa mbele ya Feliki kwa hukumu. Mshitaki, ndiye Tertulo, alishitaki Paulo juu ya maneno mane: alikuwa mtu wa matata, alijaribu kuanza fitina katikati ya Wayuda, alikuwa mwongozi wa dini ya Wanazareti, na alijaribu kuchafua hekalu.

Paulo alijisimamia mbele ya Feliki (24:10-21)

Paulo alijibu mashitaki haya na utaratibu wote. Hakuleta matata hata kidogo wakati alipofikia Yerusalem kwa kuabudu. Alishinda pale kwa siku 12 na hakujaribu kuanza fitina katikati ya Wayuda hata mara moja. Paulo hakukana ya kwamba alikuwa mwongozi wa “dini ya Wanazareti”, lakini alisema ya kwamba kwa njia hii alitumikia Mungu wa Wayuda, akiamini Maandiko ya Agano la Kale, zaidi mafundisho yao juu ya ufufuko. Hakuchafua hekalu, lakini alikuwa akileta matoleo wakati Wayuda wengine toka Asia walipoleta mashitaki ya uwongo juu yake kusema alileta watu wa Mataifa kwa sehemu ya hekalu iliyokatazwa kwa mataifa.

Feliki alikusudi kuendelea na hukumu siku nyingine (24:22-23)

Feliki alifahamu ya kwamba Paulo hakuwa na kosa, lakini alitaka

MATENDO

kubembeleza Wayuda, akasema atangoja kwanza kufika kwa mkubwa wa askari toka Kaisaria. Kufika siku ile aliamuru Paulo alindwe, laki-ni bila kufungwa.

Feliki alikawia kupokea Kristo (24:24-27)

Nyuma ya wakati Feliki na mke wake walisemezana na Paulo peke yao. Paulo alishuhudia Kristo na uaminifu na uhodari. Feliki alikawia kuamini Habari Njema, lakini kwa miaka miwili aliiita Paulo tena na tena, akitaraji Paulo atampa rushwa. Wakati Festo alipoko-mboa Feliki, Feliki aliacha Paulo katika kifungo kupendeza Wayuda.

Paulo mbele ya Festo (25:1-8)

Wakati Festo alipofikia Yerusalem, Wayuda waliomba Paulo aletwe pale kwa hukumu, lakini Festo aliwaagiza kufikia Kaisaria kama wakiwa na mashitaki juu yake. Siku moja nyuma ya kurudi kwake kwa Kaisaria alikaa katika kiti chake cha hukumu. Wayuda walikuwa na mashitaki mengi juu ya Paulo, lakini hawakuhakikisha hata moja lao. Paulo akifahamu ya kwamba mashitaki yao yalikuwa zaifu, alijibu tu na kubisha ya kwamba alikosa juu ya sheria au hekalu, au Kaisari.

Paulo aliomba kusimama mbele ya Kaisari (25:9-12)

Wakati Festo alipouliza kama akikubali kwenda Yerusalem kuhukumiwa, mtume alikataa, akisema ingepasa neno hili kukatwa katika Kaisaria tu. Kisha Paulo aliongeza kusema, “Ninataka kuhukumiwa na Kaisari.” Basi ilikuwa lazima kwa Festo kutuma Paulo kwa Roma.

Festo alipasha Agripa habari za Paulo (25:13-21)

Nyuma ya wakati Mfalme Herode Agripa II na ndugu mke yake Berenike walifikia Kaisaria kutakia Festo heri kwa kazi yake mpya. Saa yenye Festo alimwambia habari za mashitaki ya Paulo, ya kwamba Wayuda walitaka auawe, namna alivyohukumiwa na utaratibu kwa Kaisaria, ya kwamba Paulo hakukosea Roma katika neno lo lote, mafundisho yake juu ya ufufuko wa Yesu na ya kwamba alikataa kwenda Yerusalem, akiomba kuhukumiwa na Kaisari.

Matayarisho kusikia Paulo (25:22-27)

Kesho take Agripa na Berenike walikuja na mapambo kusikiliza Festo akiwapasha habari za Paulo. Alieleza ya kwamba ilikuwa lazima kwaye kutuma Paulo kwa Kaisari bila kuwa na mashitaki ya kweli.

Paulo mbele ya Agripa (26:1-23)

Agripa alimpa Paulo njia kujisimamia. Nyuma ya kuanza habari

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

zake na masemo ya adabu Paulo alipasha juu ya ujana wake kama Mfarisayo aliyesikana sana na mafundisho na desturi zao. Sasa alikuwa akihukumiwa kwa sababu aliamini wafu watahukumiwa. Hii ndiyo kweli ya lazima kama ahadi za Mungu kwa baba za zamani zitamizwa siku nyingine. Paulo alisema ya kwamba mbele alitesa Wakristo na bidii sana, kisha alipasha habari za kuokolewa kwake mwenyewe njiani mwa Damasiki na za kazi aliyopewa na Mungu kupelekeea Mataifa Habari Njema. Alikuwa akihubiri Habari Njema kwa uwanja wa hekalu wakati Wayuda walipojaribu kumwua. Lakini Mungu alimlinda naye alikuwa akitangaza hata sasa ya kwamba ilikuwa lazima kwa Masiya kuteswa, kufufuliwa toka wafu na ya kwamba ataonyesha nuru kwa Wayuda na Mataifa.

Paulo anasihi Agripa yeye mwenyewe (26:24-32)

Halafu Festo alimwambia Paulo kwamba alikuwa na wazimu. Mtume alikana masemo haya na roho ya upole, akisema ya kwamba bila shaka Agripa alifahamu maneno ambayo aliyasema, akamwuliza na adabu kama aliamini manabii. Agripa hakumjibu waziwazi. Kisha Agripa, Berenike na Festo walizungumuza peke yao, wakasema Paulo hakufanya neno la kustahili kufa. Agripa alisema vile kwamba mtume angweza kufunguliwa kama asingaliitia Kaisari.

16. SAFARI KWENDA ROMA NA KUHARIBIKA KWA MERIKEBU (27:1 – 28:16)

Tufani baharini (27:1-20)

Safari kwenda Roma ilianza kwa Kaisaria. Paulo alilindwa na akida mmoja, jina lake Yulio. Walishinda muda mfupi kwa Sidona na mtume alipata njia kwenda kuangalia mitume, ndio waamini, kisha merikebu iliendelea na safari yake ikizunguka pwani ya mashariki ya Kipuro na Mira kwa upande wa kusini-mashariki wa Asia Ndogo. Kwa Mira akida na watu wengine waliokuwa wakisafiri kwenda Roma waliingia merikebu nyingine. Merikebu hii ilipita kwa upande wa mangaribi kufika Kinido, kisha kwa kusini hata Krete hata kwa paiali palipoitwa Bandari Nzuri. Paulo alionya viongozi vyta merikebu wasiendelee na safari yao kwa sababu ya tufani za wakati wa baridi, lakini kapiteni na mwenye merikebu walianza safari kwenda kwa upande wa mangaribi kufika Foinike. Lakini nyuma kidogo tufani kubwa ilipiga merikebu na kuitembeza kwa kusini-mangaribi kwa upande wa kisanga kidogo jina lake Kauda. Walikuwa karibu na kupoteza chombo kidogo ambacho walikikokota. Walifunga merikebu kubwa na kuitisha kamba chini yake isiharibiwe na mawimbi, wakaanza kutupa mizigo waliyobeba baharini, na nyuma ya siku tatu

MATENDO

walitupa vitu vya merikebu vilevile. Zoruba iliendelea kwa siku nyin-gi na tumaini la watu lilikwisha pia.

Paulo alitumainisha watu waliosafiri pamoja naye (27:21-26)

Kisha Paulo alisimama na habari za tumaini. Alisema nao ya kwamba, hata mizigo yao ilikuwa imepotea, hakuna mtu atakayepoteza uzima wake. Malaika alikuwa amemwambia ya kwa-mba atafikia Roma salama, na watu wote ndani ya merikebu watapona vilevile.

Walikaribia inchi kavu (27:27-32)

Nyuma ya kuchukuliwa na bahari kwa siku 14 wabaharia walifa-hamu ya kwamba walikuwa wakikaribia inchi kavu, hivi walishusha nanga ndani ya maji. Wengine walitaka kujiponyesha ndani ya cho-mbo kidogo kwenda inchi kavu, lakini Paulo alisema neno hili halifai, hivi askari walikata kamba zilizofunga chombo kidogo na merikebu kubwa, wakaacha kichukuliwe na maji.

Vyakula kusaidia mwili (27:33-37)

Mtume alisukuma wabaharia na wasafiri kula chakula kwani maju-ma mawili yalikuwa yamepita tangu walipoweza kufanya hivi. Aki-waambia tena ya kwamba wao wote watafikia inchi kavu salama, alit-waa mkate, akashukuru Mungu, akaanza kula mbele yao. Neno hili liliwapa wote hamu kula chakula.

Merikebu inaharibika (27:38-44)

Halafu walipunguza uzito wa merikebu kwa njia ya kutupa baki la mizigo baharini, kisha waliiacha kukwama katika udongo chini ya maji. Watu wengine waliogelea kufika inchi kavu na wengine walifika wakishikamana na mbaao za kipande cha nyuma cha merikebu kili-choharibika kwa sababu ya nguvu ya mawimbi.

Paulo aliponyeshwa kwa njia ya ajabu toka sumu ya nyoka (28:1-6)

Hawakujua ya kwamba walikuwa wamefikia kisanga cha Melita. Wengine wa wenyeji wa kisanga waliwashaa moto kwa wasafiri. Wakati Paulo aliposaidia ndani ya kazi hii, nyoka ya sumu alifungana na mkono wake. Kwanza watu walifikili maana ya neno hili ndiyo ya kwamba Paulo alikuwa mwuaji, lakini wakati asipopata matata kwa njia ya sumu ya nyoka, walifikili ye ye ni mungu!

Maajabu ya kuponyesha kwa Melita (28:7-10)

Publio, mkubwa wa Melita aliruhusu wasafiri kukaa kwake kufika wakati walipotayarishiwa makao mengine kwa muda wa wakati wa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

baridi. Wakati baba ya Publia alipopata homa na kuhara damu, Paulo alifika kwake, akaomba, akamwekea mikono na kumponyesha. Habari za ajabu hili zilienea katikati ya wenyiji wa kisanga na watu wengine walifika wapate kuponyeshwa.

Safari kwenda Roma (28:11-16)

Kwa mwisho wa muda wa wakati wa baridi akida alianza safari tena na wafungwa wake. Walifika Sirakuse, wakapita kwa Regio kwa upande wa kusini-mangaribi wa pwani wa Italia, wakageuka kwenda kwa kaskazini hata Puteoli. Toka pale walisafiri kwa inchi kavu hata Roma. Pale Paulo alipewa ruhusa kukaa kwake mwenyewe pamoja na askari ambaye alimlinda.

17. USHUHUDA WA PAULO KWA WAYUDA KATIKA ROMA TOKA NYUMBA ALIPOFUNGWA (28:17-31)

Ushuhuda wa Paulo kwa Wayuda wa Roma (28:17-22)

Mtume aliita viongozi vya Wayuda kufika nyumbani mwake ili aweze kuwaelezea maneno yake. Walisema ya kwamba hawakusikia habari juu yake mbele lakini walitaka kusikia maneno ambayo alitaka kuwaambia.

Mawazo mbalimbali juu ya Habari Njema (28:23-29)

Wakati Paulo alipokutana na viongozi vya Wayuda mara ya pili, Paulo aliwaelezea habari za Yesu toka Maandiko yao wenyewe. Hata kama wengine waliamini maneno yake, alifahamu tu ya kwamba baki lao walikataa Habari Njema, hivi aliwaambia ya kwamba walikuwa wakitimiza unabii wa Isaya juu ya watu wenyewe masikio mazito ya kusikia na macho yaliyofungwa. Kwa sababu hii atapelekeea Mataifa Habari Njema, kwani alijua wao watasikiliza.

Utumishi wa Paulo bila kizuizo katika Roma (28:30-31)

Paulo alishinda miaka miwili ndani ya nyumba yake ambayo alilipa, akihubiri habari za ufalme na kufundisha juu ya Bwana Yesu. Watu wanafikili ya kwamba nyuma yake alisimama mbele ya Nero kwa hukumu na alifunguliwa. Tunapata habari nusu tu za safari zake nyuma ya muda ule ndani ya barua ambazo aliziandika.

Barua kwa Waroma

MWANZO

Mwanzo wa Kanisa katika Roma

Labda kanisa katika Roma lilianzwa na Wayuda waliokuwa katika Yerusalem siku ya Pentekote na waliorudia Roma (ona Matendo 2:10).

Barua hii iliandikwa na nani na kwa wakati gani

Paulo alikuwa hajafikia Roma bado wakati alipoandika barua hii, lakini alitumaini kufika kule nyuma kidogo. Kwa safari yake ya tatu ya kuhubiri alishinda miezi mitatu katika Yunani; tunafikili alishinda muda huu zaidi kwa Korinto. Aliandika barua hii kwa waamini wa Roma toka Korinto karibu na AD 56 na 58.

Muhtasari wa barua kwa Waroma

Ndani ya barua hii mafundisho ya Habari Njema yanaelezwa wazi kupita pahali pote pengine ndani ya Biblia. Paulo anafundisha juu ya hali ya zambi na upotevu ya mtu, juu ya kuhesabiwa haki kwa njia ya imani, juu ya kutakaswa na mwishoni juu ya kutukuzwa. Sehemu ya barua ni unabii na inasibitisha haki ya namna Mungu anavyotendea kwa wakati wa sasa watu wake wa zamani, ndio Waisraeli, na kuyonyesha ya kwamba kwa wakati wa kuja watarudishwa tena karibu naye. Ndani ya sura za mwisho kuna mafundisho kwa mwenendo wa wale waliohesabiwa haki.

UMBO LA WAROMA

1. Habari Njema — maana yake (1:1-17)
2. Watu wote wanahitaji Habari Njema (1:18 – 3:20)
3. Msingi na sharti ya Habari Njema (3:21-31)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

4. Habari Njema na Maandiko ya Agano la Kale yanapatana (Sura 4)
5. Faida ya Habari Njema (5:1-11)
6. Kazi ya Kristo inashinda zambi ya Adamu (5:12-21)
7. Mwenendo Mtakatifu kwa sababu ya Habari Njema (Sura 6)
8. Sheria ndani ya maisha ya mwamini (Sura 7)
9. Roho Mtakatifu ndiye uwezo kwa maisha matakatifu (Sura 8)
10. Habari Njema na historia ya Israeli zamani, sasa na kwa wakati wa kuja (Sura 9-11)
11. Mwenendo unaofaa waamini (12:1 – 15:13)
12. Maelezo, maonyo ya mwisho, na salama (15:14 – 16:27)

1. HABARI NJEMA — MAANA YAKE (1:1-17)

Nyuma ya kufahamisha wasomaji kama ye ye ni nani na kuwasalimu na maneno ya sifa, mtume alianza mara moja na neno lililokuwa rohoni mwake, ndilo Habari Njema. Ni habari nzuri toka Mungu, kama alivyoahidi ndani ya Agano la Kale, juu ya Mwana wa Mungu, Bwana Yesu. Ni uwezo wa Mungu hata wokovu kwa kila mtu ana-yeamini.

2. WATU WOTE WANAHITAJI HABARI NJEMA (1:18 – 3:20)

Mataifa wapotevu wanahitaji Habari Njema (1:18-32)

Habari Njema ni matengenezo ya Mungu kwa wapotevu na wapotovu. Watu namna zote wamepotea. Kwanza, wapagano wasiosikia Habari Njema kamwe wamepotea. Wanajua kwa njia ya vitu vya ajabu Mungu alivyoumba ya kwamba kuna Mungu. Hata hivi wanachagua kuabudu sanamu kwa pahali pa kujua Mungu. Kwa kipimo wanachozidi kuabudu sanamu wanazidi vilevile kuwa wapotovu, wakitenda zambi namna namna za mwili. Zaidi ya kutenda zambi hizi wao wenye wanasukumu watu wengine kuzifanya vilevile.

*Wapotevu wenye mwenendo mzuri wanahitaji
Habari Njema (2:1-16)*

Wenye mwenendo mwema, si neno kama wao ni Wayuda au Mataifa, wamepotea vilevile. Kwa njia ya kushitaki watu wengine wanaonyesha ya kwamba wanafahamu tofauti kati ya maneno yaliyo mema na yale yaliyo zambi. Hata hivi wao wenye wanafanya maneno ambayo wanashitaki watu wengine juu yao. Sharti wafahamu habari nyingine juu ya hukumu ya Mungu. Hukumu ya Mungu ni haki

WAROMA

na kweli. Hakuna njia kuiepuka hata kama mara nyingine hukumu yenye inakawa. Wenye hatia kubwa zaidi watapata hukumu kubwa kupita wengine. Hukumu ya Mungu itakuwa haki kabisa. Itakuwa kwa kadiri ya matendo na kazi ya mtu, na kwa kipimo mtu alichokuwa na njia kujua Mungu. Itakuwa bila upendeleo, na hata zambi ambazo watu wanazitenda kwa siri zitahukumiwa, si zambi zile tu watu wengine wanazoonaa.

Wapotevu wa Wayuda wanahitaji Habari Njema (2:17-29)

Wayuda walipewa sheria, lakini wamepotea vilevile. Wanafikili ya kwamba wanakubaliwa na Mungu kupita wengine kwa sababu ya mapendeleo haya na kwa sababu ya kujua maneno ya Mungu zaidi, lakini sivyo. Kuwa na sheria hakutoshi. Ni lazima kuitii vilevile. Tohara ina faida tu kama mtu aliyetahiriwa akitembea katika utakatifu. Mungu haweki roho juu ya desturi za dini lakini juu ya kweli rohoni. Hivi mtu wa Mataifa asiyetahiriwa lakini anayetii anapendeza Mungu kupita Myuda mwasi aliyetahiriwa.

Hukumu ya Mungu ni haki (3:1-8)

Wakati tunaposoma maneno yanayoandikwa ndani ya sura 2 tunaweza kuwa na shaka kama Wayuda wakipita watu wengine kweli na kama faida ya tohara ni nini. Walikuwa wenye mapendeleo mazuri sana kwa sababu walipewa Maandiko ya Agano la Kale, lakini wengi wao hawakuamini. Kutokuamini kwao hakuwezi kufanyiza ahadi za Mungu bule. Atahukumu kwa haki. Hata kama Mungu akishinda zambi za mtu, neno hili halimpi mtu ruhusa kukaa kufanya zambi. Hata uzalimu wa mtu ukifanyiza haki ya Mungu kungaa zaidi, neno hili si ruhusa kwa mtu kufanya zambi wala halimsukumi kufanya zambi.

Watu wote wamefanya zambi (3:9-18)

Hivi tunaona ya kwamba watu wote ni wenye zambi — wasioamini wa Mataifa, wapotevu wenye mwenendo mzuri, na Wayuda — wote walipungukiwa na kawaida kamilifu ya Mungu. Zambi imegeuza kila mtu wa dunia na kila sehemu ya mtu yule.

Sheria haiwezi kuhesabia mtu haki (3:19-20)

Mungu alijaribu Israeli kwa njia ya sheria na kwa sababu ya kuanzuka kwao alitangaza ya kwamba ulimwengu wote ni chini ya hukumu yake. Sheria haiwezi kufanyiza mtu haki lakini inamjulisha zambi zake tu.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

3. MSINGI NA SHARTI YA HABARI NJEMA (3:21-31)

Kuhesabiwa haki kwa neema kwa njia ya imani (3:21-25)

Sasa Mungu amefunua njia yake ya haki kwa wapotevu kuhesabiwa haki. Kuna unabii juu ya njia hii ndani ya Agano la Kale nayo ni mbali kabisa na kushika sheria. Mungu anahesabia haki kila mtu anayekiri kwamba yeche ni mwenye zambi, si neno kama ni Myuda au Mtaifa, na anayeaminu Bwana Yesu. Kuhesabiwa haki ni zawadi ya neema, bila bei, na kunawezekana kwa sababu ya kazi ya ukombozi ya Kristo kwa Kalvari. Kazi ile inaonyesha ya kwamba Mungu alikuwa mwenye haki kweli wakati alipookoa waamini wa Agano la Kale; kufa na ufufuko wa Kristo ulimpa njia ya haki kabisa kufanya hivi.

Neema inafunga njia kwa kujisifu (3:26-30)

Habari Njema inaonyesha namna gani Mungu anaweza kuhesabia wenye zambi haki (kwa njia ya ukombozi wa Kristo) na hata hivi kuwa mwenye haki (kwani deni ya zambi imelipwa na Mkombozi mkamilifu.) Wakati mtu anapohesabiwa haki kwa njia ya imani hawezikujisifu; angaliweza kujisifu kama angalihesabiwa haki kwa njia ya kushika sheria. Lakini kweli mtu anahesabiwa haki kwa njia ya imani, bila matendo ya sheria.

Kusudi la sheria linasimamishwa (3:31)

Si kusema ya kwamba sheria haina faida. Sheria inasema lazima mwenye kuivunja afe. Habari Njema inasema ya kwamba maagizo ya sheria yalitimizwa kabisa kwa msalaba. Kristo alikufa kwa pahali pa mwenye zambi, na sasa Mungu anaweza kuokoa mwenye zambi anayeaminu kwa sababu deni ya zambi zake imelipwa.

4. HABARI NJEMA NA MAANDIKO YA AGANO

LA KALE YANAPATANA (sura 4)

Abrahamu na Daudi walihesabiwa haki kwa njia ya imani (4:1-8)

Paulo anasema sasa juu ya maneno yaliyopata Abrahamu na Daudi kwa kuhakikisha ya kwamba Habari Njema inapatana kabisa na mafundisho ya Agano la Kale. Maandiko yanasema wazi ya kwamba Abrahamu alihesabiwa haki kwa njia ya imani, maana hakutenda matendo fulani kwa kuhesabiwa haki kwani neema na matendo ni mbalimbali. Ilikuwa vivyo hivyo ndani ya maisha ya Daudi aliyesema mtu wa heri ndiye mwenye zambi ambaye Mungu alimhesabia haki bila kutaja matendo ya sheria.

WAROMA

Namna ya imani ya Abrahamu (4:9-25)

Abrahamu alihesabiwa haki mbele ya kupata tohara, maana yake mbele ya kugeuka “Myuda”. Neno hili linaonyesha ya kwamba Mungu anahesabia haki vilevile watu wa Mataifa wanaoamini, kama anavyofanya na Wayuda wenye imani. Sasa Abrahamu ni baba ya waamini wote, si neno kama wao ni Wayuda au watu wa Mataifa. Kama watu wangalipata haki kwa njia ya kushika sheria, hakuna hitaji kwa neema. Lakini haki ni kwa neema kwa njia ya imani, na hivi waamini wanawenza kujuu kabisa ya kwamba wamekubaliwa na Mungu. Abrahamu ni baba ya waamini wote wa kweli. Neno hili lina-hakikishwa ndani ya Mwanzo 17:5 pahali anapoitwa “baba ya mataifa yote”. Aliitwa hivi kwa sababu aliamini ahadi ya Mungu kwamba atakuwa na mwana hata kama kwa watu neno hili halikuwezekana kwa sababu ya uzee wa Sara na uzee wake mwenyewe. Hivi alihesabiwa haki. Maneno haya yote yaliandikwa kwa ajili yetu vilevile. Tunahesabiwa haki kama tukimwamini yeye aliyefanya kazi iliyohitajwa kwa kutupatia sisi wokovu.

5. FAIDA YA HABARI NJEMA (5:1-11)

Salama na Mungu na baraka nyingine (5:1-5)

Mwamini anapata faida nyingine kwa njia ya kuhesabiwa haki: salama na Mungu; pahali pa kushangaza pa ukubali; tumaini la utukufu kwa wakati wa kuja; uwezo kufurahi katika mateso. Mateso haya yanafanya ndani yetu saburi, uvumilivu na tumaini lisilopatiza haya kamwe.

Mwamini hawesi kupotea kamwe (5:6-10)

Faida nyingine ya kuhesabiwa haki ni ya kwamba hatuwezi kupotea kamwe. Kristo alikufa kwa ajili yetu wakati tulipokuwa pasipo nguvu, wenye zambi, wapotevu na adui. Hatatuacha sasa wakati tunapokwisha kuhesabiwa haki, kuokolewa na kupatanishwa na Mungu!

Furaha katika Bwana (5:11a)

Faida ya sita ndiyo furahi tuliyo nayo ndani ya Mungu, si ndani ya zawadi zake tu lakini ndani ya mwenye kutoa zawadi hizi, ndiye Mungu mwenyewe.

Upanisho na Mungu (5:11b)

Mwishoni, tunapatanishwa na Mungu. Sasa tuna salama na Mungu kwa pahali pa uadui amba tulikuwa nao mbele.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

6. KAZI YA KRISTO INASHINDA ZAMBI YA ADAMU (5:12-21)

Baki la sura 5 linafunga pamoja maneno tuliyosoma mbele na mafundisho ya sura 6-8. Linaonyesha ya kwamba baraka ya kazi ya Kristo inapita mbali hukumu na taabu yaliyo matunda ya zambi ya Adamu. Kwa njia ya zambi ya Adamu watu wengi walikufa, lakini kwa njia ya kazi ya Kristo, neema imezidi kwa watu wengi zaidi. Zambi ya Adamu ilileta hukumu, lakini kwa njia ya kazi ya Kristo watu wanawenza kuhesabiwa haki. Kwa sababu ya zambi ya Adamu, mauti ilitawala, lakini kwa sababu ya kazi ya Kristo waamini wana-tawala katika uzima. Kosa la Adamu linaleta hukumu kwa wote wanaozaliwa na Adamu, lakini matokeo ya kazi ya Kristo ni kuhesabi-wa haki na uzima kwa wote walio ndani yake kwa sababu ya imani yao. Kuasi kwa Adamu kulifanyiza watu kuwa wenye zambi, lakini kwa sababu ya kutii kwa Kristo hata mauti watu wengi wamehesabiwa haki. Pahali zambi ilipozidi, neema ilizidi zaidi sana.

7. MWENENDO MTAKATIFU KWA SABABU YA HABARI NJEMA (Sura 6)

Wafu kwa zambi, hai kwa Mungu (6:1-10)

Watu waliuliza, “Tudumu katika zambi, neema izidi zaidi sana?” Jibu kwa ulizo hili ni “Sivyo, hata kidogo.” Hatuwezi kuendelea katika zambi kwa sababu tuliikufia. Wakati Kristo alipokufa, sisi tulikufa, na kwa sababu yeeye alikufia zambi, sisi tumekufa kwa zambi vilevile. Ubatizo ni mfano wa mauti na kuzikwa kwa mtu wetu wa zamani pamoja na Kristo na wa ufufuko wetu kutembea katika uzima mpya.

Kujihesabu wafu kwa zambi (6:11-14)

Lazima maneno haya yanayokwisha kufanyikana yaonekane wazi ndani ya maisha yetu: wakati tunapojaribiwa ingetupasa kukaa kama maiti isiyoweza kufanya kitu, na kujitoa kwa Mungu kufanya mapenzi yake. Neema inatuokoa toka utawala wa zambi.

Si watumwa wa zambi tena lakini watumwa wa Mungu (6:15-23)

Hata tukiwa chini ya neema sasa, si chini ya sheria, neno hili halitupi sisi ruhusa kufanya zambi. Mbele tulijitoa kuwa watumwa wa zambi, tukifanya maneno ambayo tuna haya juu yao tena sasa. Kuanza sasa ni sharti kwa sisi kuwa watumwa kwa haki na utakatifu. Tume-funguliwa toka utumwa wa zambi na sasa tunafurahi kuwa watumishi wa Mungu. Mishahara ya zambi imekombolewa na zawadi ya uzima toka Mungu.

WAROMA

Ona tofauti katikati ya maneno haya: zambi na Mungu; mishahara na zawadi; mauti na uzima wa milele.

8. SHERIA NDANI YA MAISHA YA MWAMINI (Sura 7)

Uhuru toka sheria (7:1-6)

Mauti inamaliza utawala wa sheria. Kwa mfano, mauti inavunja sheria ya ndoa. Wakati mume ni kwanza hai, mke wake anafungwa kwa mume wake kwa njia ya sheria. Lakini mume akikufa, mke ni huru kuolewa na mtu mwengine. Vivyo hivyo waamini wamewekwa huru toka sheria kwa njia ya mauti ya Kristo. Sasa tunaolewa na yeye, hivi tunaweza kuzaa matunda kwa Mungu. Wakati tusipookolewa bado tulizaa matunda kwa mauti, lakini sasa tumekufa kwa sheria na utumishi wetu ni katika uhuru, si utumwa.

Kazi ya sheria (7:7-14)

Si kusema kuna ubaya ndani ya sheria. Paulo anahakikisha neno hili kwa njia ya kuonyesha kazi kubwa ambayo sheria ilifanya ndani ya maisha yake wakati asipookolewa bado. Zamani aliweza kufanya zambi bila kufahamu kwamba ni zambi, lakini wakati sheria ilipoanza kutawala roho yake, iliamsha ndani yake tabia ya zambi; halafu mawazo yake kwamba yeye ni mwenye haki yalikuwa. Neno hili halikuwa kosa la sheria. Lakini wakati sheria ilipoagiza: Usitamani, zambi ndani ya roho ya Paulo ilionekana wazi kwa njia ya kutamani. Tabia yetu ya zambi inataka kufanya kila kitu kinachokatazwa na sheria.

Sheria haiwezi kutakasa mtu (7:15-25)

Sheria haina uwezo kuzaa utakatifu ndani ya mtu hata wakati anapokwisha kuokolewa. Paulo anaonyesha sasa vita ndani ya roho ya mwamini asiyejua bado kwamba yeye ni mmoja na Kristo ndani ya mauti na ufufuko. Tabia ya zamani na tabia mpya ndani yake zinashindana wakati wote. Anataka kufanya yaliyo haki lakini hana uwezo kutimiza maneno anayotaka kufanya. Ni kama kwa pahali pa kushinda anashindwa kila mara. Tabia ya zambi ni mbaya sana na hakuna kitu kinachoweza kuigeuza. Ni kama maiti inayofungwa kwa mgongo wa mtu. Kushinda ni ndani ya Kristo Yesu tu — lakini inawezekana namna gani?

9. ROHO MTAKATIFU NDIYE UWEZO KWA MAISHA MATAKATIFU (Sura 8)

Kutembea katika Raho (8:1-4)

Ndani ya sura 8 Paulo hasemi tena juu yake mwenyewe lakini juu

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

ya Roho Mtakatifu. Tutashinda kwa uwezo wa Roho Mtakatifu tu.

Roho ya uzima ulio katika Bwana Yesu anafungua mwamini tok Sheria ya zambi na mauti. Zambi ndani ya mtu inamkokota chini, lakin ni uzima wa Kristo ndani yake unamwezesha kushinda. Wale wanatembea katika Roho wanatimiza haki iliyoagizwa na sheria lakini sheria isiyoweza kuzaa ndani yao.

Shindano la mwili na Roho (8:5-14)

Wasioamini wanatawaliwa na mwili. Wanafikili maneno ya mwili, lakini nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu na haitii sheria yake, na mwisho wake ni mauti. Lakini waamini wanatawaliwa na Roho. Wanaweka roho juu ya maneno ya milele, yanayoleta uzima na salama, na ufufuko wa mwili ulio katika hali ya kufa sasa. Waamini si wadeni kwa mwili, lakini inawapasa kuua matendo ya mwili kwa njia ya kukataa majaribu yote kufanya zambi. Wote walio kweli wana wa Mungu wanaongozwa na Roho.

Roho ya kufanywa wana (8:15-18)

Waamini si watumwa wa woga, lakini Roho Mtakatifu anawafa-hamisha kwamba wao ni wana wa Mungu, wariti wa Mungu, na wariti pamoja na Kristo. Hata wakiteswa sasa, watatukuzwa pamoja kwa wakati wa kuja. Mateso kwa wakati wa sasa ni kitu bule wakati yanaposawanishwa na utukufu wa wakati wa kuja!

Toka mateso hata utukufu (8:19-25)

Viumbe vyote vinateeswa sasa kwa sababu ya zambi na vinangojea na hamu kubwa wakati waamini watakopofunuliwa kama wana wa Mungu, na wakati viumbe vyote vitakopofunguliwa toka taabu vyao. Hata waamini wanaugua, wakingojea miili yao ya utukufu. Hii ndiyo taraja tunayopokea pamoja na wokovu.

Maombi ya Roho Mtakatifu (8:26-27)

Roho Mtakatifu anatuombea mbele ya Baba wakati sisi wenyewe tusipojua namna gani inatupasa kuomba, na maombi yake yanapatana na mapenzi ya Mungu kila mara.

Maneno yote yanafanya kazi pamoja kwa mema (8:28-39)

Maneno yote ndani ya shauri kubwa la Mungu yanafanya kazi pamoja kupatia mema watu wale ambao wanampenda — tangu alipotujua katika milele inayopita kufika wakati mwishoni tutakapotukuzwa. Kwa sababu hii hakuna mtu anayeweza kutushinda. Anakwisha kutupa sisi Zawadi kubwa zaidi na hatatunyimia zawadi ndogo kupita. Hakuna mtu anayeweza kutushitaki au kutuhukumu. Hakuna

WAROMA

kitu au mtu ndani ya ulimwengu mzima anayeweza kututenga na mapendo ya Kristo.

10. HABARI NJEMA NA HISTORIA YA ISRAELI ZAMANI, SASA, NA KWA WAKATI WA KUJA (Sura 9-11)

Waisraeli walikataa Kristo (9:1-5)

Labda watu wengine wangefikili Mungu amevunja ahadi zake kwa watu wake wa zamani, ndio Israeli kwa sababu Habari Njema si kwa Wayuda peke yao lakini kwa Mataifa vilevile. Sura 9 kufika 11 zinaonyesha mashauri ya Mungu kwa wakati wa zamani, sasa, na wakati wa kuja.

Paulo anahuzunishwa sana kwa sababu ya kutoamini kwa Waisraeli wenzake hata kama walibarikiwa kwa njia nyingi.

Kukataa kwa Israeli na kusudi la Mungu (9:6-13)

Hata kama Waisraeli walikataa Kristo, si kusema ya kwamba neno la Mungu limekuwa bule. Tangu zamani alichagua watu kwa sababu ya ahadi zake na si kwa sababu ya uzazi wa jamaa. Kwa sababu hii alichagua Isaka, si Isimaeli, na alichagua Yakobo, si Esau.

Kukataa kwa Israeli na hukumu ya Mungu (9:14-33)

Mamlaka ya Mungu inaonekana kwa njia ya kuwa na rehema kwa watu wengine na kufanyiza moyo ya wengine migumu, kwa mfano Farao. Mungu hakufanyiza moyo wa Farao mgumu bila sababu. Lilikuwa kosa lake mwenyewe. Hakuna mtu anayeweza kushitaki Mungu juu ya neno hili. Kama mfinyanzi ana ruhusa kufanya neno lo lote na matope, vivyo hivyo Mungu ana ruhusa kuchagua Mataifa pamoja na Wayuda. Hata Hosea alitabiri ya kwamba Mataifa wataitwa vilevile, na Isaya alitabiri ya kwamba Waisraeli wote watakataliwa ila baki.

Mapendo ya Paulo kwa watu wake mwenyewe (10:1-4)

Paulo hakugeuka adui ya watu wake. Alipenda Wayuda sana hata alikuwa tayari kufa kwa ajili yao. Walikuwa na bidii kwa Mungu lakin ni walianguka kwa sababu walijaribu kujipatia haki kwa njia ya kushika sheria kwa pahali pa kuamini Kristo.

Kufanya kazi na kuamini kunashindana (10:5-10)

Maneno ya sheria na imani ni mbalimbali. Sheria inasema lazima tufanye maneno fulani kwa kupata wokovu. Imani inasema haifai tufanye kazi kwa kuokolewa, lakini tuamini. Haisemi kwa wewe kupanda mbinguni kuleta Kristo chini; amefika duniani mbele wakati alipogeuka mtu. Haisemi twende kwa kaburi kuleta Kristo juu kutoka

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kwa wafu; amekwisha kufufuliwa. Wakati unapoamini unahesabiwa haki, kisha unakiri kwa watu wengine ya kwamba umepata wokovu.

Matangazo ya Habari Njema ya wokovu (10:11-15)

Wokovu huu ni kwa “mtu ye yote” — Mataifa na Wayuda vilevile (mash. 11,12). Lakini ni lazima kutangaza habari hizi. Kwa sababu hii Mungu alituma watumishi wake kuhubiri Habari Njema; wenyе zambi wanasiкиа ya kwamba Mungu anataka kuwapa wokovu bila bei; wengine wanaamini habari hizi, wanaitia Bwana na kuokolewa.

Unabii ya kwamba Waisraeli watajibu na roho ya ubishi (10:16-21)

Si Waisraeli wote walioamini Habari Njema. Iilitangazwa pahali pote, na Mataifa waliiamini na kuokolewa, lakini Waisraeli wengi hawakuipokea. Bwana aliita Israeli mchana mzima na mikono ilionyoshwa, lakini walikataa na kuasi na roho ya ubishi.

Si Waisraeli wote waliokataliwa (11:1-10)

Mungu hakusukuma mbali watu wake wa zamani. Paulo ye ye mwenyewe alikuwa Myuda aliyeokolewa. Ilikuwa vivyo hivyo kwa wakati wa Elia. Zaidi ya taifa la Israeli walikuwa wameacha Mungu na waliabudu sanamu, lakini hata hivi kulikuwa na baki walioamini. Na sasa vilevile kuna baki waliochaguliwa, si kwa sababu ya matendo yao lakini kwa sababu ya neema ya Mungu mwenye enzi. Waisraeli wasioamini wana upofu rohoni, kama iliyotabiriwa katika Agano la Kale.

Kuanguka kwa Israeli si kwa milele (11:11-12)

Ndiyo, Waisraeli wameanguka kweli lakini si kwa milele. Mataifa walibarikiwa kwa njia ya kuanguka kwao. Lakini baraka hii ni kama kitu kidogo wakati inapowanishwa na ukubwa wa baraka kwa dunia nzima saa Israeli watakaporudishwa kwa wakati wa utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja!

Kusudi la kutupwa kwa Israeli (11:13-16)

Mtume alitaka baraka ya Mungu kwa Mataifa kuamsha wivu ndani ya Waisraeli wengine na kuwasukuma kuamini na kupata wokovu vilevile. Inapasa Mataifa kufahamu ya kwamba kutupwa kwa Israeli kulikuwa upatanisho kwa dunia; vivyo hivyo mwisho wa kupokewa kwao tena utakuwa uzima toka wafu duniani pote. Na kama Abrahamu (malimbuko na shina) aliwekwa mbali kwa Mungu, vivyo hivyo na wazazi wake waliokuwa Waisraeli (shina na matawi).

Mzeituni mzuri: pahali pa baraka (11:17-24)

Israeli (mengine ya matawi) walikatwa toka pahali pa baraka ya Mungu na Mataifa (mzeituni wa poli) waliingizwa. Lakini haifai

WAROMA

Mataifa kujisifu kwa sababu ingekuwa nyepesi kupita kuondosha Mataifa na kuingiza Israeli tena.

Ahadi ya kwamba Israeli wataokolewa (11:25-27)

Ugumu umepata Waisraeli wale wasioamini kufika wakati hesabu ya mataifa watakaoingizwa Kanisani itakapotimia. Kisha wakati Bwana atakapokuja tena, baki la Wayuda walioamini wataokolewa, kama Isaya na Yeremia walivyotabiri.

Waisraeli mbali na Mungu lakini wapendwa (11:28-32)

Kwa wakati wa sasa Waisraeli ni mbali na Mungu, na Habari Njema inahubiriwa kwa Mataifa. Lakini wanapendwa na Mungu hata hivi kwa ajili ya baba zao, na mwishoni Mungu atatimiza ahadi zake. Kama vile Mataifa walioamini walipata rehema, vivyo hivyo wakati Waisraeli watakapopata wivu kwa sababu ya baraka ya Mataifa, wao vilevile watapata rehema. Hivi rehema itakuwa kwa watu wote.

Ajabu ya akili ya Mungu (11:33-36)

Wakati tunapowaza juu ya matendo ya ajabu ya Mungu katika neema tunajazwa sifa na kuabudu. Hatuwezi kuvumbua utajiri, heki-ma na maarifa yake na njia zake hazitafutikani. Hakuna mwingine aliye sawasawa naye kwa njia ya akili, hahitaji mshauri kumwongoza, na hana deni karibu na mtu. Vitu vyote viliumbwaa kwa uwezo wake na ni kwa utukufu wake.

11. MWENENDO UNAOFAA WAAMINI (12:1 – 15:13)

Madaraka yao kwa Mungu, Kanisa na watu wengine (Sura 12)

Baki la barua kwa Waroma ni zaidi mafundisho kwa mwenendo wa wale wanaokwisha kuhesabiwa haki kwa njia ya imani.

Kuna neno moja tu ambalo linastahili kwa sisi kufanya kwa sababu ya rehema za Mungu, ndilo kujitoa mzima kwake, kuepuka kufanashwa na namna ya dunia, na kufanywa upya katika nia zetu (mash. 1,2). Hakuna nafasi kwa kujivuna, au kwa kufikili hatuna faida, kwa sababu kila kiungu cha mwili wa Kristo kimepewa zawadi au kazi yake (mash. 3-5). Lazima tutumike na zawadi hizi na uwezo toka Mungu (mash. 6-8). Lakini kuwa na zawadi tu hakutoshi; lazima Kristo aonekane vilevile ndani yetu na ndani ya matendo na mwene-ndo wetu, kama tunavyoona ndani ya mashairi 9-21.

Mwamini na serikali (13:1-7)

Lazima waamini watii serikali kwa sababu ni Mungu ambaye aliwapa watawala amri yao kwa kuchunga taratibu katikati ya watu na

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kuazibu waasi. Watawala ni watumishi wa Mungu mbele ya watu hata kama wasipomjua wao wenyewe. Kushindana na watawala ni kushindana na Mungu na wale wanaofanya hivi wataazibiwa. Tunatii serikali kwa njia ya kulipa kodi na kuwa na heshima kwa watawala. Sharti tutii na kuombea watawala na kulipa kodi. Lakini kama mtawala akiagiza watu kufanya kitu kisichopatana na maagizo ya Mungu, halafu inapasa waamini kukataa kutii serikali, na kuvumilia bila kunununika azabu kwa kuasi kwao (ona Matendo 5:29).

Mwamini na jirani (13:8-10)

Neno lingine la lazima ni mapendo kwa jirani. Mtu yule anayepeenda jirani yake anatimiza sheria.

Kuvaa Bwana Yesu Kristo (13:11-14)

Tunabaki na muda mfupi tu hapa duniani na wokovu wetu, maana wakati tutakapopata miili yetu ya utukufu, ni karibu kupita mbele. Hivi ni sharti kwetu kuachana na kazi chafu za giza na kuva Bwana Yesu Kristo bila kufikili tena mahitaji ya mtu wa zamani.

Sheria ya uhuru (14:1-13)

Ndani ya 14:1 – 15:13 mtume Paulo anafundisha juu ya matendo ya Wakristo yasiyo mabaya wala mazuri. Labda watu wengine ni “zaifu” na zamiri zao zinawashitaki juu ya maneno haya. Wengine ni “wenye nguvu”, maana yake wao ni huru ndani ya roho yao kufanya maneno haya bila kuwa na damiri mbaya. Basi tuone mafundisho juu ya maneno haya:

Ni lazima kupokea ndugu aliye zaifu, lakini si na kusudi la kubishana naye juu ya mawazo yake (sh.1). Haifai ndugu mwenye nguvu kuzarau yule aliye zaifu, na si vizuri kwa ndugu zaifu kuhukumu mwenye nguvu. Hatuna ruhusa kuhukumu watumishi wa Mungu juu ya maneno haya (mash. 2-4). Sharti kila mtu ajue katika akili yake mwenyewe nini inampasa kufanya kwa maneno ya vyakula na siku kubwa za sheria. Neno kubwa ndilo hili: wote wanajaribu kupendeza Bwana (mash. 5-9). Itakuwa sharti kwetu kusimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo na kutoa habari zetu mbele ya Bwana juu ya matendo yetu, si habari za matendo ya wengine. Kwa pahali pa kuhukumu wengine inatupasa kukaa na ange tusitie kitu cha kukwaza katika njia ya mtu ye yote (mash. 10-13).

Sheria ya mapendo (14:14-23)

Hakuna chakula kinachoweza kufanyiza mtu mchafu, lakini kama mtu akifikili vyakula hivi si safi, haifai kwake kuvikula. Vyakula si neno kubwa. Haifai kwetu kuhuzunisha ndugu mwingine au kuharibu

WAROMA

hali ya roho yake au ushuhuda wetu wenyewe juu ya maneno namna hii. Maneno makubwa ndiyo haki, salama na furaha nayo yanapendeza Mungu na kukubaliwa na watu (mash. 13-18). Inatupasa kukaa na salama na upatano mzuri pamoja na ndugu zetu kanisani na kujaribu kujengana. Haifai tufanye neno lo lote linaloweza kuzuiza kazi ya Mungu ndani ya maisha ya mtu mwengine. Si vizuri kwa mtu kufanya neno kama akishitakiwa na zamiri yake juu yake. Na ni vizuri kutokula nyama wala kunywa mvinyo kamwe kama maneno haya yakiweza kuangusha mtu mwengine katika imani yake. Kama sisi tukiweza kufanya maneno haya yasiyo mabaya bila kushitakiwa juu yao na zamiri zetu, inatupasa kuyafanya wakati tulipo peke yetu. Ndugu aliye zaifu anafanya zambi kama akiwa na zamiri mbaya juu ya chakula fulani anachokula (mash. 19-23).

Kubeba mizigo ya watu wengine (15:1-4)

Mashairi 13 ya kwanza ya sura 15 yanaendelea na mafundisho juu ya maneno yasiyo mabaya. Inapasa wenye nguvu rohoni kutendea wazaifu na mapendo wakikumbuka mahitaji yao, na sharti kila mtu aige Kristo aliyependeza wengine, si yeze mwenyewe. Kristo aliishi kupendeza Baba yake, na wakati watu wa dunia walipolaamu Mungu Baba, ni Kristo ambaye alibeba malaamu haya, kama mwandishi wa Zaburi alivyotabiri.

Kutukuza Mungu pamoja (15:5-13)

Tunafikili mabishano juu ya vyakula na kushika siku kubwa za sheria yalianza katikati ya Wakristo Wayuda (wazaifu) na wale wa Mataifa. Paulo anaomba wao wote waweze kukaa na salama pamoja kufuatana na mafundisho na mfano wa Bwana Yesu, wakiabudu Mungu pamoja na kukaribishana kwa utukufu wake (mash. 5-7). Kazi ya Bwana Yesu ni kwa Wayuda na Mataifa vilevile, kama mashairi haya toka Agano la Kale yanavyoonyesha, na inatupasa kupokea Wayuda na Mataifa pamoja. Paulo anamaliza sehemu hii ya barua yake na maombi ili Mungu aweze kujaza waamini na furaha na salama katika kuamini (mash. 8-13).

12. MAELEZO YA MWISHO, MAONYO, NA SALAMA (15:14 - 16:27)

Paulo aliandika barua hii na kusudi gani (15:14-16)

Paulo aliamini ya kwamba waamini katika Roma watakumbuka maneno ambayo aliwaambia na kumkubali kama mtumishi kwa Mataifa.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Mahubiri ya Paulo: toka Yerusalem hata Iliriko (15:17-21)

Paulo hakujisifu juu ya kazi Mungu aliyofanya kwa njia ya watu wengine, lakini juu ya mambo makubwa Bwana aliyofanya kwa njia ya utumishi wake mwenyewe tu kwa Mataifa. Shauri lake halikuwa kujenga juu ya msingi wa mtu mwingine, lakini kuhubiri Habari Njema pahali isipohubiriwa mbele, na kutimiza unabii wa Isaya juu ya Habari Njema ikifikia Mataifa.

Shauri la Paulo kufikia Roma (15:22-29)

Kufika wakati ule kazi nyingi ilikuwa imemzuiza asifikie Roma, lakini nyuma ya kufikisha mali toka makanisa ya mataifa kwa watakatifu wenye hitaji katika Yerusalem, alikusudi kufikia Roma kwa safari yake kwenda Spania. Zawadi hii ya mali toka makanisa ya mataifa ilikuwa malipo yao kwa deni waliyokuwa nayo kwa baraka za roho walizokwisha kupokea.

Paulo aliwasih i kumwombea (15:30-33)

Paulo alimaliza sehemu hii ya barua yake na kusihi waamini kumwombea ili asiumizwe kwa safari yake na Wayuda katika Yudea, watakatifu Wayuda katika Yerusalem wapokee na roho nzuri mali ambayo aliwaleta toka makanisa ya Mataifa, na aweze kukaa na furaha pamoja na waamini katika Roma na kuburudishwa pamoja nao.

Kusaidia ndugu mke katika Kristo (16:1-2)

Vilevile ndani ya barua hii Paulo alijulisha waamini katika Roma habari za Foibe aliyezwa mtumishi mwaminifu wa kanisa katika Kenkurea.

Salamu kwa watakatifu katika Roma (16:3-16)

Mashairi haya ni salamu kwa waamini wengine ambaeo Paulo aliwajua, hata kama hakufikia Roma mbele. Watu wengine wanashitaki Paulo bila sababu ya kwamba yeche ni adui ya wanawake. Watu hawa waone majina ya Wakristo wake wengi ambaeo anawasalimu na sifa: Maria, Yunia, Tirifena, Tirifosa, Persi, mama ya Rufo, Herma, Yulia, ndugu mke ya Nereo, na Foibe aliyezikisha barua hii kwa Roma!

Watu wengine wamesawanisha sura hii na Kiti cha Hukumu cha Kristo.

Maonyo juu ya wenye kuharibu kanisa (16:17-20)

Paulo hakuweza kumaliza barua yake bila maonyo juu ya walimu wa uwongo walioweza kujaribu kuingia kwa siri katikati ya kanisa.

WAROMA

Salamu toka rafiki za Paulo (16:21-24)

Paulo alipitisha vilevile salamu toka rafiki Wakristo waliokuwa pamoja naye, katikati yao Tertio aliyesaidia Paulo na kuandika barua hii yenye mafundisho makubwa.

Baraka (16:25-27)

Barua inakwisha na wimbo wa sifa kutukuza Mungu kwa sababu ya kufunua siri ya Kanisa kwa njia ya manabii wa Agano Jipyä.

Barua ya kwanza ya Paulo kwa Wakorinto

MWANZO

Mwanzo wa Kanisa katika Korinto

Paul alifikia Korinto mara ya kwanza kwa safari yake ya pili ya kuhubiri (Matendo 18). Kwanza alihubiri katikati ya Wayuda pamoja na Pirisila na Akila, mafundi ya kufanya hema pamoja naye. Wakati zaidi ya Wayuda walipokataa Habari Njema aligeuka kwa Mataifa na wengi wao waliokolewa na kanisa lilianzwa.

Sababu na tarehe ya 1 Wakorinto

Karibu miaka mitatu nyuma, wakati Paulo alipokuwa akihubiri katika Efeso, alipokea barua toka Korinto juu ya matata kanisani. Barua hii ilikuwa na maulizo juu ya maneno mbalimbali juu ya desturi na mwenendo wa Wakristo. Paulo aliandika barua hii ya kwanza kwa Wakorinto kujibu maulizo haya.

UMBO LA 1 WAKORINTO

1. Salamu (1:1-3)
2. Mashukuru ya Paulo (1:4-9)
3. Matengo kanisani (1:20 – 4:21)
4. Hukumu kanisani (Sura 5)
5. Kushitakiana kwa waamini (6:1-11)
6. Namna gani kujua yaliyo mema au mabaya (6:12-20)
7. Mafundisho juu ya ndoa na kutooa (Sura 7)
8. Maulizo juu ya kula nyama zilizotolewa kwa sanamu (8:1 – 11:1)
9. Mafundisho kwa wanawake juu ya kufunika vichwa vyao (11:2-16)
10. Utaratibu kwa karamu ya ukumbusho wa Bwana (11:17-34)
11. Zawadi za Roho na kazi yao kanisani (Sura 12-14)
12. Jibu la Paulo kwa wale waliosema kwamba hakuna ufufuko (Sura 15)
13. Mafundisho juu ya kutoa sadaka (16:1-4)
14. Mashauri ya Paulo (16:5-9)
15. Maonyo ya mwisho na salamu (16:10-24)

1 WAKORINTO

1. SALAMU (1:1-3)

Ilikuwa desturi ya Paulo kwa mwanzo wa barua zake kusema maneno machache kukumbusha wasomaji ya kwamba aliiwa kuwa mtume, juu ya Wakristo waliokuwa pamoja naye, na neno fulani juu ya kanisa ambalo aliwaandikia barua yenye. Halafu aliongeza salamu yake, neema na kweli. Hapa ndani ya barua yake kwa waamini katika Korinto aliongeza “waliotakaswa katika Yesu Kristo ... watakatifu.” Ndiyo, kwa macho ya Mungu walikuwa watakatifu lakini tutaona ya kwamba mwenendo wao ulikuwa mbali na mwenendo unaotosha kwa watakatifu mara nyingine.

2. MASHUKURU YA PAULO (1:4-9)

Mtume alishukuru Mungu kwa sababu Wakristo wa Korinto walitajirishwa na zawadi za Roho Mtakatifu, zaidi zawadi za kusema kwa lugha, na maarifa. Neno hili lilihakikisha ya kwamba Mungu alikuwa akitumikia ndani ya maisha yao, na Paulo aliamini kabisa ya kwamba Bwana atawasibitisha hata mwisho.

3. MATENGO KANISANI (1:10 – 4:21)

Jamii mbalimbali katika Korinto (1:10-17)

Neno la kwanza lisilokuwa taratibu lilikuwa matengo kanisani, kila jamii wakitaja kiongozi wao wenyewe. Neno hili lilikana umoja waa mwili wa Kristo na kumzarau Yule aliyesulibishwa kwa ajili yao. Lilikana vilevile maana ya ubatizo. Paulo alikuwa amebatiza watu wachache tu, akiogopa ya kwamba watu watamheshimu yeye kupita Kristo. Hakutegemea uwezo wake kusema na akili ili msalaba wa Kristo usifanyizwe kuwa bule. Ingepasa wahubiri wote wa wakati wa sasa kuwa na uangalifu na unyenyekevu namna hii!

Akili na uwezo wa Mungu (1:18-25)

Ni kama kulikuwa na wengine katika Korinto waliotaka kusaidia wenye elimu na ufahamu kwa njia ya kupunguza kidogo ukali wa msalaba wa Kristo. Paulo alisema wazi ya kwama habari za Msalaba ni mbali na maneno yote watu wa dunia wanayohesabu kuwa akili. Ni upumbavu kwa wale wanaopotea, lakini Mungu anautumia kuwaokoa wale wanaoamini. Ni kikwazo kwa Wayuda waliopenda alama, na upumbavu kwa Wayuda waliopenda akili, lakini ni uwezo wa Mungu kwao wanaoitwa naye. Mungu anautumia “upumbavu” na “uzafu” kufanya neno ambalo watu kwa uwezo na akili yao hawawezi kufanya kamwe.

Kujisifu katika Bwana (1:26-31)

Kwa nini Wakorinto wataheshimu sana hekima na elimu? Wao

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

wenyewe hawakuwa wenyewe kujifunza sana! Mungu anachagua wapumbavu na wazaifu, watu wa chini wanaozarauliwa na watu wa dunia kutimiza makusudi yake ili ye ye mwenyewe apate sifa na watu wasiwe na njia kujisifu. Kristo ni akili, haki, utakaso na ukombozi wetu; tukitaka kujivuna, vizuri tujivune juu ya Kristo!

Kuhubiri Kristo aliyesulibowi (2:1-5)

Kama mfano wa maneno aliyo sema mtume alikumbusha Wakorinto namna gani ye ye mwenyewe aliingia katikati yao. Hakujaribu ku washangaza na masemo makubwa na maneno ya akili, lakini alihubiri tu habari za Kristo aliyesulibishwa. Hakuwa na uwezo ye ye mwenyewe; alikuwa zaifu, mwenye woga na matetemeko. Walijua ya kwamba si ye ye aliye fanya maneno yale makubwa yaliyotokea ndani ya maisha yao — iliwapasa kusifu Bwana tu juu yao.

Ufunuo kwa njia ya Roho ya Mungu (2:6-10a)

Si kusema ya kwamba Habari Njema ni upumbavu; kwa wenyewe kukomea katika maneno ya roho ni akili ya Mungu ambayo ilikuwa siri tangu mwanzo wa wakati. Isaya alitabiri ya kwamba siku nyingine Mungu atafunua kweli za ajabu watu wasizowenza kujua wala kufikili. Sasa alikuwa amefunua kweli hizi kwa mitume kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Ufunuo (2:10b-12)

Kwanza, kulikuwa ufunuo. Kwa njia tusiyoweza kufahamu Roho ya Mungu alifunua kweli hizi za ndani za Mungu kwa Paulo na kwa waandishi wengine wa Agano Jipy. Roho Mtakatifu tu anajua nia ya Mungu, hivi ye ye tu anayeweza kufunua kweli za Mungu kwa watu wa Mungu.

Maongozi ya Roho Mtakatifu (2:13)

Tena kulikuwa na maongozi. Mitume waliandika kweli walizofunuliwa na maneno yale yale ambayo Roho Mtakatifu aliwaongoza kutumia. Hawakuandika maneno ambayo akili yao ya mtu yaliweza kuwaongoza kuandika na kutumia.

Utambuzi (2:14-16)

Mwishoni, kuna utambuzi. Ndiyo, Habari Njema ilifunuliwa na Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu, na ni Roho Mtakatifu aliyeongoza kuandika kwake, lakini watu wanaweza kuifahamu kwa uwezo wa Roho ya Mungu tu. Mtu wa dunia hawezi kupokea kweli za Mungu; ni upumbavu kwake. Mtu wa Mungu, mwenye nia ya Kristo anaweza kutambua kweli hizi za ajabu, hata kama wasioamini hawawezi kumfahamu ye ye.

1 WAKORINTO

Kutembea kwa mwili kunaleta wivu na ugomvi (3:1-4)

Kwa sababu Wakorinto walitawaliwa na mwili, kulikuwa na wivu na ugomvi katikati yao na walitengana ndani ya chama zilizoongozwa na viongozi mbalimbali. Ndiyo, walitenda kama watu wa dunia tu na Paulo hakuweza kuwafahamisha kweli za ndani.

Kupanda na kutia maji (3:5-9)

Ilipasa Wakristo wa Korinto kufahamu ya kwamba watu kama Apolo na Paulo walikuwa watumishi tu, si bwana. Kama watumishi, kazi yao ilikuwa kupanda na kutia maji; Mungu yeye mwenyewe tu anaweza kuleta uzima. Kwa wakati wa kuja kazi yao itapimwa na watapewa zawabu. Kufika siku ile walitumika pamoja, wakitumikia Wakorinto waliosawanishwa na Paulo kuwa shamba la Mungu na jengo la Mungu.

Wajengaji namna tatu (3:10-17)

Paulo alikuwa amefikia Korinto kama mjengaji mkubwa mwenye akili na kuweka msingi, ndizo kweli juu ya Kristo na kazi yake. Walimu wengine walifika nyuma yake na kujenga juu ya msingi huu. Mafundisho yote ni namna tatu: mengine yana faida inayodumu, mengine yana faida kwa muda mfupi tu, mafundisho mengine ni mafundisho ya kuharibu. Kila mwalmu atapewa zawabu kwa kadiri ya kazi yake. *Mwalmu mwema* anajenga na zahabu, feza, na mawe ya bei kubwa, maana yake mafundisho yake ni mazuri na yanadumu. Labda *mwalmu mwingine* anajenga na miti, nyasi, na majani, maana yake mafundisho yake ni ya juujuu tu na yana faida kwa muda mdogo tu. Labda *mjengaji wa tatu* anaharibu kanisa na mafundisho yake mabaya. Mtu wa kwanza atapewa zawabu; wa pili atapata hasara laki ni yeye mwenyewe ataokolewa. Wa tatu ataharibiwa kwa sababu hakuwa mwamini wa kweli.

Ndani ya Kristo vitu vyote ni vyetu (3:18-23)

Mtumishi mwenye akili ya kweli wa Kristo anafahamu ya kwamba yeye mwenyewe si kitu. Ni akili ya kweli kwa watu wa Mungu kufahamu ya kwamba wanaweza kusaidiwa na watumishi wote wa Mungu; haifai kwao kuwa na upendeleo kwa mtumishi fulani na kumfanyiza mkubwa wa jamii yao.

Uwakili wa siri za Mungu (4:1-5)

Viongozi Wakristo ni watumishi wa Kristo na mawakili wa kweli za Mungu. Ni lazima kwao kuwa waaminifu. Watu wengine hawawezi kujaribu kipimo cha uaminifu wao. Mtumishi wa Kristo hawezи kujua hata kipimo cha uaminifu wake mwenyewe! Mungu tu

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

anaweza kufanya hivi, hivi inapasa kuacha maneno ya hukumu mikononi mwake.

Mwanzo wa matengo (4:6-7)

Kiburi ndicho neno liloleta matengo ndani ya kanisa kwa Korinto. Lakini neno hili ni upumbavu. Ni Mungu tu ambaye anampa mwalimu mmoja zawadi kubwa kupita mwagine.

Wapumbavu kwa ajili ya Kristo (4:8-13)

Wakorinto walitegemea maneno ambayo walikuwa nayo. Walikuwa wenyewe kiburi, mali nyangi, na walikaa katika anasa bila masumbuko. Walikuwa wakitawala kama wafalme, lakini mitume walikuwa na njaa, kiu, mavazi ya kupasukapasuka. Walipigwa, walikosa pahali pa kupanga, waliteswa na kuzarauliwa na kutendewa kama uchafu wa dunia!

Paulo anawasihi kama baba (4:14-21)

Paulo alieleza ya kwamba hakutumia zihaka kupatisha waamini haya. Kama baba yao katika imani, aliwasihii kumwiga. Alikuwa aktuma Timoteo kwao kuwakumbusha namna ya maisha yake. Si kusema ya kwamba Paulo hatakwenda Korinto yeeye mwenyewe. Alikusudi kwenda, na saa yenyeewe atafahamu kama wale walioleta matengo walisema bule tu au kama Roho ya Mungu alitumika kwa njia yao. Hali yao itamwonyesha namna gani itampasa kutenda katikati yao.

4. HUKUMU KANISANI (Sura 5)

Uzalimu kanisani (5:1-8)

Halafu Paulo alifundisha juu ya neno baya lingine kanisani. Mtu mmoja alikuwa amefanya zambi kwa njia ya kulala na mama ya mke wake (ni kama hakuwa mama yake kabisa lakini mke mwagine wa baba yake). Watu wa kanisa hawakuhuzunishwa juu ya zambi hii lakin walijivuna. Paulo hakuwa pamoja nao lakini alihukumu mtu huyu katika roho yake mwenyewe na kumtoa kwa Shetani ili mwili wake uharibiwe kusudi aweze kuacha zambi za namna hii. Zambi ni kama chachu; inaenea na kuingia maisha ya watu wengine. Inagusa watu wote kwa ubaya. Ingepasa maisha ya waamini kuwa kama karamu ya daima ya mkate usiochachwa, maana yake ingewapasa kuwa wenyewe moyo safi na kweli.

Ni lazima kuhukumu uzini (5:9-13)

Haiwezekani kwetu kuepuka kukutana na watu wenyewe zambi ya

1 WAKORINTO

mwili ndani ya maisha yetu ya kila siku. Lakini ni vibaya kwa Wakristo kukubali kanisani wale waliokwisha kufanya zambi namna hii. Ni maneno ya Mungu kuhukumu wasioamini waovu, lakini ni kazi yetu kuondosha kanisani watu wanaokiri kuwa waamini lakini wao ni wenyewe kutenda uzini, wenyewe wivu, waabudaji sanamu, wenyewe kusingizia na kudanganya. Haifai kuwa na ushirika na kula pamoja na wenyewe kutenda zambi hizi.

5. KUSHITAKIANA KWA WAAMINI (6:1-11)

Kushitakiana mbele ya waamuzi wasioamini (6:1-5)

Neno lingine la matata kwa Korinto lilikuwa waamini walioshitakiana mbele ya waamuzi wasioamini. Paulo alifikili neno hili halifai hata kidogo kwa Wakristo. Waamini watahukumu dunia na *hata malaika* siku nyingine; basi ingewapasa kuweza kuhukumu maneno ya maisha ya sasa. Ingepasa kuwa hata na mtu mmoja ndani ya kanisa la pahali fulani anayeweza kuangalia maneno ya namna hii!

Kutendewa mabaya ni vizuri kupita kutenda zambi (6:6-11)

Kuvumilia kutendewa mabaya na kudanganya ni vizuri kupita kwenda kushitaki ndugu Mkristo mbele ya waamuzi. Lakini waamini walikuwa wakifanya mabaya na kudanganya. Walikuwa wakitenda kama watu waovu wasiojua Mungu na wasioriti ufalme wa Mungu. Walikuwa wameoshwa, walitakaswa na kuhesabiwa kuwa na haki; basi waonyeshe maneno haya ndani ya mwenendo wao.

6. NAMNA GANI KUJUA YALIYO MEMA AU MABAYA (6:12-20)

Ndani ya mashairi haya mtume anatusaidia kufahamu kama ikipasa mwamini kutenda namna gani. Maneno mengine si zambi lakini hayana faida vilevile. Mengine si zambi, lakini yanaweza kugeuka desturi kutufunga. Mengine yana faida kwa muda mfupi tu. Lakini ni zambi *kila mara* kutumia mwili kwa uzini. Mwili ni kwa Bwana, na Bwana kwa mwili. Mwili wa Kristo ulifufuliwa, na miili yetu itafufuliwa vilevile. Ndiyo, miili yetu ni viungo vya Kristo. Kutenda uasherati ni kukosea mwili kupita zambi yo yote nyingine. Mwili ni hekalu la Roho Mtakatifu lililonunuliwa na Kristo na lililo mali ya Mungu.

7. MAFUNDISHO JUU YA NDOA NA KUTOOA (Sura 7)

Wakristo walikuwa wameandikia Paulo na maulizo juu ya ndoa na kutooa. Mtume anajibu maulizo haya sasa.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Mafundisho juu ya ndoa (7:1-6)

Ni vizuri kutooa. Lakini ni afazali kuoaa kuepuka hatari ya kuingia zambi. Ni sharti kuoaa mtu mmoja tu na inapasa mume kumpa mke wake haki yake na vivyo hivyo mke ampe mume haki yake kwani wanahitajiana. Kuna sababu moja tu kwa kunyimana, ndiyo kwa kuji-toa kwa maombi. Lakini vizuri wanyimane kwa wakati tu, nyuma ya kupatana juu yake mbele. Ni ruhusa yao kufanya hivi, si agizo.

Maonyo kwa wale wasiooa bado na kwa wajane (7:7-9)

Paulo alifikili ni vizuri kukaa bila kuoaa, lakini alifahamu ya kwa-mba mtu anaweza kufanya hivi tu kwa uwezo wa Mungu. Hata kama alisema kwa wale wasiooa na kwa wajane kwamba ni vizuri kukaa hivi, alikubali ya kuwa ndoa ni vizuri kwa wale wasioweza kutawala miili yao.

Mafundisho kwa waamini waliooa (7:10-11)

Kama mume na mke wake ni waamini, haifai wavunje ndoa yao. Kama wakiachana, ruhusa haiko kuoana na watu wengine kusudi njia ibaki wazi kwa mume na mke wake kupatana tena.

Mafundisho juu ya ndoa ya mwamini na msiyeamini (7:12-24)

Kama Mkristo akiolewa na msiyeamini, haifai Mkristo kuachana na msiyeamini kwani msiyeamini ni kwa pahali pa baraka. Kwa sababu ameolewa na mwamini, nao wanakaa karibu karibu, msiyeamini anasikia Habari Njema na kuona matunda yake ndani ya mume (au mke) wake. Kama msiyeamini akitaka kuondoka, awe na ruhusa kufanya hivi na salama, lakini pamoja na taraja ya kwamba siku nyingine ataokolewa. Mafundisho makubwa hapa ndiyo ya kwamba hata mtu akigeuka Mkristo si sharti kwa yeze kuharibu namna alivyoo-kaa katikati ya watu mbele, kama mume wa mke wake, na mwenyezi wa inchi anayetii serikali.

Maonyo kwa wale wasiooa (7:25-28)

Maonyo haya ni kwa wale wasiooa bado, wanaume na wanawake. Ni vizuri kukaa namna walivyo, kwa sababu ya matata ya wakati wa sasa, maana yake mateso ya kuishi hapa duniani. Ni vivyo hivyo leo, kama ilivyokuwa kwa wakati wa Paulo. Lakini maana yake si kusema inapasa wale waliooa waachane, au ya kwamba ni zambi kuoaa, hata kama matata ni nyangi.

Faida ya kukaa bila kuoaa (7:29-38)

Kwa sababu ya ufupi wa wakati ni vizuri kupita kwa mtu kukaa bila kuoaa kusudi aweze kutumikia Bwana na roho moja. Kama mtu

1 WAKORINTO

akikosa adabu juu ya ubikira wake, maana ikimshinda kujitawala kwa maneno ya mwili, ana ruhusa kuoa. Lakini ni faida kupita kama akiweza kujitawala mwenyewe na kuchunga ubikira wake.

Maonyo kwa wajane Wakristo (7:39-40)

Ndoa ya mjane ilikwisha wakati mume wa mjane Mkristo alipokufa. Sasa yeche ni huru kuolewa tena lakini atakuwa na furaha kupita kama akibaki mjane.

8. MAULIZO JUU YA KULA NYAMA ZILIOTOLEWA KWA SANAMU (8:1 – 11:1)

Hekima na mapendo (8:1-3)

Hekima peke yake haitoshi kutuongoza ndani ya maneno haya kwani hekima inaleta kiburi. Neno linalohitajiwa zaidi ni mapendo.

Mungu mmoja na Bwana mmoja (8:4-6)

Kwanza kuna maneno mengine ambayo inatupasa kufahamu juu ya sanamu. Sanamu si mifano ya miungu ya kweli. Watu wengine wanafikili kuna miungu mbinguni na duniani, lakini kuna Mungu mmoja tu wa kweli, na Bwana mmoja wa kweli, ndiye Yesu Kristo.

Inapasa kukumbuka zamiri ya watu wengine (8:7-13)

Labda utakwalisha ndugu aliye zaifu katika imani kama ukikula vyakula vilivyotolewa kwa sanamu. Kama ni hivi, ni neno dogo kuacha kula vyakula vile. Ni neno kubwa, neno bayaa, kukwalisha ndugu aliye zaifu. Labda itamsukuma kufanya neno ambalo zamiri yake inamkataza kufanya, na kwa njia ya kufanya hivi mtu huyu ambaye Kristo alimkufia, anaharibu ushuhuda wake. Kuangusha mtu huyu ni kufanya zambi juu ya Kristo. Ingekuwa vema kutokula nyama hata milele nisiangushe ndugu yangu. Ni vivyo kwa maneno ya kuyuwa mvinyo. Ni vizuri kuacha kufanya maneno yaliyo halali kwetu, kupita kuzuiza mtu mwingine asiendelee katika imani.

Paulo alijikana mwenyewe (9:1-14)

Paulo alikuwa mfano wa kujikana mwenyewe ili watu wengine waweze kubarikiwa. Alikuwa mtume aliyeona Bwana, na Mungu alikuwa amebariki kazi yake, hivi ilikuwa haki yake kupewa zawadi za mali kumsaidia ndani ya mahitaji yake. Alitaja maneno sita kuhakikisha neno hili: (1) mitume wengine walisaidiwa hivi; (2) hapa duniani askari, mlinzi wa shamba la mizabibu, na mchungaji kondoo wanashiriki ndani ya matunda ya kazi yao; (3) sheria ya Musa iliagiza mwenye kupanda shamba apate nusu ya mavuno yake; (4) hata kwa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

wakati ule Wakristo wa Korinto walikuwa wakisaidia watu wengine; (5) wale wanaofanya kazi ya hekalu walipewa mali kwa mahitaji yao; (6) Bwana aliagiza kwa wale waliohubiri Habari Njema kupata maisha yao kwa Habari Njema.

Kuhubiri Habari Njema pasipo bei (9:15-18)

Lakini mtume Paulo alikataa kusaidiwa hivi, hata kama ilikuwa haki yake. Hakuweza kujisifu juu ya kuhubiri Habari Njema, kwa sababu alilazimishwa na Mungu kufanya hivi. Hivi atajisifu kwa sababu aliweza kujichunga na mali yake mwenyewe na kuhubiri Habari Njema pasipo bei kwa watu wengine.

Kutumikia watu wote (9:19-23)

Kila mara alipoweza bila kuharibu ushuhuda wake aliacha, kwa ajili ya Habari Njema, maneno yaliyokuwa haki yake, wakati alipokuwa pamoja na Wayuda waliokuwa chini ya sheria, au pamoja na wengine wasiokuwa chini ya sheria, au wazaifu — ndio watu wo wote.

Kupiga mbio kupokea zawadi (9:24-27)

Paulo alijua kabisa ya kwamba mtu anaweza kupoteza zawabu yake kwa sababu ya kukosa kujitawala mwenyewe. Kama washindaji katika michezo wanavyopiga mbio kupata zawadi, inatupasa sisi kufanya vivyo. Wanatumikisha miili yao sana kwa kupata taji itakayoharibika; ingetupasa sisi kufanya vivyo kupata taji isiyoharibika. Paulo hakupiga mbio ovyo, lakini alitiisha mwili wake ili asikataliwe ndani ya shindano. Hasemi hapa juu ya kupoteza wokovu wake, lakini juu ya kupoteza ruhusa yake kutumikia Mungu.

Maonyo katika Agano la Kale (10:1-13)

Kuna mifano mingi ndani ya historia ya Israeli kuonyesha hatari ya kuabudu sanamu na kutawaliwa na anasa. Waisraeli wote walibarikiwa sawasawa wakati walipovuka Bahari Nyekundu na kusafiri jangwani, lakini zaidi yao hawakupendeza Mungu na walikufa jangwani. Kwa nini? Kwa sababu walitamani vitu vibaya, waliabudu sanamu na kufanya uzini, walijaribu Bwana, na kunungunika. Maneno haya yote yaliyotokea ni mifano kwetu — maonyo kwa wale ambaeo wanajitegemea wenyewe, na faraja kwa wale wanaojaribiwa.

Meza ya Bwana (10:14-22)

Sasa Paulo ni tayari kutoa mafundisho juu ya nyama zilizotolewa kwa sanamu. Waamini wanakatazwa kushiriki ndani ya karamu hekaluni mwa sanamu. Kula kwa meza ya Bwana ni mfano wa ushirika naye, kama vile Waisraeli waliokula sadaka walivyokuwa na

1 WAKORINTO

ushirika na mazabahu. Wale wanaokula kwa karamu za sanamu wanashiriki na mashetani kwani sadaka zinazotolewa kwa sanamu zinatolewa kwa mashetani. Haiwezekani hata kidogo kuwa na ushirika na Bwana pamoja na kuwa na ushirika na mashetani. Wale wanaojaribu kufanya hivi wanaamsha wivu wa Bwana na kumsukuma kuonyesha uwezo wake katika hukumu.

Njia tatu kujaribu matendo (10:23-24)

Kwa maneno mengine ambayo Mkristo anataka kufanya inapasa mwamini kujiuliza maneno matatu: Ni halali? Lina faida? Lina-jenga — maana ni kwa baraka ya watu wengine?

Utukufu na hali njema ya watu wengine (10:25 – 11:1)

Waamini walikuwa na ruhusa kula vyakula vilivyotolewa katika soko. Waliweza kuvikula nyumbani mwao isipokuwa ni kikwazo kwa zamiri ya ndugu zaifu aliye pamoja nao. Kuangusha wengine kwa njia ya kula vyakula wanavyojuia vilitolewa kwa sadaka kunaleta hukumu juu ya mwenye kula na kusukuma watu wengine kusema maneno mabaya. Lazima kila kitu tunachofanya kiwe kwa utukufu wa Mungu na faida ya watu wengine.

9. MAFUNDISHO KWA WANAWAKE JUU YA KUFUNIKA VICHWA VYAO (11:2-16)

Maana ya kufunika kichwa (11:2-10)

Nyuma ya kusifu waamini, Paulo anaanza mafundisho juu ya kufunika vichwa. Alianza kwa njia ya kuonyesha kwamba kuna vipimo vitatu vya ukubwa ndani ya ulimwengu — Kristo ni juu ya mwanamume, mwanamume ni juu ya mwanamke, na Mungu ni kichwa cha Kristo. Inapasa mwanamume kuomba au kutoa unabii *bila kufunika kichwa chake*, lakini inapasa mwanamke *kufunika kichwa chake* kusudi asipatize kichwa chake haya. Ni haya kwa mwanamke kukosa kufunika kichwa chake. Utaratibu huu ulisimamishwa zamani wakati Mungu alipoumba dunia na vitu vyote, na alifanya mwanamke toka mwanamume na kwa mwanamume. Neno hili linahakikisha ya kwamba agizo hili juu ya kufunika kichwa si kwa wakati wa Paulo tu. Inapasa mwanamke kufunika kichwa chake kama mfano wa utii wake — na kwa sababu ya malaika wanaotazama.

Wanaume na wanawake wanategemeana (11:11-12)

Hata kama mwanamume na mwanamke wakitegemeana, mahali yao mbalimbali ilisimamishwa na Mungu.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Mfano wa sheria ya asili (11:13-16)

Sheria ya asili inafundisha ya kwamba inapasa kwa vichwa vya wanawake kufunika. Ni haya kwa mwanamume kuwa na nyele ndefu, lakini nyele ndefu ni utukufu kwa mwanamke. Ilikuwa desturi ya mitume na makanisa kwa wanawake kufunika vichwa vyao.

10. UTARATIBU KWA KARAMU YA UKUMBUSHO WA BWANA (11:17-34)

Desturi mbaya kwa Karamu ya Bwana (11:17-22)

Sasa Paulo alisema juu ya desturi mbaya zilizokwisha kuingia makusanyiko yao kwa karamu ya ukumbusho wa Bwana. Waamini walikuwa na matengo katikati yao wakati walipokusanyika pamoja. Vilevile namna walivyokutana haikustahili kusanyiko la ukumbusho. Kila mtu alileta na kula chakula chake mwenyewe, wengine walibaki na njaa kwa sababu ya ukosefu, na wengine walilewa!

Maana ya Karamu ya Ukumbusho ya Bwana (11:23-26)

Kusudi la karamu hii ni kukumbuka Bwana katika mauti yake kufika siku atakapokuja. Mkate unatukumbusha mwili wake ambao aliu-toa, na kikombe kinatukumbusha damu yake iliyomwangika.

Kujihukumu mwenyewe mbele ya kula (11:27-34)

Mtu akishiriki katika karamu hii kwa njia isiyofaa anakokota hukumu ya Mungu juu yake mwenyewe kwa sababu anajipatia kosa juu ya mwili na damu ya Bwana. Kwa sababu hii sharti waamini wajihukumu wenyewe na kukiri zambi zote wanazojua mbele ya kula na kunywa. Vilevile wangojeane; haifai wakutane kama kwa karamu ya watu wa dunia.

11. ZAWADI ZA ROHO NA KAZI YAO KANISANI (Sura 12-14)

Sura 12-14 ni juu ya zawadi za roho, zaidi unabii, na kusema kwa lugha.

Kujaribu zawadi kama ni kweli za Roho Mtakatifu (12:1-3)

Vizuri waamini wafahamu ya kwamba kuna *roho wabaya* duniani vilevile ambao wanajifunua kwa njia ya kazi zao, mbali na kazi za *Roho Mtakatifu*. Mtu akikiri ya kwamba Kristo ni Bwana, neno hili linahakikisha ya kwamba mtu huyu anatawaliwa kweli na Roho Mtakatifu.

Zawadi mbalimbali za roho (12:4-6)

Kuna zawadi za roho mbalimbali lakini zinafungwa pamoja kwa

1 WAKORINTO

njia tatu. Zawadi hizi zote zinaongozwa na Roho mmoja. Zote zinatukimikia Bwana mmoja, na zote zinatoka kwa Mungu mmoja.

Zawadi hizi zinaonekana kwa njia mbalimbali (12:7-11)

Kazi ya zawadi hizi zote ni kusaidia kanisa zima (sh.7). Tutaje nyingine, ndizo neno la akili, neno la kujua, imani, zawadi ya kuponyesha, matendo ya uwezo, unabii, lugha, kueleza maana ya lugha. (Zawadi nyingine zinatajwa ndani ya mashairi mengine). Roho Mtakatifu anagawa zawadi hizi kwa kila mtu namna inavyompendeza.

Mfano wa mwili wa mtu (12:12-20)

Paulo anasema juu ya mwili wa mtu kama mfano wa umoja wa Roho akitumika kwa njia mbalimbali. Kuna viungo vingi ndani ya mwili mmoja. Vivyo hivyo waamini wengi (wote) walibatizwa katika mwili wa Kristo na wanashiriki katika Roho mmoja. Mwili unahitaji viungo vingi. Ni neno la kuchekesha kwa kiungo kimoja kuwa na wivu juu ya kiungo kingine kwa sababu kila kiungo kinapewa kazi fulani na Mungu. Hakuna mwili kama kiungo ni kimoja tu; viungo vikiwa vingi kuna mwili unaofanya kazi.

Viungo vyote vinahitajiwa na kuhitajiana (12:21-26)

Hakuna kiungo kinachotumika peke yake bila kusaidiwa na vingine, na vyote vinahitajiwa. Ndiyo mara nyingi viungo vivilivo zaifu vinahitajiwa kupita, na viungo vinavyoonekana kupunguka he-shima vinahitaji kutunzwa. Mungu alifanya mwili kwa njia ya kuchanganya viungo ambavyo tunaviheshimu na vingine visivyoonekana vizuri ili vyote viweze kusaidiana na kuchungana. Neno linalogusa kiungo kimoja linavigusa vyote.

Zawadi mbalibali kwa waamini mbalimbali (12:27-31)

Wakristo ni mwili wa Kristo nao ni viungo ndani ya mwili huu. Mungu ameweka zawadi mbalimbali ndani ya Kanisa na alizigawa katikati ya Wakristo. Inapasa kanisa la kila pahali kuwa na hamu kupata zawadi ambazo wanazihitaji. Tutasoma juu ya “njia nzuri zaidi” ndani ya sura 13.

Ubora wa mapendo (13:1-3)

Zawadi hizi ni neno kubwa, lakini neno lililo kubwa kupita ni namna gani watu wanazitumia. Wenye mapendo wanafikili zaidi watu wengine, si wao wenyewe. Hivi wenye mapendo wanatumia zawadi zao kusaidia watu wengine. Hii ndiyo “njia nzuri zaidi” iliyotajwa ndani ya 13:31b.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Tabia ya mapendo (13:4-7)

Wale wanaotumia zawadi zao na roho ya mapendo wanaonyesha tabia ya Kristo ndani ya mwenendo wao, kwa njia ya maneno yanayotajwa hapa, kama wema, unyenyekevu, adabu, na roho ya ku-stahimili.

Mapendo yanadumu (13:8-11)

Zawadi za kusema kwa lugha, unabii na maarifa zitakwisha, au kwa wakati dunia hii isipoharibiwa bado au kwa wakati wa milele, lakini mapendo ni kwa milele. Labda Paulo alifikili ya kwamba wengine walitumia zawadi zao kwa kujionyesha kuwa wakubwa na kukokota macho ya watu juu yao wenyewe, kama mtoto anavyoweza kufanya ndani ya michezo yake. Mtu anayekomea katika roho ameacha mambo ya kitoto.

Ukubwa wa mapendo (13:12-13)

Kwa wakati wa sasa tunaona kwa kioo tu, kwa namna ya mfano, lakini kwa wakati wa kuja tutaona wazi kabisa. Saa yenyeewe itaonekana ya kwamba mapendo ndilo neno kubwa zaidi ndani ya maisha ya Mkristo.

Unabii ni zawadi bora kupita zawadi ya lugha (14:1-5)

Unabii ni mzuri kupita kusema kwa lugha bila kutafsiri maana kwa sababu unaleta faida kwa wenyе kusikia. Watu wanafahamu unabii kwa sababu ni wa lugha yao wenyewe. Hakuna mtu anayepata faida kwa njia ya kusikia mtu mwengine akisema kwa lugha nyingine kama mtu wa kutafsiri akikosa.

Mafundisho waziwazi yanajenga kanisa (14:6-12)

Paulo anasema tena ya kwamba ni lazima kwa watu kuweza kufahamu maana ya maneno wanayosikia. Makanisa yale wanaotamani zawadi za roho, waweke roho zaidi juu ya zile zitakazojenga waamini.

Ni sharti kwa watu kuweza kufahamu maneno wanayosikia (14:13-20)

Lugha zina faida tu kama maana yao zikielezwa. Kama mtu aki-omba, kuimba au kutoa sifa na lugha, ni lazima afanye hivi ili watu wengine waweze kufahamu. Kama sivyo, hakuna mtu anayeweza kusema "Amina" wala kujengwa katika imani yake (mash. 13-17). Kusema na maneno watu wanayoweza kufahamu ni faida kupita kusema kwa lugha watu wasiyoweza kufahamu (mash. 18-19). Haifai tutume zawadi ya lugha au zawadi yo yote nyingine namna mtoto anavyotumika na vitu vyake vya kucheza. Sharti tuwe kama watoto tu katika kutenda uovu (sh.20).

1 WAKORINTO

Lugha na unabii kama alama (14:21-22)

Namna Mungu alivyotumia lugha nyingine (lugha ya Waasuria) kama alama kwa Israeli wakati wa Isaya, vivyo hivyo zawadi ya lugha ni alama kwa wasioamini waliokataa Neno la Mungu na kufunga mioyo yao wasipokee kweli, lakini unabii ni alama kwa waamini.

Unabii unafahamisha watu makosa yao (14:23-25)

Kusikia watu wakisema kwa lugha hakufahamishi wasioamini ubaya wa zambi, lakini unabii unawafahamisha makosa yao kwa sababu wanafahamu maneno wanayosikia.

Maagizo juu ya zawadi ya kusema kwa lugha (14:26-28)

Mtume alitoa maagizo kwa wale wanaosema kwa lugha. Lazima maneno wanayosema yaweze kujenga watu. Haifai kupita watu watatu kusema ndani ya kusanyiko moja, na lazima waseme mmoja nyuma ya mwingine — si wote pamoja, na sharti mtu anayeweza kutafsiri awe pale.

Maagizo juu ya zawadi ya unabii (14:29-33)

Paulo alitoa maagizo juu ya zawadi ya unabii vilevile. Manabii wawili au watatu tu waseme kwa kusanyiko moja. Ni kazi ya wasikiaji wapime mafundisho yao. Mtu mwingine akifunuliwa neno, sharti mtu aliyetabiri mbele anyamaze. Sharti manabii waseme mmoja nyuma ya mwingine, kufundisha na kufariji. Sharti manabii wajue maneno wanayosema.

Wanawake wanyamaze kanisani (14:34-36)

Inapasa wanawake kukaa kimya kanisani; hawana ruhusa hata kuuliza maneno. Watu wakikataa agizo hili waseme kama Neno la Mungu lilitoka kwao au kama lilifika kwao tu.

Maagizo ya Paulo ni maagizo ya Mungu (14:37-38)

Paulo alisema ya kwamba manabii wote na wenye kufahamu nia ya Mungu wakubali ya kwamba maagizo haya juu ya zawadi za lugha na unabii, na juu ya wanawake kanisani ni maagizo ya Bwana.

Sharti zawadi zitumiwe kwa utaratibu (14:39-40)

Kwa mwisho wa sehemu hii ya barua yake mtume anasema tena ya kwamba zawadi ya unabii ina faida kupita lugha, ya kwamba haifai kukataza watu kusema kwa lugha, na ya kwamba maneno yote yafanywe kwa uzuri na utaratibu.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

12. JIBU LA PAULO KWA WALE WALIOSEMA KWAMBA HAKUNA UFUFUKO (Sura 15)

Sura 15 ni jibu la Paulo kwa watu wengine katika kanisa kwa Korinto waliokana kwamba kuna ufufuko.

Ufufuko na Habari Njema (15:1-11)

Ufufuko wa Kristo ni sehemu kubwa ya Habari Njema. Kuna unabii juu yake ndani ya Agano la Kale na washuhuda wengi katika Agano Jipyä walihakikisha ya kwamba Kristo alifufuka kweli. Paulo alikuwa mtume kwa sababu ya ufufuko na mitume yote walishuhudu ya kwamba Kristo alifufuka.

Bila ufufuko imani ya Wakristo ni bule (15:12-19)

Kama miili ya watu isipoweza kufufufuliwa, halafu Kristo hakufufufuliwa, mahubiri ya mitume ni bule nao ni wadanganyi, hakuna njia kwa watu kuokolewa toka zambi, waamini waliokufa wamepotea, na waamini walio hai wanakosa tumaini nao ni masikini kuliko watu wote.

Ufufuko wa Kristo unahakikisha kwamba sisi tutafufuka (15:20-22)

Lakini Kristo alifufufuliwa kweli na ufufuko wake unahakikisha ya kwamba waamini wote wa kweli watafufufuliwa.

Kawaida ya ufufuko (15:23-28)

Kuna makundi matatu ndani ya ufufuko: kwanza Kristo, malimbu-ko (ndiyе aliyefufufuliwa kwanza); kisha watu wa Kristo wakati atakapotokea; na mwishoni wasioamini wote, wakati adui zote waliopokwisha kuwekwa chini ya miguu ya Kristo na kazi yake ya upatanisho imekwisha.

Kwa sababu ya ufufuko, mateso kwa Kristo yana faida (15:29-32)

Paulo anaonyesha upumbavu wa kuteswa na kufa kwa Kristo kama usipokuwa na ufufuko. Isingalikuwa na faida kwa waamini kubatizwa kwa ajili ya wale waliokufa kwa Kristo. Hata mateso ya Paulo yasingalikuwa na faida. Ingalkuwa akili kupita kukaa vizuri na kujifurahisha na maneno ya dunia.

Ufufuko na mwenendo mwema (15:33-34)

Haifai kukubali mafundisho ya uwongo juu ya ufufuko kwa sababu mafundisho mabaya yanageuza mwenendo wetu. Kama watu wangaliishi kwa muda wa sasa tu na hakuna maisha nyuma ya mauti, namna ya mwenendo wao si neno kubwa.

Mifano ya mwili wa ufufuko (15:35-41)

Mwili unaofufufuliwa utafanana kwa njia nyingine na miili yetu ya

1 WAKORINTO

sasa, lakini utakuwa umetukuzwa, kama pando lililotoka ndani ya mbegu, na kama vile kuna tofauti katika nyama ya watu na nyama ya viumbe vingine, miili ya dunia na miili ya mbinguni, na kungaa kwa utukufu wa juu, mwezi, na nyota.

Mwili wa ufufuko na utukufu (15:42-49)

Mwili wa mwamini utakuwa mwili usioharibika, mwili wa utukufu na uwezo — mwili wa roho kama mwili wa Kristo. Mwili huu utafaa kwa maisha mbinguni, ndilo neno lisilo kweli juu ya mwili wetu wa sasa.

Ufufuko na kubadilishwa (15:50-57)

Wakati Kristo atakaporudi wale waliokufa wakiamini Kristo wata-fufuliwa na waamini watakaokuwa kwanza hai watabadilishwa.

Ahadi ya zawabu (15:58)

Ingepasa waamini kusimama imara wakijua watapokea zawabu wakati Kristo atakapokuja.

13. MAFUNDISHO JUU YA KUTOA SADAKA (16:1-4)

Juu ya sadaka kwa watakatifu wenye hitaji katika Yerusalem, mtume aliagiza watoe na utaratibu, kwa kadiri ya mapato yao na kwa saa inayofaa. Paulo alikusudi kutuma mali hii kwa mikono ya watu waliochaguliwa na kanisa, na labda yeye mwenyewe atakwenda pamoja nao.

14. MASHAURI YA PAULO (16:5-9)

Paulo aliandika barua hii toka Efeso. Alikusudi kuvuka maji kwenda Makedonia, kisha kupita kwa kusini kwenda Korinto na kushinda pale kufika Pentekote.

15. MAONYO YA MWISHO NA SALAMU (16:10-24)

Maonyo juu ya Timoteo na Apolo (16:10-12)

Kama Timoteo akifika kwao, iliwapasa kumpokea vizuri (mash. 10-11). Paulo alikuwa amesukuma Apolo kufikia Korinto, lakini Apolo hakutaka kwenda saa ile lakini atakwenda nyuma (sh.12).

Maonyo ya mwisho kabisa (16:13-18)

Nyuma ya maonyo juu ya maneno mbalimbali mtume alisihi watakatifu kutii Stefano na watu wengine kama yeye amba walijitoa wenyewe kwa kazi ya Bwana (mash.13-16). Roho ya Paulo iliburu-

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

dishwa wakati ndugu watatu toka kwao walipomfikia na kutimiliza kwake neno ambalo Wakorinto hawakuweza kufanya wao wenyewe (mash. 17-18).

Salamu na kuagana (16:19-24)

Nyuma ya kutuma salamu yake na salamu ya watakatifu katika Efeso, Paulo anamaliza barua hii na laana kwa mtu ye yote asiyependa Bwana Yesu, na baraka ya neema na mapendo kwa wale ambao wanampenda.

Barua ya pili ya Paulo kwa Wakorinto

MWANZO

Historia ya 2 Wakorinto

Paulo alitaka sana kusikia kama Wakorinto walipokea barua yake ya mbele namna gani, zaidi maneno aliyoandika juu ya mtu yule aliyeanguka kwa zambi. Hivi aliondokea Efeso, akakwenda Troa aktaraji kukutana na Tito pale. Wakati Tito asipokuwa pale, Paulo alivuka bahari kwenda Makedonia. Pale Tito alimfikia na habari nzuri na habari mbaya. Habari nzuri ndizo ya kwamba watakatifu walikuwa wameazibu mwenye kutenda zambi na neno hili lilifanya kazi rohoni mwake, akarudi karibu na Bwana. Habari mbaya zilikuwa hizi: Wakristo hawakutuma mali kwa watakatifu wenye mahitaji katika Yerusalem, kama walivyokusudi kufanya. Vilevile walimu wa uwongo walitumika sana katika Korinto wakijaribu kuharibu kazi ya Paulo na kuwaambia watu ya kwamba hakuwa na amri kama mtumishi wa Kristo.

Mutasari (jumla) na tarehe ya 2 Wakorinto

Haya ndio maneno yaliyosukuma Paulo kuandika barua hii. Aliandika karibu na A.D. 57, toka Makedonia. Ina sehemu tatu: (1) Paulo alieleza namna ya utumishi wake (sura 1–7); (2) alionya waamini kutimiza ahadi yao kutuma zawadi kusaidia watakatifu wenye hitaji katika Yerusalem (sura 8–9); na (3) alieleza ya kwamba yeze ni kweli mtume (sura 10–13).

UMBO LA 2 WAKORINTO

1. Habari za kuponyeshwa kwa Paulo toka mauti (1:1-11)
2. Masumbuko ya Paulo juu ya kuazibu wenye kutenda zambi katika kanisa kwa Korinto (1:12 – 2:13)
3. Paulo alieleza utumishi wake kwa maneno ya Agano Jipy (2:14 – 6:10)
4. Paulo alisihi Wakorinto wampende tena (6:11 – 7:16)
5. Paulo alisihi watakatifu kutimiza ahadi yao kutuma zawadi kusaidia watakatifu wenye hitaji katika Yerusalem (sura 8–9)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

6. Paulo anasimamia amri yake (10:1 – 12:18)
7. Maonyo ya mwisho na baraka (12:19 – 13:14)

1. HABARI ZA KUPONYESHWA KWA PAULO TOKA MAUTI (1:1-11)

Salamu (1:1-2)

Paulo alianza barua hii na kijiita mtume (watu wengine walikuwa wakibisha neno hili!), alitaja Timoteo pamoja naye, na kutuma neema na salama kwa watakatifu katika Korinto na Akaya nzima.

Kupitisha faraja ya Mungu kwa watu wengine (1:3-7)

Paulo alikuwa na asante kwa faraja toka Mungu kwa wakati wa taabu na mateso yake, akijua ya kwamba neno hili litamwezesha kufariji watu wengine ndani ya taabu yao. Kusudi la mateso ya *Paulo* kwa ajili ya Kristo na namna alivyofarijiwa lilikuwa kupatisha roho ya watu wengine nguvu katikati ya mateso *yao* kwa Kristo.

Paulo aliolokolewa toka mauti (1:8-11)

Mtume alikumbuka wakati alipopata matata kubwa sana kwa Asia. Alifikili ya kwamba atakufa siku ile. Aliweza kutegemea Mungu tu anayefufua wafu. Mungu alimwokoa wakati ule, na sasa wale ambao walimwombea waliweza kushukuru Mungu aliyejibu maombi yao.

2. MASUMBUKO YA PAULO JUU YA KUAZIBU WENYE KUTENDA ZAMBI KATIKA KANISA KWA KORINTO (1:12 – 2:13)

Paulo alikuwa na moyo safi (1:12-14)

Wengine walikuwa wamemshitaki kusema ye ye ni mwenye hila kwani hakufikia Korinto namna alivyokusudi kufanya mbele. Neno hili halikuwa kweli. Alikuwa amewaambia kweli kila mara. Alitaraji ya kwamba walifahamu ya kuwa waliweza kujisifu juu yake namna ye ye atakavyojisifu juu yao kwa wakati wa kuja kwa Bwana.

Paulo alikuwa mtu wa kutumainika (1:15-20)

Mbele lilikuwa shauri la Paulo kufikia Korinto kwanza, kisha kwenda Makedonia, halafu kufika kwa Korinto mara ya pili mbele ya kwenda Yudea. Lakini aligeuza shauri hili na alisafiri toka Efeso kwenda Troa. Wakati asipokuta Tito pale, alikwendea Makedonia mara moja, bila kufikia Korinto kwanza. Neno hili lilionyesha ya kwamba ye ye ni mtu wa kugeukageuka? Maana ya “Ndiyo” yake

2 WAKORINTO

ilikuwa “Hapana”? Sivyo, hakuwa mwenye kugeukageuka kama vile Mwana wa Mungu ambaye alihubiri habari zake hakuwa mwenye kugeukageuka! Paulo alikuwa amewafundisha juu ya yule kwa njia yake ahadi zote za Mungu zinatimizwa.

Kwa nini Paulo hakufikia Korinto (1:21-24)

Hakufika kwa sababu ya kuwahurumia. Hakuwa mwenye kutawala imani yao, lakini msaidizi tu. Walisimama mbele ya Mungu.

Kwa nini Paulo aliandika barua kwa Wakorinto (2:1-4)

Alifanya hivi kuepuka kuhuzunishwa na watu wale ambao walipaswa kumfurahisha. Alitaraji barua hii itatosha kufanya maneno aliyokusudi kufanya kama angalifika yeeye mwenyewe.

Kusamehe mtenda mabaya (2:5-11)

Kanisa katika Korinto walikuwa wameazibu mtu yule aliyetenda mabaya, labda kwa njia ya kumwondosha kanisa. Kwa sababu hii alikuwa ametubu kweli kweli na kurudi karibu na Bwana. Sasa iliwasapa kumsamehe na kumpokea tena katika ushirika wa kanisa, kusudi Shetani asipate kumzamisha ndani ya huzuni kubwa zaidi.

Mlango wazi kwa Habari Njema (2:12-13)

Kama tulivyosema mbele, Paulo alikuwa ameondokea Efeso na kwenda Troa pahali alipokuta njia wazi kwa kuhubiri Habari Njema. Lakini alitaka sana kupata habari kwa njia ya Tito juu ya Wakorinto, hivi alivuka bahari kwenda Makedonia.

3. PAULO ALIELEZA UTUMISHI WAKE KWA MANENO YA AGANO JIPYA (2:14 – 6:10)

Habari Njema inashinda (2:14-16)

Watu wengine waliweza kufikili ya kwamba kwa mhubiri kuondoka pahali Mungu alipokuwa akibariki mahubiri ya Habari Njema na kwenda kutafuta habari juu ya kanisa lingine ni kama kushindwa kwa kazi ya Mungu. Sivyo; Paulo alionyesha Bwana kama mwenye kumfikisha kama mshindaji ngambo ya bahari kufika Makedonia. Pahali gani Bwana anapokwenda, kwa njia ya watumishi wake, analeta kushinda. Wao ni manukato ya Kristo mbele ya Mungu, si neno kama watu wakipokea mahubiri yao au kuyakataa.

Usafi wa Habari Njema iliyohubiriwa na Paulo (2:17)

Paulo anamaliza sehemu hii ya barua yake kwa njia ya kusema na nguvu ya kwamba hakuharibu Habari Njema, lakini zilikuwa habari

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

toka Mungu ambazo alizitangaza kwa moyo safi katika jina la Kristo.

Barua hai ya Paulo (3:1-3)

Walimu wa uwongo walikuwa wamefikia Korinto, wakikana ya kwamba Paulo ni mtumishi wa kweli wa Kristo. Labda walisema vizuri alete barua ya sifa kwa kujisimamia wakati alipofika. Alijibu watu hawa na kusema ya kwamba Wakristo katika Korinto walikuwa wao wenyewe barua yake ya sifa kwa sababu ni ye ye ambaye ali-wafikisha karibu na Bwana. Wao walikuwa barua safi toka Kristo, iliyoandikwa na Roho ya Mungu juu ya mbaao za mioyo ya watu.

Utukufu mkubwa zaidi wa Habari Njema (3:4-18)

Paulo alifahamu kwamba ye ye mwenyewe hakuwa na akili ku-mwezesha kuwa mtumishi wa agano jipy, lakini ya kwamba uwezo wake ulitoka kwa Mungu (mash. 4-6a). Halafu alisawanisha sheria na Habari Njema, labda kwa sababu walimu wa uwongo walisimamia sheria na walitaka waamini kutii sheria ya Musa. Andiko, maana yake sheria, inaua; roho, ndiyo Habari Njema, inaleta uzima. Agano la Kale ni utumishi wa mauti lakini utumishi wa Agano Jipy ni utumishi wa Roho. Sheria ilikuwa na utukufu; Habari Njema ilikuwa na utukufu mkubwa zaidi. Utukufu wa sheria ulikuwa kwa wakati tu; utukufu wa Habari Njema unakaa. Musa alificha uso wake na kitambaa, lakini uso wa Mkristo hautiwi kitambaa. Utukufu ulikuwa juu ya uso wa Musa peke yake; sasa utukufu huu ni kwa kila mwamini (6b-18).

Nuru ya utukufu ya Habari Njema (4:1-6)

Paulo aliendelea kusema juu ya utumishi wake na ya kwamba ni lazima kwake kuonyesha Habari Njema waziwazi. Alikataa kabisa kwa kweli kufichwa. Itafichwa tu kwa sababu Shetani anapofusha mafikili ya wasioamini! Habari yenyewe ni wazi kabisa, ndizo ya kwamba Kristo Yesu ni Bwana. Mungu ametufunulia sisi kweli hii tuweze kuipitisha kwa watu wengine.

Hazina katika vyombo vya udongo (4:7-18)

Mtume alishangaa wakati alipowaza juu ya uzaifu wa mtu na utukufu uliokuwa mbele yake na ya kwamba amewekewa Habari Njema. Mwili ni kama chombo cha udongo kinachosongwa wakati wote lakini kisichoshindwa. Ni kama mwamini akiuawa siku zote na kwa njia hii uzima wa Yesu unafunuliwa kwa watu wengine. Kwa sababu mwamini ana tumaini ya kwamba atafufuliwa, anaona ya kwamba taabu ya utumishi wake kwa Kristo inaleta baraka kwa watu wengine na tunda lake ni mashukuru kwa Mungu. Hali ya sasa ya mwamini ni namna nyingine na hali yake wakati wa kuja. Hata mtu

2 WAKORINTO

wa inje akioza, mtu wa ndani anafanywa mpya kila siku; mateso mepesi ya wakati wa sasa ni kwa wakati tu; utukufu wa milele unaodzi di mwangi sana ni wa milele; vitu vinavyoonekana ni vya saa kidogo tu, lakini vitu visivyoonekana ni vya milele.

Hakika ya ufulufuko (5:1-10)

Paulo anakaa kuwaza juu ya mambo mazuri sana yaliyo mbele ya mwamini. Anaeleza ya kwamba Mkristo anaweza kukaa katika hali namna tatu. Ya kwanza ni “nyumba ya dunia ya hema,” maana mwili wake hapa duniani. Ya pili ni “uchi,” wakati roho na nafsi zinapokwenda kukaa pamoja na Kristo na mwili unapowekwa kaburini. Hali ya tatu ni “kuvikwa,” wakati tutakapopokea mwili wetu wa utukufu. Hali ya kwanza ni nzuri, ya pili ni nzuri kupita, ya tatu ni nzuri zaidi. Hatutaki sana mavazi ya sasa kuondolewa lakini tunaugua tukitamani kuvikwa na mwili wetu uliokombolewa. Mungu ametuweka kwa maneno haya na kutupa sisi Roho Mtakatifu kama arabuni. Tumaini letu ya kwamba tutatukuzwa pamoja na Kristo linatusukuma kumpendeza ndani ya maisha yetu ya sasa. Tunataka aweze kusema nasi, “Umfanya mema” wakati tutakaposimama mbele ya kiti chake cha hukumu.

Utumishi unaolazimishwa na mapendo ya Kristo (5:11-15)

Woga wa Bwana ulisukuma Paulo ndani ya utumishi wake wa upatanisho. Maisha yake yalikuwa wazi mbele ya Mungu, na mbele ya watu vilevile. Hakutaka kujisifu mwenyewe, lakini hata hivi alitaka Wakorinto kujua maneno juu yake ambayo yatawasaidia kujibu washitaki wake. Walisema alikuwa na wazimu; alijibu kusema kama akiwa na wazimu au sivyo, ilikuwa yote kwa utukufu wa Mungu na baraka ya watu. Alilazimishwa na mapendo ya Mungu hata hakuweza kuishi tena kwa faida yake mwenyewe; kama Yesu alimkufia, lazima aishi sasa kwa Yesu.

Maneno yote yamekuwa mapya (5:16-17)

Kuanza sasa mtume hakuweza kuhukumu watu kwa namna ya mwili tena au kufikili juu ya Kristo kama mtu au Masiya wa dunia tu. Ndani ya Kristo kuna kiumbe kipyaa, maana yake maneno ya zamani yamepita na maneno yote yamekuwa mapya.

Utumishi wa upatanisho (5:18-19)

Maneno haya yote yanatoka kwa Mungu. Ametupatanisha na anatutuma katikati ya watu na utumishi wa upatanisho, kujulisha watu wa dunia ya kwamba ndani ya Kristo Mungu alikuwa akipatanisha ulimwengu na yeze mwenyewe.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Habari kubwa za upatanisho (5:20 – 6:2)

Halafu tunasoma juu ya habari za upatanisho. Ni maneno Paulo aliyohubiri kwa wenyewe zambi. Alijiita mjumbe wa Kristo, akisihi watu kupatanishwa na Mungu, na akiwaambia namna Mungu alivyofanya Kristo kuwa zambi kwa ajili yao ili wao waweze kuwa haki ya Mungu katika yeche (mash. 20-21). Wale wanaoamini Bwana Yesu wana-hesabiwa haki mbele ya Mungu na kwa sababu hii wanastahili kwenda mbinguni.

Mashairi 1 na 2 ya sura 6 yanaendelea na habari mtume alizohubiri kwa wasioamini. Haifai wasioamini kukataa neema ya Mungu lakini kuipokea mara moja kwa sababu siku ya wokovu ni sasa.

Alama za utumishi (6:3-10)

Sasa Paulo anapasha juu ya namna yeche alivyo tunda katika utumishi huu. Hakutaka maneno ya maisha yake kuwa kikwazo na kupunguza sifa ya kazi ya Bwana. Ulikuwa utumishi wa taabu nydingi na ndani yake ilipasa mtumishi wa Mungu kuonyesha Kristo kwa njia ya matendo yake na matunda ya roho (Wagalatia 5:22-23). Ndani ya utumishi huu alisikia maneno mbalimbali rohoni, furaha na huzuni, mahitaji, aibu, njaa, utajiri katika umasikini ...

4. PAULO ALISIHI WAKORINTO WAMPENDE TENA (6:11 – 7:16)

Paulo anasihi mioyo ya Wakorinto iwe wazi kwake (6:11-13)

Mtume alikuwa amesema wazi kwa Wakorinto na mawazo ya roho yake yalifunuliwa kwao. Sasa anawasihi waweze kumwonyesha mapendo vilevile.

Kujitenga na zambi (6:14-18)

Iliwapasa kujitenga na wasioamini (labda Paulo aliwaza zaidi juu ya walimu waliokuwa wakipunguza faida ya utumishi wake). Wale wanaofuata njia mbalimbali ndani ya mwenendo wao hawawezi kuwa na ushirika mzuri. Mungu anaahidi kuwa karibu zaidi na wale ambao wanajitenga na uovu ndani ya maneno yote ya maisha yao.

Kusafisha mwili na roho (7:1)

Ahadi hizi tamu zingepasa kutusukuma kujisafisha toka uchafu wa mwili na wa roho.

Roho nzuri ya Paulo kwa Wakorinto (7:2-4)

Paulo alihuzunishwa sana kwa sababu Wakorinto hawakumpenda

2 WAKORINTO

kama mbele. Hakuwatendea mabaya. Aliwapenda, aliwatumainia na kujisifu kwa ajili yao.

Furaha kubwa ya Paulo (7:5-7)

Ndani ya 2:13 tulisoma juu ya kuondoka kwake kwa Troa na kuvuka bahari kwenda Makedonia. Sasa aliendelea na habari hizi. Hata katika Makedonia alisumbuka sana rohoni kufika wakati Tito alipokuja na habari njema toka Korinto. Halafu roho yake ilijaa tele na furaha.

Si huzuni tu lakini toba ya kweli (7:8-12)

Mtume alikuwa na shaka rohoni juu ya barua ambayo aliwaandikia mbele. Sasa alifahamu ya kwamba kweli barua hii iliwahuzunisha kwa wakati, lakini ilizaa toba ya kweli mbele ya Mungu ndani yao, si huzuni namna ya dunia tu inayoleta mauti. Walikuwa wametengeneza maneno yao kwa njia ya kuazibu mtu yule aliyefanya zambi.

Furaha na mapendo ya Tito (7:13-16)

Paulo alifarijiwa na namna watakatifu katika Korinto walivyo-kwisha kutengeneza maneno yao, na alifurahi vilevile kwa sababu ya furaha kubwa ya Tito juu yao. Tito aliweza kuona ya kwamba Paulo hakujisifu bule juu ya Wakorinto, na mapendo yake kwa yaliongeze-ka kwa sababu ya namna walivyompokea.

5. PAULO ALISIHI WATAKATIFU KUTIMIZA AHADI YAO KUTUMA ZAWADI KUSAIDIA WATAKATIFU WENYE HITAJI KATIKA YERUSALEMA (Sura 8-9)

Ukarimu wa Wakristo wa Makedonia (8:1-5)

Sasa ilipasa mtume kusihi Wakorinto kutimiza ahadi yao ya mbele kutuma mali kwa watakatifu wenye hitaji katika Yerusalem. Vizuri waige makanisa ya Makedonia walioota na ukarimu, wakijinyima wenyeewe kwa sababu walitaka kufanya hivi. Wakristo wa Makedonia walijitoa wenyeewe kwa Mungu kwanza, kisha walitoa mali yao kwa Paulo aweze kuangalia maneno ya kufikisha zawadi yao kwa Yerusalem.

Kristo mfano wa kutimia wa kutoa bila kujifikili mwenyeewe (8:6-9)

Paulo alisukuma Tito kuangalia ili Wakorinto wakusanye mali hii, na alionya watakatifu kuongeza zawadi ya ukarimu kwa zawadi zote nyingine ambazo walikuwa nazo (mash. 6-7). Hakuwaagiza kama she-ria, lakini kwa kujaribu mapendo yao akiwakumbusha mfano wa Yesu ambaye alijifanya masikini kwa kutajirisha wengine (mash. 8-9).

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Watimize ahadi yao ya kutoa (8:10-15)

Mwaka mmoja ulipita tangu Wakorinto walisema walikubali kutoa zawadi hii. Vizuri wafanye neno hili sasa na mali yo yote ambayo walikuwa nayo, si na mali ambayo walitumaini kuwa nayo! Ingekuwa vizuri kwa wenye hitaji kusaidiwa bila kuwa mzigo kwa kanisa lo lote lingine.

Mkusanyo wa mali kwa watakatifu katika Yudea (8:16-24)

Tito alikuwa na hamu na bidii kwa kazi iliyokuwa mbele yake kwa Korinto. Paulo alikuwa akituma ndugu wawili (hatuoni majina yao hapa) waweze kuangalia maneno ya zawadi hii pamoja. Hakuna njia kwa laumu kama watu kupita mmoja wakifanya kazi hii pamoja. Nyuma ya kusifu wajumbe hawa sana, Paulo walionya watakatifu kuwapokea na mapendo na kuwapa zawadi yao kusudi waweze kutimiza ujumbe wao vizuri.

Kujisifu kwa Paulo juu ya Wakorinto (9:1-5)

Paulo alikuwa amejisifu mbele ya watu wa Makedonia juu ya hamu ya Wakorinto kusaidia na zawadi yao. Sasa vizuri watimize neno hili na kukusanya mali na ukarimu zitumwe kwa Yerusalem. Kama sivyo, atapata haya kama labda watu wengine wa Makedonia wakifikia Korinto pamoja naye na kuona ya kwamba hawajafanya neno juu ya kutayarisha zawadi yao.

Sababu na kawaida ya kutoa kwa Wakristo (9:6-11)

Tutavuna kwa kipimo tunachopanda. Sharti tutoe na furaha, si kwa sababu ya lazima. Wale wanaotaka kweli kuwa wenye kutoa kwa ukarimu hawatakosa kamwe kuwa na mali kwa kuweza kufanya hivi, na watavuna zawabu za kudumu milele. Na kwa njia ya kutoa, Wakristo hawa wanatajirishwa kwa kila kila njia waweze kutoa zaidi.

Matunda ya kutoa kwa Wakristo (9:12-14)

Mali tunazotoa haisaidii tu mahitaji ya wenye kuipokea, lakini inawasukuma kushukuru Mungu; watu watasifu Bwana kwa sababu tulimtii na kutoa kwa ukarimu. Na watatuombea sisi vilevile na mapendo mengi.

Zawadi kubwa zaidi (9:15)

Mungu ni mwenye kutoa kupita wote, na Mwana wake ni Zawadi kubwa zaidi. Kweli inatupasa kumshukuru sana!

2 WAKORINTO

6. PAULO ANASIMAMIA AMRI YAKE (10:1 – 12:18)

Ndani ya sura ine za mwisho za barua hii Paulo anasimamia zaidi amri yake.

Vita ya roho ya mtume Paulo (10:1-6)

Wachunguzi wa Paulo walisema yeye ni zaifu na mpole wakati alipokuwa pamoja nao, lakini mwenye uhodari wakati alipokuwa mbali. Walisema vilevile ya kwamba alifanya kazi yake namna ya watu wa mwili. Basi atakuwa na uhodari wakati atakapokutana na washitaki hawa. Alihakikisha kwa Wakorinto ya kwamba alitumika na *silaha za roho* akibomoa na kuhukumu mawazo na mambo yote ya watu yasiyopatana na mafundisho ya Kristo. Atatendea walimu wa uwongo hivi mara moja wakati atakapojuwa Wakorinto wanafungana pamoja naye.

Paulo alikuwa na amri kweli (10:7-11)

Labda wengine wa Wakorinto walisema ya kwamba wao tu walikuwa wafuata wa kweli wa Kristo. Paulo alikuwa mtu wa Kristo vilevile na zaidi ya ile alipokea amri toka Kristo kujenga watakatifu, bila kuwaogopesha. Wachunguzi wake walisema yeye ni mwenye kuandika kwa uwezo, lakini hakujua kusema vizuri. Wataona kitu wakati atakapokutana nao.

Mpaka wa amri ya Paulo (10:12-18)

Wachongezi wa Paulo walimshitaki kusema watu wengine walikuwa wazuri kupita yeye. Aliwajibu kusema kwamba si akili njema kujifananisha na watu wengine na kwa njia hii kujifanya kuonekana vizuri. Alikusudi kujisifu tu ndani ya kazi ambayo Mungu alimpaa, na Wakorinto walikuwa sehemu ya kazi ile. Alitaka zaidi kuhubiri pahali watu wasiposikia Habari Njema mbele, si kuingia kwa nguvu ndani ya kazi ya mtu mwingine. Neno alilotaka zaidi lilikuwa sifa ya Bwana, si sifa yake mwenyewe.

“Mitume waliokuwa wakubwa sana” (11:1-6)

Mtume Paulo alitaja maneno matatu kwa sababu yao ilipasa watakatifu kumvumilia hatu kama ilionekana kwamba ilikuwa upumbavu kwaye kujisifu. Neno la kwanza ndilo hili: Alisumbuka sana juu ya roho na maisha yao kwa Bwana. La pili ni hili: Aliogopa watadanganywa wasifuate Kristo tena na roho moja. La tatu ni hili: Wakorinto walionekana kuwa tayari kusikiliza walimu wa uwongo, basi kwa nini watakataa kusikiliza mahubiri ya “mpumbavu mwenye kujisifu”? Mitume wale “wakubwa sana” hawakumpita hata kidogo. Hata kama hakujifunza kusema vizuri, alikuwa na elimu ya kutosha.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Mahubiri bila kupokea zawadi kwa mahitaji ya mwili (11:7-12)

Wakati Paulo alipokuwa kwa Korinto alikataa kupokea tokao kwa zawadi ya mali kumsaidia ndani ya mahitaji yake lakini Wakristo wa makanisa ya Makedonia walimpa zawadi kwa kumsaidia. Labda Wakorinto walifikili ilikuwa zambi kwaye kufanya hivi. Lakini Paulo alijisifu kwa sababu aliweza kuhubiri kwa bila kusaidiwa nao kwa njia ya mali, si kwa sababu hakuwapenda lakini ili aweze kunyamazisha wale walioshindana naye.

Mitume ya Shetani (11:13-15)

Wale mitume “wakubwa sana” walikuwa mitume ya uwongo, wenye kutenda kazi kwa hila, wakijionyesha kuwa mitume ya Kristo na ya haki.

Paulo hakupenda kujisifu (11:16-21)

Hata kama Paulo alijisifu, hakuwa mpumbavu. Lakini hata akiwa mpumbavu ingaliwapasa kumpokea hata hivi. Bwana Yesu hakujsifu, lakini Wakorinto waliruhusu watu wengine kufanya hivi, basi kwa nini hawataruhusu Paulo? Walivumilia watu wengine ambao waliwatendea mabaya, lakini Paulo alikuwa “zaifu” sana na hakuwatendea hivi!

Mateso ya Paulo kwa ajili ya Kristo (11:22-33)

Mtume Paulo aliweza kujisifu juu ya maneno mengi — wazazi wake, utumishi wake, mateso yake yaliyopita yale ya watu wote kwa ajili ya Kristo, masumbuko yake kila siku kwa makanisa, na namna alivyoponyeshwa tokao Damasiki iliyokuwa haya kubwa kwake.

Ono la Paulo la Paradiso (12:1-6)

Mwishoni aliweza kujisifu juu ya maono na mafunuo ya Bwana. Alisema juu ya “mtu katika Kristo” (na kuficha kwamba “mtu” huyu alikuwa yeye mwenyewe) aliyechukuliwa juu hata Paradiso na kusikia maneno yasiyoweza kusemwa. Alikubali kujitaja mwenyewe kwa kujisifu juu ya uzaifu wake, lakini wakati alipopasha habari za maono na mafunuo ya Bwana, alisema maneno haya yalitokea mtu ambaye “alimjua” (ndiye yeye mwenyewe, mash. 1-5). Hakutaka kujisifu juu ya neno hili (hata kama angalikuwa na ruhusa kufanya hivi) ili watu wasimheshimu kupita kipimo (sh.6).

Mwiba katika mwili wa Paulo (12:7-10)

Kwa kuzuiza Paulo asipate kiburi kupita kipimo, Mungu aliruhusu Shetani kumtesa na ugonjwa au uzaifu wa mwili. Mtume alikuwa ameomba Mungu mara tatu kuuondosha, lakini kwa pahali pa ku-

2 WAKORINTO

uondosha Bwana aliahidi kumpa neema kuuvumilia. Halafu Paulo alinyenyekeea uzaifu huu na kujisifu ndani yake, akijua ya kwamba kwa njia hii uwezo wa Mungu unatimizwa ndani ya uzaifu wa mtu.

Alama za utume wa Paulo (12:11-13)

Kwa nini Paulo alihitaji kujisifu? Ingalipasa Wakorinto wenyewe kumsifu. Hakupungukiwa “mitume wale wakubwa” kwa njia yo yote; alikuwa ameonyesha alama zote za mtume katikati yao. Kulikuwa na tofauti moja tu — hakuwa mzigo kwao kwa njia ya mali — basi wamsamehe kosa hili!

Tabia ya mapendo ya Paulo (12:14-18)

Wakati atakapofika kwa Korinto, hatakuja kupata faida kwao lakini kuwapatia faida, kama yeye na wajumbe wake walivyofanya mbele.

7. MAONYO YA MWISHO NA BARAKA (12:19 – 13:14)

Kusudi la barua ya Paulo (12:19-21)

Alikusudi barua hii kuwatayarisha waweze kufurahi saa atakapofika kwao, si kupata huzuni.

Atakuja na amri ya mtume (13:1-6)

Wakati atakapokuja atatafuta maneno yao yote, na kuhukumu watenda mabaya na ukali. Kama walitaka ushuhuda ya kwamba alikuwa kweli mtume, waijangalie wenyewe. Alikuwa Paulo ambaye aliwaleta kwa Bwana. Hata kama Kristo alisulibishwa katika uzaifu, alikuwa amefanya kazi ya uwezo ndani ya maisha yao. Vivyo hivyo kazi ya mtume ilikuwa katika uzaifu na uwezo vilevile.

Paulo alipenda upole kupita ukali (13:7-10)

Paulo alitaka waweze kutenda vizuri hata aweze kuwajenga wakati atakapofika kwao, si kuwahamakia.

Salamu na baraka (13:11-14)

Ndani ya salamu yake ya mwisho aliwasihii kutengeneza maneno yao, kupokea maonyo yao, kuwa na nia moja na kukaa na salama. Kisha aliongeza maombi yake, kama aliviyofanya ndani ya kila barua, neema ya Bwana Yesu, mapendo ya Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ziweze kuwa pamoja nao.

Barua ya Paulo kwa Wagalatia

MWANZO

Kusudi na shauri la Wagalatia

Kwa safari yake ya kwanza na ya pili ya kuhubiri Paulo alianza makanisa kwa Galatia, wilaya ya Asia. Nyuma ya wakati walimu wa uwongo walifika makanisa haya toka Yerusalem, wakifundisha ya kwamba watu wakitaka kupata wokovu na utakaso, sharti washike sheria vilevile pamoja na kuwa na imani. Mafundisho yao yalikuwa machanganyiko ya dini ya kikristo na kiyahudi, ya neema na sheria. Vilevile hawakukubali Paulo kama mtume wa kweli.

Paulo aliandika barua hii kuonyesha ubaya wa mafundisho haya. Aliandika kama na kasirani kidogo. Alisimamia mafundisho na utumishi wake na kueleza tena kweli kubwa ya Habari Njema iliyo kwa neema kwa njia ya kuamini Kristo tu, si kwa njia ya kushika sheria. Alieleza kusudi la sheria, kisha alionyesha kwamba ni upumbavu kwa Wakristo kutaka kuwa chini ya sheria. Ingewapasa kuepuka hatari ya kufungwa na maagizo ya sheria, na kuishi katika uhuru wa kweli na utawa wa Wakristo.

Tarehe ya Barua kwa Wagalatia

Labda barua hii iliandikwa kwa A.D 49 tu, mbele ya kusanyiko katika Yerusalem (Matendo 15). Kama ni kweli hivi, barua hii iliandikwa hata mbele ya 1 Watesalonika. Walimu wengine wanafikili iliandikwa katikati ya A.D. 52-58.

UMBO LA WAGALATIA

1. Paulo aliandika na kusudi gani (1:1-10)
2. Paulo anasimamia utumishi wake (1:11 – 2:10)
3. Paulo anahamakia Petro (2:11-21)
4. Kweli kubwa ya Habari Njema (3:1-18)
5. Kusudi la Sheria (3:19-29)
6. Watoto na wana (4:1-16)

WAGALATIA

7. Utumwa au uhuru (4:17-31)
8. Hatari ya kufungwa na sheria (5:1-15)
9. Uwezo kwa kuishi maisha ya utawa (5:16-26)
10. Maonyo kwa mwenendo (6:1-10)
11. Mwisho (6:11-18)

1. PAULO ALIANDIKA NA KUSUDI GANI (1:1-10)

Salamu (1:1-5)

Mara moja kwa mwanzo wa barua hii Paulo anasema na nguvu ya kwamba si watu ambao walimweka kuwa mtume lakini Yesu Kristo mwenyewe na Mungu Baba. Ndani ya mashairi ya kwanza ya barua hii alisema vilevile juu ya mauti ya Kristo kwa ajili ya watu na ufu-fuko wake kwa kuwakumbusha na nguvu msingi wa wokovu wao.

Habari Njema moja tu (1:6-10)

Mtume Paulo alishangaa kwa sababu Wagalatia walikuwa wame-pokea mbio habari njema isiyo kweli, akawakumbusha ya kwamba laana ya Mungu inakaa juu ya mtu ye yote anayehubiri “habari njema” iliyo namna nyingine na Habari Njema ya neema ya Mungu.

2. PAULO ANASHUHUDIA UTUMISHI WAKE (1:11 – 2:10)

Wokovu wa Paulo na mwito wake (1:11-24)

Habari hizi zinaonyesha ya kwamba Habari Njema ambayo Paulo alihubiri ilifunuliwa kwake na Bwana, si na *mitume wengine* (hata kama wao vilevile walihubiri Habari Njema *ile ile*). Anapasha habari za bidii yake katika dini ya Wayuda, na namna alivyookolewa kwa njia kwenda Damasiki, kushinda kwake katika Arabia kwa wakati, na kurudi kwake kwa Damasiki. Alikwendea Yerusalem nyuma ya miaka mitatu tu, akashinda muda mfupi tu, ndiyo majuma mawili, na Petro. Toka pale alikwenda Suria na Kilikia. Makanisa katika Yudea hawakujuana naye.

Neema ilishinda kwa Yerusalem (2:1-10)

Nyuma ya miaka 14 mingine Paulo na Barnaba walikwenda pam-oja na mwamini mmoja wa Mataifa toka Antioquia kwenda Yerusalem, kuona nini itatokea. Wayuda waliofundisha sharti watu washike sheria kama wakitaka kuokolewa walikuwa wamefikia Antioquia wakisema na nguvu ya kwamba lazima waamini watahiriwe (ndiyo alama ya kushika sheria) kama wakitaka kuokolewa. Viongozi vyta Wakristo katika Yerusalem walipatana na Paulo na Barnaba ya kwamba tohara

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

haikuwa sehemu ya Habari Njema hata kidogo. Habari Njema ya kweli ilikuwa wokovu kwa neema kwa njia ya imani kwa Wayuda na Mataifa vivyo hivyo, na ni mbali kabisa na maneno ya kushika sheria.

3. PAULO ALIHAMAKIA PETRO (2:11-21)

Nyuma, wakati Petro alipofikia Antiokia, alikula pamoja na waamini wa Mataifa na kufurahi katika uhuru toka sheria wa Wakristo. Lakini wakati watu wengine walipofika toka Yakobo katika Yerusalem, Petro aliacha kushirikiana na Wakristo wa Mataifa, akiogopa ya kwamba habari za maneno ambayo aliyafanya zitafikia Yerusalem. Hata Barnaba alifungana na Petro ndani ya udanganyifu huu. Kwa macho ya Paulo matendo yao yalikuwa kama vita na Kweli ya Habari Njema; yalionyesha kwamba waamini wa Mataifa walikuwa wenyewe upunguvu mbele ya Mungu. Hivi Paulo alihamakia Petro mbele ya watu, akimshitaki kusema Petro alikiri kwamba tunahesabiwa haki kwa njia ya imani tu, lakini matendo yake yalionyesha ya kwamba matendo ya sheria yalihitajiwa vilevile. Petro alikuwa akijiveka tena chini ya sheria, lakini alikuwa ameokolewa toka pale kwa njia ya mauti ya Kristo. Paulo alionyesha ya kwamba watu wakiweza kuwa haki kwa njia ya kushika sheria, Kristo alipoteza uzima wake bule. Ni kama Petro alipokea makemeo haya na roho nzuri kwani nyuma aliiita Paulo “ndugu yetu mpenzi” (2 Petro 3:15).

4. KWELI KUBWA YA HABARI NJEMA (3:1-18)

Kuhesabiwa haki kwa imani (3:1-5)

Sasa Paulo anahakikisha kwa njia tatu ya kwamba tunapata wokovu kwa njia ya imani, si kwa njia ya kushika sheria. Njia ya kwanza ni neno lililopata Wagalatia wenyewe. Walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu wakati walipozaliwa tena kwa njia ya imani, si kwa njia ya matendo. Hawakuweza kuokolewa kwa njia ya matendo, wala kutakaswa kwa njia yao!

Agano la Kale na imani (3:6-14)

Njia ya pili ni ushuhuda wa Agano la Kale. Abrahamu alihesabiwa haki kwa njia ya imani, si kwa sheria (Mwa.15:6). Sheria haiokoi watu lakini inawalaani wote ambao hawaii saa zote na katika kila neno (Tor. 27:26). Habakuki 2:4 linafundisha ya kwamba kitu sheria inachotaka ni “matendo”, si “iman.” Paulo alitumia Torati 21:23 kuonyesha ya kwamba Kristo, kwa njia ya kufanywa laana kwa ajili yetu alitukomboa kwa laana ya torati.

Ahadi isiyogeuka kamwe (3:15-18)

Njia ya tatu ni ya kwamba haiwezekani kuvunja mapatano watu

WAGALATIA

wanayofanya. Basi katika Mwanzo 22:18 Mungu alitoa ahadi ya kwamba atabariki mataifa yote kwa njia ya Kristo. Ahadi hii haisimami juu ya neno lo lote inalopasa watu kufanya. Sheria iliyotolewa miaka 430 nyuma haikuweza kugeuza mapatano haya, kama vile haiwezekani kugeuza hati ya kuritisha mali wakati mwenye mali anapokwisha kuiwekea mkono na muhuri. Ahadi ya Mungu haikusimama juu ya sheria; ilikuwa agano la neema na inapasa watu kulipokea kwa imani.

5. KUSUDI LA SHERIA (3:19-29)

Kusudi la sheria lilikuwa kuonyesha ubaya wa zambi, ndio uasi. Ilikuwa mapatano katikati ya Mungu na watu wanaopaswa kufanya maneno fulani na ilihitaji Mpatanishi. Sheria ni kwa wakati tu, kama mwalimu kufika wakati Kristo atakapokuja. Sasa Kristo amekuja, akakufa kwa zambi na Wakristo wamemwamini. Hawaongozwi na mwalimu tena lakini wanatendewa kama wana wenye kupata nguvu ndani ya jamaa ya Mungu. Ndani ya Kristo hakuna tofauti tena *mbele ya Mungu* kwa maneno ya taifa, rangi, utajiri au umasikini, mume au mke.

6. WATOTO NA WANA (4:1-16)

Wariti wa Mungu (4:1-7)

Waisraeli chini ya sheria walikuwa kama watoto wasiokomea bado, wanaoagizwa na wale ambao wanawalinda kufanya maneno fulani kama watumwa. Chini ya neema, waamini wanatendewa kama wana wa kukomea wenye heshima na madaraka.

Utumwa wa sheria si kwa waamini (4:8-11)

Ni upumbavu kwa Wakristo kutaka kuwa chini ya sheria tena kwa sababu ni kawaida ya utumwa. Paulo alisumbuka kwa sababu ya wale waliokuwa tayari kuacha Kristo kwa desturi za dini za sheria.

Mapendo yanapotea kwa sababu ya kushikamana na sheria (4:12-16)

Wakati mtume Paulo alipofikia Wagalatia kwanza, walimpokea vizuri sana, kama malaika au hata kama Kristo mwenyewe. Lakini neno hili liligeuka kabisa wakati walimu wa uwongo wenye kushikamana na sheria walipofika.

7. UTUMWA AU UHURU (4:17-31)

Paulo anafazaika juu ya waamini (4:17-20)

Walimu hawa wa sheria walijaribu sana kutenga waamini na

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Paulo, na Paulo alifazaika juu ya namna gani waamini waliwaruhusu kufanya hivi.

Haiwezekani kuchanganya sheria na neema (4:21-31)

Paulo anarudi sasa kwa sehemu ya historia ya Abrahamu inayonyesha ya kwamba kushikamana na sheria ni utumwa na ya kwamba haiwezekani kuchanganya sheria na neema. Sara na Isaka ni mfano wa neema, lakini Hagari na Isimaeli ni mfano wa sheria. Kama vile Hagari alikuwa kijakazi, vivi hivi sheria inaleta utumwa. Kama Isimael alivyotesa Isaka, vivyo hivyo sheria inatesa neema. Kama Sara na Hagari wasivyoweza kuishi nyumbani mmoja, vivyo hivyo haiwezekani kuchanganya neema na sheria. Kama Isimaeli asivyoweza kuriti mali ya Abrahamu, vivyo hivyo wale walio chini ya sheria hawawezi kuriti wokovu mkubwa wa Mungu.

8. HATARI YA KUFUNGWA NA SHERIA (5:1-15)

Kushika sheria kunakomesha uhuru (5:1-5)

Basi Kristo alikuwa amefanya waamini huru, hivi sharti waamini wasimame imara ndani ya uhuru huu. Ni zambi kabisa kurudia sheria. Kushikamana na sheria ni kongwa ya utumwa. Ni kuhesabu Kristo kama si kitu. Kunatuagiza kushika sheria nzima, neno lisilowezekana. Ni kuacha kutegemea Kristo kama tumaini letu la pekee kupata haki.

Chachu mbaya ya kushikamana na sheria (5:6-12)

Kushikamana na sheria hakuna faida. Ni kuasi kweli. Si mafundisho yanayotoka kwa Mungu. Kunaongeza maovu mengine. Kunaleta hukumu ya Mungu juu ya walimu wake. Kunaondosha kwazo la msalaba wa Kristo. Paulo alitaka walimu hawa wawewe kutengwa na Wagalatia (au hata kujikata nafsi zao!)

Uhuru wa Wakristo (5:13-15)

Uhuru wa Wakristo ni kuweza kutumikia, si kufanya zambi; kupendana, si kushitakiana na kugombana.

9. UWEZO KWA KUISHI MAISHA YA UTAWA (5:16-26)

Roho Mtakatifu ndiye uwezo wa mwamini kuishi maisha ya utawa. Tukitembea katika Roho, hatutatimiza tamaa ya mwili. Kuna vita isiyokwisha kamwe katikati ya mwili na Roho, lakini Roho anatupatia uwezo kushinda. Wale wanaotenda kazi za mwili hawatariti ufalme. Wale waliosulibisha mwili, maana waamini wa kweli, wanaonyesha matunda ya Roho. Basi kwa sababu tumezaliwa kwa Roho, inatupasa kutembea kwa Roho, na kuepuka uvivu wa walimu wa sheria.

WAGALATIA

10. MAONYO KWA MWENENDO MEMA (6:1-10)

Inapasa waamini wanaokomea katika imani kurudisha ndugu zao walioanguka kwa zambi, kushiriki ndani ya masumbuko ya watu wengine, kusaidia walimu wa Neno la Mungu, na kutenda mema kwa watu wote, zaidi kwa Wakristo.

11. MWISHO (6:11-18)

Kujisifu kwa wenyе kushikamana na sheria (6:11-14)

Kusudi la walimu hawa wa uwongo lilikuwa kujulikana kwa njia ya kukokota watu wengi kuwafuata. Ni nyepesi kufanya hivi kwa njia ya kufikilisha watu wanawenza kupendeza Mungu na matendo yao — kama na tohara.

Kujisifu kwa Paulo (6:15-17)

Msingi wa kujisifu kwa Paulo haukuwa miili ya watu lakini msalaba wa Kristo (sh.15). Neno kubwa si tohara, au kutotohara, lakini kiumbe kipyä kinachoonekana kwa njia ya maisha matakatifu. Salama na rehema ni kwa wale wanaotembea kupatana na amri hii. Paulo alikuwa na alama juu ya mwili wake zilizoonyesha ya kwamba alikuwa mali ya Bwana Yesu, ndizo alama alizopokea kwa mikono ya wale ambao walimtesa.

Baraka ya neema (6:18)

Barua hii inakwisha na baraka ya neema — neno lililo kama alama ya Habari Njema ya Paulo. Ni baraka kubwa bila kulipa kitu kwa wale wanaostahili kupokea hukumu tu.

Barua ya Paulo kwa Waefeso

MWANZO

Habari kubwa za Barua kwa Waefeso

Hapa Paulo anaonyesha kweli nzuri mno ya Kanisa, kundi la watu ndani yake waamini Wayuda na waamini wa Mataifa ni moja ndani ya Kristo Yesu. Wao ni wariti pamoja na washiriki wa ahadi ya Mungu ndani ya Kristo.

Muhtasari ya Waefeso

Sehemu tatu za kwanza ni juu ya kikao cha mwamini ndani ya Kristo, na sura tatu za mwisho zinaonyesha ya kwamba inapasa mwe-nendo na matendo yake kupatana na kikao chake.

Watu waliopokea barua hii

Miigo mingine ya zamani inakosa maneno haya “katika Efeso” ndani ya 1:1. Kwa sababu hii watu wengi wanaamini ya kwamba barua hii haikuandikwa kwa Waefeso tu lakini kwa makanisa mengine vilevile.

Tarehe ya Waefeso

Hii ni moja ya barua ine Paulo alizoandika wakati alipokuwa gerezani katika Roma. Barua tatu nyingine ni kwa Wafilipi, Wa-kolosayi, na Filemono. Waefeso iliandikwa karibu A.D. 62.

UMBO LA WAEFESO

1. Salamu (1:1-2)
2. Sifa ya Paulo kwa Mungu kwa baraka za neema (1:3-14)
3. Mashukuru ya Paulo na maombi kwa watakatifu (1:15-23)
4. Uwezo wa Mungu unaonekana ndani ya wokovu wa Mataifa na Wayuda (2:1-10)
5. Waamini wa Wayuda na wa Mataifa ni moja ndani ya Kristo (2:11-22)
6. Habari zinazoingizwa katikati juu ya siri ya Kanisa (3:1-13)

WAEFESO

7. Ombi la Paulo kwa watakatifu (3:14-19)
8. Sifa ya Paulo kwa Mungu (3:20-21)
9. Maonyo kwa mwenendo mzuri (4:1 – 6:9)
10. Maonyo juu ya vita ya Wakristo (6:10-20)
11. Salamu toka Paulo (6:21-24)

1. SALAMU (1:1-2)

Paulo alianza barua hii kwa njia ya kujulisha wasomaji wake ya kwamba alikuwa Mungu ambaye alimfanya mtume. Aliandika kwa watakatifu, wale walio waaminifu ndani ya Kristo Yesu, kama waamini wote wa kweli. Kama mtu mmoja alivyosema, salamu yake ndiyo kutaka kwake *kwa wale wasiostahili wapewe neema, na wale wasiotulia wapate raha.*

2. SIFA YA PAULO KWA MUNGU KWA BARAKA ZA NEEMA (1:3-14)

Barua hii inaanza na sifa kwa Mungu kwa sababu alitajirisha watu wake na baraka zote za roho katika pahali pa mbingu ndani ya Kristo – si baraka za dunia lakini baraka za roho zinazopatikana ndani ya Kristo. Hizi ndizo nyingine za baraka hizi: tulichaguliwa katika milele ya zamani kuwa takatifu na bila laumu, kuwekwa kama wana na binti ndani ya jamaa ya Mungu, kukombolewa na kusamehewa kwa njia ya damu ya Kristo (mash. 3-7). Mungu alishiriki shauri lake nasi, shauri lililokuwa siri kufika wakati ule, ndilo kusudi lake kutimiliza na kukamilisha vitu vyote mbinguni na duniani ndani ya Kristo (mash. 8-10). Waamini Wayuda wanashiriki ndani ya shauri hili la Mungu kwa sababu wameunganishwa na Kristo (mash. 11-12). Waamini wa Mataifa vilevile wana sehemu ndani ya siri hii ya Mungu iliyofunuliwa kwa sababu waliskia Habari Njema, waliamini Bwana Yesu na waliwekewa muhuri wa Roho Mtakatifu, anayetoa hakika kwa waamini wote ya kwamba watapokea uriti mzima (mash. 13-14).

3. MASHUKURU YA PAULO NA MAOMBI KWA WATAKATIFU (1:15-23)

Kwanza Paulo alishukuru Mungu kwa imani na mapendo ya watakatifu, kisha aliomba waweze kuwa na ufahamu wa roho waweze kufurahia tumaini lao la utukufu wa milele, wingi wa uriti wa Kristo ndani ya watakatifu wake, na uwezo Mungu anaotumia kutimiza makusudi yake. Kwa uwezo ule alifufua Yesu toka wafu, akamtukuza kwa mkono wake wa kuume, akampa amri juu ya vitu na mambo yote, na kumweka kama Kichwa juu ya Kanisa.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

4. UWEZO WA MUNGU UNAONEKANA NDANI YA WOKOVU WA MATAIFA NA WAYUDA (2:1-10)

Ukumbusho wa kushinda kwa neema ya Mungu (2:1-7)

Uwezo ule uliofufua Bwana wetu toka wafu uliwapa Mataifa uzima. Mataifa wale walikuwa wafu mbele, waovu, chini ya uwezo wa Shetani na waasi. Uwezo ule uliwapa Wayuda uzima vilevile, wale waliofufuata mwili mbele, waovu na chini ya hukumu (mash. 1-3). Kwa neema yake kubwa Mungu alitupa sisi uzima, alitufufua na kutuketisha katika pahali pa mbinguni. – Kwa milele tutakuwa kama mfano wa neema ya Mungu mbele ya majeshi ya mbinguni (mash. 4-7).

Habari Njema (2:8-10)

Tunaokolewa kwa neema, kwa njia ya imani bila kutumika kazi njema. Wokovu ni zawadi, na hivi hatuna njia kujisifu. Ndiyo, hatuokolewi kwa njia ya kazi njema, lakini tunaokolewa kusudi tutende matendo mema. Matendo mema ndiyo matunda ya wokovu wetu.

5. WAAMINI WA WAYUDA NA WA MATAIFA NI MOJA NDANI YA KRISTO (2:11-22)

Waamini wameletwa karibu kwa damu ya Kristo (2:11-13)

Moja la makusudi ya Mungu ni kwa waamini wa Wayuda na Mataifa kuwa moja ndani ya Kristo, na kwa maneno yote ambayo yaliwatenga mbele kuondoshwa kabisa. Mbele Mataifa walizarauliwa. Walikuwa bila Kristo, wageni, bila tumaini wala Mungu (mash. 11-12). Lakini ndani ya Kristo Yesu wameletwa karibu kwa njia ya damu yake (sh.13).

Kristo, salama yetu (2:14-18)

Kwa njia ya Kristo tofauti na vizuizo vilivyoletwa na sheria kati-kati ya Wayuda na watu wa Mataifa vimeondoshwa. Sasa wamegeuka mtu mpya mmoja ndani ya Kristo. Uadui wa zamani umekombolewa na salama. Kristo *NI* salama yetu, *amefanya* salama na alikuja na *kuhubiri* salama. Kwa njia yake waamini wa Wayuda na Mataifa wanaweza kukaribia Mungu pamoja kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Kao kwa Mungu (2:19-22)

Waamini wa Mataifa si wageni tena, lakini wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa jamaa katika nyumba ya Mungu.

WAEFESO

6. HABARI ZILIZOINGIZWA KATIKATI JUU YA SIRI YA KANISA (3:1-13)

Siri inafunuliwa (3:1-7)

Mungu alikuwa amempa mtume Paulo ufunuo mkubwa juu ya siri ya Kanisa. Watu hawakujua kweli hii mbele, lakini sasa ilifunuliwa kwa mitume na manabii ya Agano Jipy. Ni ya kwamba waamini wa Mataifa ni wariti pamoja, wenyehi pamoja katika mwili wa Kristo, na washiriki pamoja wa baraka zote zilizoahidiwa ndani ya Habari Njema. Kwa macho ya Paulo ilikuwa neema kubwa kwa Mungu kumpa kazi hizi mbili.

Kusudi la siri hii (3:8-13)

Kazi kubwa ya Paulo ilikuwa kuhubiri kweli ya utukufu ya Kanisa (mash. 8-9). Moja la makusudi ya Mungu kwa wakati wa sasa kwa maneno ya siri hii ni kufunua hekima yake ya namna namna kwa majeshi ya malaika mbinguni (mash. 10-11). Kusudi lingine ni ili waamini wote waweze kufika mbele ya Mungu na uhodari na imani kwa wakati wo wote kwa njia ya maombi (sh.12). Paulo alikuwa amepewa kazi kubwa iliyozaa matunda ya kushangaza, hivi Paulo hakutaka watakatifu kuhuzunishwa wakati walipowaza juu yake gerezani (sh.13).

7. OMBI LA PAULO KWA WATAKATIFU (3:14-19)

Halafu mtume Paulo aliombea watakatifu tena. Aliomba Mungu Baba waweze kuwa na nguvu kwa njia ya Roho, waweze kufurahi wakikumbuka ya kwamba Kristo alikaa ndani yao; waweze kusimamishwa katika mapendo; waweze kufahamu kadiri ya siri ile; waweze kufahamu uzuri wa mapendo ya Kristo, mapendo makubwa sana tusiyoweza kujua yote; na waweze kutimizwa kwa utimilifu wote wa Mungu (sh.16). Paulo hakuogopa kuomba maneno makubwa karibu na Mungu!

8. SIFA YA PAULO KWA MUNGU (3:20-21)

Anamaliza ombi lake na wimbo wa sifa kwa Mungu kwa uwezo wake kufanya kuliko mambo yote tunayoweza kuomba au kufikili, na akimtolea utukufu kwa milele katika Kanisa na katika Kristo, Kichwa cha Kanisa.

9. MAONYO KWA MWENENDO MZURI (4:1 – 6:9)

Ndani ya sura 1–3 tumepata mafundisho juu ya hali yetu katika Kristo. Kuanza sasa kuna maonyo tuwe na mwenendo unaostahili mwito wetu.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Umoja ndani ya ushirika wa Wakristo (4:1-6)

Kwanza kuna maonyo Wakristo wakae na umoja. Inapasa watakatifu kutembea kustahili mwito wetu tuliosoma juu yake ndani ya sura 1-3. Njia moja kufanya hivi ni kuwa na mapatano mzuri na Wakristo wenzetu tukikumbuka ya kwamba waamini wote wamefungwa pamoja na maneno saba yanayotajwa ndani ya mashairi 4-6. Sharti wachunge umoja wa Roho na unyenyeketu na upole.

Kanisa linajengwa kwa njia ya zawadi za roho (4:7-16)

Paulo anaeleza sasa utaratibu uliotengenezwa na Mungu ili viungo ndani ya mwili wa Kristo waweze kufanya kazi yao vizuri. Kila Mkristo amepewa zawadi fulani na alipewa vile uwezo kuitumia kwa Mungu. Lakini nyuma ya ufufuko wake Kristo alitoa zawadi fulani nyingine kusaidia Kanisa kupata nguvu na kuongezeka. Zawadi hizi ndizo mitume, manabii, wahubiri wa Habari Njema, wachungaji na walimu. Kazi ya zaidi ya zawadi hizi ni kujenga watakatifu katika utumishi wao kwa Mungu, na kwa njia hii kupatisha Mwili nguvu uweze kukamilishwa na kufananishwa na Kristo kupita na kupita. Watakatifu wasiotumia zawadi zao hawakomei lakini ni watu wa kusitasita wanaodanganywa mbio. Lakini kama viungo vya Mwili wakishika kweli katika mapendo, watakuwa wenye kukomea ndani ya maneno yote.

Ni lazima kuvaa mtu mpya (4:17-32)

Sharti waamini waache desturi zao za zamani wakati maisha yao yalipokosa shabaa, na walipoishi kama vipofu katika uzalimu na haya, watu wasioweza kutawala tamaa yao (mash. 17-19). Kristo alitufundisha kuachana na desturi zetu za zamani na kufanywa wapya katika nia zetu, ili mtu mpya aweze kuonekana ndani ya maisha ya haki na utakatifu (mash. 20-24). Sharti waamini waonyeshe ya kwamba maisha yao yamegeuka kwa njia ya kusema haki kwa pahali pa wongo, kukomboa gazabu iliyo zambi na kasirani ya haki, wizi na ukarimu, masemo machafu na yale yanayoweza kujenga, roho ya kukasirika mbio na roho ya huruma (mash. 25-32).

Mwenendo katika mapendo na nuru (5:1-14)

Inapasa waamini kuwa wenye kuiga Mungu, wakipendana namna Kristo alivyotupenda sisi – akijitoa mwenywewe kwa ajili yetu (mash. 1,2). Sharti waepukane na namna zote za zambi ya mwili na masemo yenye maana mbaya wakikumbuka ya kwamba watu wenye tabia mbaya watariti gazabu ya Mungu, si ufalme wake (mash. 3-6). Haifai watu wa Mungu kuwa na upatano nao. Ndiyo, mbele watakatifu walikuwa katika giza la roho, lakini sasa wao ni nuru, na inawapasa

WAEFESO

kutembea kama watoto wa nuru na kuonyesha mema, haki na kweli ndani ya maisha yao (mash. 7-10). Sharti wahamakie matendo ya haya ya giza. Maisha yao yafunue matendo ya giza ya wengine na kwa njia hii kuleta wale wanaolala katika mauti ya roho kwa nuru ya Kristo (mash. 11-14).

Mwenendo katika hekima (5:15-21)

Haifai waamini kuishi kama wapumbavu lakini kama wenyewe heki-ma wakitumia saa zao vizuri. Haifai wafuate mapenzi yao wenyewe kwa ujinga, lakini watambue mapenzi ya Mungu na kuyafanya. Haifai walewe kwa mvinyo lakini wajazwe na Roho wakati wote. Halafu masemo yao yatakuwa maneno ya kujenga, wataabudu Mungu na wimbo na kumshukuru siku zote pamoja na roho ya utii.

Utii wa mke kwa mume wake (5:22-24)

Utii unaonekana kwa njia tatu ndani ya nyumba za Wakristo. Kwanza, inapasa wake kutii waume wao kwani mume ni kichwa cha mke namna Kristo ni Kichwa cha Kanisa. Inapasa wake kutii waume wao namna Kanisa linavyotii Kristo.

Mapendo ya mume kwa mke wake (5:25-33)

Vivyo hivyo inapasa waume kupenda wake wao kama Kristo alivyopenda Kanisa. Mhubiri mmoja alisema ya kwamba alijua waume waliopenda wake wao, lakini hakujua hata mtu mmoja ambaye alipenda mke wake kwa kipimo Kristo anavyopenda Kanisa lake.

Tunaona mapendo ya Kristo kwa namna alivyojitoa mwenyewe zamani, kazi yake ya kutakasa kwa wakati wa sasa, na namna atakavyojitolea mwenyewe Kanisa bila kipaku, katika uzuri na utukufu. Namna mume na mke wanavyokaa pamoja ni mfano mzuri sana wa Kristo na Kanisa. Namna Kristo na viungo vyake ni mwili mmoja, ni vivyo hivyo kwa mume na mke. Kwa njia ya kupenda mke wake mume anajipenda mwenyewe. Kwa njia ya kuheshimu mume wake, mke anatii kichwa chake.

Utii wa watoto kwa wazazi (6:1-3)

Watoto wanaagizwa kutii wazazi wao. Kwa nini? Kwa sababu ni haki; ni agizo la Maandiko Matakatifu; ni kwa baraka yao wenyewe, na kutawasaidia kuishi maisha marefu.

Mafundisho ya baba kwa watoto (6:4)

Haifai baba kuchokoza watoto wao bule. Wanaagizwa kuwalea na saburi na mapendo na kuwafundisha kupenda na kutii Bwana.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Utii wa watumishi kwa bwana wa kazi (6:5-8)

Inapasa watumishi Wakristo wawe wenyewe kutii bwana zao na heshima na uaminifu. Sharti wafanye kazi yao kama kwa Kristo mwenyewe. Inafaa waifanye na bidii na furaha, wakikumbuka kwamba ni kazi ya Bwana isiyoweza kukosa zawabu ya Mungu. Maagizo haya ni kwa wakati wa sasa vilevile.

Wema wa bwana wa kazi kwa watumishi (6:9)

Halafu lazima bwana wa kazi watendee watumishi wao wema bila kuwaogofya. Wakumbuke ya kwamba wao ni watumishi vilevile na ya kuwa Bwana wao hana upendeleo.

10. MAONYO JUU YA VITA YA WAKRISTO (6:10-20)

Silaha zote za Mungu (6:10-17)

Wakristo ni askari za Kristo na wanahitaji uwezo na silaha toka Mungu ili waweze kusimama na nguvu na kushindana na Shetani (mash. 10-13). Silaha hii ndiyo maisha bila laumu ya Mkristo, mkaba wa haki na uaminifu kwa kweli ya Mungu; silaha ya mwenendo wa haki, viatu vya utayari wa kuhubiri Habari Njema ya salama; ngabo ya imani ndani ya Bwana na Neno lake; kofia ya wokovu, ndio kujua ya kwamba watashinda, na upanga ulio Neno la Mungu (mash. 14-17).

Silaha ya siri: Maombi (6:18-20)

Askari anakutana na adui na roho ya maombi. Sharti aongozwe na Roho Mtakatifu ndani ya maombi haya, aangalie na kudumu katika maombi, na aombee watakatifu wote pamoja na kujiombea mwenyewe vilevile. Paulo alitaka wasomaji wa barua hii kumwombea aweze kuwa na uhodari na masemo wazi kutangaza Habari Njema. Alitaka sana waamini wenzake wamwombee. Alifahamu ya kwamba alihitaji sana ulinzi wa Bwana na uwezo toka kwake.

11. SALAMU YA PAULO (6:21-24)

Paulo alimaliza barua yake na salamu kwa wasomaji wake. Ali-kuwa ametuma Tikiko na habari toka kwake, na masemo kupatisha watakatifu nguvu rohoni. Sasa aliwatachia salama, mapendo pamoja na imani, na, kama ndani ya barua zake zote, neema.

Barua ya Paulo kwa Wafilipi

MWANZO

Mwanzo wa kanisa kwa Filipi

Kanisa kwa Filipi ndilo kanisa la kwanza la Wakristo katika Europe. Lilianzwa wakati Paulo alipohubiri pale kwa wakati wa safari yake ya pili ya kuhubiri. Ludia, mwenye kuuza nguo za rangi nyekundu, alikuwa mwamini wa kwanza. Wakati Paulo alipokwisha kutoa pepo mchafu ndani ya kijakazi mmoja bwana zake walikasirika sana, wakaagiza Paulo na Sila wafungwe, wapigwe na kuwekwa gerezani. Usiku ule mlinzi wa gereza na jamaa yake waliokolewa na kuingizwa kanisani. Watawala wa mji walifahamu ya kwamba walikuwa wame-tendea wenyeji hawa wawili wa Roma vibaya, wakawasukuma kutoka mji. Nyuma ya wakati, saa wahubiri walipofikili kazi yao ilikwisha, walikwenda zao hata Tesalonika.

Barua kwa Wafilipi iliandikwa wakati gani

Paulo alifikia Filipi mara mbili kwa safari yake ya tatu ya kuhubiri (Matendo 20:6). Tunafikili aliandika barua hii karibu na A.D. 61 wakati alipokuwa gerezani kwa Roma mara ya kwanza (Matendo 28:30-31). Saa yenyeje alilindwa ndani ya nyumba na kufungwa na mnyororo pamoja na mlinzi Mroma.

Habari kubwa za barua hii

Wafilipi walikuwa wametuma Epafradito karibu na Paulo na zawi-di, hivi aliandika kuwashukuru kwa kusaidia kwao ndani ya kazi ya Bwana. Maneno makubwa mawili ndani ya barua hii ni furaha na kufurahi. Yanaonekana karibu mara 17. Haifai msingi wa furaha ya Mkristo kuwa maneno ya dunia ambayo anakaa katikati yao.

UMBO LA WAFILIPI

1. Salamu ya Paulo, sifa na maombi (1:1-11)
2. Kufungwa kwa Paulo; anasihi waamini kudumu (1:12-30)
3. Maonyo kwa umoja. Kristo ni mfano kwetu kwa njia ya unyenye-kevu na kujitoa mwenyewe (2:1-16)
4. Maonyo kwa umoja, kama ulivyoonekana ndani ya maisha ya Paulo, Timoteo na Epafradito (2:17-30)
5. Maonyo juu ya walimu wa uwongo (3:1-3)
6. Paulo aliacha uriti wake na kazi zake bora aweze kufuata Kristo, 3:4-16)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

7. Maonyo kwa mwenendo unaofaa kwa wenyiji wa mbingu. Paulo ndiye mfano wao (3:17-21)
8. Maonyo kwa umoja, kusaidiana, furaha, mawazo mema (4:1-9)
9. Asante ya Paulo kwa watakatifu kwa zawadi zao za mali (4:10-20)
10. Salamu ya Paulo (4:21-23)

1. SALAMU YA PAULO, SIFA NA MAOMBI (1:1-11)

Salamu ya Paulo kwa Wafilipi (1:1-2)

Ndani ya salamu ya Paulo tunaona ya kwamba mwanafunzi wake, ndiye Timoteo, alikuwa pamoja naye wakati alipoandika, na ya kwamba wao wawili walikuwa watumwa wa Kristo Yesu. (Waamini katika Filipi hawakuwa na shaka ya kwamba Paulo alikuwa mtume, hivi Paulo hakutaja neno hili hapa.) Tunaona vilevile watu gani ni ndani ya kanisa katika Agano Jipy, ndio watakatifu, waangalizi na watumishi. Ndani ya salama yake ya “Neema ... na salama” anafunganisha pamoja maneno kwa baraka ya Wayunani na Wayuda. Anasema ya kwamba baraka hizi zinatoka kwa Mungu Baba na Bwana Yesu pamoja, na kwa njia hii anaonyesha wazi ya kwamba Baba na Mwana ni mamoa.

Sifa ya Paulo kwa Wafilipi (1:3-8)

Ilikuwa desturi ya mtume Paulo kusifu Wakristo kama ikiwezekana. Hapa aliletä asante kwa Mungu kwa namna walivyosimama pamoja naye kwa njia ya maombi yao na zawadi zao. Mungu atatimiza kazi njema aliyoanza ndani ya maisha yao kwa njia ya kuwapatisha nguvu kufika wakati wa kurudi kwa Bwana. Paulo aliwapenda sana akijua ya kwamba yeze nao walishindana ndani ya neema ya Mungu pamoja, si neno kama yeze ni katika kifungo au akipigania na kusimamia Habari Njema. Aliwapenda sana na mapendo ya Kristo na alikuwa na hamu kubwa kuwa pamoja nao.

Maombi ya Paulo kwa Wafilipi (1:9-11)

Nyuma ya kuwasifu aliendelea na maombi: waweze kupenda na akili na kutambua yaliyo mema, waweze kuwa na moyo safi bila laumu, na matunda ya haki yaweze kuonekana ndani ya maisha yao.

2. KUFUNGWA KWA PAULO. ANASIHI WAAMINI KUDUMU (1:12-30)

Kuhubiri Kristo (1:12-18)

Alitaka wafahamu neno moja: maana ya kufungwa kwa Paulo si ya kwamba Habari Njema ilishindwa lakini ya kuwa ilishinda. Askari za

WAFILIPI

mfalme walikuwa wamesikia Habari Njema. Ndugu Wakristo walipata uhodari kupita kuhubiri Habari Njema. Ndiyo, labda wengine hawakufanya hivi na kusudi safi, lakini hata hivi Paulo alifurahi kwa sababu Habari Njema ilihubiriwa. Lilikuwa neno kubwa sana kwa watu kusikia habari za Kristo.

Kuishi au kufa kwa Kristo (1:19-26)

Paulo alifikili ya kwamba atafunguliwa toka gereza nyuma kidogo, lakini si neno kwake kama ataishi au kufa. Kama akibaki na uzima ataweza kukaa kutumikia watakatifu na kuzaa matunda katikati yao; kama akifa, atakwenda kukaa pamoja na Kristo, ndilo neno lililo zuri zaidi.

Kushindana na kuteswa kwa Kristo (1:27-30)

Hata neno gani likimpata yeze mwenyewe, alitaka sana waweze kutembea kama inavyostahili na kuvumilia mateso na uhodari. Aliweza kujua ya kwamba atakaa pamoja nao kwanza kwani alitembea karibu na Bwana, na Roho Mtakatifu aliweza kumjulisha neno hili.

3. MAONYO KWA UMOJA. KRISTO NI MFANO KWETU KWA NJIA YA UNYENYEKEVU NA KUJITOA MWENYEWE (2:1-16)

Umoja kwa njia ya unyenyeketu (2:1-4)

Wengine ndani ya kanisa katika Filipi hawakupatana vizuri (4:2), hivi mtume alisihi ndugu kuwa na roho moja na mapendo na kwa kila mtu kuhesabu wengine mzuri kuliko yeze mwenyewe.

Kristo alijinyenyekeza na alitukuzwa (2:5-11)

Ingepasa Wakristo kufikili kama Kristo. Hata akiwa Mungu, alikubali kuacha pahali pake pa heshima mbinguni, kusudi afikie dunia hii kama mtumwa na Mtu kabisa, kujinyenyekeza na kufa kwa watu, hata kusulibishwa kwa ajili yao. Kwa sababu alijifanya hivi kuwa hana utukufu, Mungu alimtukuza, akampa jina lililo juu ya kila jina na litakaloheshimiwa na viumbe vyote kwa wakati wa kuja.

Wenye kungaa katika dunia ya giza (2:12-16)

Paulo alikuwa ameonyesha neno lililosumbusha kanisa (ndilo magomvi katikati ya ndugu wawili), na namna gani kutengeneza neno hili (kuwa na nia ya Kristo). Sasa aliwaonya kutengeneza neno hili (wokovu), akijua ya kwamba Mungu atawapa hamu na kuwawezesha kufanya hivi (mash. 12-13). Hivi wanaweza kutimiza wokovu wao kwa njia ya kuepuka magomvi na manunguniko na kwa njia ya kungaa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kama nuru katika dunia ya giza. Kama wakishika hivi neno la uzima, Paulo atafurahi wakati atakaposimama mbele ya Kiti cha Hukumu cha Kristo (mash. 14-16).

4. MAONYO KWA UMOJA, KAMA ULIVYOONEKANA NDANI YA MAISHA YA PAULO, TIMOTEO NA EPAFRODITO (2:17-30)

Mfano wa Paulo (2:17-18)

Ndani ya baki la sura 2 Paulo anataja mifano mitatu ya watu waliokuwa na nia ya Kristo, ambao walijinyenyeyeza na kuhesabu wengine vizuri kupita wao wenyewe.

Paulo alifikili maisha ya Wafilipi ambao walikuwa tayari kujitoo wenyewe kwa Bwana yalikuwa na faida kupita maisha yake mwenyewe. Kazi yao ilikuwa sadaka kubwa sana kwa Bwana. Paulo alifurahi kuwa kama toleo la kinyweo tu, maana kuuawa kwa ajili yao.

Mfano wa Timoteo (2:19-24)

Timoteo aliweka roho sana juu ya Wafilipi, akaweka maneno ya Kristo mbele ya faida yake mwenyewe. Paulo alimtuma kwa Filipi kulinda watakatifu kwa maneno ya roho, na alitaraji kumfuata nyuma kidogo.

Mfano wa Epafroditu (2:25-30)

Epafroditu alipata ugonjwa wa nguvu kwa sababu ya safari yake ndefu toka Filipi kwenda Roma. Lakini hakusumbuka kwa sababu ya ugonjwa huu, lakini kwa sababu Wakristo wa Filipi walisikia habari zake. Hakutaka wajishitaki wenyewe juu ya ugonjwa wake. Basi wakati atakaporudi na barua hii, wampokee vizuri na kumheshimu kwa sababu pamoja na kuhatarisha maisha yake mwenyewe aliwa-wezesha kutuma zawadi kwa Paulo.

Neno kubwa ndani ya sura 2 ni “wengine” (mash. 3,4,20). Kristo, mwenye utukufu wa kungaa, ni kama jua, na wafuata wake watatu walikuwa kama miezi inayorudisha utukufu wa nuru.

5. MAONYO JUU YA WALIMU WA UWONGO (3:1-3)

Mkristo anaweza kufurahi hata wakati wa taabu na ugonjwa kwa sababu furaha yake ni ndani ya Bwana, si ndani ya maneno ya dunia.

Nyuma ya kusema na Wafilipi kufurahi, Paulo anaendelea kuwanya juu ya walimu wa uwongo ambao waliwasukuma kurudi kwa dini ya Wayuda. Aliwaita imbwa, watenda mabaya, wenyе kujikata wenyewe (kwani waliweka roho sana juu ya tohara). Lakini waamini

WAFILIPI

wa kweli ndio wale wanaoabudu kwa Roho na wanaojisifu ndani ya Kristo, na hawatumaini mwili wao wenyewe.

6. PAULO ALIACHA URITI WAKE NA KAZI ZAKE BORA AWEZE KUFUATA KRISTO (3:4-16)

Halafu Paulo alitaja maneno ambayo angaliweza kujisifu juu yao kwa njia ya mwili — wazazi wake, dini yake na haki yake kwa maneno ya sheria (mash. 4-6). Lakini alikuwa ameacha maneno haya, aliyasahau na kuyahesabu kama kitu bule, kama mavi, kusudi aweze kupata Kristo. Alitaka kufanywa mamaja na Kristo kwa maneno ya uwezo, mateso, mauti, na ufufuko, si neno kama bei yake ni kubwa sana. Aliwaza juu ya maisha kama mashindano na alikaza mwendo aweze kufikia mwisho wake aweze kujuua zawabu ya mwito na makusudi ya Kristo kwaye. Wakristo wanaokomea kwa imani wanafikili kama Paulo, na Mungu ni tayari kufunua maneno haya kwa wengine wanaotaka kuyajua. Kufika saa ile inapasa kila mtu kukaa kutembea kupatana na maneno anayokwisha kujifunza na kipimo cha kukomea anachokwisha kufikia (mash. 7-16).

7. MAONYO KWA MWENENDO UANAOFAA KWA WENYEJI WA MBINGU; PAULO NDIYE MFANO WAO (3:17-21)

Njia mbili zinalinganishwa (3:17-19)

Paulo alikuwa mfano mzuri ambao iliwapasa kuiga, si kama mfano wa walimu wa sheria. Wadanganyi hawa walichukia Msalaba wa Kristo na mambo yake yote. Walihubiri kwa kujipatia mali, walijivu-muu juu ya mwenendo wao wa haya, na waliweka roho juu ya maneno ya dunia hii.

Wenyeji wa mbingu (3:20-21)

Mwamini ni mwenyeji wa mbingu, hivi anaweka roho juu ya maneno ya mbingu. Kila dakika anangojea kutokea kwa Mwokozi na kupata mwili wa utukufu ambao atapata kwa uwezo wake.

8. MAONYO KWA UMOJA, KUSAIDIANA, FURAHA, MAOMBI NA MAWAZO MEMA (4:1-9)

Halafu mtume anaonya waamini wa Filipi juu ya mambo mbali-imbali: wasimame imara, ndugu wake Wakristo wawili wapatane; wafurahi siku zote katika Bwana, wavumuliane, wasikae kusumbuka lakini waishi maisha ya maombi na mashukuru na mawazo safi, na waweze kutii mfano na mafundisho ya Paulo.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

9. ASANTE YA PAULO KWA WATAKATIFU KWA ZAWADI ZAO ZA MALI (4:10-20)

Anaendelea na kushukuru Wakristo wa Filipi kwa zawadi waliyotuma kwa mikono ya Epafroditu. Walitaka kuituma mbele, lakini walikosa mtu aliyeweza kuipeleka. Paulo alikaa na furaha hata gerezani. Alikuwa amejuana na kuwa na vitu vingi au na ukosefu wa vitu. Alijua aliweza kubeba *mambo yo yote* yaliyo mapenzi ya Kristo. Pamoja na kusifu Wafilipi kwa zawadi yao ya sasa, mtume alikumbuka zawadi walizotuma mbele — mara mbili wakati alipokuwa katika Tesalonika na mara moja kwa Korinto. Alifurahi juu ya zawadi yao ya sasa, lakini zaidi alitaka ili wao wapewe **zawabu**. Alisifu zawadi hii na kuisawanisha na zabihu yenyе harufu tamu inayokubaliwa na kupendeza Mungu. Kwa sababu *wao* walikuwa wakili waaminifu, Paulo alijua Mungu atajaza mahitaji *yao* kwa kadiri ya utajiri wake. (Ahadi hii **si** kwa Wakristo *wasiotoa* kwa Bwana!)

10. SALAMU YA PAULO (4:21-23)

Paulo anamaliza barua hii na sifa kwa Mungu, salamu kwa watakatifu, na baraka yake, kama ilivyokuwa desturi yake.

Barua ya Paulo kwa Wakolosayi

MWANZO

Tarehe ya Wakolosayi

Walimu wengi wanafikili ya kwamba Paulo aliandika barua hii wakati alipokuwa gerezani kwa Roma mara ya kwanza, karibu na A.D. 60.

Mwanzo wa kanisa katika Kolosayi

Mji wa Kolosayi ulikuwa kwa upande wa mangaribi wa Asie Ndogo, ndiyo inchini inayoitwa Turkey kwa wakati wa sasa. Paulo hakufika pale yeye mwenyewe (2:1). Labda kanisa lilianzwa na Epafra (1:7).

Mafundisho ya Wakolosayi

Tukisoma barua hii, inaonekana wazi ya kwamba waamini walikuwa katika hatari ya kuangushwa na mafundisho ya uwongo kama kawaida ya desturi za kuabudu, kujikana mwenyewe, elimu, kushika sheria, na kuabudu viumbe vyenye kusimama kati ya Mungu na watu.

Ni kama Epafra na wengine waliulizana na Paulo kwa Roma juu ya mafundisho haya. Jibu la Paulo lilikuwa “Kristo” — Kristo aliye mkubwa kupita viumbe vyote na anayetosha kabisa.

Tikiko na Onesimo walipeleka barua hii kwa Kolosayi.

Wakolosayi na Waefeso

Barua hizi mbili zinafanana sana. Mashairi 54 ni karibu sawasawa. Lakini barua kwa Waefeso inafundisha zaidi juu ya Kanisa kama *mwili* wa Kristo, na barua kwa Wakolosayi inaonyesha Kristo kama *Kichwa* aliyetukuzwa cha Kanisa.

UMBO LA WAKOLOSAYI

1. Salamu ya Paulo, mashukuru na maombi kwa Wakolosayi (1:1-14)
2. Utukufu wa Kristo, Kichwa cha Kanisa (1:15-23)
3. Utumishi wa Paulo (1:24-29)
4. Kristo anatosha kushinda hatari ya elimu, sheria, mafundisho ya siri, na kujinyima mwenyewe (Sura 2)
5. Maisha mapya ya mwamini, kuondosha mtu wa zamani na kuваяa mtu mpya (3:1-17)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

6. Matendo yanayofaa kwa jamaa ya Wakristo (3:18 – 4:1)
7. Maisha ya maombi ya mwamini na ushuhuda wake kwa njia ya mwenendo na masemo yake (4:2-6)
8. Rafiki za Paulo, na salamu (4:7-18)

1. SALAMU YA PAULO, MASHUKURU NA MAONYO (1:1-14)

Nyuma ya kusalimu Wakristo wa Kolosai namna ilivyo desturi yake (mash. 1-2), Paulo alianza barua hii na sifa kwa Mungu kwa imani, mapendo na tumaini lao (mash. 3-8). Aliendelea na maombi, ili watakatifu wajazwe kujua mapenzi yote ya Mungu (sh.9); waweze kutembea kama inavyostahili na Bwana (sh.10); waweze kupatishwa nguvu kwa uwezo wote (sh.11); na kushukuru Mungu kwa maneno yote ambayo aliwatendea katika Kristo (mash. 12-14).

2. UTUKUFU WA KRISTO, KICHWA CHA KANISA (1:15-23)

Wakati Paulo aliposema juu ya Mwana mpendwa wa Mungu, neno hili lilimsukuma kusema juu ya utukufu wa Kristo, kwa namna alivyo na kwa maneno ya kazi yake. Yeye ni mfano wa Mungu; mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote (sh.15), aliyeumba vyote mbinguni na duni-ani na kuvitegemeza vyote, kwa ajili yake mwenyewe (mash. 16-17). Yeye ni Kichwa cha Kanisa (sh.18); mzaliwa wa kwanza toka wafu (sh.18); mwenye utimilifu wote (sh.19), atakayepatanisha vitu vyote kwake kwa wakati wa kuja (sh.20), na mwenye kupatanisha waamini kwa wakati wa sasa (mash. 21-23).

3. UTUMISHI WA PAULO (1:24-29)

Nyuma ya kusema juu ya mwili, ndio Kanisa (sh.18), na Habari Njema (sh.23) Paulo aliendelea kusema juu ya utumishi wake mwenyewe (mash.24-29). Ulikuwa utumishi wa mateso kwa ajili ya Habari Njema na Kanisa; kusudi lake lilikuwa kuleta kila mtu mtimili-fu katika Kristo; na ulifanywa kwa uwezo wa Bwana.

4. KRISTO ANATOSHA KUSHINDA HATARI YA ELIMU, SHERIA, MAFUNDISHO YA SIRI, NA KUJINYIMA MWENYEWE (Sura 2)

Halafu Paulo aliombea watakatifu tena (mash. 1-3). Aliomba waweze kupatishwa nguvu kushinda hatari, miyo yao iweze kuunganishwa pamoja katika mapendo, waweze kufahamu kwa hakika, na waweze kujua siri ya Mungu, ndiye Kristo. Kama wakijua na kuamini

WAKOLOSAYI

kweli kama Kristo ni nani, hawatadanganywa na mafundisho ya uwongo, kwani hazina zote za hekima na kujua zinafichwa ndani yake (mash. 4-5).

Walikuwa wamepokea Kristo Yesu Bwana kama yule anayetosha kabisa kwa maneno yote; hivi sasa iliwapasa kuendelea ndani yake, wakishikamana na nguvu na imani (mash. 6-7).

Mwalimu mwingine, jina lake Phillips, alitafsiri shairi 8 hivi: “Kaa na ange ili neno lo lote lisiharibu imani yako kwa njia ya akili ya watu, maneno yanayosikiana vizuri lakini yasiyo na maana. Akili hii inasimama juu ya mawazo ya watu juu ya namna ya dunia na inaona Kristo bule.”

Njia ya kushinda mafundisho ya uwongo ni Kristo. Utimilifu wote wa Mungu unakaa katika yeye kwa mwili. Mwamini anatimilika ndani yake, maana hahitaji neno lingine kwa kuweza kusimama mbele ya Mungu (mash. 9-10). Katika tohara ya Kristo, maana yake katika mauti yake, Mkristo ametahiriwa, maana amefunguliwa toka utawala wa tabia ya mwili inayosumbuka saa zote kujipatia haki mbele ya Mungu. Ubatizo ni mfano wa mauti ya tabia ya mtu wa zamani inayojaribu kupendeza Mungu kwa nguvu ya mwili. Ni mfano wa ufufuko vilevile kwa maisha mapya (mash. 11-12). Mwamini amesamehewa zambi zote na Kristo aliyeshinda majeshi yote ya uovu na kumfungua toka maagizo na kawaida ya matendo ya dini ya Wayuda (mash. 13-15).

Baki la sura linaonyesha mengine ya mafundisho ya uwongo ambayo Paulo alishindana nayo:

- a. Ya kwamba inapasa mtu kujaribu kupata wokovu kwa njia ya kutii maagizo juu ya vyakula na siku kubwa (mash. 16-17).
- b. Kujinyenyeka kwa mapenzi ya mtu, kuabudu malaika kama wenyewe kusimama katikati ya Mungu na watu, kujua maneno kwa njia ya maono ambayo watu wengine hawayajui, bila kutegemea Kristo, kwake unatoka uzima na kukua (mash. 18-19).
- d. Kujitawala mwili na ukali kwa kukubaliwa na Mungu. Kufanya hivi kunaonekana kama utawa lakini hakuwezi kutawala tamaa ya mwili (mash. 20-23).

5. MAISHA MAPYA YA MWAMINI, KUONDOSHA MTU WA ZAMANI NA KUVAA MTU MPYA (3:1-17)

Ndani ya sura 2 tumeona ya kwamba kwa macho ya Mungu mwamini amekufa pamoja na Kristo na amefufuliwa pamoja naye (2:11-12). Ni mahali pake ndani ya Kristo sasa. Halafu ikiwa hivi, lazima aishi kama mtu aliyefufuliwa na Kristo, mwenye maisha

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

yanayofichwa pamoja na Kristo katika Mungu (mash. 1-4). Inampasa kuacha desturi za zambi za maisha yake ya mbele wakati asipozaliwa tena bado, zambi kama uasherati (mash.5-7), kuchukia (sh.8), na masemo ya uwongo (sh.9). Kwa pahali pa maneno haya inampasa kuvala mtu mpya na matendo yake mema, kama upole, wema, unyenyekevu, uvumilivu (sh.12), kuchukuliana na kusameheana (sh.13), na mapendo.

Inapasa waamini kujuana na salama ya Kristo ikitawala miyoni mwao na Neno la Mungu likikaa kwa wingi ndani yao ili watu wengine waweze kujengwa vilevile. Lazima wafanye maneno yote kwa jina la Bwana Yesu pamoja na kushukuru (mash. 16-17).

6. MATENDO YANAYOFAA KWA JAMAA YA WAKRISTO (3:18 – 4:1)

Halafu mtume anatoa maonyo kwa jamaa za Wakristo. Inapasa wake kunyenyeka waume wao; waume kupenda wake wao; watoto kutii wazazi wao; baba kutokukasirisha watoto, watumishi kutii bwana wao; bwana wa kazi kutenda kwa haki.

7. MAISHA YA MAOMBI YA MWAMINI NA USHUHUDA WAKE KWA NJIA YA MWENENDO NA MASEMO YAKE (4:2-6)

Maombi ni neno kubwa kwa waamini, hivi Paulo alionya Wakolosayi kudumu katika maombi pamoja na kuangalia na kushukuru, na kutaja maombi yao wazi, maana wamwombee yeye mwenyewe (mash. 2-4). Sharti watembee kwa hekima wakifanya na roho moja maneno ambayo wanapata njia kuyafanya (sh.5). Masemo yao yawe na neema, na ya kufaa kujibu kila mtu (sh.6).

Paulo aliwakumbusha ya kwamba aliandika barua hii toka gereza na ya kwamba “zambi” yake ilikuwa kuhubiri siri ya Kristo, kweli kubwa juu ya kanisa, ndani yake Wayuda na Mataifa wanafanywa kuwa moja ndani ya Kristo.

8. RAFIKI ZA PAULO, NA SALAMU (4:7-18)

Ndani ya mashairi 7-14 kuna habari nusu juu ya wengine wa rafiki za Paulo. Alimaliza barua hii na salamu na maonyo (mash. 15-17), na maneno aliyosema ndani ya karibu zote za barua zake (sh.18).

Barua ya kwanza ya Paulo kwa Watesalonika

MWANZO

Mwanzo wa kanisa kwa Tesalonika

Kwa safari yake ya pili ya kuhubiri mtume Paulo alisafiri tokat Tarso kwenda kwa upande wa mangaribi kutambuka Asia, kisha alivuka Bahari ya Kati toka Troa kufikia Makedonia (upande wa kaskazini wa inchi inayoitwa Uyunani kwa wakati wa sasa). Wakati ye ye na wale waliosafiri pamoja naye walipofikia Tesalonika, aliingia sunagogi na kuhubiri Habari Njema ya Kristo. Alifanya hivi kwa sabato tatu. Wengine waliamini lakini wengine walileta matata kwa watu wale waliopangisha nyumbani mwao Paulo na wale waliosafiri pamoja naye, hivi ndugu walituma Paulo na Sila kwa Beroya.

Tarehe ya 1 Watesalonika

Toka Beroya mtume alikwenda Atene. Pale alisikia habari ya kwamba Wakristo wa Tesalonika walikuwa wakipata mateso. Wakati alipozuizwa asiwafikie ye ye mwenyewe, alituma Timoteo, aliyerudi kwake nyuma kidogo na habari nzuri. Neno hili lilisukuma Paulo kuandika barua hii. Labda ilikuwa barua ya kwanza ya Agano Jipyajiyoandikwa; tunafikili ni barua ya kwanza ambayo Roho Mtakatifu aliongoza Paulo kuandika (karibu A.D. 51).

Mambo yaliyo ndani ya 1 Watesalonika

Mtume aliandika juu ya maneno mengi, lakini zaidi juu ya kurudi kwa Bwana Yesu. Alitaja kweli hii kubwa ndani ya sura zote tano. Paulo alifikili kurudi kwa Kristo kunatusukuma kumtumikia na kutumaini kwamba tutapewa zawabu kwa kiti cha hukumu cha Kristo. Kunatusukuma kuwa na umoja na mapendo kwa Wakristo wengine, ni tumaini la kutufariji, na kutusukuma kujitakasa katika roho, nafsi na mwili.

UMBO LA 1 WATESALONIKA

1. Salamu na mashukuru (1:1-3)
2. Hakika watakatifu wa Tesalonika walikuwa Wakristo kweli (1:4-5a)
3. Namna gani Watesalonika waligeuka wenye kuleta watu wengine kwa Kristo (1:5b-10)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

4. Mambo Paulo aliyokumbuka juu ya Tesalonika (2:1-12)
5. Namna Watesalonika walivyopokea Habari Njema (2:13-16)
6. Elezo kwa nini Paulo hakurudia Tesalonika (2:17-20)
7. Kwa nini Timoteo alitumwa kwa Tesalonika (3:1-10)
8. Maombi ya Paulo kwa kanisa katika Tesalonika (3:11-13)
9. Maisha matakatifu (4:1-8)
10. Maisha ya utaratibu na yenyé mapendo kwa ndugu (4:9-12)
11. Tumaini linalofariji waamini (4:13-18)
12. Siku ya Bwana (5:1-11)
13. Maonyo mbalimbali kwa watakatifu (5:12-22)
14. Salamu ya mwisho kwa Watesalonika (5:23-28)

1. SALAMU NA MASHUKURU (1:1-3)

Paulo alitaja Sila na Timoteo pamoja naye ndani ya salamu yake (sh.1). Kisha aliendelea na mashukuru kwa Wakristo wa Tesalonika — kwa sababu waliokolewa, na kwa sababu walitumikia Mungu na mapendo, na kungojea Bwana Yesu na saburi (mash. 2-3).

2. HAKIKA WATAKATIFU WA TESALONIKA WALIKUWA WAKRISTO KWELI (1:4-5a)

Bila shaka waliwachaguliwa na Mungu; Paulo alijua neno hili kwa sababu ya namna walivyokuwa wamepokea Habari Njema wakati waliposikia mahubiri yake.

3. NAMNA GANI WATESALONIKA WALIGEUKA WENYE KULETA WATU WENGINE KWA KRISTO (1:5b-10)

Watesalonika walikuwa wamegeuka wenye kuiga Paulo na Bwana kwa njia ya kupokea Neno la Mungu na furaha hata pamoja na mate-so. Walikuwa mfano wa Wakristo wazuri wakitangaza neno la Bwana si katika Yunani tu lakini kila pahali. Habari zilienea mbio katikati ya watu namna walivyoyeuka kwa Mungu toka sanamu, ya kwamba sasa walikuwa wakitumikia Bwana, na kungojea kurudi kwa Mwokozi.

4. MAMBO PAULO ALIYOKUMBUKA JUU YA TESALONIKA (2:1-12)

Kufika kwa Paulo kulibarikiwa hata katikati ya mashindano (mash. 1-2)

Wakati Paulo alipowaza juu ya kufika kwake kwa Tesalonika alikumbusha watakatifu ya kwamba hakufika bule. Alikuwa amepigwa sasa tu katika Filipi na kutupwa gerezani, lakini maneno haya

1 WATESALONIKA

hayakumwogopesha. Aliendelea kuhubiri na uhodari hata kama kulikuwa na mashindano mengi.

Habari za Paulo kwa Watesalonika (2:3-4)

Mafundisho ya Paulo yalikuwa kweli kwa sababu yalitoka kwa Mungu. Aliyatoa na roho ya kweli, si kwa hila. Aliamini ya kwamba Mungu alimpa kazi ya kuhubiri Habari Njema na aliifanya na bidii kupendeza Mungu, si watu.

Mwenendo wa Paulo katika Tesalonika (2:5-12)

Paulo aliweka roho sana juu ya mwenendo wake mwenyewe. Neno hili linatukumbusha ya kwamba *mwenendo wa mtu ni mahubiri* vilevile. Hakuhubiri Habari Njema kwa kujipatia mali (mash. 5-6). Alikuwa mpole katikati yao, mwenye mapendo na alijitoa kwa kazi yake, akitumika na mikono yake kujipatia vitu alivyo hitaji (mash. 7-9). Alikaa katikati yao kwa utakatifu na haki, pasipo laumu, na aliwaonya na kuwasibitisha kama inavyofaa kwa baba mzuri wa roho (mash. 10-12).

5. NAMNA WATESALONIKA WALIVYOPOKEA HABARI NJEMA (2:13-16)

Paulo alikumbuka vilevile namna Watesalonika walivyopokea Habari Njema kama neno la Mungu, si neno la watu (sh.13). Nyuma ya kuokolewa kwao waliteswa na watu wa inchi yao kama vilevile makanisa katika Yuda walipata mateso toka Wayuda. Ushindani wa Wayuda ulikuwa kali zaidi. Walikuwa wameua manabii wa Mungu, waliua Bwana Yesu, walifukuza Paulo kila pahali alipofika, wakijaribu kwa kila njia kumzuiza asihubiri Habari Njema kwa mataifa. Kwa sababu ya zambi yao kubwa gazabu ya Mungu ilikuwa juu yao. Labda Paulo alikuwa akiwaza juu ya uharibifu kwa Yerusalem katika A.D.70 uliokuwa karibu (mash. 14-16).

6. ELEZO KWA NINI PAULO HAKURUDIA TESALONIKA (2:17-20)

Mwishoni, mtume alieleza kwa sababu gani hakurudia Tesalonika. Alikuwa amejaribu mara mbili kurudi, lakini Shetani alimzuiza kila mara. Si kwa sababu hakufikili watakatifu na mapendo mengi. Ni ye ye ambaye aliwaleta kwa Kristo nao watakuwa taji ya utukufu na furaha yake siku watakaposimama wote mbele ya Bwana mbinguni.

Shairi 19 linasaidia kujibu ulizo kama tutatambuana mbinguni. Bila shaka Paulo aliamini kwamba atatambua Wakristo wa Tesalonika.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

7. KWA NINI TIMOTEYO ALITUMWA KWA TESALONIKA (3:1-10)

Mashaka ya Paulo katika Atene (3:1-5)

Paulo hakuweza kufikia Tesalonika ye ye mwenyewe, hivi alituma Timoteo kuwasaidia rohoni na kuwatia moyo kwenda mbele hata katikati ya mateso. Alikuwa amewaambia mbele kwamba itawapasa kuteswa kwa ajili ya Kristo (mash. 1-4). Mtume alitaka sana kujuu namna gani walishinda ndani ya mateso haya, na kama walismama imara katika imani. Maneno makubwa ndani ya sura hii ni “imani yenu” (sh.5).

Timoteo alileta habari za kufurahisha (3:6-10)

Timoteo alirudi na habari nzuri. Watakatifu walismama na nguvu katika imani na mapendo, na walikuwa wakitamani kuona Paulo, kama ye ye vilevile alivyokuwa na hamu kuwaona (sh.6). Habari hizi ziliondosh a mziguo uliokuwa rohoni mwa Paulo juu yao na kumfariji sana. Ni kama kujuu kwamba walismama imara kulitia uzima mpya ndani ya roho yake.

8. MAOMBI YA PAULO KWA KANISA KATIKA TESALONIKA (3:11-13)

Alishukuru Bwana kwa furaha yote aliyopata kwa sababu yao na alikaa kuomba ya kwamba atakuwa pamoja nao tena na kuwapatisha nguvu kwa njia ya Neno la Mungu. Aliomba vilevile mapendo yao yaweze kuongezeka katika maisha yao ya sasa kusudi wawe bila laumu kwa wakati wa kuja. Zawabu yao itafunuliwa wakati Kristo atakapokuja pamoja na watakatifu wake kutawala juu ya dunia.

9. MAISHA MATAKATIFU (4:1-8)

Kwa mwanzo wa sura 4 Paulo alisih i Wakristo waweez kupendeza Mungu kwa njia ya kutembea katika utakatifu, na kwa mwisho wake alifundisha juu ya kupelekwa kwa watakatifu mbinguni. Alikuwa amewaagiza mbele kutimiza mapenzi ya Mungu kwa njia ya kuepuka uasherati. Sharti wajue kutawala mili yao katika utakaso, mbele na nyuma ya ndoa, kwa sababu Mungu ametuita kuishi maisha matakati fu, si maisha ya tamaa mbaya. Kama wakiasi agizo hili walizara Neno la Mungu na kuhuzunisha Roho Mtakatifu aliye kaa ndani yao.

Labda ndani ya shairi la kwanza Paulo aliwaza juu ya Enoka aliyetembea pamoja na Mungu (Mwa. 5:24a) na kumpendeza (Ebr. 11:5b), na aliyechukuliwa mbinguni na Mungu (Mwa. 5:24b; Ebr. 11:5a). Paulo alisif waamini kwa mwenendo wao mtakatifu, lakini

1 WATESALONIKA

aliwasihi sana kuendelea ndani yao na kuzidi. Kuwa na utakatifu si neno linalotimia mara moja, lakini neno ambalo inatupasa kukua ndani yake kwa njia ya kufuata Bwana Yesu karibu karibu kila siku.

10. MAISHA YA UTARATIBU NA YENYE MAPENDO KWA NDUGU (4:9-12)

Mtume anarudi tena kwa maneno ya mapendo. Watakatifu wali-kuwa wamefundishwa kupendana. Walijulikana kwa sababu ya mapendo yao. Vizuri waendelee na kuzidi kufanya hivi (mash. 9-10). Lakini ni kama wengine katikati yao walikuwa wameacha kutumika kazi kusudi wangojee kuja kwa Bwana. Neno hili halikuwa taratibu. Vizuri wawe na ushuhuda mzuri kwa njia ya kutumika kazi na bidii. Haifai wategemee watu wengine kuwalisha (mash. 11-12).

11. TUMAINI LINALOFARIJI WAAMINI (4:13-18)

Wafu katika Kristo (4:13-14)

Ni kama waamini wengine waliogopa ya kwamba wapenzi wao waliokufa katika Kristo (maana waliokuwa waamini) hawatashiriki ndani ya baraka yao walio hai wakati Kristo atakaporudi kusimamisha ufalme wake duniani. Paulo anasema, Sivyo. Bila shaka kama Kristo alivyokufa na kufufuka tena, vivyo hivyo Mungu ataleta watakatifu waliokufa mbele, pamoja na Kristo wakati atakapokuja kutawala. Basi neno hili litawezekana namna gani? Maiti zao zilizikwa kaburini. Namna gani Mungu anaweza kuwarudisha duniani toka mbinguni?

Namna matukio yatakayyofuatana wakati Kristo atakapoleta watakatifu mbinguni (4:15-18)

Ona jibu kwa ulizo hili: mbele ya kurudia duniani kusimamisha ufalme wake Kristo atapeleka waamini mbinguni. Kwa wakati ule waamini walio hai na wale waliokwisha kufa watakuwa sawasawa. Bwana atashuka toka mbinguni. Wafu katika Kristo watafuliwa, waamini walio kwanza hai watabadilika (1 Wakorinto 15:51), kisha wote watanyanyuliwa pamoja kukutana na Bwana katika hewa na kukaa pamoja naye kwa milele. Ni tumaini la faraja kabisa kwa watu wa Mungu.

12. SIKU YA BWANA (5:1-11)

Nyakati na majira (5:1-5)

Sasa Paulo aliachaa kusema juu ya kwenda kwa watakatifu mbinguni na anaendelea na habari juu ya siku ya Bwana, zaidi sehemu hii ya siku ya Bwana inayojulikana kama Mateso Makubwa. Ni miaka saba

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

ya hukumu itakayofuata kwenda kwa waamini mbinguni. Watesalonika walikuwa wamejifunza juu ya muda huu na ya kwamba utakuja kama mwizi katika usiku (mash. 1-2). Kutakuwa na uharibifu wakati watu wote wanapowaza yote ni salama, lakini Paulo aliwambia wasomaji wake ya kwamba hawahitaji kuogopa kwa sababu wao ni watu wa muchana, si wa usiku. Siku ya Bwana itafikia watu wale walio katika giza rohoni (mash. 3-5).

Mwenendo wa waamini (5:6-8)

Inapasa waamini kuishi kama wana wa nuru kwa njia ya kuwa na kiasi na imani, tumaini na mapendo.

Wokovu, si gazabu (5:9-11)

Mtume anawaambia waamini ya kwamba gazabu ya siku ya Bwana haitawapata. Wao watapokea wokovu wakati Mwokozi atakapokuja kwa watu wake. Kwa sababu tutaishi pamoja naye kwa wakati ule, ingetupasa kuishi pamoja na ndugu zetu na salama sasa.

13. MAONYO MBALIMBALI KWA WATAKATIFU (5:12-22)

Ndani ya mashairi 12-22 kuna maonyo kwa watu namna mbalimbali ndani ya jamaa ya Mungu. Inapasa Wakristo kujua na kuhe shimu viongozi wao kwa maneno ya Mungu na roho ya salama (mash. 12,13). Sharti viongozi waonye wale wasiokaa kwa utaratibu, maana wale wasiotumika kazi; kupatisha nguvu wale wanaolegea na kutia moyo walio zaifu, na kuwa na uvumilivu kwa watu wote (sh.14). Haifai Wakristo kulipa mabaya kwa mabaya lakini kufurahi siku zote, na kuomba na kushukuru (mash. 16-18). Haifai wazimishe Roho, kanisani au pahali po pote pengine, wala kubeua unabii. Sharti wapime mafundisho yote na Neno la Mungu na kushika yaliyo mema. Na wajitenge na ubaya wa kila namna (mash. 19-22).

14. SALAMU YA MWISHO KWA WATESALONIKA (5:23-28)

Paulo alimaliza barua yake kwa njia ya kuomba Mungu kuwatakasa kabisa, roho na nafsi na miili yao ili waweze kuwa bila laumu wakati Yesu atakaporudi. Aliamini ya kwamba Mungu wetu mwaminifu atafanya hivi. Aliwasihii wamwombee yeze vilevile, akasalimu ndugu zote kwa busu takatifu na kuwalapiza waangalie ili barua hii isomwe kwa ndugu zote. Mwishoni, kama ilivyokuwa de sturi yake, aliomba neema ya Bwana Yesu Kristo iwe pamoja nao.

Barua ya pili ya Paulo kwa Watesalonika

MWANZO

Tarehe ya 2 Watesalonika

Watu wanafikili kwamba barua hii iliandikwa toka Korinto muda mdogo nyuma ya 1 Watesalonika (karibu A.D. 51). Paulo, Silvano na Timoteo walikuwa kwanza pamoja, kama walivyokuwa wakati barua yake ya kwanza kwa Watesalonika ilipoandikwa (1:1), na Korinto ndio mji wa pekee pahali tunaposoma juu ya watu hawa watatu wakiwa pamoja (Matendo 18:1,5).

Mafundisho ya 2 Watesalonika

Paulo aliandika barua hii ya pili muda mdogo tu nyuma ya barua ya kwanza kwa sababu tatu. Wakristo walikuwa wakipata mateso na *walihitaji kutiwa nguvu rohoni* (sura 1). Walikuwa wamesikia mafundisho yasiyo sawa juu ya Siku ya Bwana, hivi *walihitaji maelezo* juu ya neno hili (sura 2). Wengine walikuwa wakikaa bila kutumika kazi kwa sababu ya kungojea kuja kwa Bwana, na *walihitaji maonyo* juu ya neno lile (sura 3).

UMBO LA 2 WATESALONIKA

1. Salamu na mashukuru ya Paulo (1:1-5)
2. Hukumu ya haki ya Mungu (1:6-10)
3. Ombi la Paulo kwa watakatifu (1:11-12)
4. Matukio mbele ya na wakati wa Siku ya Bwana (2:1-12)
5. Mashukuru ya mtume kwa sababu watakatifu wataepuka hukumu (2:13-14)
6. Maonyo ya Paulo kwa watakatifu (2:15)
7. Ombi la Paulo kwa watakatifu (2:16-17)
8. Paulo alitaka wamwombee yeeye vilevile (3:1-2)
9. Tumaini la Paulo juu ya watakatifu (3:3-5)
10. Maagizo juu ya wale wasiotii (3:6-15)
11. Baraka (3:16-18)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

1. SALAMU NA MASHUKURU YA PAULO (1:1-5)

Salamu ya Paulo ndani ya barua hii inafanana na ile ya 1 Watesalonika. Nyuma ya kusalimu watakatifu alishukuru Mungu kwa ajili yao. Alitaja imani, mapendo na kudumu katika mateso na taabu. Hakutaja tumaini lao hapa, labda kwa sababu walihitaji mafundisho mengine juu ya kuja kwa Bwana. Namna walivyovumilia mateso ilionyesha ya kwamba walistahili kutawala pamoja na Kristo ndani ya ufalme wake kwa wakati wa kuja.

2. HUKUMU YA HAKI YA MUNGU (1:6-10)

Wakati Kristo atakapokuja tena, wenyewe kuwatesa wataazibowi waziwazi na watu wa Mungu walioneswa watapata pumziko. Kristo atakuja katika moto wa kuwaka na ataa zibu wasioamini na kuwatenga na uso wa Bwana kwa milele. Watakatifu watatkuza Bwana na kumshangalia sana siku ile.

3. OMBI LA PAULO KWA WATAKATIFU (1:11-12)

Paulo aliomba mwenendo wa Watesalonika ustahili mwito wa Mungu, na wapewe nguvu kwa uwezo mkubwa wa Mungu kutenda na kutimiza kila hamu njema na kila kazi ya imani.

4. MATUKIO MBELE NA WAKATI WA SIKU YA BWANA (2:1-12)

Faraja kwa sababu ya kuja kwa Kristo (2:1-2)

Watesalonika walisumbushwa rohoni kwa sababu wengine walise-ma siku ya Bwana ilikuwa imefika, na ya kwamba hata kwa wakati ule walikuwa katika muda wa mateso makubwa. Kwa sababu ya mate-so makali ambayo waliyapata haikuwa nguvu kwao kuamini habari hizi. Paulo aliwakumbusha mafundisho juu ya kuja kwa Bwana kwa mawingu kupeleka waamini mbinguni mbele ya kuja kwake tena kwa hukumu siku ya Bwana. Wakumbuke ya kwamba watapelekwa mbi-nguni mbele ya kufika kwa siku ile.

Ukafiri mkubwa (2:3-7)

Maneno matatu mengine yatatokea mbele ya siku ya Bwana: (1) Ukafiri mkubwa, maana watu wengi wataacha imani. (2) Mtu wa kuasi, ndiye mpinga Kristo, atafunuliwa. (3) Mwenye kuzuiza ataondoshwa — tunafikili ni Roho Mtakatifu. Kwa wakati wa kuhamishwa kwa waamini mbinguni Roho Mtakatifu ataondoshwa vilevile kama mwenye kukaa ndani ya Kanisa na ndani ya waamini mmoja mmoja.

Mshindani mkubwa wa Kristo na Mateso Makubwa (2:8-12)

Mwenye uasi atashindana na dini namna zote; ataagiza watu

2 WATESALONIKA

kumwabudu yeye, na atadanganya watu na maajabu atakayofanya (mash. 4,9,10a). Wale wanaokataa kuamini Kristo kwa muda huu wa neema na walio kwanza hai kwa muda wa Mateso Makubwa watadanganywa na uwongo wake ya kwamba yeye ni Mungu (mash. 10b-11). Atahukumiwa pamoja na watu wote ambao wanamwabudu wakati Kristo atakaporudia dunia kwa uwezo na utukufu mkubwa (mash. 8b,12).

5. MASHUKURU YA MTUME KWA SABABU WATAKATIFU WATAEPUKA HUKUMU (2:13-14)

Paulo alishukuru Mungu kwa sababu waamini wataepuka hukumu hii. Mungu aliwachagua tangu mwanzo, aliwaita kumwamini kwa muda wa sasa, na atawatukuza pamoja na Kristo kwa wakati wa kuja.

6. MAONYO YA PAULO KWA WATAKATIFU (2:15)

Kwa sababu ya habari hizi zote iliwapasa kusimama kwa nguvu na kushikamana na kweli.

7. MAOMBI YA PAULO KWA WATAKATIFU (2:16-17)

Kwa mwisho wa sura hii Paulo aliomba Mungu kufariji mioyo yao na kuwasimamisha katika kila kazi na neno jema.

8. PAULO ALITAKA WAMWOMBEE YEYE VILEVILE (3:1-2)

Paulo aliwasihhi kumwombea yeye ili Neno la Bwana liweze kudenye na kusitawi, na ili yeye mwenyewe aweze kuokolewa toka watu waovu wenye hamu ya uuaji.

9. TUMAINI LA PAULO JUU YA WATAKATIFU (3:3-5)

Paulo aliamini kabisa ya kwamba Bwana, aliye mwaminifu, atawalinda na ya kwamba watacaa kutii Neno la Mungu, wakiwa na mapendo kama Mungu, na saburi kama Kristo.

10. MAAGIZO JUU YA WALE WASIOTII (3:6-15)

Wengine wa Wakristo katika Tesalonika hawakutembea katika utaratibu, maana yake waliacha kufanya kazi wakingojea kurudi kwa Bwana. Paulo aliagiza baki la Wakristo waonyeshe kutokubali kwao kwa njia ya kutoshirikiana na ndugu hawa wavivu ndani ya maneno ya kila siku (sh.6) Yeye mwenyewe alikuwa mfano mzuri kwao kwa njia ya kutumika sana kwa kujipatia mali kwa mahitaji yake bila kuwa mzigo kwa watu wengine na kuwaomba kumkulisha (mash. 7-9).

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Mtu akikataa kufanya kazi, haifai apewe vyakula vilevile. Kwa pahali pa kutembea pasipo utaratibu, kuwa mvivu na kujitia katika mambo ya wengine, ingempasa kutumika kazi kujisaidia mwenyewe na watu wa jamaa yake (mash. 10-12). Kama akikataa kufanya hivi, haifai Wakristo wachanganyikane naye, lakini wakae kumwonya; haifai wamtendee kama adui (mash. 13-15).

11. SALAMU (3:16-18)

Paulo aliandika salamu ya mwisho na mkono wake mwenyewe akiomba salama na neema ya Bwana ziwe pamoja nao.

TOFAUTI KATI YA KUJA KWA KWANZA NA KUJA KWA PILI WA KRISTO

Kuja kwa Kwanza kwa Kristo

1. Kristo anakuja kwa mawingu (1 Tes. 4:17).
2. Anakuja kwa watakatifu wake (1 Tes. 4:16,17).
3. Anakuja kwa siri, maana yake kweli hii haikufunuliwa katika Agano la Kale (1 Kor. 15:51).
4. Hatusomi kwamba maajabu mballimbalı mwınguni yatatangulia Kuja kwa Kristo kwa watakatifu wake.
5. Kuja kwa kwanza ni mamoja na Siku ya Kristo (1 Kor. 1:8; 2 Kor. 1:14; Flp. 1:6,10).
6. Kuja kwa kwanza ni wakati wa baraka (1 Tes. 4:18).
7. Kuja kwa kwanza kutatimizwa kwa dakika moja, kwa kufunga na kufungua jicho (1 Kor. 15:52). Neno hili linaonyesha bila kutaja wazi ya kwamba watu wa dunia (wasioamini) hawatakuona.
8. Kuja kwa kwanza kwa Kristo ni kwa Kanisa (Yn. 14:1-4; 1 Kor. 15:51-58; 1 Tes. 4:13-18).
9. Kristo anakuja kama nyota yenye kungaa ya asubui (Ufu. 22:16).
10. Hakuna habari juu ya kuja kwa kwanza kwa Kristo ndani ya Habari Njema ya Matayo, Marko na Luka, lakini Yoane alisema juu yake kwa maficho ndani ya kitabu chake.
11. Wale wanaochukuliwa wanachukuliwa kwa baraka (1 Tes. 4:13-18). Wale wanaobaki wanabaki kwa hukumu (1 Tes. 5:1-3).
12. Hakuna tarehe inayotajwa kwa matukio yatakayotangulia Kuja kwa kwanza kwa Kristo.
13. Jina la "Mwana wa watu" halikutumiwa ndani ya Maandiko juu ya Kuja kwa kwanza kwa Kristo.

Kuja kwa Pili kwa Kristo (Ufunuo)

1. Anakuja duniani (Zek. 14:4).
2. Anakuja *pamoja na* watakatifu wake (1 Wates 3:13; Yuda 14).
3. Ufunuo (Kuja kwa pili) si siri. Kuna unabii wingi juu yake ndani ya wa Agano la Kale (Zab. 72; Isa. 11; Zek. 14).
4. Kuja kwake *pamoja na* watakatifu wake kutatangazwa na alama nyingi mbinguni (Mt. 24:29,30).
5. Ufunuo (Kuja kwa pili) ni mamoja na siku ya Bwana (2 Tes. 2:1-12).
6. Neno kubwa juu ya Ufunuo ni hukumu ya Mungu kwa watu (Mt. 24:27; Ufu. 1:7).
7. Watu wote duniani wataona Ufunuo (Kuja kwa pili kwa Kristo) (Mt. 27; Ufu. 1:7).
8. Ufunuo ni kwanza kwa Waisraeli, kisha kwa Mataifa vilevile (Mt. 24:1 – 25:46).
9. Anakuja kama Jua la Haki na kuponu katika mabawa yake (Mal. 4:2).
10. Ufunuo unaonekana tena na tena katika Matayo, Marko, na Luka, lakini kidogo tu katika Habari Njema ya Yoane.
11. Wale wanaokamatwa wanakamatta kwa hukumu. Wale wanaobaki wanabaki kwa baraka (Mt. 24:37-41).
12. Tarehe nyingi zilitajwa kwa Ufunuo wa Kristo, kama siku 1260, miezi 42, miaka mitatu na nusu. (Ona Dan. 7:25; 12:7, 11,12; Ufu. 11:2; 12:14; 13:5).
13. Tunasoma juu ya Ufunuo wa Kristo kama kuja kwa Mwana wa watu (Mt. 16:28; 24:27,30,39; Mk. 13:26; Lk. 21:27).

Barua ya kwanza ya Paulo kwa Timoteo

MWANZO

Barua kwa wachungaji wa Kanisa

Barua za Paulo kwa Timoteo na Tito ni mafundisho kwa wachungaji wa makanisa. Timoteo na Tito walikuwa wasaidizi wa Paulo ndani ya kazi ya Bwana.

Historia ya 1 Timoteo

Mtume Paulo alikutana na Timoteo wakati alipofikia Listra mara ya kwanza. Timoteo alikuwa mwanafunzi hata mbele (Matendo 16:1). Kuanza wakati ule Paulo na Timoteo walifungana pamoja ndani ya kazi ya Mungu. Labda Paulo alimwita mwana wake kwa sababu walikuwa na nia moja, si kwa sababu Timoteo aliamini Kristo kwa mkono wa Paulo.

Tarehe ya 1 Timoteo

Watu wanafikili Paulo aliandika barua hii ya kwanza *nyuma* ya kufunguliwa toka kifungo katika Roma, katika A.D. 63 na 67, hivi *nyuma* ya matukio yaliyoandikwa ndani ya kitabu cha Matendo.

Neno kubwa la 1 Timoteo

Tunaona kusudi la barua hii ndani ya 3:15: "... upate kujuua sana namna gani inavyokupasa kutenda katika nyumba ya Mungu, iliyoko kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli."

UMBO LA 1 TIMOTEO

1. Salamu kwa Timoteo (1:1-2)
2. Agizo kunyamazisha walimu wa uwongo (1:3-11)
3. Mashukuru kwa neema ya kweli ya Mungu (1:12-17)
4. Paulo anaagiza Timoteo tena (1:18-20)
5. Mafundisho juu ya namna gani kutenda kanisani (sura 2-3)
6. Maonyo juu ya ukafiri (watu wakikana kabisa imani ya kikristo) uliokuwa ukikaribia (4:1-5)
7. Mafundisho kwa Timoteo juu ya ukafiri uliokuwa karibu (4:6-16)
8. Maagizo juu ya waamini wenye kazi mbalimbali (5:1 – 6:2)

1 TIMOTEO

9. Walimu wa uwongo na mapendo ya mali (6:3-10)
10. Maagizo ya mwisho kwa Timoteo (6:11-21)

1. SALAMU KWA TIMOTEO (1:1-2)

Paulo alisalimu Timoteo na mapendo mengi akimwita “mwana wangu wa kweli, katika imani.”

2. AGIZO KUNYAMAZISHA WALIMU WA UWONGO (1:3-11)

Kusudi la agizo la Paulo (1:3-5)

Paulo alianza mara moja kuagiza Timoteo, kama alivyofanya mbele, kunyamazisha walimu wa uwongo waliokuwa wakifundisha hadizi na maneno ya vizazi pasipo mwisho (mash. 3-4). Kusudi kubwa la maagizo haya halikuwa tu kwa *kweli* ya Neno la Mungu kufundi-shwa, lakini yawefe kuzaa mapendo toka moyo safi na zamiri njema, na imani pasipo udanganyifu (sh.5).

Kusudi la sheria (1:6-11)

Walimu wa uwongo walisema ni lazima kushika sheria kwa kupata ukubali mbele ya Mungu (mash. 6-7). Sharti wafahamu ya kwamba sheria ni njema kama mtu akiitumia namna inavyofaa, na ya kwamba kusudi la sheria ni kufahamisha watu zambi zao. Sheria haikufanywa kwa wenye haki lakini kwa wenye kuvunja sheria na kwa waasi — Paulo alitaja watu namna kumi na tano au zaidi wanaofanya hivi.

3. MASHUKURU KWA NEEMA YA KWELI YA MUNGU (1:12-17)

Wakati mtume alipotaja zambi hizi namna namna, alikumbuka wokovu wake mwenyewe na neema ya Mungu ambayo ilimwita kutumikia Bwana. Alikuwa mtukanaji na mtesaji na mtu wa jeuri mbele — ndiyo, mwenye zambi nyingi zaidi. Lakini Kristo alikuwa kwa wenye zambi kama yeye, akamrehemu kusudi aweze kuwa mfano wa kazi kubwa neema ya Mungu inayoweza kufanya ndani ya maisha ya mtu. Wakati Paulo alipowaza juu ya maneno haya, roho yake ilifurika na sifa kwa Mungu.

4. PAULO ANAAGIZA TIMOTEO TENA (1:18-20)

Ni kama mbele kulikuwa na unabii juu ya Timoteo ya kwamba atakuwa mtumishi wa Bwana. Paulo alimkumbusha neno hili kwa njia ya kumwagiza tena kuhamakia walimu wa uwongo. Ndani ya vita hii nzuri inampasa kushikamana na imani na zamiri safi. Wengine wa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

watu ambao mtume alijua walikuwa wameacha kuwa na zamiri safi, wamegeuka wenye kutukana na kuharibisha imani. Paulo alikuwa amewatoa kwa Shetani wafundishwe na kuazibiwa.

5. MAFUNDISHO JUU YA NAMNA GANI KUTENDA KANISANI (Sura 2-3)

Maombi kwa watu wote (2:1-7)

Mbele ya maneno yote ilipasa kanisa kuombea watawala, ili waamini waweze kuishi na salama. Ombi hili linapatana na mapenzi ya Mungu kwa watu wote kuokolewa. Paulo alijitaja mwenyewe kuhakikisha ya kwamba Mungu anataka watu wote kuokolewa; Bwana alikuwa amemweka yeeye mhubiri kupeleka habari hizi kwa Mataifa.

Kazi ya wanaume kanisani (2:8)

Paulo anafundisha kwamba ni kazi ya wanaume kuomba na sauti kanisani na kuongoza waamini katika maombi, lakini sharti wale wanaofanya hivi wawe watu wa salama na utawa.

Kazi ya wanawake kanisani (2:9-15)

Juu ya wanawake Paulo anasema haifai wanawake wavae mavazi ya mapambo mengi kwa kukokota macho ya watu juu yao. Neno lililo zuri zaidi ni kuwa na moyo wa kiasi unaoonekana kwa njia ya kazi njema. Ndani ya kanisa inapasa wanawake kukaa kimya na kujifunza na roho ya kutii. Haifai wasimame kufundisha wanaume au kuwatawala. Msingi wa mafundisho haya si desturi za wakati ule, lakini namna Mungu alivyoumba mume na mke kwa wakati wa mwanzo, na kuingia kwa zambi duniani kwa njia ya Hawa aliyedanganywa. Lakini hata kama mwanamke akiagizwa kuwa mwenye kutii, ana kazi ya faida kanisani. Amepewa kazi kubwa ya kulea watoto wake kwa Mungu. Kazi hii ndiyo wokovu wake kanisani, maana yake amepewa nafasi ya heshima kubwa kanisani.

Maneno yaliyo sharti kuonekana ndani ya maisha ya wazee (waangalizi) (3:1-7)

Sasa Paulo anafundisha Timoteo kama inapasa wazee ndani ya kanisa kuwa watu wa namna gani. Mtu ye yote anayetaka kuwa mzee anataka kazi nzuri. Haifai mtu huyu kuwa na laumu, sharti awe na mke mmoja tu, awe mwenye kiasi, mtu anayejua kujitawala mwenyewe, mtu wa utaratibu, mkaribishaji wageni, mwenye kujuja kufundisha. Haifai awe mtu wa kulewa, mpigaji, au mwenye kupenda feza. Lazima awe mpole, si mtu wa magomvi, lakini mwenye ku-

1 TIMOTEO

ongoza watu wa nyumba yake vizuri, si mwamini wa sasa. Sharti awe na ushuhuda mzuri mbele ya watu.

Maneno yaliyo sharti kuonekana ndani ya maisha ya watumishi (3:8-13)

Watumishi ndio watu wanaotumikia kanisa kwa kazi yo yote ila kazi ya wachungaji. Sharti watumishi wawe watu wa utaratibu, si wenye kusema maneno kwa hila, si watu wa kulewa, si wenye choyo. Sharti mwenendo wao na maneno wanayoamini na kufundisha yawe taratibu. Inapasa kujaribu watu hawa kwanza kujua kabisa kama ni watu pasipo laumu. Inafaa wawe na mke mmoja na kuwa wenye kuongoza watu wa nyumba zao vizuri (mash. 8-10,12). Inafaa wana-wake (wale wanaotumikia kanisa vilevile, au wake wa watumishi) kuwa watu wa utaratibu, si wasingiziaji, lakini wenye kujitawala wenyewe, waaminifu katika maneno yote (sh.11). Kwa njia ya kufanya kazi ya mtumishi vizuri watumishi wanajipatia heshima ya watu wengine na wanawenza kushuhudia Kristo na imani yao na uhodari (sh.13).

Siri kubwa ya imani (3:14-16)

Saa Paulo alipokuwa akiandika barua hii alitaraji kuonana na Timoteo nyuma kidogo, lakin kama akikawa, alitaka mwana wake wa kweli kujua namna gani ilimpasa kutenda kanisani, lililo nguzo na msingi wa kweli. Alijumlisha kweli kubwa za imani, akiziita siri ya utawa. Alitaja kweli kubwa juu ya Kristo, ya kwamba alionekana katika mwili wakati alipotwaa utu, alihesabiwa kuwa na haki katika Roho wakati wa ubatizo wake, saa alipogezwa sura, wakati alipofufuka na kurudi mbinguni. Malaika walimwona wakati wa kuzaliwa kwake, wakati alipojaribiwa jangwani, taabu yake katika shamba la Getesemane, ufufuko wake na kwenda kwake mbinguni. Alihubirwa katika mataifa toka wakati wa mitume kufika sasa, aliaminiwa *katika ulimwengu* lakin si *na* watu wa ulimwengu; alipokewa katika utukufu wakati aliporudi mbinguni.

6. MAONYO JUU YA UKAFIRI (watu wakikana kabisa imani ya kikristo) ULIOKUWA UKIKARIBIA (4:1-5)

Paulo alifahamu ya kwamba kwa wakati wa kuja watu wataacha kweli, na watasikiliza roho za kudanganya na mafundisho ya mshetani. Aliita watu hawa wawongo wa hila, wenye zamiri zilizochomwa moto. Maneno mawili wanayofundisha ni ya kwamba haifai watu kuo, wala kula vyakula fulani. Mtume alikumbusha Timoteo ya kwamba vyakula vyote ni vizuri na ni zawadi toka Mungu kwani vimetakaswa kwa Neno la Mungu na kwa maombi, na inatupasa kuvipokea na asante.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

7. MAFUNDISHO KWA TIMOTEO JUU YA UKAFIRI ULIOKUWA KARIBU (4:6-16)

Kwa sababu ukafiri huu ulikuwa karibu, ilipasa Timoteo kukaa kukumbusha Wakristo juu ya hatari hii. Lazima yeye mwenyewe aishi maisha ya utawa, aweze kuwa mfano mzuri kwa watu wengine. Aweke roho juu ya kusoma Maandiko katikati ya watu na atumie zawadi ya roho aliyopewa. Sharti atumikie Mungu na roho moja na kuangalia mwenendo wake kusudi maisha na mafundisho yake yawe na faida kwa watu wengine.

8. MAAGIZO JUU YA WAAMINI WENYE KAZI MBALIMBALI (5:1 – 6:2)

Ndani ya 5:1 – 6:2 kuna maagizo juu ya waamini wenye kazi mba-limbali kanisani.

Namna gani kutendea ndugu katika kanisa (5:1-2)

Haifai mtu aliye kijana kwanza, kama Timoteo, kuhamakia mzee, lakini kumwonya kama baba. Inampasa kutendea wenzake kwa njia ya miaka kama ndugu, wanawake wazee kama mama, wanawake vijana kama ndugu wake.

Namna gani kutendea wajane (5:3-16)

Inapasa wajane walio na ndugu walindwe na ndugu hawa. Wale wasio na ndugu hai ni “wajane kweli”. Inapasa kanisa kusaidia wajane namna hii kama wakiwa na miaka kupita 60, watawa na wenye kufuata Mungu kabisa, waliotumikia Kristo na watu wake. Ni vizuri kupita kwa wajane vijana kuolewa tena kwa sababu ya majaribu ya tamaa na uvivu zinazoweza kuwaingiza ndani ya zambi.

Namna gani kutendea wazee (5:17-20)

Wazee wanaotawala vizuri wanastahili kupewa heshima na kusaidiwa na mali vilevile. Mzee akishitakiwa juu ya neno fulani, sharti washuhuda wawe wawili au watatu. Lazima mzee anayefanya zambi ahamakiwe mbele ya watu wote.

Maonyo ya Paulo kwa Timoteo juu ya maneno ya maisha yake mwenyewe (5:21-25)

Inapasa Timoteo kutii maagizo haya bila upendeleo. Haifai achague watu mbio kwa kazi fulani, na sharti ajilinde mwenyewe safi. Aache kunywa maji yasiyo safi na kumpa ugonjwa, na anywe mvinyo kidogo kama dawa. Akumbuke ya kwamba zambi, na matendo mema vilevile yataonekana wazi siku nyingine — hayawezi kufichwa.

1 TIMOTEO

Namna gani kutendea bwana wa kazi (6:1-2)

Sharti watumwa walio Wakristo watendee na heshima bwana wao wasioamini kwani neno hili ni ushuhuda mzuri. Haifai wazarau bwana walio waamini lakini kuwatumikia vizuri kwa sababu wao ni waamini wenzao. Maagizo haya ni kwa watumishi Wakristo pahali pote duniani na kwa kila wakati.

9. WALIMU WA UWONGO NA MAPENDO YA MALI (6:3-10)

Roho mbaya ya walimu wa uwongo (6:3-5)

Halafu mtume alihukumu walimu wa uwongo. Alisema wao ni wenye kiburi, wajinga, wenye kubishana wanaoamsha wivu ndani ya roho za watu, na magomvi, matukano, na mafikili mabaya zinazotoka kwa hasidi. Zaidi ya ile, wanafikili juu ya utumishi wao kama njia kujipatia mali.

Utawa pamoja na furaha ni utajiri mkubwa (6:6-8)

Lakini utawa pamoja na furaha ni utajiri mkubwa wa kweli. Tukiwa na vitu tunavyohitaji kwa maisha yetu ya kila siku tunaweza kukaa na furaha.

Shina moja la mabaya yote (6:9-10)

Tamaa kwa mali inaleta majoribu na mitego, masumbuko, woga, kurudi nyuma, na huzuni nyingi. Kweli mapendo ya mali ni shina moja la namna zote za ubaya.

10. MAAGIZO YA MWISHO KWA TIMOTEO (6:11-21)

Kukiri kuzuri (6:11-16)

Ndani ya maagizo yake ya mwisho kwa Timoteo Paulo alisema naye kukimbia, kufuata, na kupiga vita. Inampasa *kukimbia* hatari ya mali. Inampasa *kufuata* haki, utawa, imani, mapendo, vivi hivi. *Apige vita* vizuri ya imani, na aonyeshe ndani ya maisha yake mwito wake kwa uzima wa milele. Mtume alisema vilevile na Timoteo kuwa *mwaminifu* kwa kweli ya Mungu kufika siku ya kuonekana kwa Bwana.

Mafundisho kwa watajiri (6:17-19)

Vizuri Timoteo aonye watajiri bila woga wasijivune na wasitege-mee mali yao. Sharti wategemee Mungu na kutumia mali yao kusaidia watu wengine. Kwa njia hii watakuwa na hazina ya milele.

Linda imani (6:20-21a)

Mwishoni Paulo alionya Timoteo kulinda mafundisho ya kweli ya

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

imani aliyowekewa akiba, na kugeuka toka mabishano bule yasiyo na faida na kila namna ya elimu isiyo elimu ya kweli na isiyopatana na kweli ya Biblia. Maneno namna hii yanaondosha watu toka imani.

Baraka (6:21b)

Paulo alimaliza barua yake na “neema.” Ni kwa Timoteo na watu wote watakosoma barua hii pamoja naye. Hapa si zaidi neema ya Mungu katika wokovu, lakini nguvu yake kusaidia Wakristo ndani ya mwenendo wao.

Barua ya pili ya Paulo kwa Timoteo

MWANZO

Tarehe ya 2 Timoteo

Hii ni barua ya mwisho ya Paulo; iliandikwa wakati alipofungwa katika Roma mara ya mwisho, karibu A.D. 67-68.

Historia ya 2 Timoteo

Paulo alifahamu ya kwamba atauawa nyuma kidogo na alitaka sana kufundisha Timoteo na kutia roho yake nguvu. Wakati wa matata ulikuwa mbele ya Kanisa. Ilipasa Timoteo kuwa na uhodari na kutimizia utumishi wake bila haya. Ilimpasa kufundisha wengine, kuvumilia taabu, na kuepuka uovu. Neno litakalosaidia Timoteo sana wakati uovu katika mwenendo na mafundisho utakapozidi duniani lilikuwa Maandiko Matakatifu. Lazima afanye kazi yake na uaminifu, ahubiri Neno, aangalie na kuvumilia — kusudi kutimiza utumishi wake kama mtumishi wa Mungu.

UMBO LA 2 TIMOTEO

1. Salamu kwa Timoteo (1:1-5)
2. Maonyo kwa Timoteo (1:6 – 2:13)
3. Hitaji kubwa kwa kusimamia imani ya Wakristo (2:14-26)
4. Ukarifiri unaokaribia (3:1-13)
5. Neno linaloweza kusaidia mtu wa Mungu anayetazamia kukaribia kwa ukafiri (3:14 – 4:8)
6. Maombi na habari za Paulo mwenyewe (4:9-22)

1. SALAMU KWA TIMOTEO (1:1-5)

Fikili juu ya mawazo ya Paulo wakati alipoandika barua hii ya mwisho kwa mwana wake mpendwa (mash. 1-2)! Alishukuru Mungu wakati alipowaza juu ya kijana huyu, ndugu katika imani — machozi yake, labda saa walipoagana mara ya mwisho; imani yake ya kweli iliyokaa kwanza ndani ya mama na tata yake wenye imani (mash. 3-5).

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

2. MAONYO KWA TIMOTEO (1:6 – 2:13)

Haifai kuwa na haya juu ya Habari Njema (1:6-12)

Haifai Timoteo akae na woga. Awe mwenye mapendo na nguvu na moyo wa kiasi (mash. 6-7). Haifai awe na haya juu ya Habari Njema, au juu ya Paulo gerezani, lakini akae tayari kupata taabu kwa ajili ya Habari Njema (sh.8). Neno hili tu linafaa wakati tunapokumbuka utukufu mkubwa wa Habari Njema na maneno yote ambayo Mungu alitufanyia. Hata Paulo mwenyewe alikuwa akiteswa, hakuwa na haya lakini aliamini kabisa kwamba Mungu anaweza kumlinda (mash. 9-12).

Kushika imani (1:13-18)

Ilipasa Timoteo kushika imani aliyowekewa na mtume Paulo (mash. 13-14). Na sharti afungane na rafiki zake Wakristo (mash. 15-18). Rafiki za Paulo katika Asia walikuwa wamemwacha, ila mtu mmoja, ndiye Onesiforo. Mtu huyu alimtumikia na uaminifu gerezani.

Kuwa mhodari katika neema (2:1-10)

Paulo aliendelea na maonyo yake ya baba kwa mwana wake. Sharti Timoteo awe hodari katika neema ya Kristo Yesu. Na afundishe kweli ya Mungu kwa wanaume waaminifu watakaoweza kufundisha kweli hii kwa watu wengine (mash. 1-2). Kama *askari*, avumilie taabu bila kujitia katika maneno ya dunia hii (mash. 3-4). Kama *mwenye kushindana katika michezo*, lazima atii amri za mashindano (sh.5). Kama *mlimaji*, atumike na imani ya kwamba atashiriki ndani ya mavuno (mash. 6-10).

Neno lililo aminifu na kweli (2:11-13)

Ni kama ndani ya mashairi haya Paulo alitaja maneno ya wimbo mmoja wa Wakristo, maana yake hii: "Tutapokea zawabu kama tukitumikia Mwokozi na uaminifu, lakini kama tukimkana yeze atatukana sisi. Matendo yake yanapatana kila mara na namna alivyo." Paulo alisema hapa juu ya kukana kwa msiyeamini, si mwanafunzi wa kweli kama Petro. Bwana hatakana watu wake mwenyewe kamwe.

3. HITAJI KUBWA KWA KUSIMAMIA IMANI

YA WAKRISTO (2:14-26)

Wenye kazi wanaokubaliwa (2:14-15)

Ilipasa Timoteo kuonya walimu wengine wasiingizwe ndani ya mabishano ya maneno (sh.14). Sharti yeze mwenyewe aweke roho kabisa juu ya kuwa mfanya kazi anayekubaliwa na asiyeha, akitafasiri vema neno la kweli (sh.15).

2 TIMOTEO

Wenye kazi wasiokubaliwa (2:16-19)

Paulo alirudi tena na tena kwa maneno ya walimu wa uwongo. Mafundisho yao hayatoki kwa Mungu na yanaongoza watu katika njia isiyio ya Bwana. Alitaja watu wawili waliofundisha ya kwamba ufu-fuko umepita, na walioharibu imani ya watu wengine (mash. 16-18). Alifarijiwa wakati alipokumbuka ya kwamba Mungu hashindwi; ana-jua watu wake. Mtu akisema yeye ni mtu wa Mungu, sharti ahaki-kishe neno hili kwa njia ya kuishi maisha matakatifu (sh.19).

Nyumba kubwa ya jamii ya Wakristo wote (2:20-21)

Ndani ya jamii hii kuna wengine walio Wakristo wa kweli na wengine wasio wa kweli. Lazima mtumishi wa faida ajitenge na uovu wote, watu waovu na mafundisho yao maovu.

Imani, mapendo na salama (2:22-26)

Ni sharti kwa Timoteo kukimbia tamaa za mwili, na kufuata utawa na haki (sh.22). Aepuke mabishano yasiyo na faida na magomvi, na afundishe na saburi wale wanaoshindana naye akitaraji ya kwamba watatoka katika mtego wa Shetani na kufungana na kweli ya Bwana (mash. 23-26).

4. UKAFIRI UNAOKARIBIA (3:1-13)

Nyakati za hatari na watu wa hatari (3:1-5)

Paulo alifahamu ya kwamba siku za mwisho zitakuwa nyakati za hatari. Alionyesha kama wakafiri watakuwa watu wa namna gani — watu waovu kabisa. Haifai Timoteo kuwa na ushirika wo wote nao.

Wachuuzi wa mafundisho yasiyopatana na Neno la Mungu (3:6-9)

Wanajaribu kufundisha zaidi wanawake wajinga wanaosumbuka na mizigo ya zambi na wanaokubali mafundisho yo yote ambayo wanafikili yatawasaidia, lakini hawapokei kweli ya Mungu kamwe. Wakafiri ni kama wachawi wale wawili Wamisri walioshindana na Musa, nao watashindwa vilevile.

Mwenendo wa mtu wa Mungu (3:10-13)

Mwenendo na kazi ya mtume Paulo zilikuwa namna nyingine. Alitaja taabu na maneno mane mengine hapa (mash. 10-11), na alikumbusha Timoteo ya kwamba bila shaka wale wanaotaka kuishi maisha ya utawa watapata mateso. Waovu watazidi katika uovu (mash. 12-13).

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

5. NENO LINALOWEZA KUSAIDIA MTU WA MUNGU ANAYETAZAMIA KUKARIBIA KWA UKAFIRI (3:14 – 4:8)

Neno kamilifu la Mungu (3:14-17)

Neno litakalosaidia mtu wa Mungu kwa wakati wa ukafiri ni kuendelea bila kusita ndani ya Neno la Mungu. Timoteo amejeua Maandiko Matakatifu toka ujana wake. Maandiko haya yalipewa kwa maongozi ya Mungu na yanafaa kumwezesha kwa kila kazi njema, kama vile yalifaa kuokoa roho yake mbele toka uharibifu.

Kazi ya mtumishi wa Mungu wakati ukafiri unapoongezeka (4:1-8)

Haya ni maonyo ya mwisho ya Paulo kwa Timoteo. Kwanza alimwagiza kutangaza Neno la Mungu waziwazi (mash. 1-2). Kwa nini? Kwa sababu watu watakataa mafundisho ya kweli, na vilevile kufa kwa Paulo kulikuwa karibu (mash. 3-4). Ilipasa Timoteo kuangalia katika maneno yote, kuvumilia mateso, kuhubiri na kutimiza utumishi wake (mash. 5-8).

6. MAOMBI NA HABARI ZA PAULO MWENYEWE (4:9-22)

Habari za Paulo juu yake mwenyewe (4:9-13)

Alikuwa na hamu sana kwa Timoteo kufikia Roma na kuleta Marko vilevile. Mmoja wa washiriki wake alikuwa ameondoka na kwenda pahali pengine, na Luka tu alikuwa pamoja naye. Aliomba Timoteo kuleta joho na vitabu vyake, zaidi vile vyaya ngozi. Labda vingie vilikuwa Maandiko Matakatifu, na labda vingine vilikuwa kwa barua zake.

Bwana mwaminifu katikati ya watu wasio waaminifu (4:14-18)

Alesanduro alifanyia Paulo mabaya mengi wakati aliposimama kuhukumiwa na serikali. Labda alishitaki Paulo juu ya maneno yasi-yokuwa kweli na alishindana na ushuhuda wa Paulo. Wakati Paulo alipojibu mashitaki mara ya kwanza hakuna mtu aliyetoea ushuhuda kumsimamia, lakini Bwana alisimama pamoja na Paulo, naye aliaachwa kwa wakati. Aliamini kabisa ya kwamba Bwana atamsaidia asimkane, na atamchunga hata afike kwa ufalme wake wa mbingu.

Maagano ya mwisho ya Paulo (4:19-22)

Nyuma ya kuongeza habari nyingine, Paulo alisihi Timoteo kufika kwake mbele ya wakati wa baridi. Halafu alitoa ombi lake la mwisho kwa mwana wake wa kweli na kwa wote waliokuwa pamoja naye. Kazi yake ilikwisha na nyuma kidogo alitoa uzima wake, lakini harufu tamu ya maisha yake na baraka ya utumishi wake zinatusaidia hata leo. Kweli tuna deni kubwa kwa sababu ya barua zake ambazo Mungu alimwongoza kuandika.

Barua ya Paulo kwa Tito

MWANZO

Historia ya Tito

Nyuma ya kufungwa katika Roma mara ya kwanza na mbele ya kufungwa tena, Paulo alikuwa ameacha Tito katika Krete aweze kuangalia utaratibu usimamishwe na kuchungwa ndani ya makanisa ya pale. Tito alikuwa mmoja wa wale waliosafiri pamoja na Paulo, na alikuwa mjumbe wake aliyepewa kazi ya kutengeneza mambo magumu katika kanisa.

Mafundisho ya Tito

Ndani ya barua hii Paulo alitaja mengine ya maneno yaliyo lazima ili kanisa liweze kuendelea na utaratibu. *Kwanza*, sharti wazee wawe wenye kuonyesha maneno fulani ndani ya maisha yao. *Neno la pili*, lazima walimu wa uwongo wanyamazishwe. *Neno la tatu*, ni sharti kufundisha kweli ya Mungu na kuitii. *Neno la mwisho*, inapasa Wakristo kutii serikali na kujitoa kufanya kazi njema kwa pahali pa kufikirifiki maneno bule.

Tarehe ya Tito

Paulo aliandika barua hii karibu A.D. 65, *mbele ya kuandika 2* Timoteo.

UMBO LA TITO

1. Salamu kwa Tito (1:1-4)
2. Wazee kanisani (1:5-9)
3. Mafundisho ya uwongo kanisani (1:10-16)
4. Kazi kanisani (Sura 2)
5. Maonyo kanisani (3:1-11)
6. Salamu ya mwisho (3:12-15)

1. SALAMU KWA TITO (1:1-4)

Salamu ya Paulo kwa Tito ni ndefu kupita salamu yake ndani ya barua zake nydingine. Ndani ya mashairi haya Paulo alisema kazi yake ni zaidi *kuhubiri Habari Njema, kufundisha*, na *kutumaini*. Aliongoza watu kuamini Yesu, aliwafundisha kweli ya Mungu, na aliweka mbele yao tumaini la utukufu kwa wakati wa kuja. Mungu aliahidi kwa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

nyakati za milele kuleta Habari Njema, akafunua kwa njia ya mahubiri. Paulo (na wengine vilevile) waliwekewa kazi ya kuihubiri.

Paulo aliita Tito mwana wake katika imani.

2. WAZEE KANISANI (1:5-9)

Paulo aliacha Tito katika Krete kumaliza kazi mtume aliyoanza, na kuweka wazee katika makanisa ya kisanga kile. Ndani ya mash. 6-9 tunaona kama inapasa mzee kuwa mtu wa namna gani nyumbani mwake, ndani ya mwenendo wake mwenyewe, na kanisani. Sharti awe mtu wa kukomea katika imani na mwenye kujua kuongoza watu wengine.

3. MAFUNDISHO YA UWONGO KANISANI (1:10-16)

Wadanganyi wakemewe (1:10-11)

Sharti Tito akemee walimu wa uwongo, zaidi Wayuda waliojaribu kuchanganya sheria na neema, na kusudi la kujipatia wenyewe mali.

Wakrete wakemewe (1:12-15)

Sharti Wakrete wakemewe vilevile kwani walikuwa “wawongo, nyama waovu, walafi wavivu.” Haifai waamini wakubali hadizi za Wayuda, na sheria juu ya vyakula zisizo na maana sasa. Zaidi ya Wakrete walikuwa wenyе machukizo, wenyе kuasi, watu wasiofaa kwa tendo jema lo lote.

4. KAZI KANISANI (Sura 2)

Maneno yanayoonekana ndani ya kanisa jema (2:1-10)

Paulo anaonyesha sasa namna gani mafundisho mazuri yanokane ndani ya watu namna tano kanisani: waume wazee, wana-wake wazee, wanawake vijana, wanaume vijana, na watumishi.

Neema ya Mungu na mafundisho yake (2:11-15)

Kusudi kubwa moja la wokovu wetu ni kuzaa utakatifu ndani ya maisha yetu. Neema ile inayoleta wokovu inatufundisha vilevile kuishi maisha mema kabisa tungali tunangojea kurudi kwa Mwokozi. Kusudi moja la kuja kwa Kristo duniani na kujitoa mwenyewe kama sadaka kwa Mungu lilikuwa kutukomboa toka uovu wote na kujisafishia watu wawe mali yake mwenyewe, wenyе bidii sana katika kazi njema. Sharti Tito afundishe maneno haya pamoja na kuonya na kukemea bila woga.

5. MAONYO KANISANI (3:1-11)

Wariti wa tumaini la uzima wa milele (3:1-8)

Sharti Wakristo watii serikali ya inchi yao na kukaa tayari kwa kila kazi njema. Inawapasa kuwa wapole na wenyewe adabu, na kuepuka matukano na magomvi. Mbele ya kuokolewa tulikuwa watu wenyewe zambi namna namna (sh.3). Halafu Mungu alituokoa kwa neema yake, si kwa njia ya matendo yetu. Tiliofsha na Roho Mtakatifu kwa kuzaliwa mpya, na tuligeuka wariti wa uzima wa milele. Mwokozi alilipa bei kubwa sana kutuokoa toka mabaya mengi, hivi inatupasa kuishi maisha yanayofaa, na kudumu katika kila kazi njema (mash. 4-8).

Kuepuka mabishano na mitengo (3:9-11)

Tito aliagizwa kuepuka mabishano yasiyo na maana. Ilimpasa kukataa mtu anayeleta mitengo nyuma ya kumwonya mara mbili, kwa sababu mtu huyu amegeuka mbali na kweli, ni mwenye kufanya zambi, naye amejihukumu mwenyewe.

6. SALAMU YA MWISHO (3:12-15)

Kwa mwisho wa barua hii kuna maagizo kwa Tito juu ya wenyewe kushiriki naye ndani ya kazi ya Bwana, na maonyo kwa waamini wajitoe kabisa kutenda matendo mema. Maneno haya “matendo mema” au “kazi njema” yanaonekana mara ine au zaidi ndani ya barua hii fupi. Ni moja la mambo makubwa yanayofundishwa ndani ya barua hii.

Barua ya Paulo kwa Filemono

MWANZO

Historia ya Filemono

Wakati Paulo alipokuwa gerezani kwa Roma, alikutana na mtumwa jina lake Onesimo, akamleta kwa Kristo. Paulo alijua bwana wa mtumwa huyu (ndilo neno la kushangaza!), aliyekuwa Mkristo katika Kolose, jina lake Filemono.

Kusudi la barua kwa Filemono

Wakati Paulo aliporudisha Onesimo kwa Filemono, alifikili vizuri amwombee vilevile kusudi Filemono aweze kumpokea tena, si kama mtumwa tu lakini sasa kama ndugu katika Bwana.

Tarehe ya Filemono

Barua hii nzuri na yenze neema iliandikwa karibu na A.D. 62. Tunafikili iliandikwa kwa wakati Paulo alipoandika barua kwa Wakolosayi. Paulo alituma Tito kupeleka barua mbili zote, na alituma Onesimo pamoja naye (Kol. 4:7-9).

UMBO LA FILEMONO

1. Salamu (mash. 1-3)
2. Mashukuru na maombi ya Paulo kwa Filemono (mash. 4-7)
3. Maombi ya Paulo kwa Onesimo (mash. 8-16)
4. Paulo alitia Filemono moyo aweze kutii (mash. 17-20)
5. Maneno ya mwisho (mash. 21-25)

1. SALAMU (mash. 1-3)

Timoteo alikuwa pamoja na Paulo aliyekuwa mfungwa, kwa wakati barua hii ilipoandikwa. Barua hii si kwa Filemono tu, lakini vilevile kwa Apia na Arkipo, (watu wanafikili Apia na Arkipo walikuwa mke na mwana wa Filemono), na kwa kanisa waliokutana nyumbani mwao.

2. MASHUKURU NA MAOMBI YA PAULO KWA FILEMONO (mash. 4-7)

Paulo alituma salamu yake ya neema na salama, kama ilivyokuwa

FILEMONO

desturi yake. Alisifu roho ya Filemono, zaidi mapendo na imani yake, na aliomba ya kwamba mema aliyotendea watu wengine yaweze kufahamisha wengi wao kutambua mambo mazuri yaliyo yetu ndani ya Kristo Yesu. Paulo alifarijiwa sana kwa sababu ya ukarimu na mape-ndo ya Filemono.

3. MAOMBI YA PAULO KWA ONESIMO (mash. 8-16)

Paulo, hata alikuwa mzee na mfungwa wa Kristo, hakuagiza Filemono kupokea Onesimo vizuri, lakini alimwomba kufanya hivi (mash. 8-10). Maana ya jina hili “Onesimo” ni “ya kuleta faida”. Onesimo hakuwa mtu wa faida kwa bwana wake. Lakini sasa alikuwa ameokolewa na atakuwa na faida kwa Filemono na kwa Paulo, baba yake katika imani (sh.11). Wakati aliporudisha Onesimo kwa Filemono ilikuwa kama Paulo alituma nusu ya moyo wake mwenyewe. Angalipenda kwa Onesimo kukaa pamoja naye, na kwa njia ile Filemono angaliweza kusaidia mtume na kumpatia msaidizi. Lakini Paulo hakutaka kufanya hivi bila ukubali wa Filemono (mash. 12-14). Bwana wa kazi alipotewa mtumwa kwa muda mfupi, lakini sasa atapata mtumishi na ndugu atakayebaki daima, ambaye atamtumikia na nguvu ya mwili wake na kushiriki naye kama mwamini (mash. 15-16). Habari Njema tu inaweza kugeuza maneno hivi.

4. PAULO ALITIA FILEMONO MOYO AWEZE KUTII (mash. 17-20)

Ilipasa Filemono kupokea Onesimo namna angalipokea Paulo mwenyewe. Kama mtumwa alikuwa ameiba mali ya bwana wake, mtume, ndiye Paulo, atalipa mali ile, hata kama Filemono alikuwa amepokea uzima wa milele kwa njia ya ushuhuda wa Paulo. Filemono atafurahisha Paulo sana na kuburudisha moyo wake kama akipokea Onesimo.

5. MANENO YA MWISHO (mash. 21-25)

Paulo aliamini ya kwamba Filemono atafanya neno aliloomba, laki- ni ya kwamba zaidi ya ile atatengenezea Paulo pahali pa kukaa wakati atakapofika kwa Kolose (mash. 21-22). Kwa mwisho wa barua kuna salamu toka watano wa watu waliokuwa pamoja na Paulo, na ombi kwa neema kuwa pamoja na roho za wale watakaosoma barua hii (mash. 23-25).

Barua kwa WAEBRANIA

MWANZO

Mwandishi na tarehe ya Waebrania

Hatujui nani aliandika barua hii lakini kwa njia ya barua yenye we tunafahamu iliandikwa ndani ya muda ulioanza na A.D. 30 (wakati Kristo aliporudi mbinguni) na A.D. 70 (wakati hekalu lilipoharibiwaa). Kristo alikuwa ameketi kwa mkono wa kuume wa Mungu (10:12), lakini hekalu lilisimama kwanza wakati barua ilipoandikwa (13:10-11).

Hatari kwa imani ya Waebrania

Kwa wakati ule, kama sasa vilevile, Wayuda walioamini Kristo waliskumwa na nguvu kurudi kwa dini ya Wayuda. Walikumbushwa utukufu wa ukuhani, hekalu, na sadaka. Haikuwa nguvu kwa wale waliokiri Kristo bila kuamini kweli kukana Kristo na kurudi kwa dini yao ya mbele na kawaida yake.

Mafundisho ya Waebrania

Mafundisho makubwa ya barua kwa Waebrania ni kuonyesha ya kwamba Kristo alitimiza mifano na vivuli vyote vya Agano la Kale. Anapita wakubwa wote wa zamani wa Wayuda, na kazi yake ni nzuri kupita sadaka zote za zamani. Wale wanaoacha dini ya Wayuda na kuamini Kristo wanaacha maneno ya kawaida na kupata maneno ya hakika. Wale wanaoacha Kristo na kurudi kwa dini ya Wayuda wana-tenda na kusudi zambi ya ukafiri.

UMBO LA WAEBRANIA

1. Kristo ni mkubwa kupita manabii (1:1-3)
2. Kristo ni mkubwa kupita malaika (1:4 - 2:18)
3. Kristo ni mkubwa kupita Musa (3:1 - 4:13)
4. Ukuhani wa Kristo unapita ule wa Haruni (4:17 - 7:28)
5. Utumishi wa Kristo unapita ule wa Haruni (Sura 8)
6. Sadaka ya Kristo inapita sadaka zote za Agano la Kale (9:1 - 10:18)
7. Maonyo (10:19 – 13:17)
8. Mwisho (13:18-25)

1. KRISTO NI MKUBWA KUPITA MANABII (1:1-3)

Kristo ni *mkubwa kupita manabii*. Mungu alisema na malaika kwa njia mbalimbali nyingi, lakini sasa amesema kwa njia ya *Mwana wake*. Mwana yule ni mriti ambaye Mungu alimweka, mwumba wa vyote, kungaa kwa utukufu wake, mwenye sura yake kabisa, mwenye kutegemeza vitu vyote, zabihu inayosafisha zambi, na Bwana juu ya kiti cha kifalme.

2. KRISTO NI MKUBWA KUPITA MALAIKA (1:4 – 2:18)

Kutukuzwa kwa Mwana (1:4-14)

Kristo ni mkubwa kupita malaika kwani ye ye ni Mwana wa Mungu. Ana cheo na jina kubwa kupita malaika. Malaika wanamwabudu, na Mungu Baba anamwitwa “Mungu”. Yeye ni mwenye enzi wa milele, Mfalme wa haki, na Mwumba mkubwa. Aliahidiwa amri zote, lakini malaika ni watumishi tu.

Hatari ya kutoweka roho juu ya wokovu mkubwa namna hii (2:1-4)

Kuna maonyo machache ndani ya barua hii na sasa tunaona onyo la kwanza. Ni hatari kwa sisi wakati wote kuacha kuponyoka maneno ambayo tuliyasikia juu ya Kristo. Watu walioasi sheria waliazibwi na ukali, lakini kuna azabu kali kupita kwa wale wasioweka roho juu ya wokovu mkubwa unaopatikana kwa njia ya Kristo, ulioshuhudiwa na mitume, na kuhakikishwa na Mungu kwa njia ya maajabu.

Mamlaka juu ya dunia (2:5-9a)

Kristo ni mkubwa kupita malaika, si kama Mwana wa Mungu tu, lakini kama Mwana wa watu. Ni nguvu kidogo kufahamu mawazo ya mwandishi hapa. Zamani Mungu aliweka mtu, si malaika, kuwa na amri juu ya dunia (mash. 5-8b). Lakini sasa, mtu amepoteza amri hii kwa njia ya zambi, hivi sasa watu hawatawali vitu vyote tena. Lakini tunaona Yesu aliyewekewa taji ya utukufu na heshima, na ndani ya maneno haya tunaona ya kwamba kwa wakati wa kuja mtu atatawala dunia. Kristo atarudi kama mtu kutawala dunia na kurudisha tena mamlaka ambayo Adamu aliipoteza, na maneno mengi zaidi (mash. 8c-9a).

Baraka kwa njia ya kunyenyekewa kwa Kristo (2:9b-18)

Mbele ya kutukuzwa mbinguni kama alivyo sasa, Kristo alifanywa *chini* ya malaika kwa njia ya kugeuka mtu, kuteswa na mauti (mash. 9b-10). Maandiko ya Wayuda yanahakikisha ukamilifu wa utu wake (mash. 11-13). Mengine ya matunda ya kunyenyekewa kwake ni

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

uharibifu wa Shetani, uondolewa wa woga, malipo kwa zambi, msaa-da kwa wale wanaojaribiwa (mash. 14-18).

3. KRISTO NI MKUBWA KUPITA MUSA (3:1 – 4:13)

Mtumishi na Mwana (3:1-6)

Sasa tunaona ya kwamba Kristo ni *mkubwa kupita Musa*. Wao wawili walikuwa waaminifu kwa pahali pao, lakini Bwana Yesu ni mkubwa kupita kwani yeye ni *mjengaji* wa nyumba (Musa alikuwa *mtumishi* tu ndani ya nyumba), na kwa sababu yeye ni Mungu na Mwana.

Hatari ya kufanya miyo yetu migumu (3:7-19)

Sasa tunaona onyo la pili. Roho Mtakatifu anatuonya juu ya hatari ya ya kufanya miyo yetu migumu. Ni kwa sababu ya zambi hii kizazi kizima cha Waisraeli walizuizwa wasiingie raha ya Mungu katika Kanana (mash. 7-11). Lazima watu wote wanaosema wao ni waamini waangalie wasiwe na moyo mbaya wa kutokuamini unaofanywa mgumu kwa udanganyifu wa zambi (mash. 12-15). Askari zote wa Waisraeli wenye miakak 20 au zaidi waliotoka Misri walikasirisha Mungu, walikufa jangwani, na hivi hawakuingia raha ya Mungu. Hawakuweza kuingia kwa sababu ya zambi ya kutokuamini (mash. 16-19).

Bidii kuingia raha ya Mungu (4:1-13)

Endeleo la onyo la pili. Sharti tuangalie sana tusikose kufikia raha ya Mungu. Tunasoma juu ya raha namna mbalimbali hapa. Mungu alipumzika siku ya saba. Nyuma aliapa ya kwamba Waisraeli wasioamini *hawataingia* raha yake. Kama Yosua angaliwfikisha kwa raha ya mwisho ya Mungu katika Kanana, Daudi asingalisema juu ya raha kwa wakati wa nyuma. Sisi tunaoamini tumeingia raha kwa wakati wa sasa. Na kunabaki raha ya sabato kwa watu wa Mungu, maana yake, raha ya milele mbinguni. Inatupasa kudumu sana kuingia raha ile, tukikumbuka ya kwamba bila shaka uasi na kutokuamini zitafunuliwa wazi na Neno la Mungu na Bwana wetu anayejua yote.

4. UKUHANI WA KRISTO UNAPITA ULE WA HARUNI

(4:14 – 7:28)

Kuhani mkubwa wetu mwenye huruma (4:14-16)

Sasa tunaanza kusoma juu ya ukuhani mkubwa wa Kristo na tunaona ya kwamba unapita ule wa Haruni (4:14-16). Tuna kuhani mkubwa aliyetukuzwa mbinguni, Yesu Mwana wa Mungu. Yeye ni mwenye huruma, amejaribiwa yeye mwenyewe, naye ni mkamilifu

WAEBRANIA

kabisa, bila zambi. Kwa sababu hii inatupasa kushika imani yetu na kukaribia kiti cha neema na uhodari katika maombi. Pale tutapokea rehema, na kupata neema kwa wakati tunapoihitaji.

Tabia ya makuhani wa ukuhani wa Haruni (5:1-4)

Kuhani wa ukuhani wa Haruni alichaguliwa katika watu, alitoa matoleo na sadaka kwa zambi kwa ajili yao. Alikuwa na huruma kwa uzaifu wa watu, alitoa sadaka kwa ajili yake mwenyewe na kwa watu, na aliitwa na Mungu.

Ukuhani mkamilifu na wa daima wa Kristo (5:5-10)

Kristo aliweka na Mungu kuwa kuhani kwa namna ya ukuhani wa Melkisedeki. Wakati alipokuwa mtu mkamilifu hapa duniani alitoa maombi na machozi. Alikuwa na tumaini, na kwa sababu ya tumaini hii alifufuliwa. Hata akiwa Mwana wa Mungu, alijifunza kutii kwa njia ya mateso, na alikamilishwa, na kwa sababu hii alikuwa mte-ngenezaji wa kutimia wa wokovu wa milele kwa wote ambao wanamtii.

Kutokukomea katika maneno ya roho (5:11-14)

Onyo la tatu ni juu ya hatari ya ukafiri au kuanguka (5:11 – 6:20). Mwandishi angalipenda kutoa mafundisho ya ndani ndani kupita juu ya ukuhani wa Kristo, lakini kwa sababu ya kutokomea kwa wasomaji wake waliweza kufahamu nusu tu ya kweli ya Mungu, si maneno ya ndani ndani. Walihitaji kufundishwa wao wenyewe maneno ambayo ingaliwapasa kuweza kufundisha watu wengine. Walikuwa kama watoto kwa imani, si watu wazima wenye kuweza kutambua maneno. Waamini waliokomea wanaweza kutambua ya kwamba ukuhani wa Kristo unapita ule wa Haruni.

Hatari ya kukosa kuendelea mbele (6:1-8)

Mwandishi anaendelea hapa na onyo la tatu. Ingaliwapasa kuacha kuwaza juu mafundisho ya kwanza tu ya Agano la Kale kama toba, imani ndani ya Mungu, mafundisho ya mabatizo, kuwekea nyama za sadaka mikono, ufufuko, na hukumu, na kuendelea hata utimilifu (mash. 1-3).

Mashairi 4 na 5 ni juu ya watu waliokiri kuwa Wakristo, hata kama hawakuzaliwa tena kweli. Walipewa nuru (maana walijifunza maneno mengi juu ya Kristo), walionja (bila kupokea) zawadi ya mbingu, walifanywa washiriki wa Roho Mtakatifu (ambaye aliwafahamisha zambi zao), wameonja neno Neno zuri la Mungu (bila kilitii), na kuona maajabu yatakayofanywa tena nyuma kwa muda wa utawala wa Kristo duniani kwa miaka 1000. Kama watu wale

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

wakianguka, kusulibisha Mwana wa Mungu tena na kumpa haya mbele ya watu, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakitubu. Wao ni kama inchi inayozaa miiba na magugu, si mapando ya faida, nayo itateketezwa. Wao ni wakafiri (mash. 4-8).

Kusudi la Mungu ndani ya Kristo (6:9-20)

Waamini wa kweli ni namna nyiningine na wakafiri. Kazi zao zina-hakikisha kwamba wameamini kweli. Waendelee hata mwisho, na kuriti ahadi kwa njia ya imani na uvumilivu (mash. 9-12). Abrahamu ni mfano wa maneno haya. Akiapa kwa yeze mwenyewe, Mungu ali-ahidi kumpa wazao wengi. Abrahamu alivumilia na saburi na ahadi ya Mungu ilitimizwa. Mungu aliongeza hata kiapo juu ya ahadi yake ya wokovu wa milele ili watu wake walioamini waweze kujua hakika. Ahadi na kiapo chake vinatutia moyo wa nguvu wakati tunapoachana na maneno ya dunia hii ya kufa na kukimbilia mbingu. Tunajua ya kwamba tutaweza kuingia kule kwa saba Bwana Yesu alitutangulia na kuingia yeze mwenyewe (mash. 13-20).

Yesu na Melkisedeki (7:1-3)

Mwandishi aliendelea kuonyesha ya kwamba ukuhani wa Kristo ni mkubwa kupita ule wa Haruni. Kwa kufanya hivi alijulisha wasomaji maneno mengine juu ya Melkisedeki. Alikuwa mfalme wa Salemu na ukuhani wa Mungu. Alibariki Abrahamu na kupokea zaka (sehemu ya kumi) ambazo Abrahamu alimletea. Maana ya jina lake ni “mfalme wa haki,” na kwa sababu maana ya Salemu ni “salama”, alikuwa mfalme wa salama vilevile. Kwa maneno ya ukuhani, Melkisedeki hakuwa na kizazi na hatusomi habari za mwanzo au mwisho wake. Alifanana na Mwana wa Mungu kwa njia ya ukuhani wake unaoende-lea bila kwisha.

Ukuhani wa Melkisedeki (7:4-10)

Mwandishi anaendelea kuhakikisha ya kwamba ukuhani wa Melkisedeki ulipita ule wa Haruni. Neno la kwanza, Abrahamu alitoa zaka kwa Melkisedeki. Basi Lawi alikuwa mzao wa Abrahamu, hivi ni kama Lawi alitoa zaka kwa Melkisedeki. Tendo la Melkisedeki la kubariki Abrahamu lina maana vilevile: ni desturi kwa mkubwa kubariki mdogo. Ukuhani wa Lawi ulikwisha na mauti, lakini ukuhani wa Melkisedeki unaendelea milele.

Ukuhani mpya ulihitajiwa (7:11-22)

Kama kusudi la Mungu lingalitimizwa kwa njia ya ukuhani wa Lawi, ukuhani mwingine usingalihitajiwa. Lakini kulikuwa na mwingine; ukuhani wa Kristo uliweka kando ukuhani wa Lawi. Sheria nzima juu ya ukuhani imegeuzwa. Kristo alikuwa mzao wa

WAEBRANIA

Yuda, hakuwa mtu wa khabila la Lawi, khabila la makuhani. Haku-geuka kuhani kwa njia ya vizazi, lakini kwa njia ya uwezo ulio ndani yake mwenyewe. Anaishi kwa milele. Sheria ya zamani imeondo-shwa na matumaini mazuri zaidi yaliingizwa pahali pake. Yesu alitangazwa kuwa kuhani kwa kiapo cha Mungu ambaye alimfanya kuhani kwa milele. Kwa sababu hii yeche ni mzamini wa agano zuri kupita.

Ukuhani wa Kristo usioweza kubadilika (7:23-25)

Kulikuwa na makuhani mengi waliokuwa wazao wa Haruni, lakini wao wote walikufa. Lakini ukuhani wa Kristo haukwishi kwa sababu *anaishi milele*. Kwa sababu hii anaweza kuokoa kabisa wote wanaokuja kwa Mungu kwa njia yake, kwani yeche ni hai milele kuwambea mbinguni.

Ukuhani mkamilifu wa Kristo (7:26-28)

Ukuhani wa Kristo unapita ule wa Haruni kwa njia nyingine vilevile — Haruni alikuwa mtu ambaye ilimpasa kutoa sadaka kwa zambi zake mwenyewe, lakini Mungu Mwana *amekamilika kabisa* na kutukuzwa juu sana, alitoa zabihu kamilifu moja tu inayotosha kabisa. Hakuwekwa kuhani na torati, lakini kwa kiapo cha Mungu.

V. UTUMISHI WA KRISTO UNAPITA ULE WA HARUNI (Sura 8)

Kuhani mukubwa wetu (8:1-3)

Tutaona sasa kwa njia ya kusawanisha pahali patakatifu pawili ya kwamba utumishi wa Kristo unapita ule wa Haruni (mash. 1-13). Katika pahali patakatifu pa mbingu kuna kuhani mkubwa aliye keti kwa mkono wa Mungu. Pahali patakatifu palifanywa na Bwana, si na mtu. Kama makuhani wote, ilipasa Bwana wetu kuwa na kitu kwa kutoa (tutaandika juu yake nyuma).

Utumishi, agano, na ahadi bora zaidi (8:4-6)

Sheria iliagiza kwamba watu fulani tu waliweza kuwa makuhani ndani ya pahali patakatifu pa dunia. Kristo hakuweza kuwa kuhani ndani ya pahali patakatifu pale kwa sababu alikuwa wa khabila la Yuda. Hema ya dunia ilikuwa mwigo na kivuli tu wa ile mbinguni. Utumishi wa Kristo ni mzuri kupita kwa sababu yeche ni mpatanishi wa agano zuri zaidi, lenye kusimama kwa ahadi nzuri zaidi.

Agano Jipyaa (8:7-13)

Maneno ya agano yanatufikilisha tofauti katikati ya sheria na neema. Kuna agano jipyaa sasa, hivi agano la kwanza halikuwa kami-

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

lifu. Mungu yeye mwenyewe hakupendezwa kabisa na agano la kwanza, akaahidi kufanya agano jipy. Agano hili jipy linategemea Mungu tu, na linaahidi ya kwamba watu watajua Mungu miyoni mwao, watapata usamehe wa zambi, na Mungu atasahau zambi zile. Agano jipy linageuza agano la mbele kuwa la zamani.

6. SADAKA YA KRISTO INAPITA SADAKA ZOTE ZA AGANO LA KALE (9:1 – 10:18)

Hema ya dunia (9:1-5)

Tunajifunza sasa ya kwamba sadaka ya Kristo inapita zile za Agano la Kale (9:1 – 10:18). Kwa wakati wa ukuhani wa Lawi hematifikali ikuwa na vyumba viwili, pahali patakatifu na pahali patakatifu sana. Kila chumba kilikuwa na vitu vya kufaa ndani yake. Mwandishi alitaja vitu hivi kimoja kimoja, lakini hakuweza kusema maneno mengi juu yao.

Kadiri ya utumishi ndani ya hemu ya dunia (9:6-10)

Muhani waliingia chumba cha kwanza saa zote, lakini kuhanimkubwa tu aliweza kuingia chumba cha pilii, mara moja tu kila mwaka, na pamoja na damu tu ndani ya bakuli kwa zambi zake na zambi za taifa zima. Amri hizi zinaonyesha ya kwamba njia ya kukaribia Mungu haikuwa wazi kabisa wakati hemu ya kwanza ili-posimama kwanza. Na vilevile, sadaka hizi haziwezi kumpa mwenye kuabudu zamiri safi kabisa. Zilikuwa zaidi sadaka kumsafisha kama alianguka ndani ya kawaida ya dini ya wakati ule.

Hema mbinguni (9:11-14)

Tusawanishe habari hizi na kazi ya Kristo, Kuhani Mzuri zaidi ndani ya hemu nzuri kupita. Aliingia *mara moja tu* ndani ya pahali patakatifu mbinguni, aikikwisha kutupatia ukombozi wa *milele*. Hakupeleka damu ya nyama lakini damu yake mwenyewe. Majivu la kindu la ngombe katika Agano la Kale yalilettea mwabudaji kusafishwa kulikopatana na kawaida ya dini, lakini damu ya Kristo inasafisha moyo wake, na zamiri vilevile na matendo ya kufa aweze kutumikia Mungu aliye hai.

Hitaji kwa upatanisho wa damu (9:15-22)

Kristo ni mpatanishi wa agano jipy, na mauti yake inakombua watakatifu wa wakati wa Agano la Kale toka makosa yao kwa maneno ya sheria ya Musa ili wawezekupokea uriti wa milele. Lakini agano la uriti halina nguvu wakati mwenye kulifanya ni kwanza

WAEBRANIA

hai, vivyo hivyo agano la kwanza lisibitishwa tu kwa njia ya mauti, mauti za nyama za sadaka. Musa alikamata damu ile na kuinyunyiza juu ya kitabu cha sheria, watu na hema. Damu ilihitajiwa kwa namna nyingi za utakaso na inahitajiwwa kwa usamehe wa zambi.

Ukubwa wa sadaka ya Kristo (9:23-28)

Kawaida hizi za dini zilitosha kusafisha pahali patakatifu pa dunia, lakini sadaka nzuri kupita ilihitajiwa kwa pahali patakatifu pa mbinguni. Kristo alitimiza hitaji hili kabisa. Aliingia mbinguni, si ndani ya pahali patakatifu palipofanywa na watu, na alitokea mbele ya Mungu kwa ajili yetu. Hakuleta damu ya sadaka za nyama, kama kuhani mkubwa wa zamani alivyofanya, lakini alitokea mara moja tu kuondoa zambi kwa njia ya kujitoa mwenyewe kuwa sadaka. Agano la zamani lilihukumu wenyewe zambi kufa. Agano jipyga ni juu ya kuja kwa kwanza kwa Kristo na kutolewa kuwa sadaka kwa zambi, na kuja kwake mara ya pili kuokoa wale amba wanamngojea na hamu.

Sadaka za nyama hazitoshi (10:1-4)

Sadaka hizi zilizotolewa wakati wa Agano la Kale hazikuweza kusafisha zamiri za watu kamwe, lakini walikumbushwa zambi zao kila mwaka. Kabisa kabisa damu ya nyama haikuondoa hata zambi moja.

Mauti ya Kristo ilitimiza mapenzi ya Mungu (10:5-10)

Wakati Kristo alipofika duniani alifahamu kwamba Mungu Baba hakupendezwa kabisa na utaratibu wa zamani wa sadaka, hivi alijitoa na kutaka kwake mwenyewe kuwa sadaka. Kwa njia ya kufanya hivi aliondoshya utaratibu wa mbele wa zabihu na kuuomboa na zabihu yake kubwa kwa zambi, zabihu inayotakasa waamini *mara moja kwa milele*.

Mauti ya Kristo inakamilisha wale wanaotakaswa (10:11-14)

Makuhani wa zamani walismama kila siku na kutoa zabihu zisizoweza kuondoa zambi, lakini Kristo alitoa zabihu moja inayotosha milele. Kisha aliketi kwa mkono wa Mungu. Kwa njia ya zabihu yake moja waamini wanakamilishwa mbele ya Mungu, na wanaweza kusimama mbele yake wenyewe zamiri safi kwa maneo ya zambi.

Uwezo wa daima wa agano jipyga (10:15-18)

Kwa njia ya maandiko ya Agano la Kale Roho Mtakatifu anashuhudu ya kwamba kwa njia ya agano jipyga, Mungu hatakumbuka tena zambi zinazokwisha kusamehewa.

7. MAONYO (10:19-13:17)

Tunaweza kukaribia Mungu (10:19-22)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Kwa sababu tunaweza kuingia pahali patakatifu na uhodari, na kwa sababu tuna Kuhani mkubwa, ingetupasa kukaribia na moyo wa kweli, wenyewe tumaini na zamiri zinazokwisha kusamehewa, na maisha matakatifu.

Tushike sana kukiri kwa tumaini letu (10:23-25)

Sharti tushike sana kukiri kwa tumaini letu, kusukumana katika mapendo na kazi nzuri. Vilevile haifai kwetu kuacha makusanyiko ya kanisa. Maana ya “kuacha” hapa si kukosa kufika tu, lakini ni kugeuka mafakiria.

Maonyo juu ya ukafiri (10:26-31)

Onyo la ine ni juu ya kuchagua kugeuka mafakiria, ndiyo kukana Kristo na kufungana na dini nyingine. Watu wanaokiri kuwa Wakristo (bila kuzalia tena kamwe), wanaofungana na Wakristo wa kanisa fulani, kisha wanageuka mali na Kristo na kusudi, ni wakafiri. Haiwezekani kwa watu wale kuokolewa, lakini wanatazamia hukumu ya kuogopesha na moto mkali. Kama mutu aliyeasi sheria ya Musa alikuwa kwa zambi yake, azabu ya wakafiri itakuwa kubwa zaidi kwani wanakataa Mwana wa Mungu, wanahesabu damu ya damani kuwa kitu kichafu, na kutukana Roho Mtakatifu. Hawataweza kuepuka azabu kali sana ya Mungu.

Kutia moyo wakati wa mateso (10:32-39)

Watu wanaopata mateso wanahitaji kutiwa moyo wawewe kuvumilia. Ingalipasa maneno yaliyopata waamini Waebrania mbele kuwatia roho nguvu kuvumilia taabu yao. Kukumbuka kwamba zawabu yao ilikuwa karibu kungepasa kuwapatisha nguvu rohoni kushikamana na imani. Woga wa kukasirisha Mungu ungewazuiza wasirudi nyuma.

Kuona yasiyoonekana kwa macho (11:1-3)

Maneno mawili yanayoonekana zaidi ndani ya sura hizi ni *uvumilivu na imani*. Sura 11 ni juu ya kuona na kuvumilia kwa imani. Tunasoma juu ya wanaume na wanawake wa Agano la Kale waliokuwa na macho makali kwa maneno ya roho na waliovumilia haya na maumivu makubwa bila kukana Bwana wao. Kwa sababu ya imani yao ahadi za Mungu zilikuwa kwao kama maneno yaliyokwisha kutimizwa. Neno hili lilipatisha imani yao nguvu na kuwawezesha kuona maneno yasiyoonekana kwa macho ya watu. Kwa njia ya imani tunaweza kufahamu kuumbwa kwa dunia, ya kwamba iliumbwa na Mungu, na kama vitu duniani vilifanywa na nini.

Imani kwa wakati wa mwanzo (11:4-7)

Kwa njia ya imani Abeli alikaribia Mungu na zabihu. Tunafikili

WAEBRANIA

Mungu alikubali zabihu yake kwa sababu ya damu yake iliyomwangika. Kwa sababu Enoka alipendeza Mungu kwa njia ya kuamini ahadi yake, alipelekwa mbinguni bila kufa. Haiwezekani kupendeza Mungu bila imani. Kwa imani Noa na jamaa yake waliponyeshwa toka garika iliyofunika dunia nzima.

Imani ya Abrahamu (11:8-12)

Abrahamu alionyesha imani yake kwa njia ya kuondokea inchi yake bila kujua pahali alipokwenda, kisha kukaa kama msafiri ndani ya inchi ambayo Mungu alikwisha kumpa. Kwa imani Sara aliweza kupata mimba wakati alipokuwa mwanamke mzee, na hivi Abrahamu aligeuka baba ya mataifa mengi wakati mwili wake ulipokuwa kama mfu.

Inchi ya mbinguni (11:13-16)

Watu hawa wa Mungu wa zamani walikuwa bila kupokea ahadi zote walizopewa, lakini waliamini kabisa ya kwamba ahadi za Mungu zitatinizwa, hivi hawakujaribu kurudi nyuma. Walitazamia makao yao *mbinguni*.

Imani ya watu wakuu wenyewe heshima (11:17-22)

Jaribu kubwa la imani ya Abrahamu lilikuwa kutoa Isaka awe zabihu. Alijua kwamba Mungu aliweza kufufua Isaka toka wafu, kama ikihitajiwa, kwa kutimiza ahadi yake ya kwamba Isaka atakuwa na wazao wengi (mash. 17-19). Hata kwa saa ya kufa, Isaka, Yakobo na Yosefu walikuwa na imani ya nguvu (mash. 20-22).

Imani ya Musa (11:23-28)

Ni kama wazao wa Musa walifahamu kwamba Mungu alikusudi maneno makubwa kwa mtoto wao, wakamficha asiuawe. Musa mwenyewe alikataa heshima, anasa, utajiri, utwala na dini ya Misri na kufungana na watu wa Mungu walioreswa.

Kushinda kwa imani (11:29-35a)

Kwa imani maji ya Bahari Nyekundu yalitengwa, kuta za Yeriko zilibomolewa, na Rahaba pamoja na jamaa yake waliokolewa wasi-haribiwe (mash. 29-31). Kwa imani inchi nyingi zilishindwa, watu walitenda haki, walishinda kwa maneno ya roho, miili yao iliponyeshwa wakati wa hatari, walishinda vitani, na wafu wengine walifufuliwa (mash. 32-35a).

Kushinda taabu kwa njia ya imani (11:35b-40)

Imani iliwezesha waamini wengine kuvumilia kuuawa bila kukana imani yao, kuzihakiwa, kufungwa, kutupiwa mawe, kuvunjwa viungo

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

vyo mwili, kunyanganywa yitu vyao, na kufukuzwa. Walikufa bila kuona kutimia kwa nyingine za ahadi za Mungu, lakini wataona kutimia kwa ahadi zote wakati tutakaponyanyuliwa wote pamoja kukutana na Bwana katika hewa.

Mashindano ya imani (12:1-4)

Mfano wa washuhuda hawa wote wa Agano la Kale ndani ya sura 11 ungepasa kutusukuma kupiga mbio na bidii bila kulegea ndani ya mashindano ya imani na bila kuacha maneno yo yote kutuzuiza, tukitazama Yesu, mfano wetu. Alivumilia hata damu, maana yake mauti — hata mmoja wetu hajafanya hivi bado.

Mapigo ya Bwana (12:5-8)

Mungu anatumia mateso na taabu kufundisha wana na binti zake. Si ye ye anayeleta taabu hizi, lakini anatumika nazo ndani ya maisha ya watu wake. Wana wote wa kweli wanaitwa kuvumilia bila kulegea mapigo ya Bwana.

Wazazi wanaazibu watoto (12:9-11)

Wazazi wa dunia wanafundisha na kuazibu watoto wao kwa ujana wao. Hata wakianguka mara nydingi ndani ya neno hili, watoto wana-jifunza kuheshimu wazazo wao. Zaidi sana ingetupasa sisi kuyenyekeea azabu ya Mungu! Azabu yake ni chungu saa yenyewe, lakini nyuma inazaa faida kubwa.

Kuendelea mbele katika Roho (12:12-14)

Haifai tushindwe na mateso na majaribu, lakini tutumike na maneno haya kutia nguvu mioyo ya wengine wanaojaribiwa kukata tamaa. Saa zote tufuate salama na utakaso.

Onyo juu ya ukafiri (12:15-17)

Onyo la tano ni kwa mtu ye yote katikati ya Wakristo anayepungukia neema ya Mungu, au kuacha shina la uchungu la ukafiri kuchipuka, au anayetenda uasherati, au kuona bule maneno yaliyo na faida kwa roho, kama Esau alivyofanya. Esau aligeuka tena nyuma, lakini saa yake ilikuwa imepita.

Maogopesho ya sheria (12:18-21)

Wale waliojaribiwa kurudi kwa sheria wakumbuke maneno ya kuogopesha yaliyotokea wakati ilipotolewa. Maneno haya yote yalonyesha umbali wa Mungu na watu, na ya kwamba ilikuwa hatari kwa watu kumkaribia. Ni kama alisema nao, “Musifike karibu.”

Kundi la utukufu (12:22-24)

Lakini agano jipyä linasema juu ya ukaribu wa Mungu na ya kwamba anakaribisha watu kwa neema. Kwa imani waamini wana-ingia pahali pa mbingu na kusimama mbele ya majeshi ya malaika, waamini wa kanisa waliokwisha kufa, Mungu, watakatifu wa Agano la Kale, Bwana Yesu, na faida kubwa ya damu yake ambayo ali-imwanga.

Sauti ya Mungu ilitetemeshu mbingu na dunia (12:25-27)

Wale waliosikia sauti ya sheria na kuiasi waliazibiwa. Wale walio-barikiwa kupita watahukumiwa kupita vilevile. Ndani ya Kristo, Mungu alitoa ufunuo wake mzuri zaidi na wa mwisho. Wale wan-aoakataa sauti yake wakati inaposema toka mbinguni sasa wanahukumiwa kupita wale waliovunja sheria. Hawatakuwa na njia kuepuka azabu.

Ufalme usioweza kutetemeshwa (12:28-29)

Waamini wa kweli wana ufalme usioweza kutetemeshwa kamwe. Neno hili lingepasa kuwasukuma kutumikia Mungu na bidii pamoja na heshima na woga.

Maagizo ya mwisho (13:1-6)

Tunaona hapa maneno yanayopasa kuonekana ndani ya maisha ya Wakristo. Kuna maonyo kupenda ndugu, kukaribisha wageni, kusaidia waamini waliofungwa gerezani, kuhurumia watakatifu wanaoteswa, kukaa na usafi katika ndoa, kukaa na furaha na vitu walivyo navyo. Barua hii iliwakumbusha maneno mazuri yote tuliyo nayo ndani ya Kristo. Basi namna gani tutanunganika?

Mafundisho ya mwisho juu ya kuabudu (13:7-17)

Sharti tuheshimu viongozi vyetu kwa maneno ya roho, na kuiga imani yao. Haifai tudanganywe na mafundisho ya kigeni. Sharti tukae mbali kwa Kristo, mzabahu wetu na kwenda kwake inje ya kambi tukichukua laumu yake. Kama makuhani, inatupasa kutoa zabihu za sifa na mali (mash. 7-16). Mwishoni, inatupasa kutii viongozi vyetu, kwa sababu itawapasa kutoa hesabu juu ya hali ya roho zetu kwa maneno ya Mungu. Litakuwa na faida kwetu vilevile kama wataweza kufanya hivi na furaha.

8. MWISHO (13:18-25)

Kwa mwisho wa barua hii nzuri sana mwandishi alisihi wasomaji kumwombea, aliwatolea baraka tamu sana, na kuwasalimu.

Barua ya Yakobo

MWANZO

Tarehe ya Yakobo

Hii ni barua ya Yakobo kwa Wakristo Wayuda waliosambazwa kwa inchi malimbali za dunia ambazo watu walizijua kwa wakati ule. Labda iliandikwa mbele ya barua zote nyingine za Agano Jipya, karibu A.D. 45.

Mafundisho ya Yakobo

Ndani ya barua hii mwandishi anahamakia zambi kama tofauti katikati ya watajiri na wamasikini, kutotawala kwa ulimi, vivu, magomvi, na kuonea watu masikini.

Neno kubwa la Yakobo

Yakobo anaonyesha wazi tofauti katikati ya imani ya kinywa tu na imani inayozaa kazi njema. Anasema “Unionyeshe kazi zako nami nitaamini kwamba una imani ya kweli. Barua hii inakwisha na maonyo kuwa na saburi wakati wa mateso na kucombeana.

UMBO LA YAKOBO

1. Salamu (1:1)
2. Taabu na majoribu (1:2-18)
3. Neno la Mungu (1:19-27)
4. Kupendelea watu (2:1-13)
5. Imani na matendo (2:14-26)
6. Namna gani kutumia ulimi (3:1-12)
7. Akili ya kweli, na ile isiyotoka juu (3:13-18)
8. Choyo, sababu yake, na namna gani kuishinda (Sura 4)
9. Watajiri, na juto lao kwa wakati wa kuja (5:1-6)
10. Maonyo kuvumilia na saburi (5:7-12)
11. Maombi na kuponyeshwa kwa wagonjwa (5:13-20)

1. SALAMU (1:1)

Tunafikili Yakobo alikuwa mmoja wa ndugu za Yesu kwa njia ya mama yake, lakini anajiita mtumwa. Kama tulivyoona mbele, aliandi-ka kwa waamini Wayuda waliosambazwa toka Yudea.

YAKOBO

2. TAABU NA MAJARIBU (1:2-18)

Kupata faida kwa njia ya taabu (1:2-8)

Kwanza Yakobo aliandika juu ya taabu (majaribu) isiyo tunda la zambi, na majaribu kutenda zambi. (Neno hili ‘majaribu’ lina maana mbili ndani ya barua hii: 1) taabu, na 2) majaribu kutenda zambi. Namna hizi mbili zinatafsiriwa majaribu ndani ya barua hii.) Tunaweza kufurahia *taabu*, tukijua itazaa uvumilivu ndani yetu. Tukivumilia hata mwisho, tutageuka Wakristo wenyewe kukomea na kuonyesha kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya maisha yetu (mash. 2-4). Tunahitaji akili kuvumilia taabu, lakini Mungu ni tayari kuitoa kwa wale wanaoomba kwa imani. Wenyewe kusitasita hawataipokea (mash. 5-8).

Taabu ya watajiri na wamasikini (1:9-11)

Taabu ya maisha ya sasa inaweza kuwa na faida kwa watajiri na wamasikini vilevile. Mtu masikini anaweza kufurahi ndani ya utajiri wake wa roho, na mtajiri anaweza kufurahi wakati anapopoteza mali yake, kama akijifunza ya kwamba mali yake na yeze mwenyewe ni kwa wakati tu, na ya kwamba maneno ya roho tu yataendelea milele.

Kuvumilia majaribu (1:12-18)

Mtu anayeshinda ndani ya taabu atapokea taji ya uzima (sh.12). Sasa tunageuka kusoma juu ya *majaribu kufanya zambi*. Majaribu haya hayatoki kwa Mungu, lakini kwa tabia zetu za zamani za zambi. Majaribu haya yanaanza ndani ya nia zetu, yanazaaz zambi, na hata mauti. Mambo mema tu yanatoka kwa Mungu, Baba ya nuru. Yeze ni Baba yetu vilevile, kwa njia ya kuzaliwa tena, naye anataka tuwe watakatifu watakaokuwa mfano mzuri.

3. NENO LA MUNGU (1:19-27)

Tunaweza kuwa malimbuko ya viumbi vyake kwa njia ya: kujitawala kwa maneno tunayosikia na kusema, na kasirani; na kuweka mbali uchafu na uovu wote, kupokea Neno la Mungu na kulitii, kutawala ulimi, kwenda kuangalia yatima na wajane, na kujilinda wenyewe kwa machafu ya dunia.

4. KUPENDELEA WATU (2:1-13)

Ndani ya maisha yetu kama Wakristo haifai tupendelee watu; maana, haifai kukaalisha mtajiri kwa pahali pa heshima, na mtu masikini kwa pahali pa nyuma. Upendeleo namna hii unasahau ya kwamba Mungu amechagua wamasikini, lakini ni desturi ya watajiri

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kutesa na kuonea wamasikini na kutukana jina la Bwana. Amri kubwa zaidi ni kupenda jirani zetu kama sisi wenyewe. Tukipendelea watu tunaasi sheria hii, na ni kama kuasi sheria nzima. Kama tusipokuwa na upendeleo hukumu iliyoweza kutupata itakombolewa na huruma.

5. IMANI NA MATENDO (2:14-26)

Imani pasipo matendo imekufa (2:14-20)

Imani pasipo matendo haina faida kama vilevile masemo ya huruma hayana faida kama matendo ya kusaidia mwenye huzuni yakikosa. Imani namna hii haiwezi kuokoa mtu (mash. 14-17). Mtu anayesema ana imani bila kutenda matendo mema hawezi kuhakikisha imani ile. Imani inaweza kuonkana kwa njia ya maisha yenye kazi njema tu. Kuamini tu kwamba kuna Mungu mmoja hakutoshi. Imani bila matendo haina faida. *Si* kusema kwamba tunaokolewa kwa njia ya kazi njema, au imani *pamoja na* kazi njema, lakini tunaokolewa kwa imani inayozaa maisha ya kazi njema (mash. 18-20).

Abrahamu na Rahaba (2:21-26)

Abrahamu, baba ya waamini, alihesabiwa haki kwa njia ya matendo wakati alipotoa Isaka juu ya mazabahu, lakini alifanya hivi *nyuma ya kuhesabiwa haki kwa imani miaka mingi mbele* (Mwanzo 15:6). Rahaba, kahaba Mkanana. alionyesha ya kwamba aliamini kweli kwa njia ya kupokea wapelelezi. Kama Abrahamu na Rahaba walikosa imani, matendo haya yangalikuwa mabaya — uuaji na maasi, lakini kwa sababu yalikuwa matunda ya imani, yalikuwa kazi njema. Kama mwili aliye na uzima unaonyesha kwamba kuna roho, vivyo hivyo kazi njema zinaonyesha kwamba mwenye kuzitenda ana imani.

6. NAMNA GANI KUTUMIA ULIMI (3:1-12)

Ni neno la lazima kwa Mkristo kutawala masemo yake. Inapasa zaidi walimu kukumbuka neno hili. Mtu yule anayeweza kutiisha ulimi wake anaweza kutawala maneno yote ya maisha yake. Ulimi ni mdogo, kama vile lijamu ya farasi au usukani wa merikebu ni mdogo, lakini unaweza kufanya kazi kubwa, njema au mbaya. Unaweza kuharibu kama moto unavyoharibu mwitu. Inawezekana kutiisha viumbe vya poli, lakini haiwezekani kutiisha ulimi. Ulimi *si* kama chemchemi kwani ulimi unaweza kubariki na kulaani pamoja, lakini chemchemi inaweza kutoa maji namna moja tu, maji yenye chumvi au maji yanayokosa chumvi. *Si* kama mtini unaozaa tini tu, au mzabibu unaozaa zeituni tu. Hakuna kitu kingine kama ulimi kinachowea kuleta mema au mabaya.

YAKOBO

7. AKILI YA KWELI, NA ILE ISIYOTOKA JUU (3:13-18)

Hapa tunaona tofauti katikati ya mwenye akili ya kweli na mwenye akili ya dunia. Mwenye akili ya kweli anaonyesha akili yake kwa njia ya kutembea vizuri pamoja na unyenyekevu. Anaishi maisha safi, anapenda salama, anafikili wengine, ni mnyenyekevu na mwenye rehema na matendo mema, bila upendeleo na pasipo udanganyifu. Mwenye akili ya dunia tu ni mwenye choyo na anajitafutia mwenyewe faida na ukubwa. Yeye ni mkali, mdanganyifu na akili yake ni akili ya Shetani. Pahali gani anapokwenda kuna machafuko na matendo mabaya namna zote.

8. CHOYO, SABABU YAKE, NA NAMNA GANI KUISHINDA (Sura 4)

Neema na unyenyekevu zinashinda mapigano na kiburi (4:1-6)

Kuna matata katikati ya Wakristo wakati wasipoweza kupata maneno wanayotaka. Tunaweka roho sana juu ya kupata vitu bila kuyenyekeea Mungu katika maombi. Au kama tukiomba, tunaomba kwa faida yetu wenyewe (mash. 1-3). Choyo namna hii ni uzini kwa maneno ya roho. Tamaa na choyo hazitoki kwa Roho Mtakatifu. Mungu anawapa wanyenyekevu neema (mash. 4-6).

Maneno mazuri sita ndani ya maisha ya Mkristo (4:7-10)

Matendo sita ya sharti kwa toba ya kweli ni: nyenyekeea Mungu; shindana na Shetani; safisha mikono (maana matendo) na takasa moyo (makusudi); kuwa na huzuni kubwa juu ya zambi; na ujinyenyekeze mbele ya Bwana.

Ubaya wa kusingizia (4:11-12)

Tukisingizia ndugu tunahukumu sheria ambayo inatukataza kufanya hivi, na kunyanganya nafasi ya Mungu kama mwamuzi na mwenye kutoa sheria.

Ubaya wa kujisifu (4:13-17)

Yakobo anahukumu zambi ya kujitegemea mwenyewe na kufanya mashauri bila kukumbuka Mungu ndani yao. Ni lazima kwetu kuyenyekeea Mungu ndani ya mashauri yetu yote. Ni zambi kuishi bila kutafuta kujua mapenzi ya Mungu juu ya maneno yote ya maisha yetu.

9. WATAJIRI, NA KUJUTA KWAO KWA WAKATI WA KUJA (5:1-6)

Ingepasa watajiri kulia na kuomboleza kwa sababu mwishoni watapoteza mali yao yote. Wamejivimbishia mali na kugeuka watajiri

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kwa njia ya kunyima watu wao wa kazi, wametumia mali yao kwa anasa na kujifurahisha kwa tamaa na wametesha wenyehaki kwa kiburi.

10. MAONYO KUVUMILIA NA SABURI (5:7-12)

Inapasa waamini wanaoteswa kuvumilia na saburi kufika kuja kwa Bwana, bila kuwa na mawazo mabaya rohoni mwao juu ya wale ambao wanawatesa. Manabii wa Agano la Kale walivumilia mateso na saburi, na Yobu ni mfano mzuri vilevile wa kuvumilia hivi. “Mwisho wa Bwana” kwa Yobu ulikuwa kwa Mungu kumpa mara mbili kupita aliyokuwa nayo mbele (mash. 7-11). Haifai waamini kutumia jina la Bwana au neno lo lote lingine kuhakikisha kwamba wanasema kweli. Ingepasa kutosha kusema “ndiyo” au “sivyo” (sh.12).

11. MAOMBI NA KUPONYESHWA KWA WAGONJWA (5:13-20)

Msadaa kwa mahitaji fulani (5:13-16)

Inatupasa kukaribia Bwana ndani ya maombi kwa wakati wa taabu, furaha, ugonjwa, au neno lo lote lingine. Vizuri mgonjwa aite wazee wa kanisa na kukiri zambi zo zote zinazoweza kuwa sababu ya ugonjwa wenye. Wazee waombee mgonjwa na kumpakaa na mafutta; halafu ombi la imani (maana yake ombi linalosimama juu ya ahadi ya Mungu kuponyesha mtu huyu) litaponyesha mgonjwa. Ona ya kwamba zambi, ugonjwa, kukiri zambi, maombi, na kuponyeshwa kunafungana pamoja.

Ombi la Elia (5:17-18)

Ombi la Elia lililetua ukosefu wa mvua kwa taifa la Israeli lenye zambi kwa miaka mitatu na nusu. Halafu aliomba tena, na Mungu alituma mvua.

Kurudisha yule anayekwenda mbali na Mungu (5:19-20)

Wakati tunapoombea wenyehaki nyuma, labda tunaweza kuwaponyesha wasife mbele ya wakati kwa sababu ya azabu ya Mungu, na tutaona Mungu akisamehe zambi zao.

Barua ya kwanza ya Petro

MWANZO

Tarehe na wenyе kупokea 1 Petro

Petro aliandika barua hii ya kwanza karibu na A.D. 63. Aliandika kwa Wakristo katika Asia Ndogo waliokuwa wakiteswa sana kwa imani yao.

Habari za 1 Petro

Barua yake ni habari za tumaini. Wakristo wanaweza kuona ngambo ya mateso yao ya wakati ule na kutazamia utukufu. Kufika wakati ule, neema ya Mungu ilitosha kwa mahitaji yao yote. Utajiri wao hauwezi kuharibika — ndiyo damu ya Kristo, Neno la Mungu, na uriti wao kwa wakati wa kuja. Mateso hayawezi kamwe kuwanyanganya baraka hizi.

Mafundisho ya 1 Petro

Kwa sababu hii, mtume alionya watakatifu kusimama imara; kukumbuka ya kwamba mateso yanahitajiwa, lakini ni kwa wakati tu, na kwa kuwasaidia; na ya kwamba vizuri wateswe kwa sababu ya kutenda mema, si kwa zambi zao wenyewe. Waige Kristo na kuishi maisha matakatifu. Kisha Petro alisema nao kama wenyiji, watumwa, waume na wake, na kuonyesha kwamba inawapasa kukumbuka ndani ya mwenendo wao ya kuwa wakati wa mwisho ulikaribia. Kuna maonyo kwa wazee kanisani kuwa waaminifu, na kwa vijana, watii na kunyenyeka.

UMBO LA 1 PETRO

1. Salamu (1:1-2)
2. Pahali pa mapendeleo pa mwamini (1:3-12)
3. Mwenendo wa mwamini kwa sababu ya pahali pake (1:13 – 2:3)
4. Haki ya mwamini ndani ya nyumba na ukuhani mpya (2:4-10)
5. Msafiri Mkristo na dunia (2:11-12)
6. Mwenyeji Mkristo na serikali (2:13-17)
7. Mtumishi Mkristo na bwana wake (2:18-25)
8. Mke Mkristo na mume wake (3:1-6)
9. Mume Mkristo na mke wake (3:7)
10. Mkristo na Wakristo wenzake (3:8)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

11. Mkristo na watesaji wake (3:9 – 4:6)
12. Maneno ya lazima kwa siku za mwisho (4:7-11)
13. Maonyo na maelezo juu ya mateso (4:12-19)
14. Maonyo kwa kanisa (5:1-11)
15. Salamu ya kuagana (5:12-14)

1. SALAMU (1:1-2)

Labda wageni ndani ya shairi 1 walikuwa Wakristo Wayuda wa Usambazo, au Wakristo wa Mataifa waliosambazwa ndani ya wilaya tano za Asia Ndogo kwa sababu ya mateso ya Wakristo. Wao wote walichaguliwa, kutakaswa na kuokolewa.

2. PAHALI PA MAPENDELEO PA MWAMINI (1:3-12)

Uriti wa mbinguni (1:3-9)

Petro anatoa sifa kwa Mungu kwa wokovu wake mkubwa ambao alitupa sisi kwa sababu ya neema yake. Kwa wakati wa sasa tuna tumaini lenye uzima kwa njia ya ufufuko wa Kristo; kwa wakati wa kuja tutakuwa na uriti usioharibika, usio na uchafu, na usiopunguka — tuliokekewa akiba mbinguni, sisi tunaolindwa kwa nguvu ya Mungu (mash. 3-5). Mkristo anaweza kufurahi ndani ya mateso yake, akiua ya kwamba kujaribiwa kwa imani yake ni ya damani na kuzaa sifa na utukufu kwa wakati wa kuja (mash. 6-7). Hatujaona Mwokozi wetu na macho, lakini tunampenda, kumwamini, na kufurahi ndani yake (sh.8). Mwisho wa imani yetu ni wokovu wa nafsi zetu (sh.9).

Unabii juu ya Masiya (1:10-12)

Manabii wa Agano la Kale walifazaika juu ya wokovu huu mku-bwa. Walifazaika kama Masiya alikuwa nani, kama atakuja wakati gani, na namna gani aliweza kuteswa pamoja na kutukuzwa. Wali-jifunza ya kwamba walikuwa wakitabiri maneno haya kwa sisi, si kwa ajili yao wenyewe, ndiyo maneno yaliyofichwa kwa malaika lakini yanayofunuliwa kwetu kwa njia ya mitume.

3. MWENENDO WA MWAMINI KWA SABABU YA PAHALI PAKE (1:13 – 2:3)

Kuishi mbele ya Mungu Baba yetu (1:13-21)

Sharti mwenendo wetu upatane na pahali petu. Inatupasa kuwa wenyewe kiasi na tumaini (sh.13), watakatifu kama yule ambaye alituita ni mtakatifu (mash. 14-16). Tukumbuke ya kwamba Baba ni mwa-muzi asiye na upendeleo, na kuendelea na woga, tukikumbuka ukoo-

1 PETRO

mbozi wetu mkubwa sana. Tukumbuke ya kwamba kwa damu ya Kristo tumeokolewa toka mwenendo usiofaa. Kwa sababu ya Mkombozi wetu wa ajabu, tuna tumaini lisiloweza kutikisika ndani ya Mungu ambaye alimfufua na kumtukuza (mash. 17-21).

Kupendana na bidii (1:22)

Sharti tuwe na nia inayopenda watu wengine, ndilo tunda moja la kuzaliwa tena, na tupendane na bidii na roho moyo.

Kuishi kwa njia ya Neno la Uzima (1:23-25)

Mbegu kwa njia yake tunazaliwa tena ni Neno la Mungu, neno lililo hai na lisiloweza kuharibika. Neno la Mungu si kama watu walio wa wakati tu na mapando yanayokufa mbio, lakini linadumu milele.

Kuweka mbali uovu, na kupenda maziwa ya Neno la Mungu (2:1-3)

Sharti tuweke mbali matendo yote yanayokosa mapendo, na kuwa na hamu kubwa kwa Neno la Mungu, namna mtoto mchanga alivyo na kiu kwa maziwa.

4. HAKI YA MWAMINI NDANI YA NYUMBA NA UKUHANI MPYA (2:4-10)

Baraka waamini walizopewa (2:4-8)

Sasa Petro aligeuka toka maonyo na alisema juu ya baraka ya mwamini ndani ya nyumba mpya ya Mungu na ukuhani mpya wa Mkristo. Ndani ya nyumba ile Kristo ni jiwe lenye uhai. Waamini ni mawe yaliyo hai, nyumba ya roho, na ukuhani mtakatifu (mash. 4-5). Kristo ni jiwe kubwa la pembedi, chaguliwa, lenye heshima na damani, kama iliyotabiriwa ndani ya Maandiko Matakatifu, nasi tunaweza kumwamini kabisa (sh.6). Kwa waamini ye ye ni wa damani kabisa. Hata wasioamini wakimkataa, aliheshimiwa na Mungu kupita wote. Anageuka jiwe la kukwalisha kwa wale wanaoasi na kukataa Habari Njema ya neema ya Mungu.

Baraka za zamani waamini wanazopata tena (2:9-10)

Kwa wakati wa sasa waamini wanafurahi ndani ya baraka nyingine ambazo Waisraeli katika Agano la Kale walipoteza kwa sababu ya kutoamini. Wakristo ni taifa chaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu walio mali ya Mungu mwenyewe. Wameitwa toka giza kuingia nuru watangaze ubora wake. Zamani hawakuwa taifa, lakini sasa wao ni taifa la Mungu, na wamepata rehema waliyokosa mbele (mash. 9-10).

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

5. MSAFIRI MKRISTO NA DUNIA (2:11-12)

Kama wasafiri walio *katika* dunia, lakini si *wa* dunia, inapasa Wakristo kuwa na mwenendo safi na bila laumu unaotukuza Mungu na kunyamazisha wale ambao wanawasingizia.

6. MWENYEJI MKRISTO NA SERIKALI (2:13-17)

Sharti Wakristo watii serikali na kwa njia hii kunyamazisha wale wanaoshindana nao. Waishi katika uhuru lakini bila kutumia uhuru huu kufanya maneno yasiyofaa, na waonyeshe adabu na heshima kwa watu wote.

7. MTUMISHI MKRISTO NA BWANA WAKE (2:18-25)

Inapasa watumishi Wakristo kunyenyeka bwana wao, hata wakiwa bwana wabaya sana. Ukubali wa Mungu ni juu ya wale wanaovumilia na saburi mateso wasiostahili kupata, lakini si juu ya wale wanaostahili kupata azabu. Tunaitwa kuiga Kristo. Yeye alikuwa pasipo zambi na hila, mwenye saburi na huruma, mpole, ambaye alijitoa kama sadaka kwa zambi zetu ili tuweze kuwa wafu kwa maneno ya zambi na kuishi kwa maneno ya haki. Sisi tulipotea mbele kama ko ndoo tumerudia Mchungaji na Mwangalizi wetu sasa.

8. MKE MKRISTO NA MUME WAKE (3:1-6)

Wake Wakristo wanaagizwa kunyenyeka waume wao. Kama mume ni msiyeamini, ingepasa mwenendo wa mke kuwa mzuri sana hata anaweza kuvuta bwana wake bila kusema neno (mash. 1-2). Haifai aweke roho zaidi juu ya kupamba mwili wake, lakini juu ya mapambo ya roho yasiyoharibika na yanayopendeza Mungu (mash. 3-4). Sara alijipamba na roho ya kunyenyeka, na wake kwa wakati wa sasa wanaweza kumwiga kwa njia ya kutenda haki bila woga (mash. 5-6).

9. MUME MKRISTO NA MKE WAKE (3:7)

Sharti mume Mkristo akae na mke wake na akili na kumheshimu, akikumbuka kwamba mke wake ni zaifu kupita mwilini, na ya kwa mba ye ye na mke wake ni wariti pamoja wa neema ya uzima. Pamoja wamepewa uwezo wa kuleta uzima mpya duniani, ndilo neno kubwa sana. Kama wakifikiliana na kusaidiana bila kujifikili wenywewe, wata-pata majibu kwa maombi yao.

10. MKRISTO NA WAKRISTO WENZAKE (3:8)

Ndani ya makusanyiko ya Wakristo, sharti wao wote wawe na umoja, hurumu, mapendo ya ndugu, rehema na adabu.

11. MKRISTO NA WATESAJI WAKE (3:9 – 4:6)

Kuteswa kwa sababu ya kutenda mema au mabaya (3:9-16)

Sasa Petro anafundisha juu ya Mkristo na wale ambao wanamtesa. Haifai ajilipize kisasi lakipa mabaya kwa mema, na kuriti baraka zinazoahidiwa ndani ya Zaburi 34. Si desturi kwa watu kuumiza mwenye haki. Lakini hata Mkristo akipata mateso asiyostahili kupata, ni baraka kwake. Inampasa kutenda bila woga, kutakasa Kristo kuwa Bwana moyoni mwake, kukaa tayari kujibu maulizo juu ya imani yake, na kuwa na zamiri safi.

Mateso ya Kristo kwa ajili yetu (3:17-22)

Ni wazi ya kwamba kuteswa kwa kutenda mema ni vizuri kupita kuteswa kwa kutenda mabaya. Kristo ni mfano wetu tena. Aliteswa, mwenye haki kwa wazalimu, ili atulete kwa Mungu. Kwa njia ya Roho Mtakatifu ambaye alimfufua toka wafu, alihubiri kwa wasioamini kwa wakati wa Noa, ndio watu walio katika kifungo sasa. Watu wanane tu waliokolewa kwa wakati ule, waume wane na wake wao. Ubatizo hautusafishi toka uchafu wa mwili, lakini unasafisha zamiri yetu mbele ya Mungu kwani tunajua kabisa ya kwamba maneno ya zambi zetu yametengenezwa kwa sababu ya ufufuko na kutukuzwa kwa Kristo.

Mateso yetu kwa ajili ya Kristo (4:1-6)

Kristo alipata mateso asiyostahili kupata, na inatupasa sisi kuwa tayari kuteswa vivyo hivyo. Wakati tunapochagua kupata mateso kwa pahali pa kutenda zambi, zambi haina uwezo ndani ya maisha yetu tena. Hatutawaliwi tena na anasa, lakini na mapenzi ya Mungu. Tulifanya zambi kama uasherati, ulevi, na ulafi za kutosha mbele. Sasa, wakati tusiposhiriki ndani ya zambi hizi tena watu wa dunia wanatusingizia. Watatoa hesabu kwa Mungu juu ya neno hili nasi tutasibitishwa kuwa wenye haki. Kwa sababu hii Habari Njema ilihubiriwa kwa waamini wale walioneswa na kuuawa nyuma. Watu waliwaua lakini walisibitishwa na Mungu kuwa haki, na sasa wanafurahi katika uzima wa milele pamoa naye.

12. MANENO YA LAZIMA KWA SIKU ZA MWISHO (4:7-11)

Mashairi haya yanaanza na “maneno yote ni karibu”, na yanaendelea na maonyo juu ya maneno mbalimbali. Sharti tuweke roho juu ya maombi; tupendane na kukaribishana bila kunungunika, na kutumikia Mungu bila kujifikili mwenyewe. Maneno yote yafanywe kwa utukufu wa Mungu.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

13. MAONYO NA MAELEZO JUU YA MATESO (4:12-19)

Haifai waamini kushangaa wakati wanapoteswa na kupata taabu kwani maneno haya ni ya kawaida tu. Wakati wanaposhiriki katika mateso ya Kristo, wanaweza kujua hakika ya kwamba siku nyingine watashiriki katika utukufu wake vilevile, na wanafarijiwa kwa sababu Roho Mtakatifu ya Mungu anakaa juu yao. Ni haya kwa mwamini kuteswa kwa zambi zake mwenyewe, lakini ni heshima kupata mateso kwa sababu yeche ni Mkristo, na anapata njia ya kutukuza Mungu ndani ya matedo haya. Bwana atahukumu watu wake kwanza; atahukumu dunia nyuma. Kama waamini wakiteswa sasa, matedo ya wasioamini yatakuwa makubwa zaidi na kwa milele. Hivi inapasa Wakristo wanaoteswa kutenda yaliyo haki na kukaa kuamini Mwumba wao mwaminifu.

14. MAONYO KWA KANISA (5:1-11)

Maonyo kwa wazee (5:1-4)

Petro anaonya wazee wenzake kulinda kundi la Mungu kwa kutaka kwao wenyewe, si na hamu ya kujipatia mali kwa njia ya kazi hii. Inawapasa kuongoza waamini, si kuwasukuma. Watapokea zawabu, ndiyo taji ya utukufu isiyoharibika.

Maonyo kwa kundi (5:5-11)

Inapasa waamini vijana kunyenyekrea wazee wao. Sharti sisi sote tuwe wanyenyekemu na kukaa bila masumbuko na woga. Lazima tushindane na Shetani na kukumbuka ya kwamba utukufu wa milele utafuata matedo ya wakati wa sasa.

15. SALAMU YA KUAGANA (5:12-14)

Mtume Petro aliandikisha Silvano barua hii, na kushuhudia ya kwamba imani ya kikristo ndiyo imani ya kweli na kuwaonya kusimama imara ndani yake. Alimaliza barua hii na salamu ya mapendo na neema.

Barua ya pili ya Petro

MWANZO

Habari za 2 Petro

Barua ya pili ya Petro, kama 2 Tessalonika na 2 Timoteo inasema juu ya hali ya kanisa kwa siku za mwisho wakati jamii ya Wakristo inapokwisha kuwa ovu. Petro anasihi Wakristo kuendelea kukomea katika maneno yale ambayo yanapaswa kuonekana ndani ya maisha ya Wakristo, wakijua ya kwamba ufalme wa Bwana utafuata, nao waki-tenda maneno haya wataingia ndani yake.

Aliwaonya juu ya walimu wa uwongo watakaodanganya watu wengi mbele ya kuhukumiwa wao wenyewe. Alisema juu ya wenyewe kuzihaki watakaokana kweli ya kuja kwa pili kwa Kristo. Alisibitisha tena kuja kwa Kristo na hukumu ya dunia, na alionya waamini kuwa na bidii, utakatifu, kudumu na kupata nguvu katika neema wakikumbuka ya kwamba Kristo atakuja tena.

Tarehe ya 2 Petro

Petro aliandika barua hii kwa A.D. 66 au 67.

UMBO LA 2 PETRO

1. Salamu (1:1-2)
2. Wakristo wanaitwa kukomea ndani ya mambo mema yanayopaswa kuonekana ndani ya maisha yao (1:3-21)
3. Habari juu ya kuonekana kwa walimu wa uwongo (Sura 2)
4. Habari juu ya kuonekana kwa wenyewe kuzihaki (Sura 3)

1. SALAMU (1:1-2)

Petro alichagua yeye mwenyewe kuwa mtumwa na aliiwtwa na Mungu kuwa mtume. Aliandika kwa watu wote wenyewe imani ambayo mitume walikuwa nayo katika haki ya Bwana, na alituma neema na salama kwao.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

2. WAKRISTO WANAITWA KUKOMEA NDANI YA MAMBO MEMA YANAYOPASWA KUONEKANA NDANI YA MAISHA YAO (1:3-21)

Kukomea na kuzaa matunda katika imani (1:3-11)

Tunaweza kuishi maisha ya utawa kwa sababu ya uwezo na ahadi za Mungu. Sharti tuweke roho ili maneno haya mane yaonekane ndani ya maisha yetu: imani, wema, kujua, kiasi, saburi, utawa, mapendo ya ndugu, na mapendo (mash. 3-7). Tukifanya hivi, hatutakuwa kama vipofu wanaoona vitu vilivyo karibu tu, wala wavivu, lakini tutazaa matunda kwa Bwana. Tunaingia ufalme wa Mungu kwa njia ya kuzaliwa tena, lakini tutapewa tele kuingia ndani yake kama maneno haya mema yakionekana ndani ya maisha yetu (mash. 8-11).

Mauti ya Petro ilikaribia (1:12-15)

Petro aliweka roho sana juu ya kukumbusha Wakristo maneno haya kwani alijua ya kwamba atakufa nyuma kidogo. Aliandika maneno haya ili watu wa Mungu waweze kujikumbusha tena na tena maneno yale Mungu anayotafuta ndani ya maisha yao.

Kuja kwa Kristo kulikaribia (1:16-21)

Halafu Petro alisema ya kwamba bila shaka Bwana atakuja na utukufu. Maneno yaliyotokea juu ya mlima wakati Bwana Yesu alipoonekana kwa Petro, Yakobo na Yoane yalikuwa kama malimbuko ya kuja kwake mara ya pili, na ya ufalme wake wa utukufu. Ushuhuda wa Petro ulisimama juu ya maneno aliyoona, na kusikia. Kubadilishwa sura kwa Kristo kuliyaninisha unabii ndani ya Agano la Kale juu ya kuja kwake mara ya pili. Unabii huu haukuletwa kwa mapenzi ya watu tu au kuelezwa nao, lakini watu walisema yaliyotoka kwa Mungu tu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

3. HABARI JUU YA KUONEKANA KWA WALIMU WA UWONGO (Sura 2)

Mafundisho ya uharibifu na hila (2:1-3)

Mtume alitabiri ya kwamba bila shaka walimu hawa wa uwongo watakuja. Alionyesha hila yao, ya kwamba watasingizia kweli, watakuwa wenye choyo, wakidanganya watu kwa kujipatia wenyewe faida, na ya kwamba uharibifu wao ulikaribia.

Uharibifu wa walimu wa uwongo (2:4-10b)

Katika Agano la Kale, Mungu alihukumu wakafiri namna tatu: malaika walioanguka kwa zambi, watu walioishi mbele ya garika, na watu wa Sodomo na Gomora. Anaweza kuokoa watawa katika

2 PETRO

majaribu na kuweka wasio haki katika hali ya azabu hata siku ya hukumu, zaidi wale wanaoishi kwa tamaa ya mwili na waasi.

Uovu wa walimu wa uwongo (2:10c-22)

Walimu wa uwongo ni wenye kiburi, wasio na akili, na wataharibiwa. Wanafanya karamu za ulevi na ulafi, wanafanya uzini na anasa, nao ni wenye choyo kama nabii Balama (10c-16). Hawatimizi ahadi zao kwa wafuata wao, basi wamewekewa akiba weusi wa giza kwa milele. Na masemo yao ya kiburi wanakokota watu kuwafuata, wanawabembelea katika tamaa za mwili na kuwaahidi uhuru, lakini wanawageuzea kuwa watumwa wa uovu wenye hali mbaya kupita mbele. Ingalkuwa heri kwa watu wale kama wasingalijua njia ya haki, kuliko kuijua na kuiacha kurudi tena kwa uchafu wa dunia, kama mbwa anayerudia matapiko yake, na nguruwe kugaagaa ndani ya matope.

4. HABARI JUU YA KUONEKANA KWA WENYE KUZIHAKI (Sura 3)

Waamini wakae kukumbuka maneno ya manabii na mitume (3:1-2)

Ndani ya barua hii ya pili Petro alionya wasomaji wake kukumbuka maandiko ya Agano la Kale, na maagizo ya Agano Jipyा.

Wongo za wenze kuzihaki (3:3-7)

Wasomaji wake wajue ya kwamba wenze kuzihaki watakuja kwa siku za mwisho, wenze kufuata tamaa zao, watakaosema haiwezekani kwa Kristo kuja mara ya pili. Watafundisha ya kwamba Mungu hajitii kamwe ndani ya maneno ya watu, wakikataa kukumbuka garika ili-yoharibu dunia wakati wa Noa, na bila kukumuka ya kwamba siku nyingine dunia itaharibiwa kwa moto.

Uvumilivu wa Bwana (3:8-10)

Waamini wakumbuke ya kwamba Bwana hafungwi na saa, ya kwamba yeze ni mwaminifu na atatimiza ahadi yake, na ya kwamba anakawa kwanza kusudi watu waweze kutubu. Mwandishi alifikili hapa juu ya mwisho wa wakati wa Bwana, saa nyota na hewa na dunia zitakopoharibiwa kwa moto.

Kutazamia kuja kwa siku ya Bwana (3:11-18a)

Kwa wakati wa sasa, inapasa watu wa Mungu kutembea katika utakatifu na utawa, wakitazamia siku ya Mungu, maana mbingu na dunia mpya kwa wakati wa milele. Wakae na salama, usafi, na wafahamu ya kwamba Mungu anakawa kwanza kusudi watu waweze

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kuokolewa. Paulo vilevile alifundisha ya kwamba saburi ya Mungu inaleta njia kwa watu kuokolewa. Paulo alifundisha kweli nyingi nyingine zilizo nguvu kufahamu. Watu wajinga na wasiosimama imara wanageuza kweli hizi kwa uharibifu wao wenyewe. Sharti waamini wakae na ange kwa maneno haya. Njia ya kuepuka mafundisho ya uwongo ni kupata nguvu katika neema na kujua Bwana Yesu.

Sifa kwa Bwana (3:18b)

Masemo ya mwisho ya barua hii yanaleta sifa kwa Mwokozi kwa wakati wa sasa na kwa milele.

Barua ya kwanza ya Yoane

MWANZO

Sababu kwa kuandika kwa I Yoane

Sababu moja kwa kuandika barua hii ilikuwa kuonyesha ubaya wa mafundisho yaliyoitwa Gnosticisme. Mafundisho haya yalikana ya kwamba Bwana Yesu Kristo ni kweli mtu na Mungu. Wale walioeneza maneno haya walifikili walijua maneno kupita wengine, wakafundisha ya kwamba Kristo alikuwa kitokacho kwa Mungu aliyejukaa juu ya Yesu wakati alipobatizwa na kumwondokea shambani mwa Getesemane. Maana ya mafundisho yao ni ya kwamba Yesu hakuwa Kristo, na yule aliyekufa alikuwa Yesu, si “Kristo”.

Alama za ushirika wa kweli

Kwa kuonyesha tofauti katikati ya waamini wa kweli na walimu hawa wa uwongo, Yoane anataja alama nydingine zinazoonyesha kwamba mtu ana uzima wa Mungu kweli. Alama hizi ni kutii, mape-ndo, haki, mafundisho mazuri, kudumu katika ushirika wa Wakristo, na kujitenga na dunia. Wale tu walio na alama hizi wanaweza kuwa na ushirika wa kweli ndani ya jamaa ya Mungu.

Mafundisho makubwa ya I Yoane

Ni nguvu kuandika umbo la mafundisho haya kwa sababu mwendishi anatoa sehemu ya mafundisho juu ya neno fulani ndani ya sura moja na kuongeza juu yake ndani ya sura nydingine. Labda neno hili linaonyesha ya kwamba sharti alama za uzima wa kweli zionekane ndani ya kila sehemu ya mwenendo na matendo yetu.

Tarehe ya I Yoane

Tunafikili Yoane aliandika barua hii ndani ya muda wa A.D 90 na 95.

UMBO LA 1 YOANE

1. Mwanzo wa maneno: Ushirika wa Wakristo (1:1-4)
2. Namna gani kudumisha ushirika (1:5 – 2:2)
3. Alama za wale walio ndani ya ushirika wa Wakristo: Utii, mape-ndo (2:3-11)
4. Kupata nguvu katika ushirika (2:12-14)
5. Hatari namna mbili kwa ushirika huu: Dunia, na walimu wa uwongo (2:15-28)

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

6. Alama za wale walio ndani ya ushirika wa Wakristo (endeleo):
Haki, mapendo, na tumaini kwa njia yake (2:29 – 3:24)
7. Ni lazima kutambua yaliyo kweli na yaliyo mafundisho ya uwongo
(4:1-6)
8. Alama za wale walio ndani ya ushirika wa Wakristo (endeleo):
(4:7 – 5:20)
9. Maonyo ya mwisho (5:21)

1. MWANZO WA MANENO: Ushirika wa Wakristo (1:1-4)

Ushirika wa Wakristo unasimama juu ya Yesu Kristo. Yoane anaonyesha ya kwamba yeze ni wa milele na aligeuka Mtu ambaye watu waliweza kusikia, kuona, kutazama na kugusa. Waamini waliweza kuamini ushuhuda wa mitume, ndio ushuhuda wa kusadikiwa juu ya Kristo (mash. 1-3a). Furaha yao itatimizwa kwa njia ya kuwa na ushirika na Baba, Mwana wake na waamini wenzao (mash. 3b-4).

2. NAMNA GANI KUDUMISHA USHIRIKA (1:5 – 2:2)

Kukiri zambi (1:5-10)

Mtu akitaka kuwa na ushirika na Mungu inampasa kutembea katika nuru, si giza. Inampasa kukubali kweli juu yake mwenyewe vilevile — ya kwamba yeze ni mwenye zambi na amefanya zambi.

Mwombezi kwa zambi (2:1-2)

Neno Mungu analotaka kabisa ni kwa waamini kutofanya zambi. Lakini kama wakianguka hata hivi, njia imetayarishwa kwa usamehe wao; Kristo ndiye Mwombezi na Kipatanisho.

3. ALAMA ZA WALE WALIO NDANI YA USHIRIKA WA WAKRISTO: UTII, MAPENDO (2:3-11)

Pimo la utii (2:3-6)

Pimo la utii wa Wakristo lina sehemu tatu: kutii maagizo yake, kushika Neno lake, na kutembea kama yeze alivyotembea. Tunangozwa na Neno lake lililoandikwa, mapenzi yake ambayo tunaya-jua, na mwenendo wake mwema sana.

Pimo la mapendo (2:7-11)

Nyuma ya pimo la utii ni pimo la mapendo kwa ndugu. Hili ndilo amri iliyo ya zamani nayo ni mpya vilevile. Ni ya zamani kwa sababu Yesu aliifundisha na kuonyesha mapendo haya ndani ya maisha yake tangu zamani; na ni mpya kwa sababu sasa yanaonekana ndani ya

1 YOANE

wafuata wake. Mapendo ni alama ya hakika ya waamini wa kweli. Kuchukia ni alama ya wale walio katika giza la zambi.

4. KUPATA NGUVU KATIKA USHIRIKA (2:12-14)

Tunapata nguvu polepole katika ushirika wa Wakristo (watoto wadogo, vijana, baba) kwa kipimo tunachofahamu na kufurahia Baba na Mwana na kuingia ndani ya vita ya imani.

5. HATARI MBILI KWA USHIRIKA: DUNIA NA WALIMU WA UWONGO (2:15-28)

Hatari ya kupenda mambo na anasa ya dunia (2:15-17)

Haiwezekani kupenda dunia pamoja na kupenda Baba. Mapendo kwa dunia ni mapendo kwa vitu na mambo yasiyodumu. Wenye kutii mapenzi ya Mungu watapata zawabu ya kudumu milele.

Hatari ya walimu wa uwongo (2:18-28)

Walimu wa uwongo wana roho ya mpinga Kristo. Kwa njia ya kutoka katika ushirika wa Wakristo wanaonyesha ya kwamba hawakuzaliwa tena kweli. Waamini wa kweli wanawezeshwa na Roho Mtakatifu kujua kweli (sh.20). Kwa njia ya kukiri ya kwamba Yesu ni Kristo wanaonyesha ya kwamba wamezaliwa tena kweli. Wale wanaosema ya kuwa Yesu na Kristo ni mbalimbali ni wawongo na wapinga Kristo na Mungu si Baba yao (mash. 21-23). Mafundisho ya Neno la Mungu Wakristo waliyosikia yanawalinda wasidanganywe na mafundisho ya uwongo; sharti wapime kila kitu na maneno Biblia inayosema (mash.24-25). Haifai Wakristo washawishwi na walimu wanaosema wanaojua maneno mengine kupita Biblia au yenyе faida kupita Biblia. Roho Mtakatifu anaongoza watu wake ndani ya kweli ya Neno la Mungu, nao hawahitaji walimu wanaofundisha maneno zaidi ya Biblia (mash. 26-27). Yoane anaonya watoto wake wapendwa kukaa ndani ya Kristo ili wakati Mwokozi atakaporudi, yeye na mitume wengine wawe na uhodari, si haya (sh.28).

6. ALAMA ZA WALE WALIO NDANI YA USHIRIKA WA WAKRISTO (endeleo): HAKI, MAPENDO NA TUMAINI (2:29 – 3:24)

Haki (2:29 – 3:10a)

Pimo lingine ni haki. Wale waliozaliwa tena kweli wanaonyesha neno hili kwa njia ya matendo ya haki (sh.29). Ni kweli ya kwamba waamini ni watoto wa Mungu, hata kama watu wa dunia hawatambui neno hili. Hatujui kama tutakuwa namna gani, lakini tunajua ya

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kwamba kwa njia ya roho tutafanana na Bwana Yesu. Kweli hii inatusukuma kuishi maisha matakatifu (mash. 1-3). Wakristo hawakai kutenda zambi kwani kufanya hivi hakupatani na mapenzi ya Mungu na kusudi la kuja kwa Kristo; hakupatani na tabia ya Kristo na umoja wao naye (mash. 4-6). Watoto wa Mungu wanakaa kutenda haki, lakin ni watoto wa Shetani wanatenda zambi. Kusudi la kuja kwa kwanza kwa Kristo lilikuwa kuharibu kazi za Shetani. Haiwezekani kwa watoto wa Mungu kuwa na desturi ya kufanya zambi. Wao ni mbali na watoto wa Shetani kwa njia ya kukaa kutenda haki (mash. 7-10a).

Pimo la mapendo (3:10b-24a)

Sasa tunasoma juu ya pimo la mapendo tena. Mapendo ni amri toka Mungu tangu mwanzo. Kaina alikuwa mtu wa kwanza aliyeasi amri hii, na watu wa dunia wanamwiga kwa njia ya kuchukia wenyewe haki. Mapendo yetu kwa ndugu zetu Wakristo yanahakikisha ya kwamba tumeppita toka mauti na kuingia uzima. Kuchukia ni uuaji, na hakuna mwuaji aliye na uzima wa milele. Mfano mkubwa kupita yote ya mapendo ni yale ya Kristo wakati alipojitoa kwa ajili yetu. Sisi tunaweza kuwa na mapendo kwa njia ya kutoa uzima wetu kwa ajili ya ndugu na kuwasaidia na vitu wanavyohitaji. Matendo namna hii yatahakikisha kwamba mapendo yetu ni mapendo ya kweli nayo ni hai, nayo yanatupa uhodari na imani katika maombi vilevile. Tukiwa na imani na mapendo kwa ndugu zetu tutakuwa na dhamiri safi na tumaini ya kwamba tutapokea kwa Mungu maneno tunayoomba.

Matumaini (3:24b)

Wakati tunaposhika amri za Bwana, tunajua ya kwamba anakaa ndani yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu ambaye alitupa sisi.

7. NI LAZIMA KUTAMBUA YALIYO KWELI NA YALIYO MAFUNDISHO YA UWONGO (4:1-6)

Sasa tutasoma tena juu ya pimo la mafundisho. Walimu wa kweli wanakiri ya kwamba Yesu ni Kristo akionekana katika mwili. Walimu wa uwongo wana roho ya mpinga Kristo; wanakataa kweli ya kwamba Kristo alitwaa utu (mash. 1-3). Tunaweza kuwashinda kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Wapinga Kristo wanatoka duniani na wanapata amri yao toka dunia na watu wa dunia wanawasilika. Waamini wa kweli wanakubali mafundisho ya mitume (mash. 4-6).

8. ALAMA ZA WALE WALIO NDANI YA USHIRIKA WA WAKRISTO (ENDELEO) (4:7 – 5:20)

Mapendo (4:7-21)

Tunarudi tena kwa mapendo. Ni agizo linalolingana na namna

1 YOANE

Mungu alivyo na linahakikisha ya kwamba tumezaliwa tena. Mapendo ya Mungu ni tangu zamani, sasa na kwa wakati wa kuja. Zamani alitoa Mwana wake kwa sisi. Kwa wakati wa sasa, anakaa ndani yetu. Kwa wakati wa kuja mapendo yake yatatupa sisi uhodari siku ya hukumu. Mapendo yake kwasi yanaamsha mapendo ndani yetu yana-yohakikishwa na mapendo yetu kwa ndugu. Kama tukipenda Mungu, ni lazima kwa sisi kupenda ndugu zetu vilevile.

Mafundisho ya hakika (5:1a)

Mafundisho mazuri yanatajwa tena.

Yanazaaz mapendo na utii (5:1b-3)

Matunda mane ya kuamini Yesu ni Kristo ndiyo kuzaliwa tena, mapendo kwa Mungu, mapendo kwa waamini wenzetu, na utii kwa maagizo ya Mungu.

Imani (5:4-5)

Kwa njia ya imani waamini wanaweza kutazama mbali kupita maneno yanayoonekana kwa macho, mbali kupita maneno ya sasa kwa maneno yasiyoonekana lakin yaliyo ya milele. Msingi wa imani ya kweli ni ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

Mafundisho ya hakika (5:6-12)

Kazi ya Kristo katikati ya watu ilianza na ubatizo wake (maji) na mwisho wake ulikuwa kufa kwake msalabani kwa zambi (damu) — si ubatizo tu kama walimu wale wa uwongo walivyofundisha, lakin ubatizo *na* msalaba. Roho Mtakatifu anashuhudia kweli hii kila mara (sh.6). Washuhuda watatu wanaoshuhudia kweli juu ya Bwana Yesu Kristo na kazi yake ni Roho Mtakatifu, ubatizo wa Yesu saa Mungu alipomkubali wazi mbele ya watu, na damu aliyomwanga juu ya msalaba. Kuamini maneno Mungu anayosema juu ya Mwana wake kunaleta uzima wa milele; kama tusipoamini ni kama tunasema yeze ni mwongo. Wokovu ni ndani ya Kristo. Wale wasio na Mwana wa Mungu hawana uzima (mash. 8-12).

Kujua hakika kwa njia ya Neno (5:13)

Wale wanaoamini Kristo wanaweza *kujua* kabisa kwa njia ya amri ya Neno la Mungu ya kwamba wameokolewa.

Ujasiri katika maombi (5:14-17)

Mwamini ana ujasiri ndani ya maombi yanayopatana na mapenzi ya Mungu. Mkristo akirudi nyuma anaweza kurudishwa karibu na Bwana kwa njia ya maombi ya ndugu zake. Alifanya zambi “isiyo ya mauti.” Lakini mtu anayekana kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu,

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

kama walimu wale wa uwongo, amefanya “zambi iliyio ya mauti,” na hatuagizwi kuombea mtu namna hii.

Maneno ya Roho tunayojua (5:18-20)

Yoane anamaliza barua yake na kweli kubwa za imani ya Wakristo. Wakristo hawakai kufanya zambi kwa sababu Kristo anawalinda, yule mwovu asiwaguse. Waamini ni wa Mungu, lakini dunia isiyojua Mungu inakaa katika yule mwovu. Mwana wa Mungu amekuja na kutufunulia Mungu. Sisi ni ndani yake, Mungu wa kweli, na inatupasa kukataa mawazo yote mengine juu ya Mungu.

9. MAONYO YA MWISHO (5:21)

Tukifanya hivi tutajilinda kwa sanamu.

Barua ya pili ya Yoane

MWANZO

Mwandishi na sababu ya 2 Yoane

Tunafikili mtume Yoane, “mzee” aliyejulikana sana, aliandika barua hii karibu na mwisho wa maisha yake, ndiyo karibu na A.D. 85-90, na ya kwamba aliiandika toka Efeso kwa mwanamke Mkristo na watoto wake. Walimu wengine wanafikili “mama” na “watoto” wake ni kanisa la pahali fulani na waamini ndani yake kwani mwendishi hakutaja jina la “mama” yule.

Mafundisho makubwa ya barua hii ni ya kwamba haifai waamini kupokea mtu ye yote asiyeshika mafundisho ya Kristo — kwamba ye ye ni Mungu kabisa na alikuja katika mwili, Mtu mkamilifu bila zambi.

UMBO LA 2 YOANE

1. Salamu (mash. 1-3)
2. Furaha ya mtume — watoto wanaotii (sh.4)
3. Agizo la mtume — watembee katika mapendo (mash. 5-6)
4. Mzigo wa mtume — walimu wa uwongo (mash. 7-11)
5. Tumaini la mtume — kuwafikia ye ye mwenyewe (mash. 12-13)

1. SALAMU (mash. 1-3)

Yoane aliandika kwa mama Mkristo na watoto wake akisema zaidi juu ya ukubwa wa kweli na mapendo ndani ya mwenendo wa Wakristo.

2. FURAHA YA MTUME – WATOTO WANAOOTII (sh.4)

Nyuma ya kuwasalimu, namna ilivyokuwa desturi, alisema juu ya furaha yake kuona ya kwamba maisha ya watoto wa mama huyu yali-patana na kweli ya neno la Mungu. Ona ya kwamba haifai *kuamini* tu kweli — sharti mwenendo upatane na kweli. Inapasa maisha yetu kushuhudia kweli.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

3. AGIZO LA MTUME — WATEMBEE KATIKA MAPENDO (mash. 5-6)

Anaonya mama kupenda Wakristo wenzake, na kutii maagizo ya Bwana ndani ya mwenendo wake.

4. MZIGO WA MTUME — WALIMU WA UWONGO (mash. 7-11)

Lakini sharti akae na ange kwa sababu ya walimu wa uwongo wanaokana kweli juu ya Bwana Yesu aliye Mungu na aliyekuja katika mwili. Kama mama na jamaa yake wakisimama imara katika kweli hii, kazi ya mitume haitakuwa bule, na jamaa yenyewe watapewa zawabu. Wadanganyi na wapinga Kristo wanaongeza juu ya maneno yanayoandikwa ndani ya Biblia na wanasema kwamba walifunuliwa maneno mengine mazuri kupita ufunuo wa Biblia. Hii ni desturi ya dini za uwongo: zinasimama juu ya Biblia *pamoja na* kitabu au mafundisho mengine. Haifai mama kupokea walimu wa namna hii nyumbani mwake asiwasimamie kwa pahali pa kusimamia Mwokozi. Kusimama upande wa walimu wa uwongo ni kukana Kristo.

5. TUMAINI LA MTUME — KUWAFIKIA YEYE MWENYEWE (mash. 12-13)

Yoane angependa kuandika maneno mengi mengine, lakini alitumaini kuwafikia nyuma kidogo, na halafu wao wote watajazwa furaha. Hivi anamaliza barua hii na salama toka watoto wa ndugu yake aliyechaguliwa.

Barua ya tatu ya Yoane

MWANZO

Mwanzo na sababu ya 3 Yoane

Tunafikili ya kwamba Yoane aliandika barua hii toka Efeso, kama 2 Yoane, lakini aliiandika kwa Mkristo mpendwa mmoja, jina lake Gayo.

Ndani ya 2 Yoane mtume alikataza msomaji wake kupokea walimu wa uwongo. Ndani ya 3 Yoane kuna maonyo kupokea wahubiri wanaosafiri kutangaza Habari Njema. Vilevile Yoane alilaumu na nguvu Diotrefe kwa namna alivyotawala kanisa. Na alisifu Demetrio aliyesuhudiwa na kweli ya Mungu na kusifiwa na watu wote. Tunafikili Yoane aliandika barua hii wakati alipokwisha kuwa mzee, karibu na A.D. 85-90.

UMBO LA 3 YOANE

1. Gayo, mtawa (mash. 1-8)
2. Diotrefe, mtawala (mash. 9-11)
3. Demetrio, mwenye tabia nzuri (sh. 12)
4. Shauri na baraka ya Yoane (mash. 13-14)

1. GAYO, MTAWA (mash. 1-8)

Mwenye afya njema katika roho (mash. 1-4)

Gayo alikuwa ndugu mpendwa mwenye afya njema katika roho lakini si katika mwili. Yoane alifurahi sana wakati alipoona watu walioamini Kristo kwa sababu ya ushuhuda wake, kama Gayo, wakitembea na kudumu katika imani na kweli.

Mkaribishaji wageni na ukarimu (mash. 5-8)

Gayo alikuwa mwaminifu ndani ya kazi ya kupokea wageni; mlanga wake ulikuwa wazi saa zote kupokea watumishi wa Mungu. Kwa njia ya kukaa kusaidia wale waliotegemea Bwana tu kwa mahitaji yao

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

alisaidia kweli ya Mungu kuendelea mbele.

2. DIOTREFE, MTAWALA (mash. 9-11)

Halafu mtume alilaumu Diotrefe, mwenye kupiga ubwana, ali-yejikuwa mtawala kabisa kanisani. Mzalimu huyu alikuwa amekamata barua Yoane aliyoadika kwa kanisa, alimshitaki juu ya maneno yasiyokuwa kweli, alikataa kupokea ndugu watawa, na aliondoshya kanisani Wakristo wale ambao waliwapokea. Lilikuwa shauri la Yoane kumhukumu wakati atakapofikia kanisa lile tena. Kufika wakati ule vizuri Gayo aige yaliyo mema, si mabaya. Wale wanaoatenda mabaya hawajui Mungu.

3. DEMETRIO, MWENYE TABIA NZURI (sh.12)

Demetrio alikuwa namna nyingine na Diotrefe. Alikuwa na ushuhuda mwema kwa maneno ya kweli. Alishuhudia kweli, na neno lililokuwa zuri zaidi ndilo: kweli ilimshuhudia yeche.

4. SHAURI NA BARAKA YA YOANE (mash. 13-14)

Mara hii vilevile Yoane aliacha kuandika maneno mengine kwa sababu alitaraji kufikia Gayo nyuma kidogo. Kufika siku ile acae na salamu.

Barua ya Yuda

MWANZO

Mwandishi

Tunafikili Yuda alikuwa ndugu ya Bwana wetu kwa njia ya mama yake, lakini akiwa mnyenyeketu alitaja ndugu yake Yakobo tu aliye-julikana kanisani kwa wakati wa mwanzo. Lakini ndugu hawa wawili waliamini Yesu nyuma ya ufufuko wake tu.

Mzigo wa mwandishi

Ndani ya barua yake fupi Yuda alijulisha wasomaji wake hatari ya wakafiri, wapinga Kristo walioingia makusanyiko ya kanisa, zaidi makusanyiko yale yaliyoitwa *agapes*, ndizo “karamu za mapendo” (sh.12). Wanaume hawa walikuwa walimu wa uwongo walitembea katika usherati.

Tarehe

Barua za Yuda na Petro (2 Petro) zinafanana kwa njia nyingi na karibu wanafunzi wote wa Biblia wanafikili mmoja wao alitumia andiko la mwenzake. (Watu wengine wanafikili wao wawili walitumia andiko la mtu mwingine mmoja.) Tunafikili Yuda alitumia andiko la Petro (aliyeuawa kwa imani yake katikati ya 63 na 66 A.D.). Ndani ya barua yake ya pili Petro alitabiri juu ya ukafiri utakaokuja, na ni kama ulikuwa umeanza wakati Yuda alipoandika barua yake. Hivi tunafikili barua hii iliandikwa katikati ya 66 na 80 A.D., na ilikuwa moja ya vitabu vya mwisho vya Agano Jipy.

UMBO LA YUDA

1. Salamu (mash. 1-2)
2. Tabia ya kweli ya wakafiri inafunuliwa (mash. 3-16)
3. Namna gani waamini wanaweza kujilinda kwa maneno ya ukafiri (mash. 17-23)
4. Baraka (mash. 24-25)

1. SALAMU (mash. 1-2)

Tunafikili Yuda huyu ni ndugu ya Yesu Kristo kwa njia ya mama yake; lakini hata kama labda ni Yuda mwingine, alikuwa *mtumwa* wa Kristo. Alisalimu wasomaji wake na rehema, salama na mapendo. Hakutaka wabarikiwe nusu nusu lakini baraka hizi tatu ziongezeke kwoo.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

2. TABIA YA KWELI YA WAKAFIRI inafunuliwa (mash. 3-16)

Kupigania imani (mash. 3-4)

Yuda alikusudi kuandika juu ya wokovu wa waamini wote wa kweli, lakini hakufanya hivi, lakini aliwaonya juu ya walimu wa uwongo waliokwisha kuingia kanisani. Walimu hawa walifundisha ya kwamba neema ya Mungu inawapa watu ruhusa kwa uasherati, na walikana Bwana Yesu, kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, na kazi ambayo aliifanya (mash. 3-4).

Wakafiri kwa wakati wa zamani na hukumu yao (mash. 5-7)

Bila shaka wakafiri kwa wakati wa Yuda watahukumiwa kama wale wa Agano la Kale. *Waisraeli wasioamini* walikufa jangwani nyuma ya kuponyeshwa toka Misri. *Malaika walioasi* na kuacha pahali walipopewa na Mungu wamebekwa katika vifungo nya milele. *Wafiraji* wa Sodomo na Gomora waliazibiwa na moto wa milele.

Wakafiri kwa wakati wa sasa na matendo yao maovu (mash. 8-11)

Wakafiri wa wakati wa sasa wanatenda uasherati, wanaasi serikali, wanasema bila adabu juu ya watawala, neno ambalo hata malaika mkubwa Mikaeli aliogopa kufanya na Shetani. Wamekwenda *katika njia ya Kaina*, (maana wokovu unapatikana kwa njia ya matendo), wamefuata *kosa la Balama* (maana kujitafutia mali kwa njia ya kufanya kazi ya Mungu), na wameangamia katika *maasi ya Kora* (waliasi wajumbe wa Mungu).

Wakafiri ni wapotovu na watahukumiwa (mash. 12-16)

Wao ni miamba yenyе hatari, miti isiyo na matunda, mawimbi ya bahari yasiyozuizwa, na nyota zinazopotea (mash. 12-13). Enoka alitabiri juu ya hukumu yao; watahukumiwa kwa sababu ya kunungu-nika kwao na maisha yao ya tamaa, masemo yao ya kiburi na ya kupendelea watu (mash. 14-16).

3. NAMNA GANI WAAMINI WANAWEZA KUJILINDA

KWA MANENO YA UKAFIRI (mash. 17-23)

Basi waamini wafanye nini kwa wakati wa ukafiri? Kwanza inawapasa kukumbuka ya kwamba mitume waliwapasha juu ya hatari hii mbele. Halafu inawapasa kujilinda wakae na nguvu katika imani — kwa njia ya kujijenga wenywewe, maombi, kujilinda katika mapendo ya Mungu na kungojea Bwana. Mwishoni, wawe na ufahamu wakati wanaposaidia wengine walioangushwa na wakafiri — walio na shaka, wale walio katika hatari, na kuchafuwa.

4. BARAKA (mash. 24-25)

Yuda alimaliza barua yake na moja ya baraka kubwa za Biblia. Watu wanafanya vizuri wakati wanapotaja maneno ya baraka hii mara nyingi. Inaleta heshima kubwa kwake ambaye anatulinda, kutukamiliشا, aliye Mwokozi wetu kwa sasa na kwa milele. Anaweza kutulinda tusijikwae, na kutusimamisha pasipo kilema mbele ya utukufu wake na furaha kubwa. Yeye anastahili utukufu, ukubwa, uwezo na nguvu sasa na hata milele.

Ufunuo wa Yesu Kristo

MWANZO

Habari kubwa za Ufunuo

Ufunuo ni kitabu cha hukumu na utukufu. Kinaanza na muda wa Kanisa, na kuendelea na muda wa Mateso, kurudi kwa Kristo katika utukufu kutawala, ufalme wa miaka elfu moja duniani, hukumu ya kiti kikubwa cheupe, na mbingu na dunia mpya kwa wakati wa milele.

Mwandishi na tarehe ya Ufunuo

Mtume Yoane aliandika Ufunuo wakati alipokuwa mfungwa juu ya kisanga Patemo, katika muda wa A.D. 81 na 96. Mungu alitumika na kifungo cha mtumishi wake kwa kutupa sisi ufunuo huu wa ajabu wa maneno yatakayotokea — kitabu cha mwisho cha Neno lake takatifu.

UMBO LA UFUNUO

1. Matangulizi (1:1-8)
2. Ono la Kristo akivaa mavazi ya mwamuzi (1:9-20)
3. Barua kwa makanisa saba ya Asia (Sura 2-3)
4. Mambo yanayotangulia muda wa Mateso (Sura 4-5)
5. Muda wa Mateso (Sura 6-18)
6. Kuja kwa pili kwa Kristo na ufalme wake wa utukufu (19:1 – 20:6)
7. Hukumu ya Shetani na wasioamini wote (20:7-15)
8. Mbingu na dunia mpya (21:1 – 22:5)
9. Maneno ya mwisho, ya maonyo, faraja, kuita, na baraka (22:6-21)

1. MATANGULIZI (1:1-8)

Anwani (1:1-3)

Mashairi haya yanaeleza ya kwamba kitabu hiki ni ufunuo toka Yesu Kristo kwa Yoane juu ya maneno yaliyokuwa karibu kutokeea. Kuna ahadi ya baraka kwa watu wale wanaosikia na kutii habari hizi.

Salamu (1:4-8)

Kitabu hiki kiliandikwa kwa makanisa saba katika Asia, na kinaanza na wimbo wa sifa kwa Bwana Yesu. Kwa mwisho wa wimbo huu Bwana alisema yeeye ni Alfa na Omega.

UFUNUO

2. ONO LA KRISTO AKIVAA MAVAZI YA MWAMUZI (1:9-20)

Maneno Yoane aliyoona (1:9-16)

Mtume Yoane alieleza ya kwamba Bwana alitokea kwake wakati alipokuwa mfungwa kwa Patemo, na kumpa ono hili kwa makanisa. Vinara vile saba ni mifano ya makanisa haya. Yesu alikuwa akivaa mavazi ya mwamuzi, na alishika nyota saba mkononi mwake, ndizo mifano ya malaika za makanisa haya.

Ufunguo wa kitabu (1:17-20)

Kwanza Yoane alishindwa na maneno aliyoona, lakini Bwana alimwambia asiogope, akamwagiza kuandika maneno aliyokwisha kuona (ono la sura 1), na maneno yaliyokuwa kwa wakati ule (makanisa saba ya sura 2 na 3), na maneno yatakayokuwa kwa wakati wa kuja (Mateso Makubwa na maneno yatakayotokea ndani ya sura 4-22). Nyota saba zilikuwa malaika saba, na vinara saba vya zahabu vilikuwa makanisa saba.

3. BARUA KWA MAKANISA SABA YA ASIA (Sura 2-3)

Ndani ya sura 2 na 3 tunaona Bwana, kama Mwamuzi, akiangalia sana maneno ya makanisa saba. Ni makanisa yaliyokuwa yamesimamishwa kwa wakati wa Yoane, lakini tunafikili ni mifano wa maneno yanayoonekana ndani ya makanisa pahali po pote duniani kwa wakati wo wote, nayo ni mifano vilevile wa muda saba ndani ya historia ya Kanisa. (Wakati Kanisa linapoandikwa na herufi kubwa, ni Kanisa la dunia nzima. Kanisa la pahali fulani linaandikwa na herufi ndogo kwa mwanzo, ndilo kanisa.)

Barua hizi zinafanana kwa njia nyingine. Kila barua inaonyesha maneno mengine juu ya Bwana; kuna sifa (ila kwa Laodikia); kuna mashutumu kwa kuanguka kwao, na mashauri waamini watubu (ila kwa Smurna na Filadelfia); kuna maonyo wasikilize maneno ambayo Roho anawaambia; na kuna ahadi kwa mwenye kushinda.

Barua kwa Efeso (2:1-7)

Bwana alisifu kanisa hili kwa sababu ya matendo, kazi ngumu, na uvumilivu wa waamini; hawakuvumilia watu waovu katikati yao; walijua kutambua walimu wa uwongo; walivumilia majaribu na taabu na roho ya saburi; na walichukia kazi za Wanikolayi. Lakini walikuwa wameacha mapendo ambayo walikuwa nayo wakati walipookolewa. Wakumbuke imani yao ya mbele, watubu kwa sababu walikuwa

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

wamerudi nyuma, na waanze kutumikia Bwana tena na mapendo na bidii. Kama wasipofanya hivi, ushuhuda wa kanisa lao litakwisha. Wale wanaoshinda watakula matunda ya mti wa uzima.

Barua hii inaonyesha hali ya Kanisa karibu na mwisho wa muda wakati mitume walipokuwa kwanza hai.

Barua kwa Smurna (2:8-11)

Kanisa hili liliteswa sana, na waamini walikuwa masikini na wenye mahitaji duniani, lakini kwa maneno ya roho walikuwa watajiri. Watapata mateso mengine vilevile, na wengine katikati yao watafungwa gerezani, lakini wale watakaouawa kwa sababu ya imani yao watapokea taji ya uzima. Washindaji hawataumizwa na kufa kwa pili.

Smurna ni mfano wa mateso ya Kanisa wakati wa wafalme wa Roma waliotangulia Konstantino.

Barua kwa Pergamo (2:12-17)

Hili ni jina la mji katika Asia uliokuwa makao makubwa kwa ibada ya mfalme Mroma; kwa sababu hii tunasoma juu ya pahali Shetani anapokaa. Kanisa la Pergamo lilikuwa aminifu kwa Kristo, na mmoja wa Wakristo, Antipa, alikuwa ameuawa kwa sababu ya imani yake. Hata hivi walivumilia katikati yao wale walioleta mafundisha mabaya. Bwana anawaagiza kutubu; kama wasipofanya hivi, atawahukumu. Mwenye kushinda atakula mana iliyofichwa, na kupokea jiwe jeupe juu yake liliandikwa jina asilojua mtu ila ye ye ambaye analipokea.

Kanisa hili ni mfano wa muda ulioanza na Konstantino wakati serikali ilipopendelea Kanisa, na wakati Kanisa lilipokubali desturi za wasioamini kuingia katikati yao.

Barua kwa Tuatera (2:18-29)

Kanisa hili lilikuwa likiongezeka katika kazi njema, mapendo, imani, utumishi na uvumilivu. Lakini waamini waliruhusu mwanamke ambaye alijiita nabii mke kufundisha maneno mabaya yaliyoongoza watu kuabudu sanamu na kutenda uzini. Mungu atahukuma mwanamke huyu pamoa na wafuata wake. Wale waliosimama imara waliagizwa kushika kweli. Mshindaji atatawala na Kristo kwa wakati wa utawala wake wa miaka elfu.

Walimu wengi wanafikili Tuatera ni mfano wa Kanisa kwa muda wa A.D. 600 – 1500, uliokuwa muda wa giza kabisa kwa maneno ya Mungu, mbele ya matengenezo ya Kanisa. Lakini maneno yaliyonekana ndani ya Tuatera yanaonekana hata sasa.

UFUNUO

Barua kwa Sardi (3:1-6)

Zaidi ya watu ndani ya kanisa hili hawakuwa waamini wa kweli. Bwana aliwaita kuwa na bidii tena na kujaribu kupatisha nguvu waamini wa kweli wachache waliobaki. Toba tu iliweza kuponyesha kanisa hili lisihukumiwe. Waamini wa kweli wachache waliotembea katika utawa watatembea pamoja na Kristo wakivaa mavazi meupe. Majina ya wenyewe kushinda hayataondoshwa katika kitabu cha uzima, lakini Kristo atakiri majina yao mbele ya Baba yake na malaika.

Tunafikili Sardi ni mfano wa makanisa ya serikali nyuma ya muda wa matengenezo ya Kanisa. Makanisa haya yalifungana na desturi nyingi za ibada zilizokosa uzima.

Barua kwa Filadelfia (3:7-13)

Bwana alisifu Filadelfia juu ya matendo yao mema, na kwa sababu walikuwa waaminifu kushika jina lake. Watakuwa na mlango wazi ambaeo wale walioshindana nao hawataweza kufunga. Na hawataingia mateso makubwa yatakayokuja. Tumaini ya kwamba Kristo atakuja liwasukume kusimama imara na kuvumilia bila kusita. Mshindaji atakuwa alama ya heshima, nguvu, na mustarehe wa daima, na atafanywa mamoa na Mungu, Kristo, na Yerusalem mpya.

Filadelfia ni mfano wa mwamko mkubwa kwa maneno ya Habari Njema kuanza na muda kwa karibu 1800 A.D. na kuendelea hata karibu 1925 A.D. wakati waamini walipokwenda kuhubiri Habari Njema duniani pote.

Barua kwa Laodikia (3:14-22)

Uvuguvugu wa kanisa la Laodikia ulisukuma Bwana kutapika. Walikuwa wajinga, na wenyewe kiburi waliofikili kwamba hawahitaji kitu. Walihitaji haki toka Mungu, haki ndani ya matendo yao, na ufa-hamu kwa maneno ya Roho. Kristo aliwaita kuwa na bidii na kutubu, na kutoka katika kanisa hili la uwongo waweeze kufurahi ndani ya upatano mzuri naye. Mshindaji atatawala pamoja na Kristo.

Ni wazi ya kwamba Laodikia ni mfano wa Kanisa la ukafiri kwa siku za mwisho karibu na kurudi kwa Kristo. Ndani ya baki la kitabu cha Ufunuo hatuoni Kanisa tena *duniani*.

4. MAMBO YANAYOTANGULIA MUDA WA MATESO (Sura 4-5)

Sura 4 na 5 zinaonyesha maneno mengine mbinguni mbele ya mwanzo wa hukumu za Mateso Makubwa ndani ya sura 6-18. Ni mwanzo wa “maneno yatakayotokea nyuma ya haya” (1:19).

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Kiti cha ufalme mbinguni (Sura 4)

Ni kama Yoane alihamishwa mbinguni katika Roho, na pale aliona Mungu wa utukufu akiteti juu ya kiti cha ufalme cha hukumu (mash. 1-3). Aliona vilevile wazee 24. Labda wazee hawa ni mfano wa wakombolewa mbinguni. Aliona vilevile viumbe wenyе uhai wane. Labda walikuwa mfano wa malaika waliochunga kiti cha ufalme cha Mungu. Viumbe wenyе uhai hawaachi kusema juu ya utakatifu wa Mungu, na wazee 24 wanamwabudu kama Mwumba mwenye uwemo (mash. 4-11).

Ono hili linatayarisha nia zetu kwa maneno yanayofuata. Mwamuzi wa ulimwengu, akizungushwa na viumbe wenyе kumwabudu, alikuwa karibu kuhukumu dunia.

Anastahili Mwana-Kondoo (Sura 5)

Mungu anashika mkononi mwake gombo lililofungwa na mihuri saba. Ni gombo la gazabu yake itakayomimiwa juu ya dunia iliyokataa Mwana wake. Mmoja tu alistahili kufungua gombo hili, ndiye Bwana Yesu. Wakati Kristo aliposhika gombo, viumbe wenyе uhai na wazee 24 walianza kusifu na kuabudu Kristo kama Mkombozi. Kisha jeshi lote la ulimwengu mzima walifungana pamoja kusifu Mwana-Kondoo anayeishi milele.

5. MUDA WA MATESO (Sura 6-18)

Muhuri wa kwanza: mshindaji (6:1-2)

Wakati Mwana-Kondoo alipofungua muhuri wa kwanza, mshindaji alitokea akitembea juu ya farasi mweupe. Mpindi ni alama ya vita, lakini vita ilianza tu nyuma ya kufunguliwa kwa muhuri wa pili. Labda mshindaji huyu ni mfano wa mtawala mkubwa duniani ambaye anajipatia mamlaka kwa njia ya kupiga vita bila kumwanga damu.

Muhuri wa pili: vita duniani (6:3-4)

Mpandaji wa farasi ya pili, aliye mwekundu, alibeba upanga mku-bwa, na aliondosha salama duniani.

Muhuri wa tatu: ukosefu wa vyakula duniani (6:5-6)

Wakati muhuri wa tatu ulipofunguliwa mpandaji juu ya farasi mweusi alitokea. Mizani mkononi mwake na bei kubwa ya chakula zinatufahamisha kwamba yeche ni mfano wa njaa inayofuata vita mara nyangi.

UFUNUO

Muhuri wa ine: mauti inayoenea duniani (6:7-8)

Rangi ya farasi ya ine ilikuwa nyeupe, kama rangi ya mgonjwa; jina la mpandaji wake lilikuwa ni mauti, na Hadeze alimfuata. Sehemu moja ya ine ya watu duniani wanauawa na vita, tauni, na nyama wakali, na nafsi zao zilipokewa na Hadeze.

Muhuri wa tano: kilio cha wale waliouawa kwa sababu ya imani yao (6:9-11)

Hapa tunaona wale waliota u zima wao kwa sababu ya ushuhuda wao mwaminifu, wakilia kwa Mungu kupatia damu yao haki. Wali-pewa mavazi meupe, na kuagizwa kungoja kwanza kwa sababu watu wengine watauawa vilevile kwa ajili ya jina la Bwana.

Muhuri wa sita: msukosuko wa ulimwengu mzima (6:12-17)

Kulikuwa na machafuko sana duniani wakati muhuri wa sita ulipo-funguliwa — inchi ilitetemeka, jua lilikuwa jeusi, mwezi ulikuwa kama damu, vivi hivi, hata watu wa dunia wataogopa sana sana.

Watu 144.000 wa Israeli wanatiwa muhuri (7:1-8)

Ndani ya muda unaofuata mbele ya kufunguliwa kwa muhuri wa saba tunasoma juu ya makundi mawili ya waamini. Kwanza ni habari za Wayuda 144,000, watu 12,000 wa kila kabilal la Israeli. Sharti watiwe muhuri, ndio alama juu ya vipaji vya nyuso zao, mbele ya hukumu ya uharibifu mkubwa itakayopata dunia, bahari, na mapando. Muhuri huu ni zamana ya kwamba hawatauawa katika muda wa Mateso Makubwa.

Makutano makubwa watakaokolewa wakati wa Mateso Makubwa (7:9-17)

Kundi la pili ni makutano makubwa ya Mataifa watakaokolewa kwa wakati wa Mateso Makubwa. Watazidi kukaa hai katika muda huu wa taabu kubwa kupita taabu zote zilizotangulia, na watafurahishwa na baraka za ufalme wa milele wa Kristo. Malaika, wazee, na viumbe venye uhai watafungana nao kusifu Mungu.

Mhuri wa saba: mwanzo wa baragumu saba (8:1-6)

Muhuri wa saba na wa mwisho ulianza na dakika 30 ya kimya mbinguni. Kristo alionekana kama malaika, akiongeza uvumba kwa maombi ya watakatifu wanaoteswa katika Mateso Makubwa. Uvumba huu ndio yeye mwenyewe na kazi yake. Akijibu kilio cha waamini walioneswa waweze kulipizwa kisasi, alituma makaa ya moto juu ya dunia, nayo yalileta ngurumo, umeme, na matetemeko ya inchi.

Muhuri wa saba ni mwanzo wa hukumu za baragumu saba; ndiyo

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

ni kama hukumu saba za baragumu zinazofuata *ni sehemu ya muhuri wa saba.*

Baragumu ya kwanza: mapando yanaharibiwa (8:7)

Wakati baragumu ya kwanza ilipopigwa, sehemu moja ya tatu ya dunia, miji, na nyasi iliteketezwa kwa mvua ya mawe na moto yaliyochanganyika na damu.

Baragumu ya pili: bahari inaharibiwa (8:8-9)

Wakati baragumu ya pili ilipopigwa, kitu kilichofanana na mlima mkubwa unaowaka moto, kikatupwa katika bahari na kufanyiza sehemu moja ya tatu ya maji damu, na kuharibu sehemu moja ya tatu ya viumbe baharini na kuharibu sehemu moja ya tatu za merikebu.

Baragumu ya tatu: maji yanaharibiwa (8:10-11)

Wakati baragumu ya tatu ilipopigwa, nyota kubwa, jina lake Pakanga ilianguka toka mbingu na kufanyiza sehemu moja ya tatu ya maji ya mito na chemchemi kuwa machungu na kuua watu wengi.

Baragumu ya ine: mbingu zinaharibiwa (8:12-13)

Saa ya baragumu ya ine juu, mwezi na nyota zinapigwa hata zinatoa sehemu mbili za tatu tu za nuru walijyotoa mbele (sh.12). Tai aliyeruka katikati ya mbingu alitangaza ole tatu kwa watu wanaokaa duniani, ndio wale wanaofikili maneno ya dunia tu (sh.13).

Baragumu ya tano: nzige toka shimo pasipo mwisho (9:1-12)

Nyota ilioanguka toka mbingu, labda alikuwa malaika, alifungua shimo pasipo mwisho, na halafu moshi mkubwa ulifunika dunia na tauni la nzige walioogopesha na kutesa wasioamini kwa miezi mitano. Lakini nzige hawa hawakuua watu wala kuharibu mapando. Wanasaawanishwa hapa na jeshi wanaoshinda adui, na tunafikili ni pepo wachafu. Watu wengine wanafikili ni nzige kweli. Hii ni baragumu ya tano na ole wa kwanza.

Baragumu ya sita: sehemu moja ya tatu ya watu wanaharibiwa (9:13-21)

Mwenye kupiga baragumu ya sita alifungua malaika wane waliofungwa katika mto Furati. Majeshi ya watu milioni mia moja waki tembea juu ya farasi waliwafuata. Halafu sehemu moja ya tatu ya watu wataharibiwa. Lakini hata nyuma ya ole hii ya pili watu waliona hawakutubu uovu wao.

Malaika mkubwa na gombo (kitabu kidogo) (10:1-7)

Labda malaika huyu ni Bwana Yesu. Alishuka toka mbingu na

UFUNUO

gombo. Wakati alipolia na sauti kubwa kuna ngurumo saba. Ni kama Yoane alifahamu maneno ngurumo ziliyosema, lakini alikatazwa kuyaandika. Akiweka mguu mmoja juu ya inchi na nyagine juu ya bahari, malaika aliapa ya kwamba wakati umekwisha. Baragumu ya saba itamaliza siri ya Mungu kwa njia ya kuazibu waovu wote na kuanza ufalme wa utukufu wa Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo.

Yoane anakula gombo (10:8-11)

Wakati Yoane alipotii sauti toka mbingu na kula gombo dogo, lilikuwa tamu kinywani mwake lakini chungu katika tumbo (mash. 8-10). Vivyo hivyo ni chungu kuwaza juu ya hukumu ya Mungu, lakini ni tamu kutazamia wakati Mungu atakaposhinda Shetani na majeshi yake. Yoane atafahamu neno hili wakati atakapotoa unabii tena juu ya watu na mataifa na lugha na wafalme wengi (sh.11)

Hekalu linapimwa (11:1-2)

Yoane aliagizwa kupima hekalu na mazabahu, na kuhesabu wale wanaoabudu pale. Ni mfano wa ulinzi wa Mungu. Kiwanja cha Mataifa hakipimwi na kitakanyagwa na mataifa kwa sehemu ya mwisho ya Mateso Makubwa.

Washuhuda wawili (11:3-10)

Washuhuda wawili walitokea katika Yerusalem, wakipiga kelele juu ya zambi za watu na kuonya watu juu ya hukumu ya Mungu. Kisha nyama toka shimo pasipo mwisho aliwaua nyuma ya siku tatu na nusu, na watu walifurahi sana na kuletana zawadi.

Washuhuda wawili wanafufuliwa (11:11-12)

Halafu Mungu aliwafufua toka wafu na kuwapeleka mbinguni mbele ya macho ya watu. Walimu wengine wanafikili washuhuda hawa wawili ni Musa na Elia kwa sababu maajabu waliyofanya yanafanana. Biblia haifundishi wazi juu ya neno hili, hivi ni vizuri kungoja kutimizwa kwa unabii huu kwanza.

Tetemeko kubwa la inchi (11:13-14)

Halafu tetemeko kubwa la inchi liliharibu sehemu moja ya kumi ya mji na kuua watu 7.000. Watu waliopona walikiri ya kwamba hii ni kazi ya Mungu. Huu ni mwisho wa taabu ya pili, maana yake baragumu ya sita. (Sura 10 na 11:1-13 ziliingizwa katikati.)

Baragumu ya saba (11:15-19)

Baragumu ya saba, ndiyo taabu ya tatu, inatufikisha kwa mwisho wa Mateso Makubwa na mwanzo wa utawala wa Kristo kwa miaka

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

elfu moja. Wazee 24 mbinguni waliabudu Mungu kwa sababu alishinda adui zake na kuwapa zawadi wale ambaao walimwamini (mash. 15-18). Hekalu lililofunguliwa mbinguni linatukumbusha ya kwamba Mungu hakusahau agano lake na Israeli (sh.19).

Joka, Shetani, na mtoto mwanamume (12:1-6)

Mwanamke aliyejewa karibu kuzaa mtoto alitokea mbinguni. Joka mkubwa alitokea vilevile, tayari kuharibu mtoto mara moja nyuma ya kuzaliwa kwake. Mwanamke ni Israeli, joka ni Shetani, na mtoto ni Masiya. Mtoto mwanamume alipelekwa mbinguni, na mwanamke alikimbia na kukaa jangwani kwa miaka mitatu na nusu, sehemu ya mwisho ya muda wa mateso. (Muda wetu wa sasa, wa Kanisa, unafuata shairi 5 na kutangulia shairi 6.)

Vita mbinguni (12:7-12)

Kulikuwa na vita mbinguni katikati ya Mikaeli na majeshi yake na yule joka na malaika zake. Mikaeli alishinda na joka na malaika zake walitupwa hata dunia. Kisha kuna tangazo ya kwamba siku ya kushinda kukubwa kwa Mungu imefika na siku ya kushinda kwa watu wake vilevile.

Vita duniani (12:13-17)

Akifahamu ya kwamba ameshindwa, Shetani alijaribu kuharibu mwanamke kwa njia ya kutoa maji mengi toka kinywa chake, lakini alishindwa wakati dunia ilipofunguliwa kumeza maji yale. Halafu Shetani alijaribu kuharibu wazao wake wengine (Wayuda). Tunafikili vita hii mbinguni itatokea katikati ya miaka saba ya Mateso.

Nyama toka bahari (13:1-10)

Sasa tunaona viongozi wawili wenye kujulikana kwa wakati wa muda wa Mateso: nyama toka bahari (mash. 1-10), na nyama toka dunia (mash. 11-18).

Nyama ya kwanza alikuwa na pembe kumi, vichwa saba, taji kumi juu ya pembe zake, na kidonda cha kufa ndani ya kimoja cha vichwa vyake. Labda nyama huyu ni mwongozi wa ufalme wa Roma utakaosimama tena kwa wakati wa kuja, ufalme wenye falme kumi. Nyama huyu alitoka bahari (mara nydingi bahari ni mfano wa Mataifa), hivi tunafikili atakuwa mtawala Mtaifa. Tunaona ndani yake maneno ya falme nydingine za dunia zilizotangulia ambayo Danieli aliandika juu yao — Yunani (chui), Persia (dubu), Babeli (simba). Labda vichwa saba ni sehemu za ufalme wa Roma wa mbele zilizopona, na mara nydingine walimu wanaeleza kichwa chenyenye kidonda cha kufa kuwa namna ya kutawala iliyokwisha lakini itakayotokea tena.

UFUNUO

Majina ya watu wengine hayakuandikwa ndani ya kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo. Watu hawa wataabudu Shetani na nyama, anayetukana Mungu kwa miaka tatu na nusu ya utawala wake. Atatawala dunia na ukali na kutesa watakatifu. Waamini wanajua ya kwamba watesaji wao watafungwa na kuuawa, na neno hili linawawezesha kuvumilia na saburi na imani.

Nyama toka dunia (13:11-18)

Tunafikili nyama toka dunia atakuwa kiongozi Myuda kwani mara nyingi *dunia* (neno hili linatafsiriwa *inchi* vilevile) ni mfano wa Israeli. Anafungana pamoja na nyama ya kwanza na kutengeneza utaratibu kwa watu wa mataifa yote kuabudu nyama na sanamu yake. Anaonekana kama mwana-kondoo, lakini anasema kama joka. Anafanya mastaajabu na kufanyiza moto kuanguka toka mbingu na kuwezesha sanamu ya nyama kusema. Analazimisha watu kutiwa chapa ya nyama katika vipaji vya nyuso zao au katika mkono wao wa kuume.

Mtu akikosa chapa ile hakuweza kununua au kuuza kitu. Hesabu ya nyama ni 666 (sita ni hesabu ya mtu). Wale wanaokataa kuabudu sanamu ya nyama watauawa.

Mwana-Kondoo na watu 144.000 (14:1-5)

Maono ya sura hii hayafuatani kwa njia ya saa, maana maneno tunayosoma kwanza yatatokea nyuma ya mengine yaliyoandikwa nyuma.

Ono la kwanza linatangulia mwisho wa muda wa mateso wakati watu wale 144.000 ni karibu kuingia ufalme pamoja na Kristo. Wao ni malimbuko ya mavuno ya mateso nao watajaza dunia tena na watu. Walikuwa wamejichunga safi kwa maneno ya kuabudu sanamu na kufanya uzini, walifuata Mwana-Kondoo na kukataa kuabudu sanamu. Sasa wanaimba wimbo mpya mbele ya kiti cha kifalme katika Yerusalem.

Tangazo la malaika ya kwanza (14:6-7)

Malaika ya kwanza mwenye Habari Njema ya milele alionya watu waliokaa juu ya dunia ya kwamba Mungu ni karibu kuhukumu dunia na kutengeneza maneno, kwa njia ya kurudi kwa Bwana Yesu kwa kutawala.

Tangazo la malaika ya pili (14:8)

Malaika ya pili alitangaza kuanguka kwa Babeli. Neno hili linatokea karibu na mwisho wa mateso. Tunasoma maneno mengi juu yake ndani ya sura 17 na 18.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Tangazo la malaika ya tatu (14:9-13)

Malaika ya tatu alitoa maonyo ya kwamba wote wanaoabudu nyama watateswa katika Hadeze kwa milele. Tangazo hili lilifanywa katikati ya sehemu ya mwisho ya mateso, ile miaka mitatu na nusu inayoitwa Mateso *Makubwa*. Waamini watakaouawa kwa sababu ya imani yao watapokea zawabu kwa uaminifu wao.

Mavuno ya dunia (14:14-16)

Pamoja na mashairi haya soma Matayo 13:39-43 na 25:31-46. Wakati Kristo atakapokuja mara ya pili atatuma malaika zake kusanya wote waliookolewa waingie katika ufalme wake wa utukufu. Wasioamini (magugu) watateketezwa kwa moto usiokwisha.

Kuchuma vichala vya mizabibu ya gazabu (14:17-20)

Kuvuna kwa dunia kunapasha juu ya hukumu za kuogopesha za mwisho juu ya sehemu ya taifa la Israeli wasioamini (mzabibu wa dunia). Maneno haya yatatokea inje ya Yerusalem. Damu itamwangika hata mpaka wa kamba ya kuongoza farasi, kama mwendo wa kilomètres mia tatu makumi mbili. Yatatokea kwa mwisho wa Mateso vilevile.

Nyama anashindwa (15:1-4)

Ndani ya sura hii fupi sana tunaona malaika saba wenye mapigo saba ya mwisho. Wakati mapigo haya yanapopata dunia, gazabu ya Mungu inatimia; maana yake muda wa Mateso unakwisha. Yoane aliona fungu la watu mbinguni, wakisimama juu ya bahari ya kioo iliyochanganyika na moto. Aliwatambua kuwa wale waliokataa kuabudu nyama. Bila shaka waliuawa kwa sababu ya imani yao, lakini sasa wanaimba wimbo wa Musa na wa Mwana-Kondoo. Wana-shuhudia haki ya hukumu za Mungu juu ya wale ambao waliwaua.

Mwanzo wa hukumu za machupa (15:5-8)

Halafu Yoane aliona malaika saba wakitoka hekalu mbinguni na wakivaa mavazi ya ukuhani. Mmoja wa nyama wane wenye uhai alimpa kila malaika chupa la zahabu. Hukumu hizi za mwisho za Mungu zinagusa adui zote za Mungu, si watu wachache tu. Hakuna mtu aliyeweza kuingia hekalu mbele ya mwisho wa mapigo haya saba.

Chupa la kwanza: majipu mabaya (16:1-2)

Mbele tulisoma juu ya *mihuri saba* za hukumu, na juu ya *baragumu saba* za hukumu. Sasa tunasoma juu ya *machupa saba* ya gazabu ya Mungu, ndio mapigo saba ya mwisho. Tulisema mbele kwamba hukumu za baragumu saba ni sehemu ya mhuri wa saba. Ni kama hukumu za *machupa saba* ni sehemu ya baragumu ya saba.

UFUNUO

Sauti toka mbinguni aliagiza malaika saba kumimia machupa saba ya gazabu ya Mungu juu ya dunia. Chupa la kwanza lilileta majipu mabaya kwa watu wote walioabudu nyama na sanamu yake.

Chupa la pili: bahari inageuka damu (16:3)

Pigo la pili liligeuza maji ya bahari kuwa damu na viumbe vyote baharini viliuawa.

Chupa la tatu: maji yanageuka damu (16:4-7)

Chupa la tatu liligeuza maji yote ya kunywa kuwa damu. Malaika wawili walismamia Mungu kusema alitenda kwa haki, kwa kuazibu watu waovu waliomwanga damu ya watakatifu.

Chupa la ine: watu wanaunguzwa kwa moto (16:8-9)

Hukumu ya ine iliunguza miili ya watu kwa njia ya ukali wa jua. Lakini kwa pahali pa kutubu, watu walitukana Mungu juu ya maumivu haya.

Chupa la tano: giza na maumizo (16:10-11)

Watu walizidi kuchukia Mungu juu ya maumivu yao.

Chupa la sita —mto Furato unakauka (16:12-16)

Wakati chupa la sita lilipomimiwa, maji ya mto Furati yalikaushwa na majeshi toka mashariki waliweza kukaribia Israeli. Pepo wachafu watatu waliofanana na vyura walitoka vinywani mwa joka, nyama, na nabii wa uwongo, walikusanya majeshi ya dunia kwa vita. Bwana mwenyewe atakutana nao katika bonde la Harmagedoni na kuwashinda kabisa.

Chupa la saba: dunia inaharibiwa (16:17-21)

Chupa la saba linatufikisha kwa mwisho wa muda wa mateso; “imefanyika”. Dunia iliharibiwa na mapinduzi makubwa na watu wanatukana Mungu kwa sababu ya tauni la kuogopesha la mawe ya mvua, uzito wa kila jiwe likiwa talanta moja, ndio karibu kilos 45.

Mwanamke mwekundu na nyama mwekundu (17:1-8)

Sura 17 na 18 zinapasha juu ya kuanguka kwa utaratibu mkubwa wa dini, serikali, na biashara unaoitwa “Babeli mkubwa, mama ya makahaba na machukizo ya dunia.” Utaratibu huu umeshawishi wafalme wa dunia nzima. Mwanamke aliketi juu ya nyama mwekundu, ndiye nyama yule aliyetoka baharini (13:1-10), ndio ufalme wa Roma unaosimamishwa tena. Babeli ni mchanganyio wa utajiri, uzini na waabudaji sanamu. Umemwanga damu ya Wakristo walokataa kukana Kristo katika mia za miaka inayopita.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

Maana ya mwanamke na nyama (17:9-18)

Hapa kuna maelezo juu ya nyama mwekundu, ndio ufalme wa Roma utakaosimama tena. Ni ufalme mkubwa wenyе falme wadogo kumi ndani yake watakaokwenda kupiga vita na Bwana Yesu wakati atakaporudi duniani kwa mwisho wa muda wa mateso, lakini wata-shindwa kabisa (sh.14). Mwishoni ufalme ule mkubwa unageukia kahaba na kumharibu (mash. 16-18).

Kuanguka kwa Babeli mkubwa (18:1-19)

Sura hii ni kama wimbo wa maziko juu ya kuanguka kwa Babeli, makao na boma la namna zote za uovu. Sauti toka mbinguni ilionya watu wa Mungu kutoka ndani ya utaratibu huu utakaoharibiwa mbele ya kuangamizwa kwake. Wafalme wa dunia watamwombolea na wafanya biashara watahuzunishwa sana kwa sababu ya kuharibika kwa biashara yao.

Kuangamizwa kwa Babeli (18:20-24)

Lakini wakati wasioamini wanapotoa machozi duniani kuna furaha kubwa mbinguni. Malaika anatupa jiwe kubwa ndani ya bahari kama mfano wa kuangamizwa kwa Babeli. Utaratibu ule mbaya usiokuwa na rehemu ulikuwa kama jiwe la kusagia kwa milioni za watu na kuwakokota hata Hadeze. Sasa yule kahaba atateswa vivyo hivyo. Sauti za kazi namna zote zilizofanywa ndani yake zitanyamazishwa kwa milele, na Mungu atalipiza kisasi damu ya watakatifu wake waliouawa kwa imani yao.

6. KUJA KWA PILI KWA KRISTO NA UFALME WAKE WA UTUKUFU (19:1 – 20:6)

Furaha kubwa mbinguni juu ya kuhukumiwa kwa Babeli (19:1-5)

Yoane alisikia makutano makubwa mbinguni wakisifu Mungu kwa sababu ya hukumu yake ya haki ya kahaba mkubwa. Wazee 24 na nyama wane wenyе uhai wanaabudu Mungu na kusema maneno Mungu aliyofanya sasa tu yamekuwa haki. Sauti toka kitit cha ufalme inaita watumishi wote wa Mungu kumsifu.

Arusi ya Mwana-Kondoo (19:6-9)

Arusi ya Mwana-Kondoo mbinguni inafuata kitit cha hukumu cha Kristo. (Ona Waroma 14:10-12.) Kanisa ndilo bibi-arusi ya mbingu; wale wanaoitwa kwa karamu ya arusi ndio baki la wakombolewa mbinguni, maana watakatifu wa wakati wa Agano la Kale na wa muda wa Mateso. Bibi-arusi anavikwa mavazi ya kitani nzuri nyeupe, ndiyo mfano wa matendo ya haki ya watakatifu. Malaika anatangaza kwa-

UFUNUO

mba wote wanaoitwa kwa karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo ni heri.

Kuabudu na ushuhuda wa kweli (19:10)

Yoane alikatazwa kuabudu malaika, kwa sababu inapasa watu kuabudu Mungu tu. Malaika alimwambia ya kwamba kusudi la unabii ni kushuhudia Bwana Yesu Kristo na kazi yake.

Kuja kwa pili kwa Kristo (19:11-16)

Sasa tunafika kwa habari kubwa za mwisho za kitabu cha Ufunuo — kurudi kwa Kristo duniani na utukufu kushinda adui zake na kusimamisha ufalme wake. Anakuja toka mbinguni akitembea juu ya farasi mweupe, Mshindaji mwenye uwezo, akiwa amevikwa mavazi ya utukufu. Majeshi yaliyo mbinguni wanamfuata.

Karamu ya Mungu iliyo kubwa (19:17-18)

Malaika anaita ndege mkubwa kula nyama ya wale waliouawa na Bwana; hii ndiyo karamu ya Mungu iliyo kubwa.

Azabu ya waasi (19:19-21)

Nyama na nabii wa uwongo walijaribu tena kushindana na Bwana, lakini walikamatwa na kutupa wangali hai ndani ya ziwa la moto. Baki la waasi waliouawa kwa upanga wa Bwana na ndege walikula nyama yao.

Shetani anafungwa kwa miaka 1.000 (20:1-3)

Mbele ya mwanzo wa utawala wa Kristo kwa miaka 1.000, Shetani alitupwa katika shimo pasipo mwisho. Atabaki pale kwa miaka elfu moja ya utawala wa Kristo.

Utawala wa miaka elfu moja wa Kristo (20:4)

Yoane aliona watu wa Mungu (tunafikili ni waamini wa muda wa Kanisa) wakiketi juu ya viti nya ufalme, wenyewe kazi ya kutawala na kuhukumu. Aliona vilevile wale waliouawa katika muda wa Mateso waliofufuliwa sasa toka wafu na kutawala pamoja na Kristo kwa miaka 1.000.

Ufufuko na utawala (20:5-6)

Mwanzo wa shairi 5 halisemi juu ya ufufuko wa wafu waovu kwa mwisho wa utawala wa Kristo, lakini maneno haya “ufufuko wa kwanza” yanarudia kwa watakatifu waliofufuliwa ndani ya shairi 4. Ni sehemu ya pili ya ufufuko wa kwanza; sehemu ya kwanza itatoka wakati Kristo atakapokuja kwa kanisa (1 Kor. 15:51-54). Ufufuko wa kwanza ni ufufuko wa baraka; ufufuko wa pili ni ufufuko wa hukumu na mauti ya milele.

MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA

7. HUKUMU YA SHETANI NA WASIOAMINI WOTE (20:7-15)

Shetani anafunguliwa na kuhukumiwa (20:7-10)

Kwa mwisho wa utawala wa Kristo kwa miaka 1.000 Shetani atafunguliwa toka shimo pasipo mwisho na atakusanya jeshi kubwa na kukaribia Yerusalem, mji wa Mfalme mkubwa. Lakini moto toka mbinguni utateketeza jeshi, na Shetani atatupwa ndani ya ziwa la moto.

Kiti cha ufalme, kikubwa na cheupe (20:11-15)

Nyuma ya kuharibiwa kwa mbingu na dunia kwa moto, wafu waovu watasimama mbele ya kiti kikubwa cheupe cha ufalme na kuhukumiwa na Kristo kwa kadiri ya matendo yao. Kwa sababu majina yao hayakuandikwa ndani ya kitabu cha uzima, watatupwa ndani ya ziwa la moto. Ukosefu wa majina yao ndani ya kitabu kile unaonyesha ya kwamba hawakutubu zambi zao na kuamini Bwana. Kipimo cha hukumu yao kitakuwa kadiri ya matendo yao.

8. MBINGU NA DUNIA MPYA (21:1 – 22:5)

Ndani ya sura mbili za mwisho za Ufunuo ni nguvu kufahamu mara nyininge kama Yoane anasema juu ya muda wa miaka 1.000 au juu ya wakati wa milele kwa sababu maneno mengi ni kweli juu yao wawili. Tofauti kubwa ndiyo hii: Kutakuwa na zambi na mauti wakati wa muda wa miaka 1.000, lakini hazitakuwa tena kwa wakati wa milele.

Mbingu mpya na dunia mpya (21:1-8)

Mashairi haya yanaonyesha kama mbingu mpya na dunia mpya zitakuwa namna gani kwa wakati wa milele. Yerusalem mpya ukishuka toka mbinguni ni bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo. Yoane alisikia tangazo ya kwamba hema ya Mungu ni pamoja na watu na ya kwamba atakaa pamoja nao kama Mungu wao, na ya kuwa wala mauti, wala huzuni, wala kilio wala uchungu hautakuwa tena. Waovu hawataweza kamwe kuingia Yerusalem mpya.

Yerusalem mpya (21:9-27)

Sasa tunaona Yerusalem mpya ukishuka toka mbingu na kukaa hewani juu kupita dunia kwa wakati wa utawala wa Kristo. Mwandishi alitaja vito vya damani namna namna kujaribu kuonyesha uzuri wake. Ni pahali pakubwa sana, pahali pa usafi, salama, na furaha.

Mto wa maji ya uzima (22:1-5)

Tunawaza ya kwamba mashairi 1-2 yanapasha tena juu ya muda

UFUNUO

wa miaka 1.000 kwani tunasoma hapa juu ya mti wa uzima, wenye majani kwa kuponyesha mataifa. Mti namna hii unahitajiwa duniani kwa sababu ya uharibifu tuliosoma juu yake ndani ya 20:7-8, lakini hautahitajiwa kwa wakati wa milele. Yerusalem mpya una mto wa maji ya uzima na mti wa uzima. Hakuna laana wala mauti tena. Kiti cha ufalme cha Mungu ni pale, na utukufu wa Bwana utautia nuru. Inashinda mtu kuonyesha uzuri wake.

9. MANENO YA MWISHO, YA MAONYO, FARAJA, MIITO, NA BARAKA (22:6-21)

Kitabu hiki kinakwisha na baraka kwa watu wote wanaoshika maneno ya unabii huu; na maonyo kwa Yoane asiabudu malaika ambaye alijaribu kumwelezea maneno haya. Kuna ahadi vilevile ya kwamba unabii huu utatimizwa nyuma kidogo. Bwana aliahidi mara kwa mara ya kwamba kurudi kwake kulikuwa karibu sana. Kuna maonyo ya nguvu kwa wale wasiotubu kuamini Habari Njema. Mtu ye yote anayeongeza juu ya maandiko ndani ya Kitabu cha Mungu au kuondoa neno lo lote atalaaniwa.

Mwishoni Mungu anathibitishwa, Kristo anatukuzwa, watakatifu wamefikia raha yao ya milele, Shetani anaondoshwa mbali na zambi inaondoshwa kabisa. Hakuna usiku tena, hakuna bahari, hakuna hitaji kwa jua au mwezi, hakuna laana, hakuna huzuni, hakuna maumivu wala machozi wala mauti. Kanisa la KWELI linangoja na kutazamia na hamu kubwa utimizo huu wa utukufu. Amina!